Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Kumi na Saba– Tarehe 24 Mei, 2014

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Azzan Zungu) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. SAID MOHAMED MTANDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. ZAINAB RASHID KAWAWA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na

Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. CECILIA D. PEROSSO - MSEMAJI MKUU WA KAMABI YA UPINZANI WA WIZARA YA KAZI NA AJIRA:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Kazi na Ajira kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

MHE. MOSES J. MACHALI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA UCHUKUZI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Uchukuzi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

KAULI ZA MAWAZIRI

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya kwa Mwaka 2014/2015
Wizara ya Kazi na Ajira

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyochambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira na Tume ya Usuluhishi na naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka 2013/2014. Naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa masikitiko makubwa napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa familia, ndugu na jamaa kwa kuondokewa na wenzetu Marehemu William Augustao Mgimwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Mheshimiwa Marehemu Said Ramadhani Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge

wa Jimbo la Chalinze. Tunamwomba Mwenyezi Mungu apokee Roho zao mahali pema peponi, AMINA!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kukipongeza Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ushindi wa kishindo uliopatikana katika uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni wa Wabunge na Madiwani katika maeneo mbalimbali nchini. Ushindi huo ni ushahidi tosha kwamba wananchi wanaendelea kukiamini na kukienzi Chama Cha Mapinduzi. Kwa namna ya pekee niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika kipindi hiki; Mheshimiwa Mahamoud Thabit Kombo wa Jimbo la Kiembe-Samaki, Zanzibar; Mheshimiwa Godfrey Mgimwa wa Jimbo la Kalenga, Iringa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete wa Jimbo la Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kutuongoza na kutoa maelekezo katika kuimarisha viwango vya kazi, uboreshaji wa maslahi ya wafanyakazi, ushirikishwaji wa wafanyakazi na ukuzaji wa ajira nchini. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kuendelea kuwa na utulivu katika sekta ya kazi hali ambayo imesaidia kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza nchini kwetu na hivyo kukuza ajira kwa makundi mbali mbali ya wananchi katika nchi yetu na hivyo kuwapunguzia umasikini. Tunaomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu ya kuendelea kunipa nafasi ya kuiongoza Wizara hii muhimu kwa maendeleo na ustawi wa wananchi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, kwa hotuba zao nzuri zilizoelezea vema mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2014/2015. Hotuba zilizotoa dira katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninapenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, iliyojadili na kuyakubali Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu. Wizara yangu imezingatia ushauri

walioutoa ambao umesaidia sana kuiboresha bajeti hii ninayoiwasilisha leo mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara Fungu 65 na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Fungu 15 kwa mwaka 2013/2014. Sehemu ya pili ni Mpango na Bajeti ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara Fungu 65 na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Fungu 15 kwa mwaka 2014/2015 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Kazi kwa Mwaka 2013/2014. Katika kutekeleza Mpango Kazi wa Wizara wa mwaka 2013/2014 kulingana na majukumu yake, tumezingatia Sera, Sheria, Mipango na Mikakati ya Kitaifa, Maelekezo ya Serikali, Ushauri wa Kamati ya Bunge na Ahadi za Waziri Bungeni wakati akihitimisha Hotuba yake kuhusu Mpango na Bajeti ya mwaka 2013/2014. Katika kipindi hiki tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi na Ajira. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza majukumu yake ya kusimamia viwango vya kazi, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji wa Wafanyakazi sehemu za kazi, kuboresha hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi na usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara yaani Fungu 65, iliidhinishiwa Bajeti ya jumla ya Shilingi 13,034,148,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 4,769,301,200 sawa na asilimia 37 zilitengwa kwa ajili ya kulipa mshahara ya Watumishi na shilingi 8,264,846,800 sawa na asilimia 63 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2014, Shilingi 4,344,886,775 sawa na asilimia 91 ya fedha za Mishahara ya Watumishi na shilingi 2,764,106,935 sawa na asilimia 33 ya fedha za Matumizi mengine, zilitolewa na kutumika na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Kazi na Huduma za Ukaguzi. Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ambazo ni Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Namba 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi Namba 7 ya mwaka 2004. Utekelezaji umefanyika kwa kukagua sehemu za kazi, kutoa elimu ya kuhusu Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri na kuchukua hatua za kisheria kwa wasiozingatia Sheria za Kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhimiza mahusiano mema baina ya Waajiri na Wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa

migogoro ya kikazi kwa njia ya majadiliano ya pamoja kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi hiki Wizara imekagua jumla ya maeneo ya kazi 1,843 katika sehemu mbalimbali nchini kwa lengo la kuona namna Sheria za kazi zinavyozingatiwa.

Baadhi ya Waajiri waligundulika kukiuka na kutokutekeleza Sheria zinazohusiana na viwango vya kazi, haki za msingi za kazi pamoja na haki za kuanzisha na kujiunga na vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zifautazo zilichukuliwa. Kwanza, Waajiri 11 walifikishwa mahakamani ambapo waajiri watatu walitozwa faini ya jumla ya shilingi 2,900,000 . Pili, waajiri wawili waliamuriwa kulipa haki za wafanyakazi wao jumla ya shilingi 21,000,000 na tatu waajiri 78 walipewa Amri tekelezi yaani *Compliance order*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua hizi zilizochukuliwa kwa Waajiri wanaokiuka taratibu, Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Elimu hiyo ilitolewa kwa Wafanyakazi 8,201 na Waajiri 412 wa sekta za Viwanda na Biashara, Afya, Kilimo, Ujenzi, Huduma za Hoteli, Ulinzi binafsi, Madini na Usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha wafanyakazi na waajiri kujadiliana kwa pamoja katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Katika kipindi hiki jumla ya Mikataba ya Hali Bora 53 ilisainiwa na kusajiliwa na Wizara ikuhusisha za Viwanda, Maji, Biashara pamoja na Hoteli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi. Wizara imeendelea kushughulikia suala la kuboresha maslahi ya wafanyakazi katika sekta binafsi. Kufuatia kutangazwa kwa viwango cha kima cha chini cha mishahara katika sekta mbalimbali kupitia Tangazo la Serikali namba 196 la Tarehe 28 Mwezi wa Sita, mwaka 2013. Wizara imepokea na kutataua malalamiko 17 kutoka kwa Waajiri na Wafanyakazi yaliyohusu upangaji na utekelezaji wa viwango hivi vya kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fidia kwa Wafanyakazi yaani *The Workers Compensation Fund*. Wizara imeandaa kanuni za tozo ambapo Waajiri wote wa sekta ya Umma na Binafsi watachangia katika kuendesha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 74(1) cha Sheria ya Mfuko huu wa Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2008. Mfuko utaendeshwa kwa kutumia

mfumo wa bima na pensheni kwa kutoa mafao kwa watumishi watakaoumia, kupatwa magonjwa yanayosababishwa na mazingira ya kazi au kufariki mahali pa kazi. Mfuko huu utaanza utekelezaji mwaka huu wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Jamii. Katika kuendelea kuimarisha na kupanua huduma za hifadhi ya jamii, Wizara kwa kushirikiana na SSRA imewezesha ziara za mafunzo na kupata uzoefu nje ya nchi kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Watumishi wa Wizara na SSRA katika nchi za Kenya, Uganda, Thailand, Indonesia, China na India. Uzoefu uliopatikana utaiwezesha Wizara kuandaa mapendekezo ya kuboresha na kupanua huduma za Hifadhi ya Jamii nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vita dhidi ya Ajira Mbaya kwa Mtoto. Wizara imeendelea kuratibu juhudi za kukomesha utumikishwaji na ajira mbaya kwa watoto. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* imetoa Mafunzo kuhusu Mpango Kazi wa Kitaifa wa kutokomeza utumikishwaji wa watoto kwa watumishi 35 wa taasisi zisizo za kiserikali na watumishi 190 wa Halmashauri za Wilaya za Simanjiro, Karatu, Lushoto, Kilombero, Mbeya Mjini, Songea Mjini, Dodoma, Singida, Nzega, Tabora Mjini, Kigoma, Kahama, Kishapu na Nyamagana. Aidha, katika kipindi cha sasa hadi Juni, 2014 mafunzo haya yataendelea kutolewa kwa watendaji wa Halmashauri za Wilaya za Iringa, Mufindi, Makete, Iramba, Chamwino, Arusha, Hai, Chunya, Sumbawanga, Musoma, Bariadi, Rufiji, Pangani, Sengerema, Mvomero na Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali ya *Plan International* na WEKEZA yameweza kuwazuia watoto 3,016 wakiwemo wavulana 1,611 na wasichana 1495 wenye umri kati ya miaka 5 – 13 kuingia kwenye utumikishwaji. Jumla ya watoto 2,232 wakiwemo wavulana 1,137 na wasichana 1,095 walitolewa kwenye utumikishwaji. Watoto hawa walipatiwa misaada ya vifaa vya shule na kuwawezesha kuingia shule za msingi na shule za ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikishwaji wa Wafanyakazi. Wizara imeendelea kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kuhusu ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu za kazi. Hatua hii imesaidia sana kuboresha mahusiano na kuwepo hali ya utulivu katika maeneo ya kazi. Aidha, kutokana na elimu iliyotolewa, Wizara ilitatua jumla ya migogoro 9 iliyopokelewa kutoka kwa waajiri wa sekta za Viwanda, Ujenzi na Usafirishaji walio katika Mikoa ya Dar es salaam, Tanga, Mwanza, Musoma na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ushirikishaji wa wafanyakazi nchini, Wizara iliratibu kikao kimoja cha viongozi wa vyama vya Wafanyakazi kilichomshirikisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. Kikao hicho kilijadili masuala mbalimbali kuhusiana na hali na maslahi ya wafanyakazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukuzaji wa Ajira Nchini. Wizara imeendelea na juhudi za kuratibu sekta mbalimbali katika kukuza ajira nchini kulingana na Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo nchini. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 jumla ya ajira 630,616 zilizalishwa. Ajira hizo zilizalishwa katika sekta zifuatazo:- Kilimo ajira 130,974; Elimu ajira 36,073; Ujenzi wa Miundombinu ajira 32,132; Nishati na Madini ajira 453; Afya ajira 11,221. TASAF ajira 8,686 na Sekta nyingine Serikalini ajira 2,321 wakati Sekta binafsi ajira 211,970; Viwanda vidogo na vya kati (*SMEs*) ajira 7,192; miradi ya uwekezaji kupitia Maeneo Huru ya Uwekelezaji (*EPZ*) ajira 26,381; mawasiliano ajira 13,619; na miradi kupitia kituo cha uwekezaji (*TIC*) ajira 149,594.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika juhudi za kuwajengea vijana uwezo wa kuwawezesha kujiajiri wenyewe katika maeneo yao, imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 11,500. Mafunzo hayo yalilenga katika kubadili fikra za vijina kuwa ajira ni pamoja na kujiajiri, kuwajengea uwezo vijana katika kutambua fursa zilizopo, namna bora ya kuandaa miradi, kutafuta masoko na kutunza mahesabu ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti;Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO),* pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umasikini Nchini *(REPOA),* iliandaa kongamano la kitaifa la kukuza ajira kwa vijana mwezi Desemba, 2013. Kongamano hilo lililozinduliwa na kuongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Gharib Bilal lilihusisha vijana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na; Waheshiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Vikundi vya Vijana; Wanataaluma, Wataalamu mbalimbali na Washirika wa Maendeleo.

Kongamano lilijadili changamoto, fursa zilizopo na kubadilishana uzoefu katika kukuza ajira kwa vijana nchini. Mapendekezo yaliyotolewa katika Kongamano hilo yalitumika kuboresha Mpango wa utekelezaji Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana, ambayo itaanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeratibu ushiriki wa wajasiriamali wa sekta isiyo rasmi 193 katika Maonesho ya 14 ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki yaliyofanyika mjini Nairobi, Kenya mwezi Desemba, 2013. Maonyesho hayo yamesaidia kuwapatia fursa wajasiriamali hao kujifunza mbinu na

teknolojia mpya zinazotumiwa na wajasiriamali wa nchi jirani katika kuboresha bidhaa wanazozalisha pamoja na kupata masoko mapya ya kuuza bidhaa zao na hivyo kukuza biashara na ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti;Kuimarisha ukusanyaji taarifa na takwimu za ajira.Wizara imeendelea kuimarisha utaratibu wa ukusanyaji wa taarifa za ajira nchini kwa kuanzisha mfumo wa kielekitroniki wa kupokea na kutoa taarifa za soko la ajira nchini *(Labour Market Information System)*. Mfumo huu unasaidia kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri pamoja na kutoa taarifa za wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu nchini. Mfumo huo unasaidia kutoa taarifa kwa mwekezaji mwenye nia ya kuja kuwekeza nchini popote pale alipo duniani kujua ni aina gani ya ujuzi unaopatikana nchini na hivyo kukuza ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kufanya utafiti wa hali ya Nguvu Kazi nchini *(Integrated Labour Force Survey)*. Utafiti huu utatuwezesha kupata taarifa sahihi za hali ya ajira nchini ambayo itasaidia katika kupanga Mipango ya baadaye ya kukuza ajira na kupunguza umasikini nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,pia katika mwaka 2013/2014 Wizara iliandaa mwongozo wa kubaini idadi ya ajira zitakazozalishwa na Wizara, Idara za Serikali, Tawala za Mikoa, Halmashauri na Wakala za Serikali wakati wa kutekeleza bajeti zao za mwaka za miradi ya maendeleo. Kulingana na Mwongozo huo taasisi hizo zinawajibika kutoa taarifa za hali ya ajira katika maeneo yao katika kila kipindi cha robo ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Huduma za Ajira, Wakala wa Huduma za Ajira. Kufuatia malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi walioajiriwa kupitia Wakala wa Huduma za Ajira, Wizara ilifanya uchunguzi na kubaini ukiukwaji mkubwa wa haki za watumishi ikiwa ni pamoja na malipo hafifu ya mshahara, wafanyakazi kunyimwa haki ya kujiunga na hifadhi ya jamii na haki ya likizo. Kutokana na hali hii, mwezi Disemba, 2013 Wizara ilichukua hatua ya kusitisha utaratibu huu wa kukodisha wafanyakazi. Wizara imeandaa utaratibu sahihi wakusimamia shughuli za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira nchini ambazo zitasimamia ipasavyo Huduma za ajira nchini kulingana na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Vibali vya Ajira za Wageni, katika kusimamia ajira za wageni nchini kwa lengo la kuhakikisha ajira hizo ni kwa manufaa ya nchi na pia kulinda ajira za Watanzania, mwaka 2013/2014, Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi 7,432 ya vibali vya ajira za wageni vya Daraja B. Kati ya maombi hayo, maombi 6,237 sawa na asilimia 83.9 yalipendekezwa

kupewa vibali, maombi 1,175 sawa na asilimia 15.8 yalikataliwa na maombi 20 sawa na asilimia 0.3 yalisitishwa kwa uchunguzi. Aidha, Wizara imefanya ukaguzi katika kampuni 12 na migodi 6 katika mikoa ya Dar es Salaam, Shinyanga, Mara, Geita na Tabora kwa lengo la kuhakiki vibali vya ajira. Kampuni zilizoonekana kukiuka taratibu zilichukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kusitishwa vibali vyao vya ajira. Wizara imekamilisha mapendekezo ya mswada wa Sheria ya Ajira ya Wageni ili kuimarisha na kuongeza ufanisi katika kusimamia ajira za wageni nchini. Sheria inayopendekezwa kutungwa itawezesha kuwepo kwa Mamlaka moja ya kutoa vibali vya ajira kwa wageni ili kuondoa mkanganyiko wa kisheria uliopo kwa sasa unaozipa mamlaka zaidi ya moja katika kutoa vibali vya ajira. Matokeo ya utekelezaji wa Sheria hiyo ni pamoja na kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa soko la ajira nchini na kusimamia ipasavyo ajira za wageni nchini ili kuongeza tija katika kujenga uchumi kupitia uwekezaji na kuongeza ajira za watanzania katika mameneo ya uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti;Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za Wafanyakazi na Waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Katika mwaka 2013/2014 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

Kusajili Chama kimoja cha wafanyakazi kijulikanacho kama*TAZARAWorkers' Union–Tanzania (TAWUTA)* pamoja na Shirikisho la vyama vya walimu vya Afrika Mashariki *(FEATU);*

Kukagua taarifa za hesabu za vyama 14 vya wafanyakazi, Mashirikisho mawilina vyama viwili vya waajiri;

Kufuta Chama kimoja cha waandishi wa habari *(TUJ)* baada ya kukiuka masharti ya kisheria; na Kutoa elimukwa wafanyakazi na waajiri juu ya uhuru wa kujumuika pamoja na umuhimu wa kuheshimu Katiba za vyama vya wafanyakazi na waajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti;Kujenga Uwezo wa Wizara, katika kipindi cha mwaka 2013/2014 tumetekeleza yafuatayo katika kujenga uwezo wa Wizara:-

Kuajiri watumishi wawili kupitia Tume ya Ajira Serikalini ambao ni Afisa Kazi Daraja la II mmoja na Katibu Mahsusi Daraja la III mmoja;

Wizara imewezesha watumishi 21 kupata mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi na watumishi watano ndani ya nchi ili kuongeza ujuzi na utaalamu katika utendaji wao wa kazi.

Kusimamia zoezi la *OPRAS*kwa watumishi 279 wa Wizara kulingana na muongozo wa Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Umma chini za Wizara, Wizara imeendelea kusimamia shughuli za taasisi sita za umma zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA),* Shirika la Tija la Taifa *(NIP),* Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*.

Utekelezaji wa mipango na kazi kwa mwaka 2013/ 2014 kupitia taasisi hizi, umeainishwa kwa kina katika kitabu changu kuanzia ukurasa wa 20 hadi wa 31 katika hicho kitabu cha hotuba. Kwa uupi utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)*. Wakala umesimamia na kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa kufanya yafuatayo:-

Kwanza, kukaguamaeneo ya kawaida ya kazi 3,626, Kufanya ukaguzi maalum 12,290.Kaguzi hizo zilifanywa katika maeneo ya umeme, *boilers*, mitungi ya hewa, zana za kunyanyulia vitu vizito na vipimo vya mazingira. Aidha, wafanyakazi 37,972 walipimwa afya zao.

Pili, imesajili sehemu za kazi 1,671na sehemu za kazi 133 zilipewa vyeti vya kukidhi vigezo vya Sheria Namba 5 ya mwaka 2003 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

Tatu, maafisa 1,421wa afya na usalama mahali pa kazi kutoka sekta mbalimbali walipatiwa mafunzo ya usalama na afya mahala pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wakala wa Huduma za Ajira *(TaESA)*. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA)* imetekeleza kazi zifuatazo:-

Kusajili watafutakazi 1,533 na kutembelea waajiri 296. Aidha, watafutakazi 647 waliunganishwa kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi.

Kutoa mafunzo kwa watafutakazi 581 ili kuwajengea uwezo wa nanma bora ya kuandaa wasifu binafsi*(CV),* uandishi wa barua za maombi ya kazi na kuwapatia dondoo za usaili ili waweze kuhimiliushindani katika soko la ajira;

Kutoa ushauri kwa watafutakazi 1,513 juu ya uchaguzi wa fani zinazohitajika kwenye Soko la Ajira na mafunzo ya kazi wanayostahili ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri au kuajirika;

Mheshimiwa Mwenyekiti,Shirika la Tija la Taifa *(NIP)*,katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014, Shirika la Tija la Taifa *(NIP)*lilitekeleza yafuatayo:-

Kwanza, liliendesha mafunzo 63 za umma na binafsi zilizolenga kuongeza tija na kuzijengea uwezo.

Pili, limefanya tafiti tatu zilizolenga kukuza tija na kutoa huduma za ushauri katika kukuza tija kwa wateja 8 kutoka Taasisi za umma na binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)*.Katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* imetekeleza kazi zifuatazo:-

Kwanza, imeifanyia kaguzi 16 zaMifukoya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Sheria zilizounda Mifuko hiyo na pia Sheria ya Mamlaka, Kanuni na Miongozo yake kama inafuatwa ipasavyo. Kati ya kaguzi hizo, kaguzi nne (4) zilifanyika eneo la kazi *(onsite inspection)* 12 zilifanyika kwa njia ya taarifa *(offsite inspection);*

Pili, imetoa elimu kwa watu 7,200wa makundi mablimbali kuhusu Sheria ya Hifadhi ya Jamii.

Tatu, imetoa Miongozo minne inayohusu taratibu za Mikutano ya Kila Mwaka ya Wanachama wa Mifuko. Utayarishaji wa taarifa za Mwaka za Mifuko, Utangamano wa Mifumo ya Mawasiliano ya Mifuko na Ujumuishaji wa vipindi vya kuchangia.

Nne, imeanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Mawasiliano kati ya Mamlaka, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, *NIDA*, na wadau wengine *(Core Business Application);* kwa lengo la kuboresha mawasiliano katika sekta ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*.Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*limetekeleza kazi zifuatazo:-

Kwanza, limekusanya mapato ya kiasi cha shilingi milioni 705,692.7 sawa na asilimia 74.5 ya lengo na kutumika fedha hizo katika kulipa mafao ya Wanachama, kuwekeza katika vitega uchumi, kulipa gharama za uendeshaji na kuwekeza katika miradi ya maendeleo;

Pili, limeendesha semina 1,93, kwa waajiri na wanachama nchi nzima ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii unaotekelezwa na *NSSF*;

Tatu, Shirika limeandikisha wanachama wapya 80,124 ambao ni asilimia 63.12 ya lengo lililokusudiwa. Aidha, Shirika limelipa mafao mbalimbali ya jumla ya shilingi milioni 235,559.2 ambazo ni asilimia 157.8 ya lengo kwa wanachama 73,742;

Nne, Shirika limeendelea na utaratibu wa kutoa mikopo katika Sekta isiyo rasmi *(Informal Sector),* kwa wanachama wake katika vikundi vya *SACCOS* na VICOBA ambapo shilingi bilioni 29.6 zimetolewa kwa wanachama 3,501 katika mikoa 23 ya Tanzania Bara. Wilaya zilizonufaika na mpango huu ni zifuatazo:-

Temeke, Ilala, Kinondoni, Arumeru Mashariki, Singida Mjini, Kigoma Ujiji, Masasi, Kahama, Nyamagana, Njombe, Ilemela, Karagwe, Tabora, Bukoba, Mheza, Dodoma, Arusha, Moshi, Kilosa, Tanga, Musoma, Serengeti Singida, Geita, Ifakala, Morogoro, Kibaha, Mafia, Mafinga, Bunda, Mbeya, Tandahimba, Kigoma Vijijini na Kibondo.

Nia la lengo la *NSSF*ni kuzifikia wilaya zote nchini, hivyo basi natoa wito kwa Wahehsimiwa Wabunge watumie fursa hii kuwafahamisha wananchi wao wajiunge na *NSSF* ili wapate mikopo.

Tano,Shirika linaendelea na Ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2015;

Sita, Shirika limeendelea na miradi ya ujenzi wavitega uchumi katika mikoa yaMorogoro, Shinyanga, Kilimanjaro na Wilaya ya Ilala.

Saba, katika miradi inayofanywa kwa ushirikiano na Wadau wengine. Ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma *(MP's Village),* mtaalamu/mwelekezi amekamilisha kuandaa michoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti,sasa tunaingia kwenye Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*. Tume ya Usuluhishi na Uamuzi ina jukumu la kusuluhisha migogoro ya kikazi, kuamua migogoro ya kikazi na kuratibu shughuli za Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee)*. Vile vile Tume ina jukumu la kutoa elimu ya ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi iliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,274, 978,000/=. Kati ya fedha hizo Shilingi 924,978,000/= ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 1,350,000,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2014, Tume imetumia jumla ya Shilingi 1,272,559,342/= sawa na asilimia 55.9 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida.

Maelezo ya kina ya utekelezaji wakazi mbalimbali za Tume katika mwaka 2013/14, yameainishwa kwa kina kuanzia ukurasa wa 33 hadi 35 katika kitabu cha hotuba. Kwa muhitasari utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Tume imesajili migogoro 8,584 ambapo migogoro 3,144 ilisikilizwa na kupatiwa ufumbuzi. Migogoro 1,935 ilimalizika kwa njia ya usuluhishi na migogoro 1,209 ilimalizika kwa njia ya uamuzi. Migogoro 2,296 inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali za usuluhishi na uamuzi;

Pili, kushirikiana na Shirika la Kazi la Kimataifa *(ILO)*, linaendelea kutafsiri kitabu cha mwongozo wa kuzuia na kutatulia migogoro ya kikazi *(Dispute Prevention and Resolution Training Guide)* kutoka katika lugha ya kingereza kwenda lugha ya kiswahili;

Tatu, kuwezesha uundwaji wa mabaraza 51 ya Wafanyakazi katika Taasisi mbalimbali ambazo ni Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji 13, na Taasisi za Umma 38, Wizara, Idara za Serikali, Wakala na Mashirika.

Nne, Kutoa mafunzo ya kuzuia na kutatua migogoro sehemu za kazi kwa Taasisi 35 ambazo ni Halmashauri 16 za Wilaya, Miji na ofisi za makatibu Tawala za Mikoa, Taasisi 18 za Serikali, Wizara, Idara, Wakala na Mashirika na Sekta binafsi;

Mheshimiwa Mwenyekiti; Mpango wa kazi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Kazi na Ajira. Katika mwaka 2014/2015 Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia Sheria na viwango vya kazi, ushirikishwaji wa Wafanyakazi na kusuluhisha migogoro sehemu za kazi; kusimamia usalama na afya mahali pa kazi, kukuza na kutoa huduma za ajira; kuboresha ufanisi na tija kazini na kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Aidha, Wizara itatekeleza mpango wa matokeo makubwa sasa *(BRN)* unaolenga kuboresha mazingira ya Biashara nchini.

Kazi zilizopangwa kutekelezwakatika mwakawa fedha 2014/ 2015 ngazi ya Wizara, zimeainishwa kwa kina kuanzia ukurasa wa 36 hadi 46 wa kitabu cha hotuba. Kwa muhitasari, kazi zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, Usimamizi Kazi na Huduma za Ukaguzi, Wizara inapanga kufanya kaguzi sehemu za kazi 3,274 zikiwemo kaguzi za kawaida, maalum na ufuatiliaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Lengo ni kuhakikisha kuwa Sheria za kazi zinatekelezwa ipasavyo ili kupunguza migogoro na hatimaye kuongeza tija na uzalishaji.

Pili, Wizara inapanga kutoa elimu kuhusu sheria za kazi kwawaajiri 1,200 na wafanyakazi 4,000 katika sekta mbalimbali kwa madhumuni ya kuwajengea uelewa wa namna bora ya kutekeleza viwango vya kazi kwa mujibu wa Sheria;

Tatu, Wizara inaanga kuratibu na kukuza majadiliano ya utatu kupitia Baraza la Ushauri la Kazi, Uchumi, na Jamii *(LESCO)*. Katika kipindi hiki Baraza litafanya vikao vyake kwa mujibu wa Sheria ili kuweza kujadili na kutoa ushauri kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kuhusiana na masuala ya utekelezaji wa Sheria za kazi, ukuzaji wa fursa za ajira na ukuzaji wa tija na uzalishaji nchini.

Nne, Wizara inapanga kuratibu na kuboresha upangaji wa kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi kupitia Bodi za Mishahara za Kisekta.

Tano, Wizara inapanga kuendelea na jitihada za kupambana na ajira mbaya kwa watoto kwa kushirikiana na Wizara zenye dhamana ya watoto, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wabia wa Maendeleo na Mashirika yasiyo ya kiserikali. Katika kipindi hiki, Wizara inatarajia kuzuia watoto 4,000 kuingia kwenye ajira mbaya na kuwaondoa watoto 10,000 wanaotumikishwa kwenye ajira mbaya.

Kujenga uwezo wa wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Kisekta ya Kuratibu Masuala ya Kupambana na Utumikishwaji wa Watoto nchini na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake,

Sita, Wizara inapangwa kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now)* wenye lengo la Kuboresha Uwekezaji na Mazingira ya Biashara nchini kwa kuhuisha Sheria za kazi, kuimarisha ukaguzi sehemu za kazi,uelimishaji kuhusu Sheria za kazi, kuboresha huduma za rasilimali watu na mazingira ya kufanyia kazi;

Saba, Wizara inapangwa kuendelea na hatua za kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuimarisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na kuboresha mafao ya pensheni kwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii; ikiwa nib pamoja na kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi watakaoumia, kufa au kupata magonjwa yatokanayo na kazi.

Mfuko huu utaendeshwa kwa kutumia mfumo wa bima na *pension* na utatoa mafao yafuatayo:-

Gharama za matibabu yaani *medical aids,* malipo ya ulemavu wa muda, malipo ya ulemavu wa kudumu, gharama za matunzo kwa mgonjwa, yaani

consultant attendant care, gharama za viuongo bandia, *artificial lamps,* gharama za ukarabati na ushauri nasaha *(rehabilitation benefits),* malipo ya fidia ya ulemavu wa kudumu kwa mfumo wa *pension* ya kila mwezi, gharama za mazishi endapo mhusika au mgonjwa atafariki na malipo ya fidia kwa wategemezi wa marehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kuratibu juhudi za serikali za kukuza ajira nchini. Jumla ya ajira laki saba zinategemewa kuzalishwa katika mwaka 2014/2015 kutokana na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo itakayotelezwa na Taasisi za Umma, *Program* ya Kukuza Ajira kwa Vijana pamoja na hatua mbalimbali za Uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji (*TIC),* maeneo huru ya biashara *EPZ* na sekta binafsi.

Katika eneo hili wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo. Kwanza, kuratibu uingizaji wa masuala ya ukuzaji wa ajira katika mipango ya *program* za maendeleo za kisekta kwa kutoa mafunzo katika mikoa mitatu pamoja na kufuatilia utekelezaji wa mwongozo wa namna ya kuhuisha ukuzaji ajira nchini.

Pili, kusimamia utekelezaji wa *program* ya kukuza ajira kwa vijana ambayo imelenga kuwajengea vijana uwezo wa *study* mbalimbali za kazi na ujasiriamali, kuwapatia vijana mitaji yenye masharti nafuu na nyenzo za uzalishaji na kutenga maeneo maalum ya uzalishaji wa maeneo ya kufanya biashara. *Program* hiyo itaanza mwaka wa fedha 2014/2015 ambapo jumla ya Shilingi bilioni tatu zimetengwa.

Tatu, kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa za soko la ajira nchini ikiwa ni pamoja na kuratibu ukusanyaji wa taarifa za ajira zinazozalishwa na Wizara, Idara za Serikali Tawala za mikoa na mamlaka ya Serikali za mitaa kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Nne, kuendelea kufanya utafiti wa hali ya nguvukazi nchini, tano, kuratibu na kuwezesha ushiriki wa wajasiriamali wadogo wa sekta isiyo rasmi 250 wa Tanzania katika maonesho ya 15 ya nguvukazi au jua kali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayotarajiwa kufanyika mjini Kigali Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ajira. Wizara katika kuimarisha huduma za ajira itatekeleza kazi zifuatazo. Kwanza, itakamilisha na kuwasilisha Bungeni Muswada wa sheria ya ajira ya wageni inayolenga kuimarisha na kuongeza ufanisi katika utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni nchini.

Pilii, wizara itaandaa mfumo wa ki-elektroniki wa kutoa vibali vya ajira za wageni nchini kupitia mpango wa matokeo makubwa sasa, yaani *Big Results Now* unaolenga kuboresha mazingira ya biashara nchini.

Tatu, Wizara itaandaa kanuni na taratibu kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa sheria ya ajira ya wageni nchini na.

Nne, Wizara itasimia kanuni za utoaji wa huduma za ajira zinazotolewa na mawakala binafsi wa huduma za ajira kulingana na sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa vyama vya wafanyakazi. Wizara itaendelea na jukumu la kusajili na kusimamia vyama vya waajiri na wafanyakazi nchini kama ifuatavyo:-

Kwanza, itashughulikia maombi ya usajili wa vyama vya wafanyakazi na waajiri;

Pili, itaelimisha viongozi wa vyama vya wafanyakazi na waajiri juu ya sheria za kazi na Kanuni zake;

Tatu, itashughulikia migogoro inayojitokeza kati ya vyama vya waajiri na wafanyakazi; na

Nne, itasimamia utekelezaji wa katiba za vyama kwa mujibu wa sheria ya mahusiano kazini namba sita ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga uwezo wa Wizara. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imepanga kujenga uwezo wa Wizara kutekeleza shughuli zifuatazo.

Kwanza, kuwajengea uwezo watumishi 45 wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na wengine 10 kuwawezesha kupata mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali;

Pili, kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua nyenzo na vitendea kazi pamoja na kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ulinzi, usafi na matengenezo ya vifaa vya ofisi;

Tatu, kuendelea kutoa mafunzo ya maadili kulingana na sheria na miongozo ya utumishi wa umma, vita dhidi ya rushwa, utawala bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI kwa watumishi 150 wa Wizara. Aidha Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI;

Nne, kuimarisha ofisi za kazi za mikoa ili ziweze kusimamia viwango vya kazi kwa mujibu wa sheria; na

Tano kuboresha mfumo wa Tehama, mawasiliano pamoja na tovuti ya wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za umma chini ya Wizara. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ya Kazi na Ajira itaendelea kusimamia taasisi za umma zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu yao. Kazi zilizopangwa kutekelezwa na taasisi hizo zimeainishwa kwa kina kuanzia ukurasa wa 47 hadi wa 57 katika kitabu cha hotuba. Kwa muhtasari naomba nizitaje kama ifuatavyo:-

Wakala wa usalama na afya mahala pa kazi (OSHA). Kwanza ni kufanya kaguzi sehemu za kazi za kawaida 20,000, na 16,000 maalum kuhusu afya na usalama mahali pa kazi na kupima afya za wafanyakazi 60,000 katika sehemu mbalimbali za kazi.

Pili, kusajili sehemu 2,000 mpya za kazi ili ziweze kukidhi viwango na kanuni za afya na usalama mahala pa kazi, na tatu, kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali yanayohusu afya na usalama mahala pa kazi. Wafanyakazi 1000 wanatarajiwa kupata mafunzo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala wa huduma za ajira (TaESA). Wakala wa huduma za ajira Tanzania TaESA itatekeleza kazi zifuatazo.

Kwanza, kusajili watafuta kazi 2000 na kuunganisha watafuta kazi 1000 kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi.

Pili, kutembelea waajiri 1000 kwa lengo la kubaini idadi na aina za fursa za ajira zilizopo.

Tatu, kuendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa za soko la ajira kwa watafuta kazi na waajiri.

Nne, kuandaa vipindi 12 vya redio na luninga kwa lengo la kutoa elimu kwa watafuta kazi na umma kwa ujumla.

Tano, kutoa ushauri wa kitaalam yaani *consultancy services* kwa wadau juu ya masuala ya huduma za ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Tija la Taifa *(NIP)*. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la Tija la Taifa limepanga kutekeleza yafuatayo. Kwanza ni kuendesha mafunzo 80 ya uongozi yatakayohudhiriwa na watumishi 1200 kutoka taasisi za umma, binafsi na taasisi zisizokuwa za kiserikali, yaani *NGOs*.

Pili, Shirika litatoa huduma za ushauri elekezi kwa wateja 30 katika sekta za umma na binafsi na litafanya tafiti nne katika maeneo mbalimbali yanayolenga kuboresha tija viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamalaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *SSRA*. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *SSRA* itaendelea na hatua za kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo.

Kwanza, kushirikiana na Wizara ya kazi na ajira pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na wadau wengine kuandaa mapendekezo ya kuanzisha *pension* ya wazee.

Pili, kuendelea kutekeleza mkakati wa elimu kwa umma kwa lengo la kuongeza uelewa wa masuala ya jamii. Elimu hiyo itatolewa kikanda ambapo zaidi ya wananchama 15,000 wataelimishwa.

Tatu, kuendelea na zoezi la ukaguzi wa mifuko ya hifadhi za jamii ili kuhakikisha kuwa mifuko hiyo inaendesha shughuli zake kwa mujibu wa sheria na kwa manufaa ya wanachama.

Nne, kuendelea kukamilisha hatua mbalimbali za kuwianisha mafao ya hifadhi ya jamii kwa lengo la kuimarisha mifuko ya hifadhi ya jamii na kuboresha mafao ya *pension* kwa wastaafu.

Tano, kukamilisha uwekaji wa mfumo wa mawasiliano wa ki-elektroniki baina ya mamlaka na mifuko ya hifadhi ya jamii ambayo ni *core-business application* na kufundisha mifuko, kurekebisha na kutunza takwimu za wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Shirika la Taifa la hifadhi ya jamii kwa muhtasari litatekeleza kazi zifuatazo. Kwanza, kukusanya jumla ya Shilingi bilioni moja mia nne thelathini na saba na mia sita ishirini na nukta moja na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipia mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbali mbali, kulipa gharama za uendeshaji na kuwekeza katika Miradi ya Maendeleo.

Pili, kuendelea kutoa elimu kwa wanachama, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa hifadhi ya jamii chini ya *NSSF*.

Tatu, litaendea na utoaji wa mikopo kwa *SACCOS* na *VICOBA* kwa wanachama wa *NSSF*.

Nne, kuendelea na ujenzi wa daraja la Kigamboni.

Tano, kukamilisha ujenzi wa vitegauchumi katika mikoa ya Shinyanga, Morogoro, Kilimanjaro, *NSSF-RITA* na Wilaya ya Ilala.

Sita, kushiriki katika mradi wa ujenzi wa hospitali ya Apolo, ujenzi wa vijiji vya kisasa Kigamboni, ujenzi wa kijiji cha Bunge Dodoma yaani *MPs Village*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume sha Usuluhishi (CAM). Tume imeweka vipaumbele katika kutekeleza, kama ilivyoainishwa kwa kina kuanzia ukura huu wa 57 hadi 59 wa kitabu cha hotuba, lakini kwa muhtasari naomba nitaje majukumu hayo kama ifuatavyo.

Kwanza, ni kusuluhisha na kuamua migogoro 6500 ya kikazi,

Pili, kufanya tafiti juu ya migogoro ambayo haijasajiliwa katika Tume na kuishughulikia.

Tatu, kuendesha mafunzo 200 ya uelewa na ushauri wa kisheria kwa waajiri na wafanyakazi juu ya kuzuia na kutatua migogoro sehemu za kazi.

Nne, kuwezesha uanzishaji wa vyombo vya ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi.

Tano, kupokea na kusajiri mikataba ya kuunda mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi.

Sita, kutoa mafunzo ya maadili, vita dhidi ya Rushwa na utawala bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shukrani. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2013/2014 yametokana na ushirikiano wa hali ya juu wa viongozi n a wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi wote wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Mashirika na taasisi zake. Napenda kumshukuru sana wa kwanza Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga , Naibu Waziri wa Kazi na Ajira na Mbunge wa jimbo la Segerea kwa ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

Pili, napenda nimshukuru sana Katibu Mkuu wa Wizara yangu bwana Erick Shitindi, kwa ushirikiano, kwa ushauri anaonipatia kila mara ninapotekeleza shughuli zangu.

Tatu, napenda niwashukuru sana Wakuu wa Idara, Vitengo, na Watumishi wote wa Wizara yangu.

Nne, napenda niwashukuru Watendaji, Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara pamoja na Bodi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa njia ya pekee ninaomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Kazi la Uchumi na Jamii, yaani *RESCO*. Niwashukuru Chama cha Waajiri Tanzania *ATE* na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania yaani *TUCTA* kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu ana malengo ya Wizara yangu.

Nazishukuru pia Wizara na Taasisi, Mashirika na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Serikali na Sekta Binafsi ambazo tumeshirikiana nao kwa karibu sana kwa kipindi chote cha mwaka huu katika kutimiza malengo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru kwa dhati nchi na washirika wa maendeleo ambao wamechangia katika utekelezaji na mafanikio ya Wizara yetu. Shukrani za dhati ziende kwa Shirika la Kazi Duniani *(ILO), UNDP, UNICEF, UNFPA,* Shirika la Misaada la Kitaifa la Denmark *(DANIDA),* Idara ya kazi ya Marekani, Serekali ya Brazil na Benki ya Dunia.

Nakushukuru sana wewe binafsi, namshukuru Spika, Naibu Spika kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango na stahiki. Mwenyekiti nakushukuru sana, najua na leo utaendesha vizuri sana kikao hiki.

Pia natoa shukrani zangu za dhati kwa waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa michango yao ndani ya Bunge na nje ya Bunge, inayolenga kuboresha kazi katika Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa namna ya pekee ninampongeza lakini nimshukuru Waziri Kivuli mpya Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, kwa wadhifa huo alioupata na ninajua atanipa ushirikiano katika kutenda kazi hii na ninamtakia mema katika kusoma hotuba yake ya kwanza leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa mkoa wangu wa Mara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia na kwa namna ya pekee niishukuru sana familia yangu kwa mchango mkubwa na ushauri na uvumilivu wanaonipatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka 2014/2015. Naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 18,280,136,000 kwa Wizara, yaani kwa Fungu 65, na jumla ya Shilingi 4,683,837,000 kwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, yaani Fungu 15 kwa Mwaka

wa Fedha 2014/2015, ili kutekeleza Majukumu na Malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii katika mchanganuo ufuatao.

Fungu 65, yaani Wizara ya Kazi na Ajira Shilingi 2,815,205,000 zitatumika kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara, Shilingi 12,464,931,000 zitatumika kugharamia Matumizi Mengineyo *(OC)* na Shilingi 3,000,000,000 ni Fedha za Maendeleo za ndani kwa ajili ya kutekeleza *Program* ya kukuza ajira kwa vijana. Fungu 15, yaani Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Shilingi 1,833,837,000 zitatumika kulipa Mishahara ya Watumishi wa Tume, na 2,850,000,000 zitatumika kugharamia matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.kazi.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

HOTUBA YA WAZIRI WA KAZI NA AJIRA KAMA ILIVYOWEKWA MEZANI

HOTUBAYA WAZIRI WA KAZI NA AJIRA MHE. GAUDENTIA M. KABAKA (MB) AKIWASILISHABUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YAFEDHA KWA MWAKA 2014/2015

A. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika; kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii iliyochambua bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira **(Fungu 65)** na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **(Fungu 15)**, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako tukufu sasa likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi **(CMA)** kwa mwaka 2013/2014. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Malengo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

2. Mheshimiwa Spika; awali ya yote ninamshukuru mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kwa masikitiko makubwa napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole za dhati kwa familia, ndugu na jamaa za Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliofariki katika kipindi hiki ambao ni Marehemu William Augustao Mgimwa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga na Said Ramadhani Bwanamdogo aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, **AMINA!**

3. Mheshimiwa Spika; nitumie nafasi hii kukipongeza Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa ushindi wa kishindo uliopatikana katika uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni wa Wabunge na Madiwani katika maeneo mbalimbali nchini. Ushindi huo ni ushahidi tosha kwamba wananchi wanaendelea kukiamini na kukienzi Chama Cha Mapinduzi. Kwa namna ya pekee niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika kipindi hiki; Mheshimiwa Mahamoud Thabit Kombo wa Jimbo la Kiembe-Samaki, Zanzibar; Mheshimiwa Godfrey Mgimwa wa Jimbo la Kalenga, Iringa; na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete wa Jimbo la Chalinze.

4. Mheshimiwa Spika; naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuendelea kutuongoza na kutoa maelekezo katika kuimarisha viwango vya kazi, uboreshaji wa maslahi ya wafanyakazi, ushirikishwaji wa wafanyakazi na ukuzaji wa ajira nchini.

Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kuendelea kuwa na utulivu katika sekta ya kazi hali ambayo imesaidia kukua kwa uchumi wa nchi yetu na kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kuja kuwekeza nchini kwetu na hivyo kukuza ajira kwa makundi mbali mbali ya wananchi katika nchi yetu na hivyo kuwapunguzia umasikini. Tunaomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu.

5. Mheshimiwa Spika; napenda pia kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani yake kwangu na heshima kubwa aliyoionesha ya kuendelea kunipa nafasi ya kuiongoza Wizara hii muhimu kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu ya Tanzania.

6. Mheshimiwa Spika; napenda kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb) na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, Mbunge wa Jimbo la Bunda kwa hotuba zao nzuri zilizoelezea vema mwelekeo wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha wa 2014/2015. Malengo, maelezo na vigezo vilivyomo kwenye hotuba

hizo vimezingatiwa kikamilifu katika kuandaa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2014/2015.

7. Mheshimiwa Spika; kwa namna ya pekee ninapenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, Lindi na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi iliyojadili na kuyakubali Makadirio ya Matumizi ya Wizara yangu. Wizara yangu imezingatia ushauri walioutoa ambao umesaidia sana kuiboresha bajeti hii ninayoiwasilisha leo mbele ya Bunge lako tukufu.

8. Mheshimiwa Spika; Hotuba yangu imegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014. Sehemu ya pili ni Mpango na Bajeti ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 na maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huo.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KAZI KWA MWAKA 2013/2014

9. Mheshimiwa Spika; Wizara yangu ina jukumu la kuandaa, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali kuhusu viwango vya kazi, usawa na kazi za staha, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji sehemu za kazi, masuala ya kukuza tija sehemu za kazi na hifadhi ya jamii nchini.

10.Mheshimiwa Spika; katika kutekeleza Mpango Kazi wa Wizara wa mwaka 2013/14 kulingana na majukumu yake, tumezingatia Sera, Sheria, Mipango na Mikakati ya Kitaifa, Maelekezo ya Serikali, Ushauri wa Kamati ya Bunge na Ahadi za Waziri Bungeni wakati akihitimisha Hotuba yake kuhusu Mpango na Bajeti ya mwaka 2013/2014. Katika kipindi hiki tumefanikiwa kutekeleza yafuatayo:-

I. WIZARA YA KAZI NA AJIRA

11. Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2013/14 Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza majukumu yake ya kusimamia viwango vya kazi, ukuzaji wa ajira,
ushirikishwaji wa Wafanyakazi sehemu za kazi, kuboresha hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi na usalama na afya mahali pa kazi.

12. Mheshimiwa Spika; mwaka wa fedha 2013/ 2014, Wizara (**Fungu 65**), iliidhinishiwa Bajeti ya jumla ya Shilingi **13,034,148,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **4,769,301,200** sawa na asilimia **37** zilitengwa

kwa ajili ya kulipa mshahara wa Watumishi (PE), na shilingi **8,264,846,800** sawa na asilimia **63** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengine (OC).

13. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia tarehe 30 Aprili 2014, Shilingi **4,344,886,775** sawa na asilimia **91** ya fedha za Mishahara ya Watumishi (PE) na shilingi **2,764,106,935** sawa na asilimia **33** ya fedha za Matumizi mengine (OC) zilitolewa na kutumika na Wizara.

(a) Usimamizi wa Kazi na Huduma za Ukaguzi
Kufanya Ukaguzi Sehemu za Kazi

14. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi ambazo ni **Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004** na **Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004**. Utekelezaji umefanyika kwa kukagua sehemu za kazi, kutoa elimu ya kuhusu Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri na kuchukua hatua za kisheria kwa wasiozingatia Sheria za Kazi. Aidha, Wizara imeendelea kuwa karibu na Wafanyakazi kupitia vyama vyao na kuhakikisha kuwa inashughulikia matatizo yao kwa wakati. Wizara imeendelea kuhimiza mahusiano mema baina ya Waajiri na Wafanyakazi na kuhamasisha uzuiaji na utatuzi wa migogoro ya kikazi kwa njia ya majadiliano ya pamoja kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kukuza tija mahali pa kazi.

15. Mheshimiwa Spika; katika kipindi hiki, Wizara imekagua jumla ya maeneo ya kazi **1,843** katika sehemu mbalimbali nchini kwa lengo la kuona namna Sheria za kazi zinavyozingatiwa. Katika ukaguzi huu, baadhi ya Waajiri waligundulika kukiuka na kutokutekeleza Sheria zinazohusiana na viwango vya kazi, haki za msingi za kazi pamoja na haki za kuanzisha na kujiunga na vyama vya wafanyakazi katika sehemu za kazi.

16. Mheshimiwa Spika; Waajiri waliobainika kutokuzingatia Sheria na viwango vya kazi walichukuliwa hatua mbalimbali za kisheria. Waajiri **11** walifikishwa mahakamani ambapo waajiri **watatu** walitozwa faini ya jumla ya shilingi **2,900,000,** waajiri wawili waliamuriwa kulipa haki za wafanyakazi wao jumla ya shilingi **21,000,000** na waajiri **78** walipewa Amri tekelezi *(Compliance order)*.

17. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu Sheria za Kazi kwa wafanyakazi na waajiri katika maeneo mbalimbali ya kazi nchini. Elimu hiyo ilitolewa kwa Wafanyakazi **8,201** na Waajiri **412** wa sekta za Viwanda na Biashara, Afya, Kilimo, Ujenzi, Huduma za Hoteli, Ulinzi binafsi, Madini na Usafirishaji.

Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi

18. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kushughulikia suala la kuboresha maslahi ya wafanyakazi katika sekta binafsi. Kufuatia kutangazwa kwa viwango vya kima cha chini cha mishahara katika Sekta mbalimbali kupitia **Tangazo la Serikali No. 196 la tarehe 28/6/2013,** Wizara imepokea na kutatua malalamiko **17** kutoka kwa waajiri na wafanyakazi yaliyohusu upangaji na utekelezaji wa viwango hivyo vya kima cha chini cha mshahara.
19. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kuhamasisha wafanyakazi na waajiri kujadiliana kwa pamoja katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi. Katika kipindi hiki jumla ya **Mikataba ya Hali Bora 53** ilisainiwa na kusajiliwa na Kamishna wa Kazi ikihusisha sekta za Viwanda, Maji, Biashara pamoja na Hoteli.

Fidia kwa Wafanyakazi (The Workers Compensation Fund)

20. Mheshimiwa Spika; Wizara imekamilisha kanuni za tozo ambapo Waajiri wote wa sekta ya Umma na Binafsi watachangia katika kuendesha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 74(1) cha Sheria ya Mfuko huu Fidia kwa Wafanyakazi ya mwaka 2008 *(The Workers Compensation Act, 2008)*. Mfuko wa utaendeshwa kwa kutumia mfumo wa bima na pensheni kwa kutoa mafao kwa watumishi watakaoumia, kupatwa magonjwa yanayosababishwa na mazingira ya kazi au kufariki mahali pa kazi. Mfuko huu utaanza utekelezaji mwaka 2014/2015.

Hifadhi ya Jamii

21. *Mheshimiwa Spika;* Katika kuendelea kuimarisha na kupanua huduma za hifadhi ya jamii, Wizara kwa kushirikiana na SSRA imewezesha ziara za mafunzo na kupata uzoefu nje ya nchi kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Watumishi wa Wizara na SSRA katika nchi za Kenya, Uganda, Thailand, Indonesia, China na India. Uzoefu uliopatikana utaiwezesha Wizara na SSRA kuandaa mapendekezo ya kuboresha na kupanua huduma za Hifadhi ya Jamii nchini.

Vita dhidi ya Ajira Mbaya kwa Mtoto

22. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kuratibu juhudi za kukomesha utumikishwaji na ajira mbaya kwa watoto. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), chini ya ufadhili wa Serikali ya Brazili, imetoa Mafunzo kuhusu Mpango Kazi wa Kitaifa wa kutokomeza utumikishwaji wa watoto kwa watumishi 35 wa taasisi zisizo za kiserikali na watumishi 190 wa Halmashauri za Wilaya za Simanjiro, Karatu, Lushoto, Kilombero, Mbeya Mjini, Songea Mjini, Dodoma, Singida, Nzega, Tabora Mjini, Kigoma, Kahama, Kishapu na Nyamagana. Aidha, katika kipindi cha sasa hadi Juni, 2014 mafunzo haya

yataendelea kutolewa kwa watendaji wa Halmashauri za Wilaya za Iringa, Mufindi, Makete, Iramba, Chamwino, Arusha, Hai, Chunya, Sumbawanga, Musoma, Bariadi, Rufiji, Pangani, Sengerema, Mvomero na Mpanda.

23. Mheshimiwa Spika; Wizara kwa kushirikiana na mashirika yasiyo ya kiserikali ya "Plan International" na "WEKEZA" yanayotekeleza miradi ya kukomesha utumikishwaji wa watoto katika mikoa ya Geita, Kigoma na Tanga imeweza kuwazuia watoto **3,016** wakiwemo wavulana **1,611** na wasichana **1495** wenye umri kati ya miaka 5 – 13 kuingia kwenye utumikishwaji. Aidha, jumla ya watoto **2,232** wakiwemo wavulana **1,137** na wasichana **1,095** walitolewa kwenye utumikishwaji. Watoto hawa walipatiwa misaada ya vifaa vya shule na kuwawezesha kuingia shule za msingi na shule za ufundi.

Ushirikishwaji wa Wafanyakazi

24. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi kuhusu ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu za kazi. Hatua hii imesaidia sana kuboresha mahusiano na kuwepo hali ya utulivu katika maeneo ya kazi. Aidha, kutokana na elimu iliyotolewa Wizara ilitatua jumla ya migogoro **9** iliyopokelewa kutoka kwa waajiri wa sekta za Viwanda, Ujenzi na Usafirishaji walio katika mikoa ya Dar es salaam, Tanga, Mwanza, Musoma na Kigoma.

25. Mheshimiwa Spika; katika kuimarisha ushirikishaji wa wafanyakazi nchini, Wizara iliratibu kikao kimoja cha viongozi wa vyama vya Wafanyakazi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Kikao hicho kilijadili masuala mbalimbali kuhusiana na hali na maslahi ya wafanyakazi nchini.

(b) Ukuzaji wa Ajira Nchini

26. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea na juhudi za kuratibu sekta mbalimbali katika kukuza ajira nchini kulingana na Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo nchini. Hadi kufikia mwezi Aprili 2014 jumla ya ajira **630,616** zilizalishwa. Ajira hizo zilizalishwa katika sekta zifuatazo:-

Kilimo ajira **130,974**; Elimu ajira **36,073;** Ujenzi wa Miundombinu ajira **32,132;** Nishati na Madini ajira **453;** Afya ajira **11,221**. TASAF ajira **8,686;** na Sekta nyingine Serikalini ajira **2,321;** Sekta binafsi ajira **211,970;** Viwanda vidogo na vya kati (SMEs) ajira **7,192;** miradi ya uwekezaji kupitia Maeneo Huru ya Uwekelezaji *(EPZ)* ajira **26,381**; mawasiliano ajira **13,619;** na miradi kupitia kituo cha uwekezaji (TIC) ajira **149,594**.

27.Mheshimiwa Spika; Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* katika juhudi za kuwajengea vijana uwezo wa kuwawezesha kujiajiri wenyewe katika maeneo yao, imetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana **11,500** kupitia Mradi wa Kazi Nje Nje katika Mikoa **17** ya Tanzania Bara. Mafunzo hayo yalilenga katika kubadili fikra za vijina kuwa ajira ni pamoja na kujiajiri, kuwajengea uwezo vijana katika kutambua fursa zilizopo, namna bora ya kuandaa miradi, kutafuta masoko na kutunza mahesabu ya biashara.

28.Mheshimiwa Spika; Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO), pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Kuondoa Umasikini Nchini (REPOA), iliandaa kongamano la kitaifa la kukuza ajira kwa vijana mwezi Desemba, 2013. Kongamano hilo lililozinduliwa na kuongozwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Gharib Bilal lilihusisha vijana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na; Waheshiwa Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Vikundi vya Vijana; Wanataaluma, Wataalamu mbalimbali na Washirika wa Maendeleo.

Kongamano lilijadili changamoto, fursa zilizopo na kubadilishana uzoefu katika kukuza ajira kwa vijana nchini. Mapendekezo yaliyotolewa katika Kongamano hilo yalitumika kuboresha Mpango wa utekelezaji Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana.

29.Mheshimiwa Spika, Wizara imeratibu ushiriki wa wajasiriamali wa sekta isiyo rasmi **193** katika Maonesho ya **14** ya Nguvu Kazi/Jua Kali ya Afrika Mashariki yaliyofanyika mjini Nairobi, Kenya mwezi Desemba, 2013. Lengo la ushiriki huo lilikuwa ni kuwapatia fursa wajasiriamali hao kujifunza mbinu na teknolojia mpya zinazotumiwa na wajasiriamali wa nchi jirani katika kuboresha bidhaa wanazozalisha pamoja na kupata masoko mapya ya kuuza bidhaa zao ili kukuza biashara na ajira nchini.

Kuimarisha ukusanyaji taarifa na takwimu za ajira

30. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kuimarisha utaratibu wa ukusanyaji wa taarifa za ajira nchini kwa kuanzisha mfumo wa kielekitroniki wa kupokea na kutoa taarifa za soko la ajira nchini *(Labour Market Information System)*. Mfumo huu unasaidia kuwaunganisha watafuta kazi na waajiri pamoja na kutoa taarifa za wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu nchini. Mfumo huo unasaidia kutoa taarifa kwa mwekezaji mwenye nia ya kuja kuwekeza nchini popote pale alipo duniani kujua ni aina gani ya ujuzi unaopatikana nchini na hivyo kutokuwa na haja na kuajiri wageni, na hivyo kukuza ajira nchini.

31. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kufanya utafiti wa hali ya Nguvu Kazi nchini *(Integrated Labour Force Survey)*. Utafiti huu utatuwezesha kupata taarifa sahihi za hali ya ajira

nchini ambayo itasaidia katika kupanga Mipango ya baadae ya kukuza ajira na kupunguza umasikini nchini.

32. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014 Wizara iliandaa mwongozo wa kubaini idadi ya ajira zitakazozalishwa na Wizara, Idara za Serikali, Tawala za Mikoa, Halmashauri na Wakala za Serikali wakati wa kutekeleza bajeti zao za mwaka za miradi ya maendeleo. Kulingana na Mwongozo huo taasisi hizo zinawajibika kutoa taarifa za hali ya ajira katika maeneo yao katika kila kipindi cha robo ya mwaka.

(c) Huduma za Ajira - Wakala wa Huduma za Ajira

33. Mheshimiwa Spika, kufuatia malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi walioajiriwa kupitia Wakala wa Huduma za Ajira, Wizara ilifanya uchunguzi na kubaini ukiukwaji mkubwa wa haki za watumishi ikiwa ni pamoja na malipo hafifu ya mshahara, wafanyakazi kunyimwa haki ya kujiunga na hifadhi ya jamii na haki ya likizo. Kutokana na hali hii, mwezi Disemba, 2013 Wizara ilichukua hatua ya kusitisha utaratibu huu wa kukodisha wafanyakazi. Wizara imeandaa Kanuni za kusimamia shughuli za Wakala Binafsi wa Huduma za Ajira nchini ambazo zitasimamia ipasavyo Huduma za ajira nchini kulingana na Sheria.

Vibali vya Ajira za Wageni

34. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia ajira za wageni nchini kwa lengo la kuhakikisha ajira hizo ni kwa manufaa ya nchi na pia kulinda ajira za Watanzania, mwaka 2013/2014, Wizara ilipokea na kushughulikia jumla ya maombi **7,432** ya vibali vya ajira za wageni vya **Daraja B.** Kati ya maombi hayo, maombi **6,237** sawa na asilimia **83.9** yalipendekezwa kupewa vibali, maombi **1,175** sawa na asilimia **15.8** yalikataliwa na maombi **20** sawa na asilimia **0.3** yalisitishwa kwa uchunguzi. Aidha, Wizara imefanya ukaguzi katika kampuni **12** na migodi **6** katika mikoa ya Dar es Salaam, Shinyanga, Mara, Geita na Tabora kwa lengo la kuhakiki vibali vya ajira. Kampuni zilizoonekana kukiuka taratibu zilichukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kusitishwa vibali vyao vya ajira.

35. Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha mapendekezo ya mswada wa Sheria ya Ajira ya Wageni ili kuimarisha na kuongeza ufanisi katika kusimamia ajira za wageni nchini. Sheria itakayotungwa itawezesha kuwepo kwa Mamlaka moja ya kutoa vibali vya ajira kwa wageni ili kuondoa mkanganyiko wa kisheria uliopo kwa sasa unaozipa mamlaka zaidi ya moja katika kutoa vibali vya ajira. Matokeo ya utekelezaji wa Sheria hiyo ni pamoja na kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa soko la ajira nchini na kusimamia ipasavyo ajira za wageni nchini ili kuongeza tija katika kujenga uchumi kupitia uwekezaji.

(d) Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri

36. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kuhimiza na kufuatilia haki mbalimbali za Wafanyakazi na Waajiri, ikiwemo haki ya kuanzisha, kujiunga na kushiriki katika shughuli mbalimbali halali za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri. Katika mwaka 2013/2014 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Kusajili Chama kimoja cha wafanyakazi kijulikanacho kama TAZARA Workers' Union –Tanzania (TAWUTA) pamoja na Shirikisho la vyama vya walimu vya Afrika Mashariki (FEATU);

(ii) Kukagua taarifa za hesabu za vyama **14** vya wafanyakazi, Mashirikisho **mawili** na vyama **viwili** vya waajiri;

(iii) Kukagua vyama **sita** katika ngazi ya taifa kuhusu ujazaji wa **TUF 6** na **TUF 15** kulingana na matakwa ya Sheria;

(iv) Kufuta Chama **kimoja** cha waandishi wa habari (TUJ) baada ya kukiuka masharti ya kisheria; na

(v) Kutoa elimu juu ya uhuru wa kujumuika na changamoto zake pamoja na umuhimu wa kuheshimu Katiba za vyama vyao kwa wajumbe wa Vyama vya Wafanyakazi wa Baraza Kuu la THTU, Kamati Kuu ya utendaji ya CWT na Kamati Kuu ya utendaji ya TUCTA.

(d). Kujenga Uwezo wa Wizara

(vi) ***Mheshimiwa Spika;*** katika kipindi cha mwaka 2013/2014 tumetekeleza yafuatayo katika kujenga uwezo wa Wizara:-
(i) Kuajiri watumishi **wawili** kupitia Tume ya Ajira Serikalini ambao ni Afisa Kazi Daraja la II **mmoja** na Katibu Mahsusi Daraja la III **mmoja**;

(ii) Wizara imewezesha watumishi **21** kupata mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi na watumishi **watano** ndani ya nchi ili kuongeza ujuzi na utaalamu katika utendaji wao wa kazi. Aidha watumishi **wawili** wapo kwenye mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi na mtumishi **mmoja** yupo ndani ya nchi.

(iii) Kuthibitisha ajira za watumishi **14** baada ya kutimiza masharti ya ajira katika kipindi cha majaribio;

(iv) Kusimamia zoezi la OPRAS kwa watumishi **279** wa Wizara kulingana na muongozo wa Utumishi wa Umma. Aidha, Watumishi **195** walikamilisha mapitio ya malengo ya nusu mwaka (Julai hadi Desemba, 2013);

II. TAASISI ZA UMMA CHINI YA WIZARA

37. Mheshimiwa Spika; Wizara imeendelea kusimamia shughuli za taasisi **sita** za umma zilizo chini yake. Taasisi hizo ni Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA)*, Shirika la Tija la Taifa (NIP), Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*. Utekelezaji wa mipango na kazi kwa mwaka 2013/ 2014 kupitia taasisi hizi ni kama ifuatavyo:

(a) Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)

18. Mheshimiwa Spika; Wakala umesimamia na kufuatilia uzingatiaji wa masuala ya usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa kufanya ukaguzi maeneo ya kawaida ya kazi **3,626** (*General Workplace inspection*) ambao ni sawa na asilimia **24.1** ya ukaguzi **15,000** zilizopangwa na ukaguzi maalum **12,290** sawa na asilimia **90.6** ya ukaguzi **13,565** zilizopangwa kufanyika. Ukaguzi huo ulifanywa kwenye maeneo ya umeme, *boilers*, mitungi ya hewa, zana za kunyanyulia vitu vizito na vipimo vya mazingira. Aidha, wafanyakazi **37,972** walipimwa afya zao sawa na asilimia **101.2** ya lengo la kuwapima wafanyakazi **37,500**.

39. Mheshimiwa Spika; taratibu za kupendekeza kuridhia mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi umefanyika. Mikataba hiyo ni Mkataba Na.155 *(Occupational Safety and Health Convention, 1981),* Mkataba Na.187 *(Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006)* Mkataba Na.167 *(Occupational Safety in Construction Convention, 1988)*.

40. Mheshimiwa Spika; jumla ya sehemu za kazi **1,671** sawa na asilimia **131** kati ya sehemu za kazi **1,275** zilizopangwa zilisajiliwa. Sehemu za kazi **133** zilipewa vyeti vya kukidhi vigezo vya Sheria Namba 5 ya mwaka 2003 ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

41. Mheshimiwa Spika; mafunzo na kozi mbalimbali kuhusu Usalama na Afya Mahali pa Kazi yamefanyika kwa maafisa **1,421** wa afya na usalama mahali pa kazi kutoka sekta mbalimbali. Kozi hizi zinajumuisha kozi ya Taifa ya Usalama na Afya, Kozi ya utoaji wa huduma ya kwanza katika maeneo ya kazi (*industrial first aid),* usalama katika kufanya kazi za juu *(safety in working at height),* na kozi ya namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa Kazi.

(b) Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA)

42. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i)Kusajili watafutakazi **1,533** na kutembelea waajiri **296**. Aidha, (TIA) na Taasisi ya Teknolojia (DIT) ambapo wahitimu watarajiwa **846** walipata mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na Soko la Ajira nchini; watafutakazi **647** waliunganishwa kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi;
(ii) Kusimamia na kuratibu ajira za watanzania **849** nje ya nchi ambapo watafutakazi **659** walipata ajira katika nchi ya Oman ; **175** Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE); **9** nchini India; **wawili** Saudi Arabia; **mmoja** nchini Brazil; **mmoja** nchini Denmark, **mmoja** nchini Ujerumani na **mmoja** nchini China;

(iii) Kutoa mafunzo kwa watafutakazi **581** ili kuwajengea uwezo wa nanma bora ya kuandaa wasifu binafsi, uandishi wa barua za maombi ya kazi na kuwapatia dondoo za usaili ili waweze kuhimili ushindani katika soko la ajira;

(iv) Kusajili nafasi **111** za kazi zenye fursa **371** kwa kutembelea waajiri **296** katika maeneo yao ya kazi;

(v) Kutembelea vyuo vya Elimu ya Juu **vinne** ambavyo ni Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Taasisi ya Uhasibu ;

(vi) Kutoa ushauri kwa watafutakazi **1,513** juu ya uchaguzi wa fani zinazohitajika kwenye Soko la Ajira na mafunzo ya kazi wanayostahili ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri au kuajirika; na

(vii) Kujenga uwezo wa watumishi **8** wa taasisi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika fani mbalimbali.

(c) Shirika la Tija la Taifa (NIP)

43. Mheshimiwa Spika; katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014, Shirika la Tija la Taifa (NIP) liliendelea kutoa mafunzo mbalimbali, kufanya tafiti pamoja na kutoa huduma ya ushauri ili kuinua tija sehemu za kazi nchini.

44. Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2013/2014, Shirika liliendesha mafunzo **63** ya tija na kujenga uwezo sawa na asilimia **95** ya lengo lililopangwa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa washiriki **630** sawa na asilimia **63** ya lengo. Aidha, tafiti **tatu** zilifanyika sawa na asilimia **100** ya lengo na kutoa huduma za ushauri katika kukuza tija kwa wateja **8** kutoka Taasisi za umma na binafsi sawa na asilimia **32** ya lengo.

(d) Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA)

45. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/14, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA)* imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) Imeshughulikia jumla ya malalamiko **492** yaliyopokelewa kutoka kwa Wanachama na wadau mbalimbali wa sekta ya Hifadhi ya Jamii;

(ii) Imeifanyia ukaguzi Mifuko **16** ya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Sheria zilizounda Mifuko hiyo na pia Sheria ya Mamlaka, Kanuni na Miongozo yake kama inafuatwa ipasavyo. Kati ya kaguzi hizo, kaguzi **nne** (4) zilifanyika eneo la kazi *(onsite inspection)* 12 zilifanyika kwa njia ya taarifa (offsite inspection);

(iii) Imetoa elimu kwa watu **7,200** kuhusu Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa makundi mbalimbali ambayo ni pamoja na Wabunge, Watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, Watendaji wa Vyama vya Wafanyakazi, Vyama vya Waajiri, Vyama visivyo vya Kiserikali (NGOs) na Makampuni binafsi. Aidha, elimu ya Hifadhi ya Jamii ilitolewa kupitia vyombo vya habari kama magazeti (makala **96**), runinga (vipindi **24**), redio (vipindi **12**), mikutano na waandishi wa habari mikutano **minne** na ushiriki katika maonesho **manne** (4).

(iv) Imetoa Miongozo **minne** inayohusu taratibu za Mikutano ya Kila Mwaka ya Wanachama wa Mifuko (*Conduct of Affairs of the Annual Members Conference Guidelines),* Utayarishaji wa taarifa za Mwaka za Mifuko *(Annual Reporting Guidelines),* Utangamano wa Mifumo ya Mawasiliano ya Mifuko *(Interoperability Guidelines)* na Ujumuishaji wa vipindi vya kuchangia *(Totalization of Periods of Contributions Guidelines)* na hivyo kutatua kero za wastaafu **11,000** waliokosa mafao;

(v) Imeandaa mahesabu ya mapato na matumizi ya Mamlaka na kupata hati safi ya ukaguzi wa mahesbu ya mwaka 2012/2013;

(vi) Imepata tuzo ya kwanza ya mahesabu bora inayotolewa na *NBAA* katika kundi la Mamlaka zinazotumia viwango vya mahesbu vya kimataifa vya *IPSAS;*

(vii) Imeshiriki katika kuhuisha Sheria ya Mfuko wa *GEPF,* toka mfuko wa Akiba na kuwa Mfuko wa Pensheni;

(viii) Imeanzisha mpango wa kufanya tathmini ya Mifuko yenye lengo la kutambua gharama na utenganishaji wa mifumo ya mafao *(actuarial valuation for separation of benefits accounts);*

(ix) Imesajili Mameneja Uwekezaji *(Fund Managers)* **wanane**, na Watunza mali *(Custodians)* **wanne**, zikiwa ni juhudi za kuboresha utendaji wa Mifuko kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mamlaka;

(x) Imeandaa na kuendelea kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano kwa Umma *(Communication Strategy)* na Mkakati wa kupanua wigo wa hifadhi ya jamii *(Extension of Social Security Coverage Strategy);*

(xi) Imeanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Mawasiliano kati ya Mamlaka, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, NIDA, na wadau wengine *(Core Business Application);* kwa lengo la kuboresha mawasiliano katika sekta ya Hifadhi ya Jamii.

(xii) Imeandaa rasimu ya Sera ya UKIMWI ya Mamlaka *(Institutional HIV/AIDS Strategy);*

(xiii) Imefanikisha wafanyakazi 24 wa Mamlaka kupata elimu na semina juu ya Ukimwi (HIV *AIDS)* na masuala ya rushwa *(Anti-corruption);* na

(xiv)Imeanzisha na kuzindua Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka.

(e) Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)

***46. Mheshimiwa Spika*;** katika mwaka wa fedha 2013/2014 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) limetekeleza kazi zifuatazo:-

(i)Limekusanya mapato ya kiasi cha shilingi milioni **705,692.7** sawa na asilimia **74.5** ya lengo na kutumika fedha hizo katika kulipa mafao ya Wanachama, kuwekeza katika vitega uchumi, kulipa gharama za uendeshaji na kuwekeza katika miradi ya maendeleo;

(ii)Limeendesha semina **1,931** kwa waajiri na wanachama nchi nzima ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa Hifadhi ya Jamii;

(iii) Shirika limeandikisha wanachama wapya **80,124** ambao ni asilimia **63.12** ya lengo lililokusudiwa. Aidha, Shirika limelipa mafao mbalimbali ya jumla ya shilingi milioni **235,559.2** ambazo ni asilimia **157.8** ya lengo kwa wanachama **73,742**;

(iv) Katika kuboresha Huduma kwa Wateja wake; Shirika limepata Cheti cha Kimataifa cha Utoaji Huduma Bora Kwa Wateja (***ISO 90001: 2008 Certificate***). Aidha Shirika limekamilisha Mpango wa Biashara Endelevu (*Business Continuity Management*) na pia limeweza kuunganisha Ofisi zake zote za mikoa na Wilaya katika Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa (*Fibre Cabe*), Shirika liko katika hatua za mwisho za maandalizi ya mpango wake wa kupima Afya za baadhi ya wanachama wake (*Preventive Health Checks*) na kufanya Mkutano Mkuu wa Nne wa wadau wa NSSF mwezi Mei/Juni 2014;

(v) Shirika limeshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii (*Corporate Social Responsibility*) katika maeneo yafuatayo: waliopatwa na maafa ya mafuriko Kilosa, Vikundi vya walemavu; Albino Muungano Investement Trust, Jumuiya ya Upendo Zanzibar na Temeke Albino Group. Huduma za Afya katika ujenzi wa hospitali au Maabara na hata kununua vifaa vya Huduma za afya; Uendelezaji wa Njombe Hospitali, kuboresha Muhimbili – "Paedetric emergency unit", Kijiji cha Kibamba, Mkuranga, Manispaa ya Temeke na Benjamin William Mkapa "HIV/*AIDS Foundation*". Huduma za Elimu katika ujenzi wa shule na Maabara, ununuzi wa madawati na vifaa vya shule, vikiwemo vitanda na magodoro; Shule ya Msingi Mbaya Liwale, Mnyakongo "Educational Development" Manispaa ya Mji wa Iringa – Ismani, Hassan Maajar trust, Kibada Shule ya Msingi, Shule ya Msingi Mhaji, Sumve Girls, Kijiji cha Ibuti Gairo, Ilala Sekondari, Msanga Sekondari, Wama, Nakayama Sekondari, Mwalimu Nyerere Resource Centre na Wilaya za Kahama na Maswa;

(vi) Shirika limeendelea na utaratibu wa kutoa mikopo katika Sekta isiyo rasmi (Informal Sector), kwa wanachama wake katika vikundi vya *SACCOS* na VICOBA ambapo shilingi bilioni **26.16** zimetolewa kwa wanachama **3,341** katika baadhi ya Wilaya zifuatazo: Temeke, Ilala, Kinondoni, Arumeru Mashariki, Singida Mjini, Kigoma, Masasi na Karagwe. Shirika linatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, mtumie fursa hii kuwafahamisha watu wajiunge na *NSSF* ili wapate mikopo.

(vii) Shirika linaendelea na Ujenzi wa Daraja la Kigamboni ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2015;

(viii)Shirika limeendelea na miradi ya ujenzi wa ofisi na vitega uchumi katika mikoa ya 31 Morogoro, Shinyanga, Kilimanjaro na Wilaya ya Ilala. Aidha, Shirika limeanza ujenzi wa Hoteli ya kisasa katika mkoa wa Mwanza na kuendelea na ujenzi wa jengo la Mzizima, Kijiji cha Kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu Farm) na nyumba mchanganyiko na ujenzi wa nyumba za bei nafuu Mtoni Kijichi awamu ya tatu; na

(ix) Katika miradi inayofanywa kwa ushirikiano na Wadau wengine (*Joint Venture Projects*); miradi ya ujenzi wa Hospitali ya "Clinic" ya Apollo jijini Dar es Salaam na ujenzi wa ofisi za *RITA (Registration, Insolvency and Trusteeship Agency)*. Ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma (MP's Village), mtaalamu/mwelekezi anakamilisha kuandaa michoro.

Aidha, Shirika linasubiri udhamini kutoka Serikali ili kuanza Miradi ya Jengo la Maadili. Na pia katika ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Serikali Nchi nzima, Kampuni ya Watumishi "*Housing Limited*" inasubiriwa kukamilisha taratibu, ili Shirika liweze kushiriki.

III. TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI (CMA)

47. Mheshimiwa spika, kama ambavyo nimeshaeleza katika aya zilizotangulia, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*Commission for Mediation and Arbitration)* ni taasisi ya Serikali yenye jukumu la kusuluhisha migogoro ya kikazi, kuamua migogoro ya kikazi na kuratibu shughuli za Kamati ya Huduma Muhimu (*Essential Services Committee)*. Vile vile Tume ina jukumu la kutoa elimu ya ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi.

48. Mheshimiwa spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (Fungu 15), iliidhinishiwa jumla ya shilingi **2,274, 978,000/-**. Kati ya fedha hizo Shilingi **924,978,000/-**ni kwa ajili ya mishahara (PE) na Shilingi **1,350,000,000/-** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(Other Charges)*.

49. Mheshimiwa spika, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2014, Tume imetumia jumla ya Shilingi **1,272,559,342/-**sawa na asilimia **55.9** ya Shilingi **2,274, 978,000/-** zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya kawaida.

Utekelezaji wa Majukumu na Kazi kwa Mwaka 2013/2014:-

50. Mheshimiwa spika, katika mwaka 2013/14, Tume iliendelea kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Taasisi za Kazi Na.7 ya mwaka 2004. Kazi zilizotekelezwa ni zifuatazo:-

(i) Kusajili Migogoro **8,584** ambapo migogoro **3,144** sawa na asilimia **37** ilisikilizwa na kupatiwa ufumbuzi. Migogoro **1,935** sawa na asilimia **23** ilimalizika kwa njia ya usuluhishi na migogoro **1,209** sawa na asilimia **14** ilimalizika kwa njia ya uamuzi. Migogoro **2,296** sawa na asilimia **27** inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali za usuluhishi na uamuzi;

(ii) Kuwezesha Kamati ya Huduma Muhimu kuainisha maeneo ambayo ni huduma muhimu na kuyasajili. Maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja na *TANESCO,* Maji, Afya na Hali ya Hewa;

(iii) Kushirikiana na Shirika la Kazi la Kimataifa (ILO) kutafsiri kitabu cha mwongozo wa kuzuia na kutatulia migogoro ya kikazi *(Dispute Prevention and Resolution Training Guide)* kutoka katika lugha ya kingereza kwenda lugha ya kiswahili;

(iv) Kuwezesha uundwaji wa mabaraza **51** ya Wafanyakazi katika Taasisi mbalimbali ambazo ni Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji **(13)**, na Taasisi za Umma **38** (Wizara, Idara za Serikali, Wakala na Mashirika).

(v)Kutoa mafunzo ya kuzuia na kutatua migogoro sehemu za kazi kwa Taasisi **35** ambazo ni Halmashauri **16** za Wilaya, Miji na ofisi za makatibu Tawala za Mikoa (RAS), Taasisi **18** za Serikali (Wizara, Idara, Wakala na Mashirika) na Sekta binafsi;

(vi) Imeajiri watumishi wapya **40** katika kada ya waamuzi, wasuluhishi na makatibu muhtasi; na

(vii) Imewezesha watumishi **7** kupata mafunzo katika fani ya uhasibu, utawala na ugavi.

C. MPANGO WA KAZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015I.

WIZARA YA KAZI NA AJIRA

51. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2014/2015 Wizara ya Kazi na Ajira kwa kushirikiana na Taasisi zilizopo chini yake, itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kusimamia Sheria na viwango vya kazi, ushirikishwaji wa Wafanyakazi na kusuluhisha migogoro sehemu za kazi; kusimamia usalama na afya mahali pa kazi, kukuza na kutoa huduma za ajira; kuboresha ufanisi na tija kazini na kuboresha sekta ya hifadhi ya jamii. Aidha, Wizara itatekeleza mpango wa matokeo makubwa sasa (BRN) unaolenga kuboresha mazingira ya Biashara nchini. Utekelezaji kwa mwaka 2014/ 2015 ni kama ifuatavyo:-

(a) Usimamizi Kazi na Huduma za Ukaguzi

(i)Kufanya ukaguzi sehemu za kazi **3,274** ukiwemo wa kawaida, maalum na ufuatiliaji katika maeneo mbalimbali nchini. Lengo ni kuhakikisha kuwa Sheria za kazi zinatekelezwa ipasavyo ili kupunguza migogoro na hatimaye kuongeza tija na uzalishaji. Ukaguzi huo utafanyika katika sekta mbali mbali, kipaumbele kikiwa katika sekta za madini, ulinzi binafsi, huduma za hoteli na majumbani, biashara, viwanda, uvuvi, afya, shule binafsi, mawasiliano na usafirishaji;

(ii)Kutoa elimu kuhusu Sheria za Kazi kwa waajiri **1,200** na wafanyakazi **4,000** katika sekta mbalimbali kwa madhumuni ya kuwajengea uelewa wa namna bora ya kutekeleza viwango vya kazi kwa mujibu wa Sheria;

(iii) Kuratibu na kukuza majadiliano ya utatu kupitia Baraza la Ushauri la Kazi, Uchumi, na Jamii *(LESCO)*. Katika kipindi hiki Baraza litafanya vikao vyake kwa mujibu wa Sheria ili kuweza kujadili na kutoa ushauri kwa Wizara na Serikali kwa ujumla kuhusiana na masuala ya utekelezaji wa Sheria za kazi, ukuzaji wa fursa za ajira na ukuzaji wa tija na uzalishaji. Wajumbe wa Baraza 37 watajengewa uwezo ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi;

(iv) Kuratibu na kuboresha upangaji wa kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi kupitia Bodi za Mishahara za Kisekta. Katika kipindi hiki, Bodi zitakazoundwa zitajengewa uwezo na kuwekewa mfumo mzuri wa kutekeleza majukumu yake;

(v) Kuendelea na jitihada za kupambana na ajira mbaya kwa watoto kwa kushirikiana na Wizara zenye dhamana ya watoto, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wabia wa Maendeleo na Mashirika yasiyo ya kiserikali. Katika kipindi hiki, Wizara inatarajia kuzuia watoto **4,000** kuingia kwenye ajira mbaya na kuwaondoa watoto **10,000** wanaotumikishwa kwenye ajira mbaya. Katika kufikia malengo hayo, Wizara itatekeleza yafuatayo: -

¾ Kujenga uwezo wa wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Kisekta ya Kuratibu Masuala ya Kupambana na Utumikishwaji wa Watoto nchini na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake;

¾ Kufanya ufuatiliaji na uratibu wa miradi ya kupambana na utumikishwaji wa watoto katika wilaya za Geita, Sikonge, Urambo, Kasulu, Lushoto na Pangani;

¾ Kuendelea Kujenga uwezo na kuhamasisha wadau katika ngazi ya Halmashauri za Wilaya ili kuwawezesha kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Utumikishwaji wa watoto, ‘

(vi) Kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (**Big Results Now**) wenye lengo la Kuboresha Uwekezaji na Mazingira ya Biashara nchini kwa kuhuisha Sheria za kazi, kuimarisha ukaguzi sehemu za kazi, uelimishaji kuhusu Sheria za kazi, kuboresha huduma za rasilimali watu na mazingira ya kufanyia kazi;

(vii) Kuendelea na hatua za kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kuimarisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii pamoja na kuboresha mafao ya pensheni kwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

(viii) Kuendelea kuimarisha huduma za hifadhi ya jamii nchini kwa kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi watakaoumia, kufa au kupata magonjwa yatokanayo na kazi. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kuandaa kanuni na miongozo kwa ajili ya kuendesha Mfuko na kujenga uwezo wa Mfuko kutekeleza majukumu yake; na

(ix)Kuimarisha utekelezaji wa Maazimio na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu viwango na masuala mbalimbali ya kazi na ajira kwa kushiriki kikamilifu katika majadiliano, kuridhia Mikataba na kuhuisha Sheria za nchi.

(b) Ukuzaji wa Ajira Nchini

52. Mheshimiwa Spika; Wizara yangu itaendelea kuratibu juhudi za Serikali za kukuza ajira nchini. Jumla ya ajira **700,000** zinategemewa kuzalishwa katika mwaka 2014/2015 kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo itakayotekelezwa na Taasisi za Umma, Programu ya kukuza Ajira kwa vijana pamoja na hatua mbalimbali za uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC),* Mamlaka ya Maeneo Huru ya Biashara *(EPZA)* na Sekta Binafsi.

53. Mheshimiwa Spika; Ili kukuza ajira na kazi za staha nchini, katika mwaka 2014/2015, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuratibu uingizaji wa masuala ya ukuzaji ajira katika mipango na programu za maendeleo za kisekta kwa kutoa mafunzo katika mikoa **3** pamoja na kufuatilia utekelezaji wa mwongozo wa namna ya kuhuisha ukuzaji ajira nchini;

(ii) Kusimamia utekelezaji wa Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana ambayo imelenga kuwajengea vijana uwezo wa stadi mbalimbali za kazi na ujasiriamali; kuwapatia vijana mitaji yenye masharti nafuu na nyenzo za uzalishaji; na kutenga maeneo maalum ya uzalishaji, na maeneo ya kufanya biashara. Awamu ya kwanza ya miaka mitatu ya utekelezaji wa Programu hiyo itaanza mwaka wa fedha 2014/ 2015 ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 3** zimetengwa.

(iii) Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na utoaji wa taarifa za soko la ajira nchini; ikiwa ni pamoja na kuratibu ukusanyaji wa taarifa za ajira zinazozalishwa na Wizara, Idara za Serikali, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Bajeti ya mwaka 2014/15;

(iv) Kuendelea kufanya Utafiti wa Hali ya Nguvukazi nchini ambao utatoa picha ya hali ya ajira nchini. Utafiti huu utatoa taarifa kuhusu ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi, hali ya utumikishwaji wa watoto, idadi ya ajira mpya zilizozalishwa kwa kipindi cha mwaka 2006 hadi 2014 na matumizi ya muda ya nguvu kazi inayotumika katika uzalishaji mali na utoaji wa huduma.

(v) Kuratibu na kuwezesha ushiriki wa wajasiriamali wadogo wa sekta isiyo rasmi **250** wa Tanzania katika Maonesho ya **15** ya Nguvukazi/Juakali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanayotarajiwa kufanyika mjini Kigali, Rwanda. Maonesho haya yamelenga kuwapatia wajasiriamali wadogo fursa za masoko, mbinu za kuboresha bidhaa zao, kukuza biashara na kurasimisha kazi na biashara zao hivyo kuongeza ajira kwa wananchi;

(c) Huduma za Ajira

Mheshimiwa Spika; Wizara katika kutoa huduma za Ajira ilitekeleza kazi zifuatazo:-i) Kukamilisha na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Ajira ya Wageni inayolenga kuimarisha na kuongeza ufanisi katika utoaji wa vibali vya ajira kwa wageni nchini. Aidha, Wizara itaandaa Mfumo wa Kielektroniki wa kutoa vibali vya ajira za wageni nchini kupitia mpango wa Matokeo Makubwa Sasa **(Big Results Now)** unaolenga kuboresha Uwekezaji na Mazingira ya Biashara nchini.

(ii) Kuandaa Kanuni na taratibu kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya ajira ya wageni; na

(iii) Kusimamia Kanuni za utoaji wa huduma za ajira zinazotolewa na Mawakala binafsi wa huduma za ajira kulinga na Sheria za nchi;

(d) Usajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri

54. Mheshimiwa Spika; Wizara itaendelea na jukumu la kusajili na kusimamia vyama vya waajiri na wafanyakazi nchini kama ifuatavyo:-

(i) Kushughulikia maombi ya usajili wa vyama vya Wafanyakazi na Waajiri.

(ii)Kufanyia ukaguzi kumbukumbu za wanachama, kuhakiki matumizi ya fedha za vyama na kufuatilia hesabu za mwaka za vyama ambazo zimekaguliwa.

(iii) Kuwaelimisha viongozi wa vyama vya wafanyakazi na waajiri juu ya Sheria za kazi na kanuni zake.

(iv) Kushughulikia migogoro inayojitokeza kati ya vyama vya waajiri na wafanyakazi .

(v) Kushughulikia kesi za mahakamani zinazotokana na maamuzi ya Msajili na masuala yanayohusu Katiba za vyama vya Wafanyakazi na Waajiri; na

(vi)Kusimamia utekelezaji wa Katiba za vyama kwa mujibu wa Sheria ya Mahusiano Kazini Na 6 ya mwaka 2004.

(e) Kujenga Uwezo wa Wizara

55. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara imepanga kujenga uwezo wa Wizara kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i)Kuwajengea uwezo watumishi **45** wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na wengine **kumi** kuwezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali;

(ii)Kuimarisha mahusiano kazini kwa kufanya vikao **viwili** vya Baraza la Wafanyakazi na kushiriki katika matamasha ya michezo;

(iii) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kununua nyenzo na vitendea kazi pamoja na kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma za ulinzi, usafi na matengenezo ya vifaa vya ofisi;

(iv)Kuendelea kutoka mafunzo ya Maadili kulingana na Sheria na Miongozo ya Utumishi wa Umma, Vita dhidi ya rushwa, Utawala bora sehemu ya kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI kwa watumishi **150** wa Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kuwahudumia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI;

(v)Kufanya vikao **vinne** vya Kamati ya Ajira ya Wizara (mara moja kila Robo Mwaka) kwa kuajiri, kuthibitisha kazini na kupandisha vyeo watumishi **39** wenye sifa za kimuundo na utendaji mzuri wa kazi.

(vi)Kuimarisha Ofisi za Kazi za Mikoa ili ziweze kusimamia viwango vya kazi kwa mujibu wa Sheria.

(vii) Kuboresha Mifumo ya TEHAMA, Mawasiliano pamoja na tovuti ya Wizara.

TAASISI ZA UMMA CHINI YA WIZARA

56. Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara ya Kazi na Ajira itaendelea kusimamia Taasisi za Umma zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:-

(a) Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)

(i)Kufanya ukaguzi sehemu za kazi **20,000** za kawaida na **16,000** maalum kuhusu Afya na Usalama Mahali pa Kazi na kupima afya za wafanyakazi **60,000** katika sehemu mbalimbali za kazi;

(ii)Kusajili sehemu **2,000** mpya za kazi ili ziweze kukidhi viwango na kanuni za Afya na Usalama Mahali pa Kazi pamoja na kutoa leseni ya kukidhi matakwa ya Sheria ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi *(The Occupational Health and Safety Act, 2003);*

(iii) Kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali yanayohusu Afya na Usalama Mahali pa Kazi ambapo mafunzo hayo yatajumuisha kozi ya Taifa ya usalama na afya (NOSHC), kozi ya utoaji wa huduma ya kwanza makazini *(industrial first aid)*, kozi ya usalama katika kufanya kazi za juu *(safety in working at height),* na kozi ya namna ya kuunda na kuendesha Kamati za Afya na Usalama Mahali pa kazi. Wafanyakazi zaidi ya **1,000** wanatarajiwa kupata mafunzo haya;

(iv)Kuanzisha mifumo mbalimbali ya kuboresha utendaji kazi, mfumo wa kutoa taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi, mfumo wa kutunza kumbukumbu, mfumo wa usimamizi wa fedha na mfumo wa usimamizi wa vifaa *(Asset tracking system);*

(v) Kuendelea kuelimisha wafanyabiashara wadogo na wa kati ili waweze kuboresha mazingira ya kazi kwa kuendesha warsha, semina na makongamano mbalimbali katika mikoa ya Tanzania Bara;

(vi)Kukamilisha uandaaji wa rasimu za kanuni tatu ambapo kanuni mbili ni kuhusu gesi (*"Gas safety installations and use rules"),* na (*"Vessel under pressure regulations)* na kanuni moja kuhusu utoaji taarifa za magonjwa na ajali zitokanazo na kazi (*"Recording and reporting of occupational diseases, injuries and dangerous occurrences rules);*

(vii) Kuendelea kufuatilia hatua za Serikali na Bunge za kuridhia mikataba 6 ya Kimataifa (ILO Conventions) inayohusiana na Usalama na afya mahali pa kazi. Kwa kufuatilia mapendekezo ya kuridhia Mkataba Na. I55 *(Occupational Safety and Health Convention, 1981),* Mkataba Na.187, *(Promotional Framework for Occupational Safety and Health Convention, 2006)* Mkataba Na.167 *(Occupational Safety in Construction Convention, 1988), Mkataba Na.161 (Occupational Health Services Convention,* 1985), Mkataba Na.176 *(Safety and Health in Mines Convention,* 1995) and Mkataba Na.184 *(Safety and Health in Agriculture Convention, 2001)*.

(b) Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA)

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania *(TaESA)* umepanga kufanya yafuatayo:-

(i)Kusajili watafutakazi **2,000** na kuunganisha watafutakazi **1,000** kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi.

(ii)Kutembelea waajiri **1,000** kwa lengo la kubaini idadi na aina ya fursa za ajira.

(iii)Kusimamia na kuratibu ajira za Watanzania **1,000** nje ya nchi.

(iv) Kuendelea kukusanya, kuchambua na kusambaza Taarifa za Soko la Ajira wa watafuta kazi na waajiri.

(v)Kuandaa vipindi **12** vya redio na runinga kwa lengo la kutoa elimu kwa watafutakazi na umma kwa ujumla.

(vi)Kuandaa makongamano **mawili** ya ajira kwa lengo la kukutanisha waajiri na watafutakazi.

(vii) Kutembelea taasisi za elimu ya juu 20 kwa lengo la kutoa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na soko la ajira kwa wahitimu watarajiwa.

(viii) Kuendeleza rasilimali watu wa Taasisi (TaESA) ili kuongeza tija na ufanisi.

(ix)Kutoa ushauri wa kitaalam *(consultancy services)* kwa wadau juu ya masuala ya huduma za ajira nchini.

(c) Shirika la Tija la Taifa (NIP)

58. Mheshimiwa Spika; katika mwaka wa fedha 2014/15 Shirika la Tija la Taifa limepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i)Kuendesha mafunzo **80** ya uongozi yatakayohudhuriwa na watumishi **1,200** kutoka taasisi za umma, binafsi na taasisi zisizokuwa za Kiserikali *(NGO's);*

(ii)Shirika litatoa huduma za ushauri elekezi kwa wateja **30** katika Sekta za Umma, binafsi na zisizokuwa za Kiserikali *(NGO's)*; na

(iii) Shirika litafanya tafiti **nne** katika maeneo mbalimbali yanayolenga kuboresha tija viwandani.

(d) Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii (SSRA)

59. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii **(SSRA)** itaendelea na hatua za kuboresha sekta ya Hifadhi ya jamii kwa kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kushirikiana na Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuandaa mapendekezo ya kuanzisha pensheni ya Wazee;

(ii)Kuendelea kutekeleza Mkakati wa elimu kwa umma kwa lengo la uongeza uelewa wa masuala ya hifadhi ya jamii. Elimu hiyo itafanyika zaidi kikanda, ambapo zaidi ya wanachama na **15,000** wataelimishwa, vyuo **55** vya maendeleo ya jamii vitafikiwa, na wanafunzi **100,000** wa vyuo vikuu wataelimishwa. Aidha, Mamlaka itaendelea kutumia runinga, redio na magazeti kuwafikia wanachi wengi zaidi nchi nzima;

(iii) Kuendelea na zoezi la ukaguzi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuhakikisha kuwa Mifuko hiyo inaendesha shughuli zake kwa mujibu wa Sheria na kwa manufaa ya wanachama wake ambao ndio msingi wa kuanzishwa kwa mifuko hiyo. Ukaguzi utafanyika katika maeneo 30 ya kazi, maeneo **6** yakiwa ni Eneo la Kazi *(onsite supervision)* na maeneo **24** yakiwa si Eneo la Kazi *(offsite surveillance);*

(iv) Kufanya tafiti **tatu (3)** zenye lengo la kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini.

(v)Kuendelea kukamilisha hatua mbalimbali za kuwianisha mafao ya hifadhi ya jamii *(benefits harmonization);*

(vi) Kuendelea na kazi ya usajili wa Mifuko ya hiyari *(Supplementary Schemes),* Mameneja Wawekezaji *(Fund Managers)* na Watunza Mali *(Custodians)* na kutoa miongozo na kanuni za utendaji wao wa kila siku;

(vii) Kuandaa mikakati ya kuhamasisha Mifuko iendelee kufanya maboresho ya huduma *(products and service re-designing)* zote zinazotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hapa nchini;

(viii)Kuendelea na uandaaji na uhuishaji wa kanuni na miongozo mbalimbali kama ya uhamishaji mafao *(transfer of benefits),* utendaji wa kila siku wa watoa huduma *(Service Providers)* zikiwa ni juhudi za Serikali kuhakikisha utoaji mafao bora na kwa wakati;

(ix) Kuandaa Mfumo dhabiti wa kusimamia na kukagua Mifuko na watoa huduma *(Risk Based Supervisory Framework);*

(x) Kuandaa na kuratibu maoni ya wadau kuhusu mapendekezo mbalimbali ya mabadiliko ya Sheria ya Mamlaka na Sheria za Mifuko ili kuongeza ufanisi kwenye Sekta;

(xi) Kuandaa na kupitia upya kanuni na miongozo mbalimbali ili kuwajengea mazingira bora watumishi na uwajibikaji; na

xii) Kukamilisha uwekaji wa mfumo wa mawasiliano wa kielektroniki baina ya Mamlaka na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii *(Core Business Application)* na kufundisha Mifuko kurekebisha na kutunza takwimu za Wanachama.

(I) Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)

60. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2014/15 Shirika la Taifa la Hifadhi ya jamii litatekeleza kazi zifuatazo:-

(i)Kukusanya jumla ya Shilingi milioni **1,437,629.1** na kutumia kiasi hicho cha fedha kulipia mafao ya wanachama, kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali, kulipa gharama za uendeshaji na kuwekeza katika miradi ya maendeleo;

(ii) Kuimarisha uandikishaji na ukusanyaji michango ya Wanachama katika sekta iliyo rasmi na isiyo rasmi *("informal sector"),* kuendelea na ukusanyaji wa madeni kwa waajiri na pango kwa wapangaji wa majengo ya *NSSF;*

(iii) Kuendelea kutoa elimu kwa wanachama, waajiri na umma kwa ujumla ili waweze kuelewa vizuri mfumo mpya wa hifadhi ya jamii chini ya *NSSF;*

iv) Litaendelea na utoaji wa mikopo kwa *SACCOS* na VIKOBA kwa wanachama wa *NSSF*;

(v) Shirika litaendelea na mpango wa kupima afya za wanachama wake *(Preventive Health checks);*

(vi) Kufanya mkutano mkuu wa tano wa wadau wa *NSSF*;

(vii) Kukamilisha tathimini ya uwezo wa mfuko kifedha ili kulipa mafao kwa wanachama wake kwa muda mrefu ujao;

(viii)Kuendelea na mradi wa uzalishaji umeme wa megawati **300** katika eneo la Mkuranga;

(ix) Kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigamboni;

(x) Kukamilisha ujenzi wa vitega uchumi katika mikoa ya Shinyanga, Morogoro, Kilimanjaro, *NSSF/RITA* na Wilaya ya Ilala na mradi wa nyumba za bei nafuu 400 Mtoni Kijichi awamu ya Tatu.

Pia kuendelea na ujenzi wa Kijiji cha Kisasa Kigamboni (Tuangoma na Dungu *"Farm"-"Satellite cities")* na ujenzi wa jengo la Mzizima Towers jijini Dar es Salaam;

(xi) Kuanza ujenzi wa jengo kwa ajili ya ofisi ya Makao Makuu katika Mkoa wa Dar Es Salaam, ofisi katika Wilaya za Kinondoni, Temeke, Tarime na Kasulu, na kuendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi na vitega uchumi katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, wilaya za Temeke na Kinondoni. Aidha, kuanza kukarabati majengo ya kutunzia kumbukumbu katika Mkoa wa Dar es Salaam; na

(xii) Kushiriki katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya *Appolo,* ujenzi wa Vijiji vya kisasa Kigamboni ("Azimio Satellite town" na Geza Satelite Town), ujenzi wa Kijiji cha Bunge Dodoma *(MP's Village)* , Ofisi za Bunge Dar es Salaam, Tanga "*Commercial Complex*", kituo cha usafirishaji Kigoma, Ujenzi wa Majengo ya *NSSF*/Maadili, *NSSF/TBC* na *NSSF/NIP*.

III. TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI (CMA)

61. Mheshimiwa spika, naomba sasa nitoe maelezo kuhusu mpango wa kazi za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15, Tume imeweka kipaumbele katika kutekeleza yafuatayo:-

(i)Kusuluhisha na kuamua migogoro **6,500** ya kikazi na kuandaa taarifa;

(ii)Kufanya tafiti juu ya migogoro ambayo haijasajiwa katika Tume na kuishughulikia;

(iii)Kuendesha mafunzo **200** ya uelewa na ushauri wa kisheria kwa waajiri na wafanyakazi juu ya kuzuia na kutatua migogoro sehemu za kazi;

(iv)Kuandaa na kusimamia vikao vya Makamishna wa Tume na vikao vya kamati ya huduma muhimu *(Essential Services Committee);*

(v)Kuandaa na kusambaza juzuu ya tatu ya kitabu cha rejea cha maamuzi mbalimbali ya Tume (*Case Management Guide Vol 3.)* yaliyorejewa na Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi kwa matumizi ya wadau wa Tume;

(vi) Kuwezesha uanzishwaji wa vyombo vya ushirikishwaji wa wafanyakazi mahala pa kazi;

(vii) Kupokea na kusajili mikataba ya kuunda mabaraza ya wafanyakazi sehemu za kazi;

(viii) Kufanya tathmini ya hali ya ushirikishwaji Tanzania Bara;

(ix) Kujenga uwezo wa Tume kwa kuwaendeleza watumishi kitaaluma; na

(x) Kuendeleza mafunzo ya maadili, vita dhidi ya rushwa na utawala bora sehemu za kazi na mapambano dhidi ya ugonjwa wa UKIMWI.

D. SHUKRANI

62. Mheshimiwa spika, mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2013/2014 yametokana na ushirikiano wa hali ya juu wa viongozi na wafanyakazi wote wa Wizara yangu. Napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru Viongozi wote wa Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na Mashirika na Taasisi zake, kwa juhudi zao kubwa walizoonyesha katika kutekeleza majukumu tuliyopewa na Taifa.

Shukrani zangu za kipekee nazielekeza kwa **Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga (Mb),** Naibu Waziri wa Kazi na Ajira na Mbunge wa Jimbo la Segerea kwa ushirikiano na ushauri wake wa karibu. Aidha, napenda pia nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu **Bwana Eric F. Shitindi** pia ninawashukuru sana Wakuu wa Idara, Vitengo na Watumishi wote wa Wizara yangu, Watendaji Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara pamoja na Bodi zao kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu yangu pamoja na michango yao iliyowezesha kuandaa hotuba hii.

63. Mheshimiwa Spika; kwa njia ya pekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Baraza la Kazi, Uchumi na Jamii – ***(LESCO)***, Chama cha Waajiri Tanzania **(*ATE*)** na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania **(*TUCTA*)**, kwa michango na ushauri wao mzuri walionipatia katika kutekeleza majukumu na malengo ya Wizara yangu. Nazishukuru pia Wizara na Taasisi, Mashirika na Idara mbalimbali za Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo tumeshirikiana nazo na sekta binafsi.

64. Mheshimiwa Spika; Wizara yangu inatambua na itaendelea kuthamini michango mbalimbali ya Washirika wa Maendeleo ambayo inasaidia kwa kiwango kikubwa kutekeleza majukumu ya Wizara. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru kwa dhati nchi na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia katika utekelezaji na mafanikio ya Wizara yetu. Shukrani za dhati ziende kwa Shirika la Kazi Duniani **(ILO)**, **UNDP**, **UNICEF**, **UNFPA**, Shirika la Misaada la Kimataifa la Denmark **(DANIDA)**, Idara ya Kazi ya Marekani, Serikali ya Brazil na Benki ya Dunia.

65. Mheshimiwa Spika; nakushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge letu kwa kuendesha shughuli za Bunge kwa viwango stahiki. Natoa pia shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa michango yao ndani ya Bunge na nje ya Bunge inayolenga kuboresha utendaji kazi katika Wizara yangu.

66. ***Mheshimiwa Spika***; kwa namna ya pekee naomba niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Said Mtanda, Mbunge wa Jimbo la Mchinga na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Kapteni John Damiano Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi kwa kuendelea kuisimamia vyema Wizara yangu. Wizara itaendelea kutekeleza ushauri na maelekezo ya Kamati kwani yanalenga kuboresha utendaji kazi wa Wizara.

67. Mheshimiwa Spika; naomba pia nichukue fursa hii kuwashukuru sana wananchi wote wa mkoa wangu wa Mara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Aidha, kwa namna ya pekee naishukuru familia yangu kwa mchango mkubwa wanaonipatia.

E. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015

***68. Mheshimiwa Spika*;** naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **18,280,136,000** kwa Wizara (**Fungu 65**) na jumla ya Shilingi **4,683,837,000** kwa Tume **(Fungu 15)** kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ili kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii katika mchanganuo ufuatao:-

(a) Fungu 65: Wizara ya Kazi na Ajira

(i) Shilingi 2,815,205,000 zitatumika kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara;

(ii) Shilingi 12,464,931,000 zitatumika kugharamia Matumizi Mengine; na

(iii) Shilingi 3,000,000,000 ni fedha za maendeleo za ndani kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana.

(b) Fungu 15: Tume ya Usuluhishi naUamuzi

(i) **Shilingi 1,833,837,000** zitatumika kulipa mishahara ya watumishi wa Tume; na

(ii) **Shilingi 2,850,000,000** zitatumika kugharamia Matumizi Mengine.

69. Mheshimiwa Spika; naomba tena nitoe shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Wizara kwa anwani: **www.kazi.go.tz** .

70. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MHE. SAID MOHAMED MTANDA – MWENYEKITI WA KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na ajira kwa Mwaka 2013/2014 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) za Kanuni za Bunge Toleo la Aprili 2013, na kushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikutana na Wizara ya Kazi na Ajira Jijini Dar es Salaam tarehe 3 Mei, 2014. Kamati ilipokea na kujadili kwa kina utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ha uchambuzi Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa mafungu mawili yaliyo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira ambayo ni Fungu 65 Wizara ya Kazi na Ajira na Fungu 15 Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ilitoa maoni mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Kazi na ajira. Napenda kuliharifu Bunge lako Tukufu kuwa Maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa kwa kiasi kikubwa, lakini kumekuwa na upungufu katika baadhi ya maeneo kama vile suala la uanzishwaji wa mfuko wa *pension* kwa wazee, jambo ambalo limekuwa ni kilio kikubwa kwa wazee katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii utaona kwamba, kwa zaidi ya miaka minne mfululizo Kamati imekuwa ikiitaka Serikali kutenga Bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wizara hii. Bajeti ambayo inatengwa kwa Wizara bado ni ndogo ikilinganishwa na majukumu yanayopaswa kutekelezwa. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara Fungu 65 ilikasimiwa jumla ya Shilingi bilioni 13 kwa Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizi Shilingi bilioni nne, sawa na asilimia 37 zilitengwa kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi na Shilingi bilioni nane sawa na asilimia 63 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, yaani OC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Aprili, 2014, Wizara imepokea jumla ya Shilingi bilioni nne, sawa na asilimia 91 ikiwa ni fedha za mishahara ya watumishi, na Shilingi bilioni mbili, sawa na asilimia 33 ya fedha za matumizi mengineyo ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasisitiza Serikali kuipa Wizara fedha zilizobaki kwa wakati ili iweze kukamilisha malengo na shughuli ilizojipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30 – 2014. Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo mbalimbali hasa kwenye maeneo yanayohusu:-

(i) Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee;

(ii) Migogoro ya Wafanyakazi;

(iii) Mfuko wa fidia kwa wafanyakazi;

(iv) Ukuaji wa Ajira Nchini; na

(v) Uanzishwaji wa Idara au Kurugenzi ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi. Maeneo hayo ni pamoja na Muswada wa Sheria wa Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee.

Kamati iliagiza Wizara kuja na mpango Mkakakati na hatimaye Muswada wa kuanzisha Mfuko wa Pensheni kwa Wazee. Utekelezaji wa suala ili unaenda polepole sana, kwani hadi sasa hakuna Muswada wowote kuhusu suala la uanzishwaji kwa Mfuko huu iliyoandaliwa, ingawa Wizara ilieleza Kamati kuwa imekamilisha Rasimu ya Mpango wa Pensheni kwa Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hakukuwa na Idara au Kurugenzi inayosimamia Hifadhi ya Jamii Wizarani, Kamati iliishauri Serikali kukamilisha uanzishwaji wa Idara au Kurugenzi ya Hifadhi ya Jamii, jambo ambalo halijatekelezwa mpaka hivi sasa. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza ushauri huo ili masuala ya Hifadhi ya Jamii yaweze kuratibiwa vizuri pale Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imetengewa jumla ya Shilingi bilioni 18. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 15 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na Mishahara na Shilingi bilioni tatu, ni kwa ajili

ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Wizara inategemea kupokea kiasi cha fedha zote hizo ikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwia Mwenyekiti, maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015, ni pamoja na:-

(i) Kutoa mafunzo na mitaji kwa vijana Wajasiliamali nchini;
(ii) Kufanya Kaguzi za mara kwa mara katika sehemu za kazi ili kubaini upungufu na kasoro za ukiukwaji wa sheria za kazi; na

(iii) Kutoa elimu kuhusiana na sheria, kanuni na taratibu za afya na usalama mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasikitishwa na Bajeti ndogo iliyotengwa kwa Wizara hii bila kujali umuhimu wa Wizara katika kukuza ajira na hasa kwa vijana, ikizingatia hatari inayoweza kuligharimu Taifa kwa kuwa na vijana wengi wasio na ajiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bunge kuidhinisha fedha kwa Wizara hii, bado fedha hizi hazitolewi kwa wakati na sehemu kubwa ya fedha hizi hazipokelewi kabisa. Aidha, Bajeti hii ndogo itathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza vipaumbele vyake ilivyojipangia katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitia taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 na maombi ya fedha yanayojumuisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee ni kundi muhimu sana katika jamii. Siyo hapa Tanzania, bali sehemu nyingine yoyote duniani.

Wazee wamekuwa nguzo muhimu katika kuhimiza maadili mema, malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya kitaifa hasa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kiutamaduni. Takwimu zinaonyesha kuwa, kati ya watu zaidi ya milioni 45, idadi ya wazee ni milioni 5.056. Hii ni kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ilishauri Seriklali kuanzisha Mfuko wa Pensheni kwa Wazee.

Aidha, katika kikao cha Kamati, Serikali ilitoa maelezo kuwa ilikamilisha Rasimu ya Mpango wa Pensheni kwa Wazee mwezi Septemba, 2013, ikiwa ni pamoja na kukusanya taarifa ya uzoefu kutoka nchi nyingine. Hatua inaofuata ni kuandaa mapendekezo ya Mfumo wa Pensheni ya Wazee kwa kuzingatia uzoefu na mafunzo kutoka nchi zilizotembelewa na kuleta Bungeni Muswada ili Sheria ya Pensheni kwa Wazee iweze kutungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mitazamo mingi tofauti, ikiwa ni pamoja na mtazamo kuwa Wazee ambao hawakuchangia kuweka akiba katika Mfumo Rasmi hawawezi kulipwa.

Mfumo wa Pensheni tulionao sasa hauwahusishi wazee wote. Wazee wanaohusishwa na Pensheni ni wale waliokuwa katika mfumo rasmi wa ajira kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Idadi kubwa ya Wazee ambao katika uhai wao hawakuwahi kuwa na ajira rasmi, hawafaidiki na Pensheni ya Uzeeni. Hivyo kuanzishwa kwa Mfuko huu kutasaidia kundi kubwa la Wazee kupata Pensheni ambayo kwa kiasi kikubwa itasaidia kukidhi mahitaji yao na kuwafanya Wazee pia kuchangia katika ukuajia wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na ukweli huu, Kamati inaitaka Serikali ikamilishe Mchakato wa Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni ya Wazee ili Wazee nao waweze kuboreshewa hali zao za kimaisha, kwani ngoja ngoja huumiza matumbo. Wazee wamechoka kusubiri katika jambo hili, tulitekeleze sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, elimu na mafunzo ya biashara na ujasiliamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuanzisha elimu ya mafunzo ya biashara kwani utekelezaji wake utakuza ajira. Kamati inaona kuwa utekelezaji wa *program* ya kukuza ajira kwa vijana kwa kiasi kikubwa itachangia kupunguza umasikini nchini kama ilivyoainishwa katika *program* ya MKUKUTA II na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kwamba mafunzo haya yawafikie Walengwa kwa kuanzia na kada ya elimu ya chini, mpaka elimu ya juu, kwa kuwanufaisha vijana wote. Fursa hizi za ajira zielekezwe pia kwa vijana wa vijijini ambao wanapenda kujiajiri katika kilimo. Kilimo kwanza iwe kwa vitendo na siyo maneno maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Miradi ya Maendeleo. Katika kutekeleza *program* mbalimbali za maendeleo Wizara imetengewa Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuanza utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inawapatia vijana hawa elimu itakayowawezesha kupata ujuzi na taaluma mbalimbali zitakazowasaidia kuwa wabunifu katika ulimwengu wa sasa ambao unahitaji watu wenye ujuzi na utayari wa kujiajiri na kuondokana na dhana ya kuajiriwa kama Ilani ya CCM inavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuangalia mfumo mzima wa elimu kwa kufanya utafiti wa kina wa mitaala iliyopo ili kuona ni mitaala gani itakayowezesha vijana kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni Ajira kwa Vijana. Tatizo la ajira kwa vijana limekuwa ni sugu hasa kwa vijana kutokana na fursa za ajira kutokuwepo.

Katika kikao cha Kamati na Serikali, Serikali ilieleza Kamati kuwa wameandaa programu ya kukuza ajira kwa vijana itakayotekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu na kuibua fursa za ajira 840,000.

Mheshimiwa Mwenyejiti, kulingana na takwimu na matokeo ya utafiti ya nguvu kazi na ajira ya mwaka 2005/2006, kama ilivyonukuliwa katika hotuba ya Waziri Mkuu iliyotolewa katika Kongamano la Vijana la Vyuo vya Elimu ya Juu, Kanda ya Ziwa, takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya vijana wanaomaliza Vyuo vikuu nchini kila mwaka kuwa ni wastani wa vijana 800,000 mpaka milioni moja. Kati ya hao, wanaopata ajira ni wastani wa vijana 80,000 hadi 100,000 katika Sekta za Umma na Sekta Binafsi. Hivyo kwa takwimu hizi, tatizo la ajira kwa vijana bado ni kubwa sana nchini.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia inakisiwa kwamba takriban ijana 850,000 wenye umri kati ya miaka 15 na 25 huingia kwenye Soko la Ajira kila mwaka nchini Tanzania, huku asilimia 40 ya vijana hawa ikiwa ni wale waliofeli Kidato cha Nne.

Benki ya Dunia inazidi kukadiria kwamba ifikapo mwaka 2015, kutakuwa na ongezeko la vijana milioni 1.3, katika Soko la Ajira. Kazi kwetu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatari sana kwa nchi yoyote duniani kuwa na vijana wengi wazururaji, wasio na ajira, kwani huweza kujihusisha na vitendo vya uhalifu na vinginevyo.

Kwa kuzingatia hili, Kamati inaitaka Serikali kukuza ajira katika Sekta ya Umma na Binafsi na kuboresha Sera kuhusu Vijana na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba mafunzo kwa vijana yatakayotolewa kupitia fedha za maendeleo zilizotengwa

katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, yawe ya gharama nafuu na ya muda mfupi ili fedha nyingi zitumike kwa ajlili ya vijana na mitaji badala ya kutumika katika shughuli za uendeshaji wa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyeki, nne, kuhusu Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jami *(SSRA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Uzimamizi na Udhibiti wa Hifadhi ya Jamii *(SSRA),* hii ni Tasisi, inayosimamia na Kudhibiti masuala ya Hifadhi ya Jamii na kuishauri Serikali ipasavyo juu ya uimaishaji na uboreshaji wa sekta hii.

Kamati inaitaka Mamlaka ya Hifadhi ya Mifumo ya Jamii iendelee na kazi nzuri ya kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuwafanya wananchi wengi kuwa Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kupitia *Supplementary Schemes* mbalimbali za Mifuko hiyo zilizoanzishwa badala ya asilimia sita tu, iliyopo sasa ili kupanua wigo wa Mifuko hiyo na pia kuongeza wanachama hasa katika sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuhusu Migogoro katika maeneo mbalimbali, hasa migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na migogoro ya muda mrefu katika Sekta ya Madini nchini. Miongoni mwa migogoro hiyo ni pamoja na mgogoro kati ya wafanyakazi 79 na uongozi wa Mgodi wa *African Barrick* Bulyankulu. Kamati iliwahi kupata fursa ya kukutana na Wawakilishi wa Wafanyakazi wa Mgodi wa *African Barrick* Bulyankulu, kuhusu kuachishwa kazi bila kupimwa afya zao kama sheria inavyoelekeza.

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Migodini, yaani *(TAMICO)* Ndugu Hassan Ameir ya kufuatilia migogoro baina ya Wafanyakazi na waajiri wao ili kuipatia ufumbuzi, bado Kamati inaisisitiza Serikali kuingilia kati suala hili ili wafanyakazi waweze kupatiwa haki zao, ikiwa ni pamoja na kupimwa haki zao pale wanapoachishwa kazi, kama ilivyobainishwa na sheria na kulipwa haki zao endapo watashindwa kuendelea na kazi. Uzalendo mbele.

Mheshimiwia Mwenyekiti, sita ni kuhusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*. Kamati inaipongeza *NSSF* kwa kuendeleza uwekezaji katika vitega uchumi ambavyo mbali na kulenga kuongeza kipato cha Mfuko, pia vinatoa huduma za msingi kwa jamii hasa kwa Mradi wa Daraja la Kigamboni ambalo litapunguza adha ya usafiri kwa wakazi wa maeneo hayo.

Ujenzi wa nyumba za gharama nafuu; ujenzi wa Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Arusha, na Chuo Kikuu cha Dodoma yaani *UDOM*, na Miradi mingine mingi ni ushahidi mzuri wa namna *NSSF*, inavyojitahidi kuboresha huduma za

kijamii katika sehemu mbalimbali nchini. Dkt. Ramadhani Dau na wenzio endeleeni na kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, Kamati inaushauri Mfuko huu kuangalia namna ya kuwekeza Vitega Uchumi katika maeneo mbalimbali nchini ambayo yako nyuma kimaendeleo ili kuchochea ukuaji wa Uchumi.

Aidha, Mfuko uangalie namna ya kuboresha zaidi mafao ya wanachama wake kwa kutumia faida ambayo inatokana na Vitega Uchumi, vilivyowekezwa na Mfuko huu, kwani fedha zinazotumika kama mtaji zinatokana na michango ya wanachama. Mafao bora na yanayotolewa kwa wakati ndiyo viwe msingi mkubwa wa faida inaotokana na uwekezaji huo kwa wanachama. Wanachama kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imearifiwa kuwa *NSSF* iko katika majadiliano na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kuingia Mkataba wa Ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo ya Uchaguzi nchini.

Jambo hili ni jema na Kamati inaishauri Serikali na Bunge kukamilisha mazungumzo hayo haraka ili Waheshimiwa Wabunge wapate Ofisi bora kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao ya kibunge na ikiwezekana tuanze na Jimbo la Mchinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Saba, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)*. Pamoja na mambo mengine, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (*CMA),* imekuwa ikisimamia utekelezaji wa Sheria Namba 6, ya ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004.

Aidha, Tume imekuwa ikiratibu migogoro yote ya kikazi inayowasilishwa kwake ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa Wafanyakazi, Sehemu za Kazi. Ni wazi kuwa Bajeti ndogo hii ambayo Wizara imetengewa bado itaendelea kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekii, ni ushauri wa Kamati yangu kuwa Serikali iwapatie *CMA* vitendea kazi ikiwemo Rasilimali Watu wa kutosha ambao, wataweza kufanya kazi ya usuluhishi na uamuzi katika mashauri mbalimbali yanayofikishwa na kuwasilishwa katika Tume hii kwa wakati ili watu waweze kupatiwa haki zao mapema. Kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshiiwa Mwenyekiti, Nane, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA):*

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)* imepanga kutekeleza kazi kadhaa ikiwamo kufanya Ukaguzi

maalum na wa kawaida kuhusu afya na usalama mahali pa kazi. Kamati inashauri kaguzi hizi kufanyika kila mara kubaini upungufu uliopo katika sehemu hizo ili kulishughulikia ipasavyo tatizo hili na kwa namna hiyo, kuwa sehemu ya motisha kwa watumishi kwa kujali afya zao na usalama katika sehemu ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa ni jukumu la Waajiri na Waajiriwa kuhakikisha afya na usalama wao mahali pa kazi, bado Serikali ina wajibu wa kuhakikisha inaweka viwango vya usalama na kusimamia kikamilifu utekelezaji wake ili kunusuru afya za Wafanyakazi na hivyo kulinda ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Kamati inasisitiza Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusiana na Sheria, Kanuni na Taratibu za Afya na Usalama mahali pa kazi,na kusimamia utekelezaji wake. Kwa ujumla *OSHA*, imekuwa ikifanya kazi zake kwa uweledi mkubwa chini ya usimamizi wake Dkt. Akwilina Kayumba. Hongera sana, Dkt. Kayumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushuuru wewe kwa ushauri wako katika kutekeleza majukumu yangu.

Niwapongeze pia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wengine wa Bunge kwa namna ambavyo wananisaidia katika kusimamia na kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Waziri wa Kazi na Ajira, Mheshimiwa Gaudentia Mgosi Kabaka; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga; Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Erick Shitindi na Watumishi na Wakuu wa Idara wote na Taasisi zote zilipo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa wanayoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa namna yha pekee kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti, lakini pia kunisaidia katika kuhakikisha kwamba taarifa hii inakuwa yenye maboresho makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Kashilllilah; Mkurugenzi wa Idara za Kamati ya Bunge, Ndugu Charles Mloka, na Makatibu wa Kamati hii, Ndugu Hanifa Masaninga, Ndugu Aziza Makwaia na Ndugu Abdallah Hancha kwa ushauri na uratibu wa Kazi za Kamati. Naomba Taarifa yote iliyomo katika kitabu hicho iingie kwenye *Hansard*.

Mwisho, nimalizie kwa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mchinga kwa kuendelea kuniunga mkono, ninawaahidi nitaendelea kushirikiana nao katika kazi zangu za kiuongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono hoja hii. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Taarifa ya Kamati ya Maendeleo ya Jamii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka 2014/2015 Kama Ilivyowasilishwa Mezani

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KAZI NA AJIRA KWA MWAKA 2013/2014 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2014/2015

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) na Kanuni ya 117(11) za Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niwasilishe Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ilikutana na Wizara ya Kazi na Ajira Jijini Dar es Salaam tarehe 3 Mei, 2014. Katika kikao hicho, Kamati ilipokea na kujadili kwa kina utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, pamoja na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa mafungu mawili yaliyo chini ya Wizara ya Kazi na Ajira ambayo ni **Fungu 65 – Wizara ya Kazi na Ajira** na **Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi.**

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Kamati ilitoa maoni na mapendekezo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Kazi na Ajira. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa kwa kiasi kikubwa lakini kumekuwa na upungufu katika baadhi ya maeneo kama vile suala la uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee ambao umekuwa kilio kikubwa kwa wazee nchini.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa za Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii utaona kwamba kwa zaidi ya miaka minne mfufulizo Kamati imekuwa ikiitaka Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya Wizara hii. Bajeti inayotengwa kwa Wizara bado ni ndogo ikilinagnishwa na majukumu yanayopaswa kutekelezwa. Mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara (Fungu 65) ilikasimiwa jumla ya shilingi **13,034,148,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi **4,769,301,200/=** sawa na **asilimia 37** zilitengwa kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi na shilingi **8,264,846,800/=** sawa na asilimia 63 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengine *(OC)*.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2014 Wizara imepokea jumla ya shilingi **4,344,886,775/=** sawa na **asilimia 91** ya fedha za mishahara ya watumishi na shilingi **2,764,106,935/=** sawa na **asilimia 33** ya fedha za matumizi mengineyo ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaisisitiza Serikali kuipa Wizara fedha zilizobaki kwa wakati ili iweze kukamilisha shughuli zake ipasavyo.

3.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha unaoishia Juni 30, 2014 Kamati ilitoa maoni na ushauri kweye maeneo mbalimbali hasa kwenye maeneo yanayohusu:-

i. Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee.
ii. Migogoro ya Wafanyakazi.
iii. Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.
iv. Ukuzaji wa Ajira Nchini.
v. Uanzishwaji wa Idara/Kurugenzi ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa, hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kutekeleza ushauri wa Kamati kwenye maeneo ambayo bado hayajafanyiwa kazi, maeneo hayo ni pamoja na Muswada wa Sheria ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee.

Kamati iliiagiza Wizara kuja na mpango mkakati na hatimaye Muswada wa kuanzisha Mfuko wa Pensheni kwa Wazee, utekelezaji wa suala hili unaenda polepole sana kwani hadi sasa hakuna Muswada wowote kuhusu suala la kuanzishwa kwa mfuko huu ulioandaliwa ingawa Wizara iliieleza Kamati kuwa imekamilisha Rasimu ya Mpango wa Pensheni kwa Wazee.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hakukuwa na Idara/Kurugenzi inayosimamia Hifadhi ya Jamii Wizarani, Kamati iliishauri Serikali kukamilisha uanzishwaji wa Idara/Kurugenzi ya Hifadhi ya Jamii, jambo ambalo halijatekelezwa mpaka hivi sasa. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza ushauri huo ili masuala ya hifadhi ya jamii yaweze kuratibiwa vyema Wizarani.

4.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

4.1 Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 9,606,000/= kama maduhuli.

4.2 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 Wizara imetengewa jumla ya shilingi **18,280,136,000/=** kati ya fedha hizo shilingi **15,280,136,000/=** kwa ajili ya Matumzi ya Kawaida na mishahara na shilingi **3,000,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Wizara inategemea kupokea kiasi chote hicho cha fedha zikiwa ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 ni pamoja na:-

i. Kutoa mafunzo na mitaji kwa vijana wajasiriamali.

ii. Kufanya kaguzi za mara kwa mara katika sehemu za kazi ili kubaini upungufu na kasoro za ukiukaji wa sheria za kazi.

iii. Kutoa elimu kuhusiana na sheria, kanuni na taratibu za afya na usalama mahali pa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasikitishwa na Bajeti ndogo inayotengewa kwa Wizara hii bila kujali umuhimu wa Wizara katika kukuza ajira na hasa kwa vijana ukizingatia hatari inayoweza kuligharimu Taifa kwa kuwa na vijana wengi wasio na ajira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Bunge kuidhinisha fedha kwa Wizara hii, bado fedha hizo hazitolewi kwa wakati na sehemu kubwa ya fedha haipelekwi kabisa. Aidha Bajeti hii ndogo itaathiri uwezo wa Wizara katika kutekeleza vipaumbele vyake kwa mwaka ujao wa fedha.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na maombi ya fedha yanayojumuisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

i. **Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni kwa Wazee**

Mheshimiwa Spika, wazee ni kundi muhimu sana katika jamii yoyote ile duniani na kwa Tanzania wazee wamekuwa nguzo muhimu katika kuhimiza maadili mema, malezi bora, usalama na kuwa washauri wakuu katika masuala mengine muhimu ya kitaifa hasa katika kipindi hiki ambacho jamii inapitia mabadiliko makubwa ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Takwimu zinaonesha kuwa kati ya watu milioni 45, idadi ya wazee ni 5,056,825 hii ni kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Kamati ilishauri Serikali kuanzisha Mfuko wa Pensheni kwa Wazee. Aidha, katika kikao cha Kamati, Wizara ilitoa maelezo kuwa Wizara ilikamilisha Rasimu ya Mpango wa Pensheni kwa Wazee mwezi Septemba, 2013 ikiwa ni pamoja na kukusanya taarifa za uzoefu kutoka nchi nyingine. Hatua inayofuata ni kuandaa mapendekezo ya mfumo wa pensheni ya wazee kwa kuzingatia uzoefu na mafunzo kutoka katika nchi zilizotembelewa na kuleta Bungeni Muswada ili Sheria ya Pensheni kwa Wazee kuweza kutungwa.

Mheshimiwa Spika, kuna mitazamo mingi tofauti ikiwa ni pamoja na mtazamo kuwa wazee ambao hawakuchangia kuweka akiba katika mfumo rasmi hawawezi kulipwa. Mfumo wa pensheni tulionao sasa hauhusishi wazee wote, wazee wanaohusishwa na pensheni ni wale waliokuwa katika mfumo rasmi wa ajira kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii. Idadi kubwa ya wazee ambao katika uhai wao hawajawahi kuwa na ajira rasmi hawafaidiki na pensheni ya uzee hivyo kuanzishwa kwa mfuko huu kutasaidia kundi kubwa la wazee kupata pensheni ambayo kwa kiasi itasaidia kukidhi mahitaji yao na kuwafanya wazee pia kuchangia katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na ukweli huu, Kamati inaitaka Serikali ikamilishe mchakato wa uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni ya Wazee ili wazee nao waweze kuboreshewa hali zao za kimaisha, ngoja ngoja huumiza matumbo, wazee wamechoka kungoja katika jambo hili. **Tutekeleze sasa.**

ii. **Elimu na mafunzo ya biashara na ujasiriamali**

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara kwa kuanzisha elimu ya mafunzo ya biashara kwani utekelezaji wake utakuza ajira. Kamati inaona kuwa utekelezaji wa programu ya kukuza ajira kwa vijana kwa kiasi kikubwa utachangia kupunguza umaskini nchini kama ilivyoainishwa katika Programu ya MKUKUTA II na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba mafunzo hayo yawafikie walengwa kwa kuanzia na kada ya elimu ya chini mpaka elimu ya juu kwa lengo la kuwanufaisha vijana wote na fursa hizo za ajira zielekezwe pia kwa vijana wa vijijini ambao wanapenda kujiajiri katika kilimo. Kilimo kwanza iwe kwa vitendo si maneno.

a) Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza programu mbalimbali za maendeleo Wizara imetengewa shilingi **3,000,000,000/=** kwa ajili ya kuanza utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Aidha Wizara imeainisha maeneo ya vipaumbele ambayo ni pamoja na kuwajengea uwezo vijana na ujuzi katika stadi mbalimbali za kazi na ujasiriamali, kuwapatia mitaji, nyenzo, vifaa vya uzalishaji mali, kuhamisha mazingira wezeshi kisera na kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inawapatia vijana hawa elimu itakayowawezesha kupata ujuzi na taaluma mbalimbali zitakazowasaidia kuwa wabunifu katika ulimwengu wa sasa ambao unahitaji watu wenye ujuzi na utayari wa kujiajiri na kuondokana na dhana ya kuajiriwa.
Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuangalia mfumo mzima wa elimu kwa kufanya utafiti wa kina wa mitaala iliyopo ili kuona mitaala gani itakayowawezesha vijana kijiajiri wenyewe.

iii. **Ajira kwa vijana**

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira limekuwa tatizo sugu hasa kwa vijana kutokana na fursa rasmi za ajira kutokuwepo. Katika kikao cha Kamati na Wizara kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 3 Mei, 2014 Wizara iliieleza Kamati kuwa wameandaa programu ya kukuza ajira kwa vijana itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu na kuibua fursa za ajira 840,000.

Mheshimiwa Spika, Kulingana na Takwimu za Matokeo ya Utafiti wa NguvuKazi na Ajira ya mwaka 2005/2006, kama zilivyonukuliwa katika

hotuba ya Waziri Mkuu iliyotolewa katika Kongamano la Vijana wa Vyuo vya Elimu ya Juu Kanda ya Ziwa, takwimu zinaonesha kuwa idadi ya vijana wanaomaliza vyuo vikuu nchini kila mwaka kuwa ni wastani wa vijana laki nane mpaka milioni moja na kati ya hao wanaopata ajira ni wastani wa vijana 80,000 mpaka 100,000 katika sekta za umma na sekta binafsi, hivyo kwa takwimu hizi tatizo la ajira kwa vijana bado ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia inakisiwa kwamba takribani vijana 850,000 wenye umri kati ya miaka 15 na 25 huingia kwenye soko la ajira kila mwaka nchini Tanzania, huku asilimia 40 ya vijana hawa ikiwa ni waliofeli kidato cha nne; Benki ya Dunia inazidi kukadiria kwamba ifikapo mwaka 2015 kutakuwa na nyongeza ya vijana milioni 1.3 katika soko la ajira. **Kazi kwetu.**

Mheshimiwa Spika, ni hatari sana kwa nchi yoyote duniani kuna vijana wengi na wazururaji, wasio na ajira kwani huweza kujihusisha na vitendo vya uharibifu, kwa kuzingatia hili Kamati inaitaka Serikali kukuza ajira katika sekta ya umma na binafsi kuboresha sera kuhusu vijana na ajira.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa mafunzo kwa vijana yatakayotolewa kupitia fedha za maendeleo zilizotengwa katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2014/2015 yawe ya gharama nafuu na ya muda mfupi ili fedha nyingi zitumike kwa ajili ya vijana na mitaji badala ya kutumika katika shughuli za uendeshaji wa mafunzo hayo.

iv. **Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)**

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA) ni taasisi inayosimamia na kudhibiti masuala yote ya hifadhi ya jamii na kuishauri Serikali ipasavyo juu ya uimarishaji na uboreshaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Mamlaka ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iendelee na kazi nzuri ya kusimamia mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini ili kuchochea ukuaji wa uchumi na kuwafanya wananchi wengi kuwa wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kupitia *supplimentary schemes* za mifuko hiyo badala ya asilimia sita tu (6%) ya sasa ili kupanua wigo wa Mifuko hiyo na pia kuongeza wanachama hasa kutoka katika sekta isiyo rasmi.

v. **Migogoro katika Migodi**

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na migogoro ya muda mrefu katika sekta ya madini nchini, miongoni mwa migogoro hiyo ni pamoja na mgogoro

kati ya wafanyakazi 79 na uongozi wa Mgodi wa African Barrick Bulyanhulu. Kamati iliwahi kupata fursa ya kukutana na wawakilishi wa wafanyakazi wa Mgodi wa African Barrick Bulyanhulu kuhusu kuachishwa kazi bila kupimwa afya zao kulingana na sheria inayotaka.
Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Migodi (TAMICO) Ndugu Hassan Ameir ya kufatilia migogoro baina ya wafanyakazi na waajiri wao ili kuipatia ufumbuzi, bado Kamati inasisitiza Serikali kuingilia kati suala hili ili wafanyakazi hao waweze kupatiwa haki zao ikiwa ni pamoja na kupimwa afya zao pale wanapoachishwa kazi kama inavyobainishwa na sheria na kulipwa haki zao endapo watashindwa kuendelea na kazi. **Uzalendo mbele.**

vi. **Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)**

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza NSSF kwa kuendeleza uwekezaji katika vitega uchumi ambavyo mbali na kulenga kuongeza kipato cha mfuko, pia vinatoa huduma za kimsingi kwa jamii hasa kwa mradi wa Daraja la Kigamboni ambalo litapunguza adha ya usafiri kwa wakazi wa maeneo hayo. Ujenzi wa nyumba za gharama nafuu, ujenzi wa Chuo Kikuu cha Nelson Mandela – Arusha na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na miradi mingine mingi ni ushahidi mzuri wa namna NSSF wanavyojitahidi kuboresha huduma za kijamii sehemu mbalimbali nchini. **Dkt. Ramadhani Dau na wenzako endeleeni hivyo.**

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi Kamati inashauri mfuko huu kuangalia namna ya kuwekeza vitega uchumi katika maeneo mbalimbali nchini ambayo yako nyuma kimaendeleo ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Aidha, mfuko uangalie namna ya kuboresha zaidi mafao ya wanachama wake kwa kutumia faida ambayo inatokana na vitega uchumi vinavyowekezwa na mfuko huu kwani fedha zinazotumika kama mitaji zinatokana na michango ya wanachama. Mafao bora na yanayotolewa kwa wakati viwe ndiyo msingi mkubwa wa faida inayotokana na uwekezaji huo kwa wanachama. **Wanachama kwanza.**
Mheshimiwa Spika, Kamati imearifiwa kuwa NSSF ipo katika majadiliano na Ofisi ya Bunge kwa ajili ya kuingia mkataba wa ujenzi wa Ofisi za Wabunge katika Majimbo ya Uchaguzi nchini. Jambo hili ni jema na Kamati inashauri Serikali na Bunge kukamilisha mazungumzo hayo ili Waheshimiwa Wabunge wapate Ofisi bora kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao ya Kibunge.

vii. **Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA)**

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) imekuwa ikisimamia utekelezaji wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Namba 6) ya mwaka 2004. Aidha Tume imekuwa ikiratibu migogoro yote ya kikazi inayowasilishwa kwake ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa wafanyakazi sehemu za kazi. Ni wazi kuwa kwa bajeti hii ndogo ambayo Wizara imetengewa bado itaendelea kuathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha Tume ya Usuluhishi na Uamuzi imetengewa kiasi cha shilingi **4,837,030,800/=,** kiasi hiki ni kidogo ukilinganisha na majukumu ya Tume yenyewe. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Tume ilishughulikia migogoro 5,722 na kwa mwaka 2013/2014 kumekuwa na ongezeko la migogoro 2,398 na kufanya idadi ya migororo iliyoshughulikiwa na CMA kuwa 8,120. Hivyo utaona kuna ongezeko kubwa la migogoro ambayo inahitaji fedha kuishughulikia.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iwapatie CMA vitendea kazi ikiwemo rasiliamli watu wa kutosha ambao wataweza kufanya kazi ya usuluhishi na uamuzi katika mashauri mbalimbali yanayofikishwa na kuwasilishwa katika Tume hii kwa wakati ili watu waweze kupatiwa haki zao mapema. **Kinga ni bora kuliko tiba.**

viii. **Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA)**

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imepanga kutekeleza kazi kadhaa ikiwemo kufanya ukaguzi maalum na wa kawaida kuhusu afya na afya mahali pa kazi. Kamati inashauri kaguzi hizi kufanyika kila mara kubaini upungufu uliopo katika sehemu hizo ili kulishughulikia ipasavyo tatizo hili na kwa maana hiyo kuwa sehemu ya motisha kwa watumishi kwa kujali afya zao na usalama katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, ingawa ni jukumu la waajiri na waajiriwa kuhakikisha afya na usalama wao mahali pa kazi, bado Serikali ina wajibu wa kuhakikisha inaweka viwango vya usalama na kusimamia kikamilifu utekelezwaji wake ili kunusuru afya za wananchi na hivyo kulinda ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaisisitizia Serikali kuendelea kutoa elimu kuhusiana na sheria, kanuni na taratibu za afya na usalama mahali pa kazi na kusimamia utekelezaji wake. Kwa ujumla OSHA imekuwa inafanya kazi zake kwa weledi mkubwa chini ya usimamizi wake Dkt. Akwilina Kayumba, **hongera sana.**

6.0 MWISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe kwa ushauri wako kwangu katika kutekeleza majukumu yangu. Niwapongeze pia Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna ambavyo wanavyokusaidia kutekeleza majukumu yako.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Kazi na Ajira - Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka, (Mb), Naibu Waziri - Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, (Mb) Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Erick Francis Shitindi na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kamati pia kwa michango yao katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Said Mohamed Mtanda, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Capt. John Damian Komba, Mb -M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Kiumbwa Makame Mbaraka, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Mary Pius Chatanda, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Moza Abedi Saidy, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dkt Maua Abeid Daftari, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Juma Othman Ali, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Salum Khalfan Barwany, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Nassib Suleiman Omary, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Salvatory Naluyanga Machemli, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Jaddy Simai Jaddy, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Rose Kamili Sukum, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Rosemary Kisimbi Kirigini, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Mustafa Haidi Mkulo, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Joshua Samweli Nassari, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashillilah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Ndugu Charles Mloka na Makatibu

wa Kamati hii, Ndugu Hanifa Masaninga, Ndugu Aziza Makwai na Ndugu Abdallah Hancha kwa ushauri na uratibu wa kazi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hoja, naomba kuwasilisha.

Said Mohamed Mtanda, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA MAENDELEO YA JAMII
24 Mei, 2014

MWENYEKITI: Ahsante, sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Kazi na Ajira.

Taarifa ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kazi na Ajira kwa Mwaka 2014/2015 Kama Ilivyosomwa Bungeni

MHE. CECILIA D. PARESSO - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kambi ya Upinzani ya Wizara ya Kazi na Ajira kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa msaada mkubwa wa maisha yangu. Pili, napenda kuishukuru familia yangu hasa wazi wangu Daniel na John Paresso, mume wangu Steven Andrew kwa upendo na uvumilivu wao wakati wote ninapokuwa natekeleza wajibu wangu.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe kwa kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara hii na kuisimami Serikali katika masuala ya Kazi na Ajira. Kipekee kabisa napenda kuwashukuru vijana wenzangu wa Karatu kwa kuwa nami bega kwa bega katika juhudi za ukombozi wa nchi. Naahidi kuendelea kuwawakilisha vyema katika majukumu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira nchini limezidi kuwa kubwa sana hali ambayo inahatarisha amani na utulivu wa amani wa nchi yetu. Ukosefu wa ajira nchini hasa kwa vijana umesababisha vijana wengi kujihusisha na vitendo vya ujambazi, uvutaji bangi, madawa ya kulevya, ubakaji na kadhalika. Taarifa ya Shirika la Kazi Duniani la Mwelekeo wa Ajira kwa Vijana Ulimwenguni, inaonyesha kuwa ukosefu wa ajira kwa vijana Tanzania wenye elimu kuanzia

Sekondari na kuendelea inaendelea kuwa kubwa kuliko wale wenye elimu ya kiwango cha chini.

Hata hivyo kwa kiasi kikubwa Watanzania wenye elimu ya kawaida wamepata ajira ya kawaida lakini ajira zao ni duni, ama za kipato cha chini, ama katika mazingira hatarishi. Hii ni ishara kuwa Taifa letu bado pamoja na kuzalisha idadi kubwa ya wasomi, wasomi hawana nafasi katika soko la ajira nchini, na badala yake watu wenye elimu ya msingi hupewa ajira kama njia mojawapo ya kuwanyonya, kuwakandamiza na kuwatumikisha kwa kuwa uelewao juu ya masuala ya sheria na taratibu za kazi ni mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni dalili kuwa Serikali haina mikakati mahususi kwa kundi la vijana wengi wanaohitimu elimu ya juu, kupata ajira katika mfumo rasmi. Matokeo yake ni kuwa Taifa linazalisha idadi kubwa ya watu ambao wameishia kuwa vibarua na wanaofanya kazi katika mazingira hataraishi na yasiyo na vipato vya uhakika na vya kuridhisha.

Kwa kuwa vijana wengi nchni ndio wahanga wakubwa wa tatizo la ajira nchini; na kwa kuwa vijana wengi wana imani na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, katika kutetea maslahi yao; nachukua fursa hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuwataka vijana wote nchini kutambua kwamba mafanikio katika maisha huanza na ndoto, malengo, nidhamu, bidii, uadilifu, ubunifu, kujituma na kutokukata tamaa. Hivyo ni wajibu wa kila kijana kuhakikisha kuwa anajenga fikra chanya katika kuifikia ndoto anayoiamini. Nina hakika atafanikiwa. *(Makofi)*

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka vijana kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha kidogo wanazozipata ili kujijengea uwezo na kuwa na mitaji mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kueleza uzito wa tatizo la ajira nchini, ni lazima kuwa na takwimu na taarifa sahihi za Soko la Ajira. Hata hivyo, kwa muda mrefu, takwimu na Taarifa za Soko la Ajira zilizokuwa zinatumika ni pamoja na taarifa ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2002 na 2012 na za Utafiti wa Nguvukazi ya mwaka 2006. Kutumika kwa takwimu hizi kwa muda mrefu kumepelekea kutoainishwa kwa uhalisia wa tatizo la ajira nchini.

Aidha, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia unabainisha upungufu katika upatikanaji wa takwimu za ajira Barani Afrika na Tanzania ambapo changamoto za upatikanaji wa takwimu na taarifa za ajira husababishwa na kukosekana kwa vipimo stahiki vya ajira na kukosekana kwa taarifa sahihi zinazoakisi uhalisia wa kiwango cha tatizo la ukosefu wa ajira. Lugha iliyotumika ni kuwa *unemployment measure understate the total extent of the youth unemployment problem*. Kwa maana hiyo, hata vipimo vya

kiwango cha ajira nchini vimeongezeka na hivyo kutoakisi uhalisia wa kiwango cha ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za *Integrated Labor Force Survey 2006* zinabainisha kuwa sekta za ajira zipo sita ambazo zinaajiri vijana kukanzia umri wa miaka 15 na kuendelea ambayo ni Sekta ya Kilimo inayoajiri asilimia 75 ya watu wote walioajiriwa, sekta isiyo rasmi inaajiri asilimia 10.1 ya watu wote walioajiriwa, Sekta Binafsi inaajiri 8.6, Sekta ya shughuli za kiuchumi za kaya inaajiri asilimia 3.1, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa inaajiri asilimia 2.6 na Sekta ya Mashirika ya Umma inaajiri asilimia 0.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa Serikali katika maendeleo ya vijana hususan kukuza ajira kwa vijana kupitia Mpango wa Kukuza Ajira kwa Vijana nchini na Mfuko wa Maendeleo ya vijana vinapaswa kuzingatia takwimu zilizopo katika hali ya ajira nchini ili uwekezaji uwe na tija. Tafsiri ya Taifa ya ajira kwa mujibu wa takwimu zilizopo kuhusu hali ya ajira zina walakini na kutokuweka bayana uhalisia wa kiwango cha ukosefu wa ajira nchini. Hivyo shughuli za kupanga maendeleo ya kukuza ajira kwa vijana inahitaji umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Ofisi ya Takwimu imekamilisha maandalizi ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi ya mwaka 2014 ulioanza mwezi Februari, 2014, bado kuna ukosefu wa taarifa sahihi na takwimu za soko la ajira nchini ambao ni muhimu katika mikakati na mipango ya kiuchumi kwa Taifa.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeeleza kuwa lengo la utafiti huu ni kupata viashiria mbalimbali vya soko la ajira kama vile hali ya ukosefu wa ajira, ajira isiyo timilivu, ukubwa wa nguvukazi, utumikishwaji wa watoto pamoja na matumizi ya muda katika ufanyaji wa shughuli za kiuchumi. Viashiria hivi hutumika katika uandaaji na ufuatiliaji wa sera na *program* mbalimbali zenye malengo ya kukuza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa takwimu sahihi na taarifa za kutojitosheleza za soko la ajira nchini kumechangia kuzidi kukua kwa matatizo ya ajira nchini. Ili Serikali iweze kupanga matumizi mazuri ya nguvukazi nchini, suala la upatikanaji wa taarifa za soko la ajira halikwepeki. Inashangaza kuona Serikali inashindwa kupata takwimu sahihi kutoka kwa waajiri ili kuweza kupata taarifa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza kuwa lazima Wizara iwe na mfumo thabiti wa utunzaji taarifa na takwimu za ajira ambao utakuwa na uwezo wa kuboresha taarifa hizo mara kwa mara na upatikanaji wake kwa Umma uwe ni rahisi ili kuwasaidia watu mbalimbali katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yoyote ina wajibu wa kutambua umuhimu wa juhudi za pamoja katika kuleta maendeleo ya rasilimali watu kwa kuwa rasilimali watu ndiyo msingi mkuu wa maendeleo na mapinduzi ya kiuchumi. Vilevile raslimali watu ina uwezo wa kugeuza raslimali nyingine yoyote kuwa chanzo cha kuboresha maisha ya watu. Hivyo, kuendeleza raslimali watu na kuitumia barabara kunaongeza tija na thamani ya mtaji.

Kwa hiyo, maendeleo ya raslimali watu lazima yawe ni lengo kuu katika agenda ya maendeleo ya Taifa. Serikali ina wajibu wa kutambua mahitaji na dai la uchumi wa soko huria linalokabili Taifa, mojawapo ni kwa kuwezesha wananchi wake kushindana katika soko huria la ajira kwa kutumia ujuzi na maarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanawezekana kwa kuwa na misingi ya maendeeo ya sera mpya ambayo ni kuonyesha umuhimu wa sekta binafsi, kuweka mkazo zaidi ya mahitaji ya wafanyakazi katika sekta binafsi kuanzia ngazi ya usimamizi itakayofanikisha kuunganisha mahitaji ya jamii na mipango ya kuendeleza nguvukazi nchini. Ni lazima mkabala wa kupanga raslimali watu ufanywe katika ngazi tatu, yaani ngazi ya kitaifa, kisekta na kiusimamizi.

Pili, utambuzi huu kwa upande wa Serikali una maana kwa kuwa kuna haja ya kuwa na sera itakayohakisha kuwa elimu na elimu ya ufundi katika ngazi za msingi na sekondari inahusika na mahitaji ya misingi ya soko la ajira kwa kuwa na mfumo endelevu wa maarifa na stadi kupitia maboresho ya elimu na mafunzo.

Tatu, kwa kuwa na mkakati wa Taifa wa maendeleo unaoshirikisha jamii nzima hadi vijijini utakaowezesha Serikali kupanua Elimu ya Msingi na ya Sekondari kwa kutoa elimu hiyo bure na kwamba watoto watafundishwa na kupata stadi za kiufundi zitakazowawezesha kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wetu, nguvukazi iliyo na elimu ni ndogo na iko zaidi Mijini, kwa ujumla inakadiriwa nguvukazi mpya kati ya 500,000 mpaka 600,000 huingia kwenye soko la kazi kila mwaka na wengi wakiwa vijana. Sekta isiyo rasmi imeendelea kuwa mhimili wa wananchi kwa kuwa inatoa fursa zaidi kwa soko la ajira, kuanzia kwa wanaojiajiri, hata wale walioko katika sekta isiyo rasmi lakimi wenye mifumo inayotoa nafasi za ajira.

Kwa wastani aliye katika sekta isiyo rasmi, pato lake kwa mwezi hulingana na yule aliye katika sekta rasmi hata kuzidi kima cha chini cha mshahara wa Serikali unapolipwa kwa wale wasiokuwa na ujuzi na utaalamu. Hii ina maana kuwa sekta isiyo rasmi ni njia mbadala kwa kutoa nafasi za ajira ila imepuuzwa

na kutotekelezwa na Serikali. Hivyo, ni lazima Serikali itambue umuhimu wa kuipa kipaumbele sekta hii kuliko kuitupa kapuni.

Vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inajikita katika uboreshaji na uandaaji wa sera za kitaifa za raslimali watu kwa kuwa hakuna sera moja inayotawala maendeleo ya raslimali watu kwa sekta zote. Uboreshaji wa sera hizi za raslimali watu na ajira zitachangia katika utatuzi wa ukosefu wa ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafiti mbalimbali, taarifa zimethibitisha kwamba shughuli za sekta isiyo rasmi ni muhimu sana katika ukuzaji wa kipato, kupunguza umaskini, ukuzaji wa ajira na uimarishaji wa pato la Taifa, kwani sekta isiyo rasmi inachangia kati ya asilimia 35 mpaka asilimia 40 ya *GDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutokuwa na utaratibu mzuri, sekta isiyo rasmi ina uwezo wa kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira nchini kila mwaka. Kwa mfano, ili kuongeza ukuzaji wa ajira katika kilimo, ni muhimu kuwa na mkakati wa maendeleo utakaoboresha miundombinu, elimu vijijini, ugavi wa bidhaa, umiliki wa ardhi, pembejeo ya masoko na kuwepo kwa bidhaa zitakiwazo. Juhudi hizi zitawezesha shughuli nyingine zaidi kuliko kilimo cha kujikimu na hivyo kuongeza kipato kutokana na kilimo. Kuongezeka kwa nafasi za ajira katika kilimo vijijini ni muhimu sana ili kupunguza wingi wa ukosefu wa ajira mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka nenda rudi Serikali ya CCM imekuwa katika vita ya Wamachinga ili kuwaondoa katikati ya Miji na Majiji na kuwaweka pembezoni mwa maeneo yao. Suala hili limejaribiwa kutekelezwa karibu kila Mkoa nchini lakini kwa kiasi kikubwa imeonekana ikijaribiwa sana katika Jiji la Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Iringa pamoja na baadhi ya maeneo katika Mikoa ya Kusini. Kwa bahati nzuri katika sehemu zote hizi Serikali haijafanikiwa kuwahamisha kabisa kwenda wanakotaka. Wameshindwa Dar es Salaam, wameshindwa Mwanza, wakashindwa na Iringa, ambako kote huko licha tukio la kuwahamisha Wamachinga kujaribiwa tena na tena, lakini bado linashindwa.

Serikali inashindwa kuelewa kuwa wafanyabiashara ndogo ndogo wanaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana katika kuendesha uchumi wa nchi endapo watatambuliwa kama sehemu ya uchumi wa Taifa na siyo kuonekana ama kuchukuliwa kama wadandiaji tu wa uchumi wa wafanyabiashara wakubwa. Wakitambulika kuwa wao ni sehemu ya uchumi basi wanaweza kuendesha biashara zao katika Miji na Majiji tena katikati kabisa ili kuchochoea watu kuja Mijini na kutumia fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa ahadi ya CCM ya maisha bora kwa kila Mtanzania hailengi katika kuimarisha sekta isiyo rasmi ili iweze kutengeneza nafasi zaidi za ajira na kunyanyua kuelekea kuwa sekta rasmi bali inalenga katika kuwafanya Watanzania waishi katika lindi lile lile la umasikini kwa takribani miaka 50 ya uhuru wa Taifa letu. Kuendelea kupambana na wamachinga, wafanyabiashara wadogo, mamantilie na huku mali na amana zao zikiharibiwa, ni sawa na kuipiga vita sekta isiyo rasmi ambayo ndiyo kimbilio kubwa la Watanzania wengi ambao wameachwa na mfumo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuboresha mfumo wa elimu na kuongeza thamani ya raslimali watu. Pamoja na Serikali ya CCM kuendelea kutoa taarifa mbalimbali na takwimu zinazoonyesha ufaulu pamoja na idadi kubwa ya wasomi wanaomaliza elimu ya juu, *report* ya Shirika la Kazi Duniani inaeleza kuwa pamoja na kuwepo kwa idadi kubwa ya watu wenye elimu haimaanishi kuwa utakuwa na idadi ya mtaji rasilimali watu kwa kuwa idadi kubwa ya wasomi nchini wanaongoza kwa kutokuwa na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Aidha, idadi ya wanafunzi wanaomaliza Shule za Msingi pamoja na Sekondari ni kubwa lakini kwa uwiano idadi kubwa ya wanafunzi hao hailingani na uwezo wa Vyuo vyetu kimuundo kuhimili ongezeko hili, hali inayosababisha Watanzania wengi kuwa nje ya mfumo wa Elimu ya Juu. Hii inamaanisha kuwa mfumo wetu wa elimu sasa ambao unasifiwa na Serikali ya CCM hauzalishi watu sahihi wanaohitajika katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kurekebisha mfumo wa elimu ili kuweza kuzalisha watu wenye maarifa, ubunifu, nidhamu na kujituma ili kukabiliana na changamoto za soko la ajira hasa tunapoelekea katika mfumo wa ajira za Afrika Mashariki. Ili kujenga jamii yenye thamani katika soko la ajira, mfumo mzima wa elimu unatakiwa kuakisi mahitaji ya soko la ajira ikiwemo ya kisayansi na kiteknolojia ili kujenga ushindani bora baina ya watafuta ajira nchini na wa nchi jirani.

Siyo ajabu kuona kuwa leo katika sehemu za kazi mbalimbali, tuna wafanyakazi mbalimbali kutoka nchi jirani ambao wamejengwa na mifumo imara na inayoendana na wakati kutokana na mapinduzi ya kielimu katika nchi zao. Tukichelewa kufanya mapinduzi ya kielimu, tutaendelea kuwa wasindikizaji katika soko la ajira huku tukilaumu watu wenye uwezo, ujuzi na maarifa kutoka nchi jirani. Aidha, tunaitaka Wizara kuwa mdau namba moja wa kusisitiza mapinduzi ya mfumo wa elimu utakaoendana na mazingira ya karne ya 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu juu ya uendeshaji, udhibiti na usimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii katika nchi yetu kwa mwaka huu inajieleza yenyewe. Naomba kunukuu:

"Kushindwa kwa makampuni haya, kuheshimu majukumu yao ya mikopo unatia shaka kama uchambuzi madhubuti ulifanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii juu ya uwezo wa wakopaji kulipa mikopo hiyo. Zaidi ya hayo ukubwa wa biashara inayofanywa baina ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi za Serikali na malipo yasiyokuwa na uhakika ya mikopo hiyo inatia shaka juu ya uendelevu wa mifuko husika katika siku zijazo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu bado ni halali kwa miaka miwili mpaka sasa. Kwanza, mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 hayajatekelezwa hadi leo na Serikali hii sikivu ya CCM. Hivi ndivyo anavyosema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwenyewe, naomba kunukuu:

"Katika ukaguzi wa *NSSF* nilibaini kwamba mfuko ulitumia Shilingi bilioni 231.1 kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma chini ya makubaliano ya Buni, Jenga, Endesha na Kisha Hamisha Miliki Baada ya Miaka Kumi. Mifuko mingine iliyochangia ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa makubaliano hayo hayo ni Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali Kuu *(PSPF)*, Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa *(LAPF)*, Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF)* na Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma *(PPF)* ambayo yalichangia jumla ya Shilingi bilioni 181.3.

Kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, majengo haya hayapo kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma wala katika vitabu vya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Hii inatokana na uelewa tofauti uliopo kati ya pande mbili zinazohusika. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inafahamu kwamba kiasi cha fedha kilichotumika kujenga majengo haya kilikuwa ni mikopo kwa Serikali, wakati Serikali inafahamu kwamba ilikuwa ni uwekezaji wa mifuko. Mifuko ya jamii inatakiwa kufuata mikataba ya makubaliano iliyowekeana kati yao na Serikali ili kuonyesha majengo hayo kwenye vitabu vyao vya hesabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya pili ni kwamba matatizo aliyoyagundua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuhusu usimamizi na matumizi ya fedha za wafanyakazi katika mwaka wa fedha 2010/2011 ndiyo matatizo ambayo ameyakuta tena katika *report* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Report hii ilikabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais tarehe 28 Machi, 2014 na kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu mwezi Mei. Kwa mujibu wa *report* hiyo, Serikali ilitoa dhamana ya mkopo wa Shilingi bilioni 6.65 uliotolewa na *NSSF* kwa ajili ya *Kiwira Coal and Power Limited* chini ya *Export Credit Guarantee Scheme* ilhali *KCPL* haikuwa na sifa za kupewa dhamana chini ya mpango huu. Zaidi ya

hayo, *KCPL* ilipata mkopo wa Shilingi bilioni 28.998 kutoka *NSSF, PSPF* na Benki ya *CRDB* kwa ajili ya kuongeza mtaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati na upanuzi wa shughuli za *KCPL*. Utumiaji wa mikopo hii na *KCPL* ulileta maswali kwa kuwa hakuna uwekezaji wowote uliofanywa, pia mikopo hii haikuwahi kulipika tangu ilipochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo pesa tu za wafanyakazi ambao wameweka akiba zao za uzeeni kwenye *NSSF* pekee ndiyo ambazo matumizi yake ni ya mashaka. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amesema yafuatayo kuhusu fedha za wafanyakazi zilizopo *PSPF*. Naomba kunukuu:

"Ukaguzi wa *PSPF* ulibainika kwamba kutokana na uthamani wa uwezo wa mfuko kulipa wanachama wake, yaani *actuarial valuation* iliyofanyika mwaka 2010, mfuko ulipata pungufu, yaani nakisi katika uwezo wa kulipa *actuarial deficit* ya Shilingi trilioni 6.4. Pia, mfuko uliingiza kwenye hesabu zake kiasi cha Shilingi bilioni 107.8 zilizotumika kujenga Chuo cha Elimu cha Chuo Kikuu cha Dodoma kama mkopo." Hii ni kinyume na masharti ya mkataba ambao unataka mradi kuwa katika mfumo wa kubuni, kujenga, kuendesha na kuhamisha jengo ambapo mfuko utapokea kodi iliyokokotolewa kwa misingi ya gharama za uwekezaji na riba ya uwekezaji ambayo ni asilimia 15 kwa kipindi cha miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa za wafanyakazi walioweka akiba zao uzeeni kwenye *PSPF* zimetumika pia kuikopesha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kwa mujibu wa *report* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, mkopo wa *PSPF* Shilingi bilioni 58 kwa Bodi ya Mikopo haujalipwa hadi leo. Bila kutafuna maneno, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ametupia lawama juu ya kuzorota kwa hali ya kifedha ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Serikali hii. Naomba kunukuu:

"Serikali kuingilia maamuzi katika mifumo ya Pensheni ndiyo chanzo cha matatizo ya kifedha katika mifuko ya Pensheni. Mikopo kwa taasisi ya Serikali kutoka Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imedhaminiwa na Serikali inachukua muda mrefu kulipwa huku Serikali ikiwa imekaa kimya."

Napenda kusisitiza kuwa Serikali inapaswa ichukue hatua kuhakikisha kwamba bakaa ya deni lote la mikopo iliyokopwa na *PSPF* inalipwa ili kuepuka gharama za riba na adhabu itakayotokana na kuchelewa kulipwa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo tu kwenye manunuzi yake pekee ndiyo penye uvundo wa ufisadi, hata katika kulipa mafao ya wanachama wake kuna matatizo. Hivyo kwa mfano, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anaeleza jinsi ambavyo *NSSF* imekiuka Waraka wa Serikali wa mwaka 2009 unaotaka watumishi wa

mikataba kulipwa kiinua mgongo baada ya mkataba na wasilipwe mafao ya pensheni kama watumishi wa ajira za kudumu.

Report ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inasema kwamba katika ukaguzi wake *NSSF* ilibaini kuwa mfuko ulikiuka waraka huo wa Serikali na kuwalipa Shilingi milioni 13 watumishi wa ajira ya kudumu kama malipo ya mkataba, yaani *gratuity* ambapo wafanyakazi wa pensheni wanatakiwa kulipwa mafao ya kiinua mgongo peke yake. Kukiukwa huku kwa waraka huu wa Serikali kumeliingiza shirika kwenye matumizi yasiyokuwa ya lazima na yasiyoleta tija kwa shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu ya kina kutoka kwa Waziri ambaye ndiye msimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Serikali itoe kauli rasmi Bungeni ikiwa inapingana na kauli na *report* ya *CAG* kuhusu hali ya mifuko hii na kama inapingana, kauli yake kwa mifuko hii ipo hatarini kufilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee nchini wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokupata matibabu, kuwa walezi wa watoto yatima, kupoteza mali zao na haki ya kurithi, kuuawa kwa imani za kishirikina ikiwemo wazee 2,866,000 waliuawa katika Mikoa 10 kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, sawa na wastani wa wazee 573 kila mwaka au takribani mzee mmoja anauawa kila siku. Tumeendelea kushuhudia wazee wa nchi hii ndani ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi wakiendelea kupuuzwa, kunyanyasika na kudharauliwa huku wakijisahau kuwa na wao ni wazee watarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 wazee nchini ni takribani 5,056,832. Ongezeko la wazee nchini na duniani ni jambo lisiloweza kupuuzwa tena kwani mtu mmoja katika watu tisa ni mzee. Hata hivyo, idadi hii inategemea kuongezeka hadi kufikia mzee mmoja kwa watu watano ifikapo mwaka 2050.

Katika hotuba zetu za miaka mitatu mfululizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tumeendelea kusisitiza umuhimu wazee kupewa pensheni na Serikali imekuwa ikitoa kauli kwa utoaji wa pensheni kwa wazee unaofanyika na utafiti au uko katika hatua za mwisho.

Aidha, kauli za Serikali kuwa wazee wapatiwe matibabu bure, imekuwa ni changa la macho kwa kuwa wazee wengi wamepata usumbufu katika kupata huduma za afya na wengine wameshindwa kabisa kupata huduma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kauli ya kuwapa wazee pensheni ilitumiwa na Serikali ya CCM katika uchaguzi, tunaitaka Serikali kutoa kauli katika Bunge lako Tukufu kuwa: Je, pensheni kwa wazee itatekelezwa au haitekelezeki? Kama inatekelezeka, ni lini itaana kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakala binafsi wa ajira nchini. Wakati wa maadhimisho ya Mei Mosi mwaka 2014, Rais Kikwete alipoongeza hatua ya Wizara kufuta mfumo mpya ulioanzishwa na Makampuni kuajiri kwa kupitia wakala wa ajira na kuunga mkono hatua ya Wizara kupiga marufuku utaratibu unaofanywa na Wakala binafsi wa ajira wa kukodisha wafanyakazi katika makampuni kinyume na Sheria ya Huduma za Ajira Na. 9 ya mwaka 1999 inayoelekeza kuwa majukumu ya Wakala binafsi ni kuunganisha watafuta kazi na siyo kuwa waajiri wa watafuta kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari za wakala wa ajira kuwa waajiri wa watafuta kazi ni pamoja na kuwakosesha wafanyakazi haki zao za msingi ikiwemo likizo, huduma za matibabu, huduma ya hifadhi ya jamii pamoja na kuwanyima mishahara yao wanayostahili. Kitengo cha Rais kupongeza hatua hii ya Wizara kunaonyesha kuwa kuna tatizo kubwa ambalo kwa muda mrefu Wizara ya Kazi ya Ajira imeshindwa kusimamia misingi na matakwa ya haki ya sheria ambazo Bunge lako Tukufu imezitunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya makampuni yanayokodisha wafanyakazi yamefanyiwa uhakiki na *TRA* na kubaini kukwepa kodi ya mapato ya ajira yaani *PAYEE* na kodi ya makato ya Makampuni kinyume na kifungu Na. 7 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kama ilivyorejewa mwaka 2008.

Aidha, kwa mujibu wa Kamishna wa Kazi wa Wizara ya Kazi na Ajira, mara baada ya kutolewa kwa tamko la kupiga marufuku Wakala wa Ajira, Makampuni 56 yalituma maombi ya kupewa vibali vya kufanya kazi za uwakala kwa Wizara. Hii inaonyesha kuwa, Serikali kwa muda mrefu ilishindwa kuratibu na kusimamia Makampuni ya Uwakala na hivyo kusababisha unyimwaji wa haki za wafanyakazi waliopitia katika Makampuni hayo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Wizara kulieleza Bunge lako Tukufu imechukua hatua gani kwa waajiri ambao wamebainika kutumia mfumo huu ili kukwepa kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria? Je, Makampuni mangapi mpaka sasa yameshapata usajili na Makampuni mangapi yamenyimwa usajili wa kutoa huduma za ajira na mangapi yamechukuliwa hatua za kisheria? *(Makofi)*

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua, pamoja na kuwa Mawakala hawa wataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria: Je, Wizara ya Kazi na Ajira nayo isiwajibishwe kwa kushindwa kufuatilia Mawakala hawa kwa miaka mitatu na kuisababishia Serikali hasara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi na Ajira na Taasisi zake zina wajibu wa kushughulikia matatizo ya wafanyakazi na kusimamia Sheria za Kazi na ajira katika Makampuni na maeneo mbalimbali. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri wa Kazi na Ajira kutoa maelezo ya sababu ya Wizara na Taasisi zake kushindwa kuwezesha ufumbuzi wa migogoro ya wafanyakazi na mwajiri wao katika Kampuni ya *Starbag* pamoja na madai ya ukiukwaji wa Sheria za Kazi na Ajira katika kampuni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi. Malengo ya sheria hii yalikuwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa kulipa fidia kwa wafanyakazi wanapopata ajali na kukumbwa na majanga wakiwa kazini. Aidha, sheria inalenga kuunda Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ambao utachangiwa na waajiri wote wa Sekta za Umma na sekta binafsi.

Majukumu ya mfuko huo ni kutathmini na kuboresha viwango vya fidia vinavyotakiwa kulipwa kwa fanyakazi wanaoumia, kupata magonjwa, kupata madhara ya kiafya na kufariki wakiwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Waziri aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba maandalizi ya kuanzisha mfuko huu yamekamilika. Aidha, Waziri aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba Kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo zilikuwa zimeishapitishwa.

Licha ya kauli ya Mheshimiwa Waziri, hadi leo hii Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi haujaanzishwa. Hii inathibitishwa na maelezo ya Waziri juu ya utekelezaji wa maagizo hayo Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni lini mfuko huu sasa utaanzishwa rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utaratibu uliopo sasa, kodi ya mapato ya wafanyakazi ni kati ya asilimia13 hadi 30 ya mshahara wa mfanyakazi. Kwa mujibu wa *CAG* katika mwaka huu wa fedha, Mamlaka ya Kodi *(TRA)* imekusanya kodi kutoka kwa wafanyakazi jumla ya Shilingi trilioni 1.5.

Aidha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali anaonesha kwamba, katika kipindi hicho Serikali ilitoa msamaha kwa walipa kodi wakubwa na Makampuni ya nje liliyofikia kiasi cha Shilingi trilioni 1.5, sawa na kodi iliyokusanywa na Serikali kutoka kwa wafanyakazi. Misamaha hiyo ya kodi ni sawa na asilimia 3.1 ya pato la Taifa kwa mwaka huu.

Hii ina maana kwamba kama Serikali isingetoa misamaha hiyo ya kodi, mapato ya Serikali kutokana na kodi ya walipa kodi wakubwa yangeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kwa nini Serikali ya CCM inaendelea kuwabebesha wafanyakazi mzigo mkubwa wa kodi wakati ikitoa misamaha ya kodi kwa Makampuni makubwa matajiri ya nje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania, limependekeza Sh. 315,000/= kama kima cha chini cha mshahara kwa sekta zote. Hata hivyo, tarehe 7 Februari, 2014 Katibu Mkuu wa *TUCTA*, aliwaambia Mkutano wa Viongozi wa Shirikisho hilo kwamba kiwango cha chini cha mshahara ambacho *TUCTA* imependekeza kwa miaka ya nyuma kimepitwa na wakati.

Kwa mujibu wa Bwana Mgaya, kima cha chini cha mshahara kinachoweza kukidhi mahitaji ya sasa ya wafanyakazi kutokana na uhalisia wa kupanda kwa gharama za maisha, ni Sh. 720,000/= kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Watumishi wa Umma, katika sherehe za Mei Mosi za mwaka 2011, Mheshimiwa Rais Kikwete alitangaza kuwa Serikali yake imeongeza kima cha chini cha mshara kwa Watumishi wa Umma kutoka Sh. 65,000/= hadi Sh. 135,000/= kwa mwezi kati ya mwaka 2006 na 2010.

Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 38.5 ya mapendekezo ya Vyama vya wafanyakazi kwa kipindi hicho. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na gazeti la Mwananchi la tarehe 27 Julai, 2013, kima cha chini cha mshahara ya Watumishi wa Serikali kuu na Serikali za Mitaa kimepanda hadi Sh. 240,000/= kwa mwezi.

Hata hivyo, ongezeko hili nalo halikidhi mahitaji halisi ya wafanyakazi wa Tanzania kwa kuzingatia kupanda kwa gharama za maisha. Kwa vyovyote vile, ongezeko hili liko chini ya mapendekezo ya *TUCTA* ya mwaka 2006 na hata ya mwaka huu. Ni wazi vilevile kwamba Serikali haina mpango wowote wa kuwapatia Watumishi wa Umma wa ngazi za chini kipato kinachowawezesha kukabiliana na kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu juu ya baadhi ya raia wa kigeni kuwepo nchini bila ya vibali vya kazi. Vilevile, Wizara ya Kazi na Ajira haijaweka wazi mikakati yake kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 juu ya ukaguzi wa vibali vya ajira kwa wageni katika maeneo ya kazi.

Pamoja na taarifa kwamba kuna watu wengi nchini ambao wamejiriwa katika hoteli makubwa, migodi, Makampuni makubwa, Shule za watu binafsi, Saluni na Migahawa mikubwa nchini ambao hawana vibali vya kufanyia kazi nchini, Serikali haijaonyesha kwa vitendo ari yake katika kukabiliana na changamoto hii na ndiyo maana mpaka sasa Serikali inapoteza mapato kwa

kushindwa kukusanya fedha za vibali vya wageni nchini. Ni jukumu la Wizara ya Kazi na Ajira kuhakikisha kuwa kaguzi za mara kwa mara zinafanyika ili kuwanasa wale wote ambao wanafanya kazi nchini kinyume na taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la kuanzishwa kwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *(CMA)* lilikuwa ni kuondoa urasimu uliokuwepo wa rufaa za wafanyakazi kwenda kwa Waziri, jambo ambalo lilikuwa linachukua muda mrefu sana na haki kucheleweshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Wizara, Tume hii imefanya kazi ya usuluhishi na kutoa maamuzi kwa kiwango cha chini ya asilimia 50, jambo linaloashiria kuwa migogoro ya kazi ambayo inahitaji kutolewa maamuzi na kusuluhishwa huchukua muda mrefu, hivyo malalamiko mengi dhidi ya Tume yamegusiwa, jambo ambalo limepelekea...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. CECILIA D. PARESSO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo. *(Makofi)*

Taarifa ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka 2014/2015 Kama Ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (MB) MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WIZARA YA KAZI NA AJIRA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015.

(Inatolewa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge kanuni ya 99(9) toleo la mwaka 2013).

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa msaada mkubwa wa maisha yangu. Pili, napenda kuishukuru familia yangu hasa wazazi wangu Daniel na Joan Paresso, mume wangu Steven Andrew kwa upendo na uvumilivu wao wakati wote ninapokuwa natekeleza wajibu wangu. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mhe. Freeman A. Mbowe kwa kunipa dhamana ya kuiongoza wizara hii na kuisimamia Serikali katika masuala ya Kazi na Ajira. Kwa kipekee

kabisa, napenda kuwashukuru Vijana wenzangu wa Karatu kwa kuwa nami bega kwa bega katika juhudi za ukombozi wa nchi. Naahidi kuendelea kuiwakilisha vyema Kambi katika majukumu mengine ikiwemo na kusimamia upatikanaji wa Katiba bora ya maoni ya wananchi itakayotetea na kulinda maslahi ya watanzania katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, aliyekua Rais wa 26 wa Marekani, Theodore Roosevelt (1858-1919) aliwahi kusema,

> *"Ni kwa kupitia kazi na juhudi chungu, kwa nguvu yenye maumivu na ushujaa wa kijasiri, ndivyo vinavyopelekea sisi kuendelea na mambo mazuri".*
>
> *"It is only through labor and painful effort, by grim energy and resolute courage that we move on to better things".*

2.0 UKOSEFU WA AJIRA NCHINI

Mheshimiwa Spika, Tatizo la ajira nchini limezidi kuwa kubwa sana hali ambayo inahatarisha amani na utulivu wa nchi yetu. Ukosefu wa ajira nchni hasa kwa vijana umesababisha vijana wengi kujihusisha na vitendo vya ujambazi, uvutaji bangi, madawa ya kulevya, ubakaji na kadhalika. Taarifa ya shirika la Kazi Duniani ya mwelekeo wa ajira kwa vijana Ulimwenguni (Global Employment Trends For Youth) inaonyesha kuwa ukosefu wa ajira kwa vijana wa Tanzania wenye elimu kuanzia Sekondari na kuendelea inaendelea kuwa kubwa kuliko wale wenye elimu ya kiwango cha chini[1]. Hata hivyo kiasi kukubwa cha watanzania wenye elimu za kawaida wamepata ajira lakini ajira zao ni duni ama za kipato cha chini au katika mazingira hatarishi. Hii ni ishara kuwa taifa letu pamoja na kuzalisha idadi kubwa ya wasomi, wasomi hawana nafasi katika soko la ajira nchini na badala yake watu wenye elimu ya msingi hupewa ajira kama njia mojawapo ya kuwanyonya, kuwakandamiza na kuwatumikisha kwa kuwa uelewa wao juu ya masuala ya sheria na taratibu za kazi ni mdogo.

Mheshimiwa Spika haya yote ni dalili kuwa Serikali haina mikakati mahsusi kwa kundi la vijana wetu wengi wanaohitimu elimu ya juu kupata ajira katika mfumo rasmi. Matokeo yake ni kuwa taifa limezalisha idadi kubwa ya watu ambao wameishia kuwa vibarua na wanafanya kazi katika mazingira hatarishi nayasiyo na vipato vya uhakika na vya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wengi nchi ndio wahanga wakubwa wa tatizo la ukosefu wa ajira nchini na kwa kuwa vijana wengi wana imani na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika kutetea maslahi yao, nachukua fursa hii kwa niaba ya Kambi kuwataka vijana wote nchini kutambua kwamba mafanikio katika maisha huanza na ndoto, malengo, nidhamu, bidii, uadilifu, ubunifu, kujituma na kutokukata tamaa. Hivyo ni wajibu wa kila kijana

kuhakikisha kuwa anajenga fikra chanya katika kuifikia ndoto anayoiamini. Na hakika, atafinikiwa!

---

[1] International Employment Trends for Youth, International Labour Organisation 2013
Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka vijana kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha kidogo wanazozipata ili kujijengea uwezo wa kuwa na mitaji mikubwa.

2.1 TAKWIMU NA TAARIFA ZA SOKO LA AJIRA NCHINI

Mheshimiwa Spika, ili kuelezea uzito wa tatizo la ajira nchini ni lazima kuwa na takwimu na taarifa sahihi za soko la ajira. Hata hivyo kwa muda mrefu takwimu na taarifa za ajira nchini zilizokua zinatumika ni pamoja na Sensa ya watu ya mwaka 2002 na za utafiti wa nguvu kazi za mwaka 2006. Kutumika kwa takwimu hizi kwa muda mrefu kumepelekea kutokuoneshwa kwa uhalisia wa tatizo la ajira nchini, hali iliyoipa mwanya Serikali kuweza kuchezea takwimu na taarifa za soko la ajira kuudanganya umma kuhusu ukubwa wa tatizo la ukosefu wa ajira nchini.Kauli ya aliyekua Waziri Mkuu, Mhe. Edward Lowassa kuwa ukosefu wa ajira kwa ni bomu kubwa na zigo jingine kwa Serikali ya awamu ya nne endapo halitadhibitiwa mapema kwa kupatiwa ufumbuzi, inathibitishwa na mchezo unaofanywa na Serikali hii katika kutoa takwimu halisi za ajira na soko la ajira nchini. Kukosekana kwa taarifa na takwimu sahihi za ukosefu wa ajira nchini, kumesababisha mipango, mikakati na programu zote zinazoandaliwa na wizara kuwa ni usanii tu.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia (WB, 2008) unabainisha upungufu katika upatikanaji wa takwimu za ajira barani Afrika na Tanzania ambapo changamoto za upatikanaji wa takwimu na taarifa za ajira husababishwa na kukosekana kwa vipimo stahiki vya ajira, kukosekana kwa taarifa sahihi zinazoakisi uhalisia wa kiwango cha tatizo la ukosefu wa ajira. Lugha iliyotumika ni kuwa "Unemployment measures understate the total extent of the youth unemployment problem" ("*Vipimo vya ukosefu wa ajira haviakisi kwa ujumla tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana")* Kwa maana hiyo hata vipimo vya kiwango cha ajira nchini vimeongezwa na hivyo kutoweka uhalisia wa kiwango cha ajira nchini.
Mheshimiwa Spika, takwimu za ILFS, 2006 (Integrated Labour Force Survey, 2006) zinabainisha kuwa sekta za ajira (Employment by Sector) zipo sita ambazo zinaajiri vijana kuanzia umri wa miaka 15+ na kuendelea ni Sekta ya Kilimo inayoajiri 75.1% ya watu wote walioajiriwa, Sekta isiyo rasmi inaajiri 10.1% ya wote walioajiriwa, Sekta binafsi inaajiri 8.6%, Sekta ya Shughuli za kiuchumi za

kaya (Household economic activities) 3.1%, Serikali kuu na Serikali za mtaa zinaajiri 2.6% na Sekta ya Mashirika ya Umma 0.4%.

Wakati huo huo, (ILFS, 2006) zinabainisha kuwa jumla ya watu walioajiriwa nchini ni asilimia 79.2% ya watu wote nchini walio na umri wa miaka 15 na kuendelea. Hata hivyo, mbili ya tatu ya watu wote nchini ambayo ni sawa na asilimia 65 ni watu chini ya umri wa miaka 24, na zaidi ya watu milioni 8 nchini ni vijana kati ya umri wa miaka 15-24 ambapo ni sawa na asilimia 17% ya watu wote nchini (NBS and ICF Macro, 2011). Sera ya maendeleo ya vijana (URT,2008) inabainisha kuwa vijana ni kati ya umri wa miaka 15-35.

Uwekezaji wa Serikali katika maendeleo ya vijana, hususan kukuza ajira kwa vijana kupitia mpango wa Kukuza ajira kwa vijana nchini, na Mfuko wa maendeleo ya Vijana vinapaswa kuzingatia takwimu zilizopo katika hali ya ajira nchini ili uwekezaji uwe na tija. Tafsiri ya taifa ya ajira kwa mujibu wa takwimu zilizopo kuhusu hali ya ajira zinawalakini wa kutoweka bayana uhalisia wa kiwango cha ukosefu wa ajira nchini, hivyo shughuli ya kupanga maendeleo ya kukuza ajira kwa vijana inahitaji umakini mkubwa mno.

Mheshimiwa Spika, aidha, tafsiri ya kitaifa ya ajira inabainisha sifa za ajira kuwa ni

> "*shughuli yoyote ya kiuchumi inayofanywa kwa mujibu wa Sheria inayomuwezesha mtu kupata kipato au ujira kutokana na shughuli hiyo*".

Hii ni bila kujali anapata ujira unaokidhi mahitaji yake kwa mwaka, mwezi, juma au siku. Kiwango cha ukosefu wa ajira nchini kwa mujibu wa takwimu ni asilimia 10.4% ya watu wote nchini hawana ajira (unemployed population) , watu wasiokuwa na shughuli yoyote (inactive population) ni asilimia 10.4 na watu walioajirwa (employed population) ni asilimia 79.2% (ILSF,2006).

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu imekamilisha maandalizi ya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2014[2] ulioanza Mwezi wa Pili mwaka huu bado kuna ukosefu wa taarifa sahihi na takwimu za soko la ajira nchini ambazo ni muhimu katika mikakati na mipango ya kiuchumi kwa taifa. Ofisi ya Takwimu ya Taifa imeeleza kuwa lengo la utafiti huu ni kupata viashiria mbalimbali vya Soko la Ajira kama vile; Hali ya Ukosefu wa Ajira, Ajira Isiyo Timilifu, Ukubwa wa Nguvukazi, Utumikishwaji wa Watoto pamoja na Matumizi ya Muda Katika Ufanyaji wa Shughuli za Kiuchumi. Viashiria hivi hutumika katika uandaaji na ufuatiliaji wa sera na programu mbalimbali zenye lengo la kukuza ajira.

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo kwa takwimu sahihi na taarifa za kujitosheleza za soko la ajira nchini, kumechangia kuzidi kwa matatizo ya ajira nchini. Ili serikali iweze kupanga matumizi mazuri ya nguvu kazi nchini suala la upatikanaji wa taarifa za soko la ajira halikwepeki, inashangaza kuona kuwa Serikali inashindwa kupata takwimu sahihi kutoka kwa waajiri ili kuweza kupata taarifa sahihi.

Mheshimiwa Spika, kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza kuwa lazima wizara hii iwe na mfumo thabiti wa utunzaji taarifa na takwimu za ajira ambao utakua na uwezo wa kuboresha taarifa hizo mara kwa mara na upatikanaji wake kwa umma uwe ni rahisi ili kuwasaidia watu mbalimbali katika soko la ajira.

---

[2] **Ofisi Ya Taifa Ya Takwimu :** http://www.nbs.go.tz/nbs/index.php?option=com_content&view=article&id=469:utafiti-wa-watu-wenye-uwezo-wa-kufanya-kazi-2014-umeanza&catid=106:labour-force-&Itemid=148 tarehe 19.05.2014

2.2 UKUZAJI WA AJIRA

Mheshimiwa Spika, Serikali yoyote, ina wajibu wa kutambua umuhimu wa juhudi za pamoja katika kuleta maendeleo ya rasilimali watu kwa kuwa rasilimali watu ndiyo msingi mkuu wa maendelo na mapinduzi ya kiuchumi. Vilevile rasilimali watu ina uwezo wa kugeuza rasilimali nyingine yoyote kuwa chanzo cha kuboresha maisha ya watu. Hivyo kuendeleza rasilimali watu na kuitumia bara-bara kunaongeza tija na thamani ya mtaji. Kwa hiyo maendeleo ya rasilimali watu lazima yawe ni lengo kuu katika ajenda ya maendeleo ya Taifa. Serikali ina wajibu wa kutambua mahitaji na dai la uchumi wa soko huria linalokabili taifa, mojawapo ni kwa kuwawezesha wananchi wake kushindana katika soko huria la ajira kwa kutumia ujuzi na maarifa.

Mheshimiwa Spika, hayo yote yanawezekana kwa kuwa na misingi ya malengo ya sera mpya, ambayo ni kuonyesha umuhimu wa sekta binafsi, kuweka mkazo zaidi wa mahitaji ya wafanyakazi katika sekta binafsi kuanzia ngazi ya usimamizi itakayofanikisha kuunganisha mahitaji ya jamii na mipango ya kuendeleza nguvu kazi nchini. Ni lazima mkabala wa kupanga rasilimali watu ufanywe katika ngazi tatu: kitaifa, kisekta na kiusimamizi. Pili, utambuzi huu kwa upande wa serikali una maana kuwa kuna haja ya kuwa na sera itakayohakikisha kuwa elimu na elimu ya ufundi katika ngazi za msingi na sekondari inahusika na mahitaji ya msingi ya soko la ajira kwa kuwa na mfumo endelevu wa maarifa na stadi kupitia maboresho ya elimu na mafunzo. Tatu, kwa kuwa na mkakati wa taifa wa maendeleo unaoshirikisha jamii nzima hadi vijijini, utakaowezesha serikali kupanua elimu ya msingi na sekondari kwa kutoa elimu hiyo bure; na

kwamba watoto watafundishwa na kupata stadi za kiufundi zitakazowawezesha kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wetu Nguvukazi iliyo na elimu ni ndogo na iko zaidi mijini. Kwa jumla inakadiriwa nguvukazi mpya 500,000-600,000 huingia kwenye soko la kazi kila mwaka, wengi wakiwa vijana. Sekta isiyo rasmi imeendelea kuwa mhimili wa wananchi kwa kuwa inatoa fursa zaidi kwa soko ajira, kuanzia kwa wanaojiajiri hata wale walio katika sekta isiyo rasmi lakini wenye mifumo inayotoa nafasi za ajira. Kwa wastani aliye katika sekta isiyo rasmi pato lake kwa mwezi hulingana na yule wa sekta rasmi, hata kuzidi kima cha chini cha mshahara wa Serikali unaolipwa kwa wale wasiokuwa na ujuzi na utaalamu. Hii ina maana kuwa, sekta isiyo rasmi ni njia mbadala kwa kutoa nafasi za ajira ila imepuuzwa na kutelekezwa na serikali. Hivyo, ni lazima serikali itambue umuhimu wa kuipa kipaumbele sekta hii kuliko kuitupa kapuni.

Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inajikita katika uboreshaji na uaandaji wa sera za kitaifa za rasilimali watu kwa kuwa hakuna sera moja inayotawala maendeleo ya rasilimali watu kwa sekta zote. Uboreshaji wa Sera hizi za rasilimali watu na ajira, zitachangia katika utatuzi wa ukosefu wa ajira nchini.

2.3 UKUZAJI WA AJIRA KWA SEKTA ISIYO RASMI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa tafiti[3] mbalimbali za karibuni, taarifa zimethibitisha kwamba shughuli za sekta isiyo rasmi ni muhimu sana katika Ukuzaji wa kipato, Kupunguza umaskini, Ukuzaji wa ajira na uimarishaji wa pato la Taifa kwani sekta isiyo rasmi inachangia kati ya asilimia 35-40ya GDP.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutokua na uratibu mzuri Sekta isiyo rasmi ina uwezo wa kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira nchini kila mwaka. Kwa mfano, ili kuongeza ukuzaji wa ajira katika kilimo ni muhimu kuwa na mkakati wa maendeleo utakao- boresha miundombinu, elimu vijijini, ugavi wa bidhaa, umiliki wa ardhi, pembejeo na masoko, na kuweko bidhaa zitakiwazo. Juhudi hizi zitawezesha shughuli nyingine zaidi kuliko kilimo cha kujikimu, na hivyo kuongeza kipato kutokana na kilimo. Kuongezeka kwa nafasi za ajira katika kilimo vijijini ni muhimu sana ili kupunguza wingi wa ukosefu wa ajira mijini.

---

[3]Road map towards the informal sector, Labor force survey 2001, SMEs Development policy 2003, Informal construction workers in Tanzania 2005 na Household Budget survey 2002,

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa, Serikali na Halmashauri zake zimeshindwa kuwashirikisha vijana katika upangaji na utekelezaji wa miradi inayolenga sekta

isiyo rasmi hapa nchini. Mipango mingi na program za vijana hupangwa Dar Es Salaam lakini utekelezaji wake huwalenga wananchi wa nje ya Dar Es Salaam ambao hawajashirikishwa kikamilifu katika upangaji na utekelezaji wa miradi na hali hii imechangia kuathiri sana suala la ajira kwa vijana**.** Aidha, Sekta isiyo rasmi ina nafasi ya kutoa nafasi zaidi za ajira kwa ufanisi zaidi kuliko mashirika makubwa. Hata hivyo ajira nyingi katika sekta hii haziaminiki, na hazina ujira wa uhakika. Hatua muhimu za kuongeza nafasi ya ajira katika sekta ni pamoja na kuendeleza mikopo ambayo inaendana na hali za wakopaji wasiokuwa na dhamana; kuboresha upatikanaji wa mali ghafi na masoko, kutoa mafunzo ya ujuzi na kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, leo tunashuhudia Serikali hii ikiwa vitani na raia wake wenyewe ambao wanajihusisha na shughuli mbalimbali katika sekta isiyo rasmi ikiwemo wamachinga, Serikali hii imekua wakala wa wafanyabiashara wa kichina ambao nao ni wamachinga lakini wanaonekana wafalme katika taifa la watu masikini wasio na mitaji ya kutosha kufanya biashara endelevu. Mikakati na sera zisizotelezeka za Serikali ndiyo leo imezalisha taifa la watu wasio na muelekeo, watu tegemezi wasio na matumaini, wanaoishi kwa mashaka na wenye uadui, chuki na machungu dhidi ya Serikali yao. Wakati Serikali ya CCM ikiwa daraja la mteremko kwa wachina nchini kwa kuwafungulia milango ya kufanya biashara hizo ndogo ndogo ambazo Watanzania wanaweza kuzifanya, serikali inapaswa kutambua kuwa haikuwatendea haki wananchi wake, kwani hata China biashara kama hizo hakuna Mtanzania anayeruhusiwa kuzifanya.

Mheshimiwa Spika, miaka nenda rudi Serikali ya CCM imekuwa katika 'vita dhidi ya Wamachinga' ili kuwaondoa katikati ya miji na majiji na kuwaweka pembezoni mwa maeneo hayo. Swala hili limejaribiwa kutekelezwa karibu kila mkoa nchini lakini kwa kiasi kikubwa imeonekana ikijaribiwa sana katika Jiji la Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Iringa pamoja na baadhi ya mikoa ya kusini. Kwa bahati nzuri, katika sehemu zote hizo serikali ya CCM haijafanikiwa kuwahamisha kabisa wamachinga kwenda inakotaka. Wameshindwa Dar, na wameshindwa Mwanza; wakashindwa na Iringa; ambapo kote huku licha ya tukio la kuwahamisha wamachinga kujaribiwa tena na tena bado linashindwa. Serikali ya inashindwa kuelewa kuwa wafanyabiashara ndogondogo wanaweza kuchangia kwa kiasi kikubwa sana katika kuendesha uchumi wa nchi endapo watatambulika kama sehemu ya uchumi wa taifa na si kuonekana ama kuchukuliwa kama wadandiaji tu wa uchumi wa wafanyabiashara wakubwa. Wakitambulika kuwa wao ni sehemu ya uchumi basi wanaweza kuendesha biashara zao katika miji na majiji tena katikati kabisa ili kuchochea watu kuja mijini na kutumia fedha zao.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa ahadi ya CCM ya maisha bora kwa kila mtanzania haielengi katika kuimarisha sekta isiyo rasmi ili iweze kutengeneza

nafasi zaidi za ajira na kuinyanyua kuelekea kuwa sekta rasmi bali inalenga katika kuwafanya watanzania waishi katika lindi lile lile la umasikini kwa takribani miaka 50 ya uhuru wa taifa letu. Kuendelea kupambana na wamachinga, wafanyabiashara wadogo, mama ntilie na huku mali na amana zao zikiharibiwa, ni sawa na kuipiga vita sekta isiyo rasmi ambayo ndio kimbilio kubwa la watanzania wengi ambao wameachwa na mfumo rasmi.

2.4 UMUHIMU WA KUBORESHA MFUMO WA ELIMU NA KUONGEZA THAMANI YA RASILIMALI WATU

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali ya CCM kuendelea kutoa taarifa mbalimbali na takwimu zinazoonesha ufaulu pamoja na idadi kubwa ya wasomi wanaomaliza elimu ya juu, ripoti ya Shirika la Kazi Duniani inaeleza kuwa pamja na kuwepo kwa idadi kubwa ya watu wenye elimu haimaanishi kuwa utakua na idadi kubwa ya mtaji-rasilimali watu kwa kuwa idadi kubwa ya wasomi nchini wanaongoza kwa kutokua na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira[4].

---

[4] SparreBoom na Nubler
Aidha, Idadi ya wanafunzi wanaomaliza Shule ya Msingi pamoja na Sekondari ni kubwa lakini kwa uwiano idadi kubwa ya wanafunzi hao hailingani na uwezo wa vyuo vyetu kimuundo kuhimili ongezeko hili. Hali inayosababisha watanzania wengi kuwa nje ya mfumo wa elimu ya juu. Hii inamaanisha kuwa mfumo wetu wa elimu sasa ambao unasifiwa na Serikali ya CCM, hauzalishi watu sahihi wanaohitajika katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kurekebisha mfumo wa elimu ili kuweza kuzalisha watu wenye maarifa, ubunifu, nidhamu na kujituma ili kukabiliana na changamoto za soko la ajira hasa tunapoelekea sasa katika mfumo wa ajira za Afrika Mashariki. Ili kujenga jamii yenye thamani katika soko la ajira, mfumo mzima wa elimu unatakiwa kuakisi mahitaji ya soko la ajira ikiwemo ya kisayansi na teknolojia ili kujenga ushindani bora baina ya watafuta ajira wa nchini na nchi jirani. Si ajabu kuona kuwa leo katika sehemu za kazi mbalimbali tuna wafanyakazi kutoka nchi jirani ambao wamejengwa na mifumo imara na inayoenda na wakati kutokana na mapinduzi ya kielimu katika nchi zao. Tukichelewa kufanya mapinduzi ya kielimu, tutaendelea kuwa wasindikizaji katika soko la ajira huku tukilaumu watu wenye uwezo, ujuzi na maarifa toka nchi jirani. Aidha, tunaitaka Wizara kuwa mdau namba moja wa kusisitiza mapinduzi ya mfumo wa elimu utakaoendana na mazingira ya karne ya 21.

3.1 MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII

Mheshimiwa Spika, Miaka miwili iliyopita Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililiambia Bunge lako tukufu kwamba "… *ahadi pekee kuhusu hifadhi ya jamii*

iliyotekelezwa na Serikali hii ya CCM ni kuendelea kutumia fedha za wafanyakazi zilizomo katika Mifuko mbali mbali ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza katika miradi ambayo haina manufaa yoyote kwa wafanyakazi wenyewe." Tuliliambia Bunge lako tukufu kwamba Serikali hii ya CCM "… *imechota mabilioni ya fedha za Mifuko hiyo na kuziingiza katika miradi ambayo haina manufaa yoyote kwa Mifuko yenyewe na hasa kwa wafanyakazi ambao ndio wenye fedha hizo.*"
Tulionyesha, kwa kutumia takwimu zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwamba hadi *kufikia* mwaka 2010/2011, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ilikuwa imekwishawekeza jumla ya shilingi bilioni 661.903 za wafanyakazi katika miradi mbali mbali kama vile Chuo Kikuu cha Dodoma, Jengo la Idara ya Usalama wa Taifa, nyumba za Jeshi la Polisi, Machinga Complex na viwanda kadhaa vya wamiliki binafsi. Kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, vitega uchumi vyote hivyo vilikuwa 'non-performing', yaani vilikuwa havirudishi fedha za mikopo ya Mifuko husika.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu juu ya uendeshaji, udhibiti na usimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika nchi yetu kwa mwaka huo inajieleza yenyewe: "*Kushindwa kwa makampuni haya (baadhi yao yakiwa yamedhaminiwa na Serikali) kuheshimu majukumu yao ya mikopo kunatia shaka kama uchambuzi madhubuti ulifanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii juu ya uwezo wa wakopaji kulipa mikopo hiyo. Zaidi ya hayo, ukubwa wa biashara inayofanywa baina ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na taasisi za Serikali na malipo yasiyokuwa na uhakika ya mikopo hiyo yanatia shaka juu ya uendelevu wa Mifuko husika katika siku chache zijazo.*"

Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu bado ni halali miaka miwili baadae. Kwanza, mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 hayajatekelezwa hadi leo na Serikali hii sikivu ya CCM. Hivi ndivyo anavyosema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu mwenyewe: "*Katika ukaguzi wa … NSSF nilibaini kwamba Mfuko ulitumia shilingi bilioni 234.1 kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma … chini ya makubaliano ya buni, jenga, endesha na kisha hamisha miliki baada ya miaka kumi…. Mifuko mingine iliyochangia ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma kwa makubaliano hayo hayo ni Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali Kuu (PSPF), Mfuko wa Pensheni kwa Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (LAPF), Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Pensheni kwa Mashirika ya Umma (PPF) ambayo yalichangia jumla ya shilingi bilioni 181.3.*"
Kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, "*majengo haya hayapo kwenye vitabu vya Chuo Kikuu cha Dodoma wala katika vitabu vya mifuko ya hifadhi ya jamii. Hii inatokana na uelewa tofauti uliopo kati ya pande mbili zinazohusika. Mifuko ya hifadhi ya jamii inafahamu kwamba kiasi cha fedha kilichotumika kujenga majengo hayo kilikuwa ni mikopo kwa serikali, wakati serikali inafahamu kwamba ilikuwa ni uwekezaji wa mifuko hiyo. Mifuko ya jamii inatakiwa kufuata*

mikataba ya makubaliano iliyowekeana kati yao na serikali ili kuweza kuonyesha majengo hayo kwenye vitabu vyao vya hesabu."

Sababu ya pili ni kwamba matatizo aliyoyagundua Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuhusu usimamizi na matumizi ya fedha za wafanyakazi katika mwaka wa fedha 2010/2011, ndio matatizo ambayo ameyakuta tena katika *Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013*. Ripoti hii ilikabidhiwa kwa Rais Jakaya Kikwete tarehe 28 Machi, 2014 na kuwasilishwa kwenye Bunge lako tukufu mwezi huu.

Kwa mujibu wa Ripoti hiyo, *"Serikali ilitoa dhamana ya mkopo wa shilingi bilioni 6.65 uliotolewa na NSSF kwa ajili ya Kiwira Coal and Power Ltd. (KCPL) chini ya 'Export Credit Guarantee Scheme' ilihali KCPL haikuwa na sifa ya kupewa dhamana chini ya mpango huo. Zaidi ya hayo, KCPL ilipata mkopo wa shilingi bilioni 28.998 kutoka NSSF, PSPF na benki ya CRDB kwa ajili ya kuongeza mtaji, ukarabati na upanuzi wa shughuli za KCPL. Utumiaji wa mikopo hii na KCPL unaleta maswali kwa kuwa hakuna uwekezaji wowote uliofanywa. Pia, mikopo hii haikuwahi kulipika tangu ilipochukuliwa."*

Mheshimiwa Spika, sio pesa za wafanyakazi ambao wameweka akiba zao za uzeeni kwenye NSSF pekee ndio ambazo matumizi yake ni ya mashaka. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu amesema yafuatayo kuhusu fedha za wafanyakazi zilizoko kwenye PSPF: *"Ukaguzi wa … PSPF ulibaini kwamba kutokana na uthamini wa uwezo wa mfuko kulipa wanachama wake (actuarial valuation) iliyofanyika mwaka 2010, Mfuko ulipata mapungufu (nakisi) katika uwezo wa kulipa (actuarial deficit) ya shilingi trilioni 6.49…. Pia Mfuko uliingiza kwenye hesabu zake kiasi cha shilingi bilioni 107.843 zilizotumika kujenga Chuo cha Elimu cha Chuo Kikuu Dodoma kama mkopo. Hii ni kinyume na masharti ya mkataba ambao unataka mradi kuwa katika mfumo wa kubuni, kujenga, kuendesha na kuhamisha jengo … ambapo Mfuko utapokea kodi iliyokokotolewa kwa misingi ya gharama za uwekezaji na riba ya uwekezaji ambayo ni asilimia 15 kwa kipindi cha miaka 10."*

Mheshimiwa Spika, pesa za wafanyakazi walioweka akiba zao za uzeeni kwenye PSPF zimetumika pia kuikopesha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kwa mujibu wa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, mkopo wa PSPF wa shilingi bilioni 58 kwa Bodi ya Mikopo haujalipwa hadi leo. Bila kutafuna maneno, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu ametupia lawama juu ya kuzorota kwa hali ya kifedha ya mifuko ya hifadhi ya jamii kwa serikali hii sikivu ya CCM: *"Serikali kuingilia maamuzi katika mifuko ya pensheni ndio chanzo cha matatizo ya kifedha katika mifuko ya pensheni. Mikopo … kwa taasisi za Serikali kutoka mifuko ya jamii ambayo imedhaminiwa na serikali inachukua muda mrefu kulipwa huku serikali ikiwa imekaa kimya. Ningependa kusisitiza kuwa serikali*

inapaswa ichukue hatua kuhakikisha kwamba bakaa ya deni lote la mkopo … uliokopwa kutoka PSPF inalipwa, ili kuepuka gharama zaidi za riba na adhabu itokanayo na kuchelewa kulipa mikopo hiyo."

Mheshimiwa Spika, sababu ya tatu ya hukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuwa halali miaka miwili tangu alipoitoa ni kwamba kuna harufu mbaya ya uvundo wa ufisadi katika usimamizi wa fedha za mifuko ya hifadhi ya jamii. Mahali pa kuanzia juu ya uvundo huu ni Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Kwa mujibu wa Ripoti hiyo, *"ukaguzi umegundua kwamba Bodi ya Zabuni ya … NSSF iliidhinisha na kumpa mkataba wa kununua vipooza hewa katika nyumba za biashara za NSSF zilizopo Kaloleni katika Manispaa ya Arusha kwa muuzaji ambaye bei yake ilikuwa shilingi milioni 430. Bei waliyokubaliana ni kubwa kwa shilingi milioni 230 zaidi ya makadirio ya wahandisi…. Katika maelezo yaliyotolewa na menejimenti ni kwamba makisio haya yalikuwa ni ya mwaka 2009 na hivyo yalikuwa yameshaathiriwa na mfumuko wa bei. Hata hivyo sababu hii haikutosheleza kuelezea sababu za kupanda kwa gharama kwa zaidi ya asilimia 87 kama ilivyoelezwa kwenye dokezo la kamati ya tathmini waliyoituma kwenye Bodi ya Zabuni ya tarehe 29/02/2012. Katika hali ya kawaida tofauti inayokubalika na makisio ya mhandisi yanatakiwa yawe kati ya 10%."*

Sio kwenye manunuzi peke yake ndio penye uvundo wa ufisadi dani ya NSSF. Hata katika kulipa mafao kwa wanachama wake kuna matatizo. Hivyo, kwa mfano, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu anaelezea jinsi ambavyo NSSF imekiuka Waraka wa Serikali wa mwaka 2009 unaotaka watumishi wa mikataba kulipwa kiinua mgongo baada ya mkataba na wasilipwe mafao ya pensheni kama watumishi wa ajira za kudumu. Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inasema kwamba katika ukaguzi wake wa NSSF *"ilibainika kuwa Mfuko ulikiuka waraka huo wa serikali na kuwalipa shilingi milioni 13.062 watumishi wa ajira ya kudumu kama malipo ya mkataba (gratuity) ambapo wafanyakazi wa pensheni wanatakiwa kulipwa mafao ya kiinua mgongo peke yake. Kukiukwa huku kwa waraka huo wa serikali kumeliingiza shirika kwenye matumizi yasiyokuwa ya lazima na yasiyoleta tija kwa Shirika."*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka majibu ya kina kutoka kwa Waziri ambaye ndiye msimamizi wa mfuko wa taifa wa Hifadhi ya Jamii na Serikali itoe kauli rasmi Bungeni ikiwa inapingana na kauli na ripoti ya CAG kuhusu hali ya mifuko hii na kama pia inapingana na kauli yake kuwa mifuko hii ipo hatarini kufilisika.

3.1 PENSHENI KWA WAZEE NCHINI.

Mheshimiwa Spika, Wazee nchini wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokupata matibabu bure,kuwa walezi wa watoto yatima,kupoteza mali zao na haki ya kurithi,kuuwawa kwa imani za kishirikina ikiwemo wazee

2,866 waliuwawa katika mikoa 10 kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita sawa na wastani wa wazee 573 kila mwaka au takribani mzee mmoja anauwawa kila siku.Tumeendelea kushuhudia wazee wa nchi hii ndani ya uongozi wa chama cha mapinduzi wakiendelea kupuuzwa,kunyanayasika na kudharauliwa huku wakijisahau kuwa na wao pia ni wazee watarajiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa sensa ya Watu na Makazi, 2012 wazee nchini ni milioni 2,507,568 sawa na asilimia 5.6 ya idadi yote ya watanzania. Ongezeko la wazee nchini na duniani ni jambo lisilowezwa kupuuzwa tena kwani mtu mmoja katika watu tisa ni mzee,hata hivyo idadi hii inategemewa kuongezeka hadi kufikia mzee mmoja katika watu watano ifikapo 2050.

Katika hotuba zetu za miaka mitatu mfululizo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tumeendelea kusisitiza umuhimu wa wazee kupewa pensheni, na Serikali imekua ikitoa kauli kuwa utoaji wa pensheni kwa wazee unafanyiwa utafiti ama uko katika hatua za mwisho. Aidha, kauli za Serikali kuwa wazee wapatiwe matibabu bure imekua ni change la macho kwa kuwa wazee wengi wamepata usumbufu katika kupata huduma za afya na wengine wameshindwa kabisa kupata huduma hizo. Kwa kuwa kauli ya kuwapa wazee pensheni ilitumiwa na CCM katika uchaguzi, tunaitaka Serikali kutoa kauli katika Bunge lako tukufu kuwa je, pensheni kwa wazee inatekelezeka au haitekelezeki? Na kama inatekelezeka ni lini itakelezwa?

4.0 HAKI, SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA KAZI

4.1 MAZINGIRA YA KAZI KWA WATU WENYE ULEMAVU

Mheshimiwa Spika, hali ya wanawake na wanaume walemavu kwenye soko la ajira linatia hofu na mashaka makubwa kwani wana fursa ndogo zaidi ya kuajiriwa kuliko wasio walemavu na hata wakiajiriwa wengi wao huwekwa katika sekta ambazo malipo yake ni haba. Kwa muda mrefu, tumekua tukisema kwa sauti kubwa kuhusu nafasi ya watu wenye ulemavu katika mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Spika, ingawa Tanzania inasisitiza haki kwa walemavu, dhamira hiyo inatekelezwa kwa nadharia tu.Tafiti zinaonyesha kuwa, watu wenye ulemavu walioajiriwa katika ajira rasmi ni kidogo sana kulinganisha na wasio na ulemavu. Mwaka 2012 ulifanyika utafiti chini ya programu ya utetezi wa ajira na kuonyesha kuwa idadi ya watu wenye ulemavu walioko katika ajira rasmi inapungua badala ya kuongezeka. Utafiti huo uliofanyika chini ya Hospitali ya CCBRT kwa kushirikiana na wadau wengine, ulibaini kuwa walemavu 86 tu, sawa na asilimia 0.4, wameajiriwa katika kampuni 72 za sekta binafsi. Idadi hiyo ni ndogo sana kulinganisha na jumla ya wafanyakazi 20,568 wasiokuwa na ulemavu walioajiriwa katika kampuni hizo 72.

Aidha, Taasisi 10 za sekta ya afya, yenye jumla ya wafanyakazi 738, wenye ulemavu walioajiriwa ni 17 tu, sawa na asilimia 2.3, na pia hakuna mwenye ulemavu ambaye ni mkuu wa idara, kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo. Baadhi ya idara za sekta hizo, hazina kabisa wafanyakazi wenye ulemavu, hali hiyo inasababisha dhana ya haki ya ajira kwa walemavu kutotekelezwa kwa vitendo. Vilevile, maeneo mengi ya kazi hayana mazingira rafiki kwa ajili ya huduma za watu wenye ulemavu hivyo kuwaletea shida za kiutendaji na kisaikolojia watu hawa ambao ni kundi la muhimu katika ustawi wa taifa lolote lile.

Mheshimiwa Spika, kambi rasmi ya Upinzani inaendelea kuwa mtetezi wa haki za walemavu katika masuala ya ajira kwa kuwa watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii yetu na wana haki sawa na watu wote. Tunaitaka wizara, itupe takwimu za watu wenye ulemavu ambao wameajiriwa katika sekta binafsi na umma ili kuweza kuwapa motisha na morali watu wenye ulemavu wa kuomba nafasi za kazi zinazotangazwa na kuachana na hofu kuwa hawana nafasi katika jamii yetu iliyostaharabika. Vilevile, Wizara ituambie ni kwa kiasi gani imechukua hatua kuhakikisha kuwa waajiri wanatakeleza Sheria na Kanuni za kazi katika kuzisimamia haki za msingi za watu wenye ulemavu? Tunasisitiza uwepo wa dhamira njema juu ya haki kwa wenye ulemavu itakayotekelezwa kwa vitendo, pamoja na nia ya dhati ya kuhakikisha kuwa watendaji mbalimbali wa sekta ya umma, sekta binafsi na asasi nyingine za hiari zinafuata sheria na taratibu za kimataifa za haki za walemavu.

4.2 WAKALA BINAFSI WA AJIRA NCHINI

Mheshimiwa Spika, wakati wa maadhimisho ya Mei Mosi ya mwaka huu wa 2014 Rais Jakaya Kikwete alipongeza hatua ya Wizara kufuta mfumo mpya ulioanzishwa wa makampuni kuajiri kwa kupitia wakala wa aira na kuunga mkono hatua ya wizara kupiga marufuku utaratibu unaofanywa na baadhi ya wakala binafsi wa ajira wa kukodisha wafanyakazi katika makampuni kinyume na Sheria ya Huduma za Ajira Na. 9 ya mwaka 1999 inayoelekeza kuwa majukumu ya wakala binafsi ni kuunganisha watafuta kazi na si kuwa waajiri wa watafuta ajira.

Mheshimiwa Spika, athari za wakala wa ajira kuwa waajiri wa watafuta kazi ni pamoja na kuwakosesha wafanyakazi haki zao za msingi ikiwemo likizo, huduma za matibabu, huduma za hifadhi za jamii pamoja na kuwanyima mishahara yao wanayostahili. Kitendo cha Raisi kupongeza hatua hii ya wizara, kunaonesha kuwa kuna tatizo kubwa ambalo kwa muda mrefu Wizara ya kazi na ajira imeshindwa kusimamia misingi na matakwa ya haki ya Sheria ambazo Bunge lako tukufu imezitunga.

Mheshimiwa Spika, k makampuni haya kufanya kazi kwa muda mrefu bila kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria, ni dhahiri kuwa Serikali ya CCM imeshindwa. Kwa mujibu wa taarifa ya waziri wa Kazi na Ajira Mhe. Gaudentia Kabaka aliyoitoa jijini Dar Es Salaam, Januari mwaka huu, Mhe. Waziri aliitaja kampuni ya Erolink kama mojawapo ya wakala wa ajira ambao wameikosesha Serikali mapato ya takribani shilingi Bilioni tatu kwa miaka mitatu. Kwa miaka mitatu, wakala wa huduma za ajira wanafanya kazi bila kuratibiwa na wizara, hii ni aibu kubwa kwa Serikali inayojigamba kuwa ni Serikali makini.

Mheshimiwa Spika, Baadhi ya makampuni yanayokodisha wafanyakazi yamefanyiwa uhakiki na TRA na kubainika kukwepa kodi ya mapato ya ajira (PAYE) na kodi ya mapato ya kampuni kinyume na Kifungu cha 7 cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 [Sura 332 kama ilivyorejewa Mwaka 2008]. Aidha, kwa mujibu wa Kamishna wa Kazi wa Wizara ya Kazi na Ajira, Saul Kinemela mara baada ya kutolewa kwa tamko la kupiga marufuku uwakala wa ajira, makampuni 56 yalituma maombi ya kupewa vibali vya kufanya kazi za uwakala kwa Wizara. Hii inaonesha kuwa Serikali ya CCM kwa muda mrefu ilishindwa kuratibu na kusimamia makampuni ya uwakala na hivyo kusababisha uminywaji wa haki za wafanyakazi waliopitia katika makampuni hayo. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara kulieleza Bunge lako tukufu imechukua hatua gani kwa waajiri ambao wamebainika kutumia mfumo huu ili kukwepa kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria? Je, makampuni mangapi mpaka sasa yameshapata usajili na makampuni mangapi yamenyimwa usajili wa kutoa huduma za ajira na mangapi yamechukuliwa hatua za kisheria?

Aidha, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kujua pamoja na kuwa mawakala hawa wataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria, je ni kwanini wizara ya Kazi na Ajira nayo isiwajibike kwa kushindwa kufuatilia mawakala hawa kwa miaka mitatu na kuisababishia Serikali hasara? Kwa kauli ya Waziri Kabaka ya kuzuia mawakala hawa huku Serikali yake ya CCM ikilisababishia taifa hasara ni dhahiri kuwa CCM wanakumbuka shuka kumekucha!

4.3 MIGOGORO YA WAFANYAKAZI NA WAAJIRI

Mheshimiwa Spika; Wizara ya Kazi na Ajira na taasisi zake zina wajibu wa kushughulikia matatizo ya wafanyakazi na kusimamia Sheria za Kazi na ajira katika makampuni na maeneo mbalimbali. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Waziri wa Kazi na Ajira kutoa maelezo ya sababu ya Wizara na Taasisi zake kushindwa kuwezesha ufumbuzi wa mgogoro wa wafanyakazi na mwajiri wao katika Kampuni ya Starbag pamoja na madai ya ukiukwaji wa Sheria za Kazi na Ajira katika kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika; Wizara ya Kazi na Ajira izingatie kwamba mgogoro huu umekuwepo kwa muda mrefu na Wizara ina taarifa kuhusu migomo iliyojitokeza

mwaka 2013 na migomo mingine iliyojirudia mwaka 2014 ambayo ina athari kwa maendeleo ya mradi.

Mheshimiwa Spika; Wafanyakazi wameeleza malalamiko dhidi ya mwajiri wao kampuni ya Strabag kuhusu uonevu wa wafanyakazi na ukiukwaji wa sheria na kutaka majibu na mamlaka mbalimbali kuingilia kati hata hivyo ufumbuzi endelevu haujapatikana mpaka hivi sasa. Wafanyakazi wanalalamikia unyanyasaji uliokithiri mahala pa kazi, kufukuzwa kazi wakiugua au wakiumia kazini bila kufuata utaratibu. Wafanyakazi wametoa mwito kwa mamlaka husika kufika na kuchukua vielelezo kuhusu madai yao.

Mheshimiwa Spika; Tangu kauli ya Mhe. Rais Jakaya Kikwete na Serikali ya mwaka 2013 ya nyongeza ya mshahara wa kima cha chini, Strabag kwa ujumla inatajwa kukaidi kutoa nyongeza huku baadhi ya viongozi wake wageni wakitoa kauli za kejeli kwa wafanyakazi kila wanapodai haki yao. Kilichofanywa na Starbag kutaka kujitetea kuwa wamepandisha mishahara ni nyongeza dogo kwa waliokuwa wakilipwa chini ya laki tatu na ishirini lakini wakati huo huo posho (allowances) zote kwa wafanyakazi wazalendo ziliondolewa hali ambayo ilifanya nyongeza hiyo isilete mabadiliko ya msingi katika maisha ya wafanyakazi. Aidha, wafanyakazi wengine wazalendo hawakupata nyongeza yoyote lakini wakati huo huo nao posho (allowances) zao ziliondolewa.

Mheshimiwa Spika; Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa kutoka kwa wafanyakazi kwamba zipo nafasi za kada ambazo kisheria haipaswi kuajiri wageni zimejazwa na wageni. Wafanyakazi wametueleza kwamba hata ilipofanyika Operesheni Kimbunga ya kuondoa wahamiaji haramu au kaguzi nyingine zinazofanyika za kufuatilia wanaofanya kazi kinyume cha sheria waliopo kwenye Kampuni ya Starbag hawajaguswa. Wafanyakazi wanayo mifano ya watu hao kwa majina na nafasi zao kuwa ni: Store ameajiriwa Ivan (mgeni), data entry wa store Tariq (mgeni),data entry wa site agent Faisal (mgeni), workshop Peter kirchtiger (mgeni), Accountant Jennifer (mgeni), Payrol Mr Maruki (mgeni). Wafanyakazi hawa wageni katika nafasi ambazo zingeweza kabisa kushikwa na wazawa wanapewa mishahara mikubwa zaidi, posho mbalimbali na usafiri tofauti na watanzania wanaofanya kazi katika kada hizo hizo.

Mheshimiwa Spika, huku kukiwa na malalamiko mengi juu ya Starbag kampuni hiyo imepewa kandarasi nyingine mkoani Arusha. Ifahamike kwamba palikuwa na mgomo mwingine wa wafanyakazi wa kampuni hiyo mwaka huu wa 2014. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Bunge lifahamu kwamba kurudi kwa wafanyakazi hao kazini hakutokani na madai yao ya msingi kushughulikiwa bali vitisho vya muajiri kuwafukuza kazi wote. Wafanyakazi wamefanya hivyo kwa kuzingatia kwamba katika mgomo wa Agosti 2013 mwajiri alitoa vitisho kama

hivyo na hatimaye alimfukuza Katibu wa Chama cha Wafanyakazi katika Kampuni huku wafanyakazi wenzake wakieleza kwamba alifukuzwa kinyume na taratibu. Aidha, Wafanyakazi wameeleza kwamba Mwanasheria wa Kampuni hiyo ambaye hapo kabla amekuwa Serikalini amekuwa akiwaeleza kwamba kampuni itatumia kesi za mahakamani kuchelewesha haki za wafanyakazi mpaka mradi utakapokamilika.

Mheshimiwa Spika; Haya yanatokea huku ofisi za Starbag ikiwa karibu na ofisi za vyombo vingine vinavyosimamia masuala ya wafanyakazi na mamlaka nyingine za kiserikali zenye wajibu wa kufuatilia kuhakikisha masharti ya mikataba ya ujenzi katika mradi huo yanazingatiwa. Mambo hayo yanaendelea pamoja na kuwa kumekuwepo na migomo ya wafanyakazi kuanzia mwezi Agosti 2013 kwa nyakati mbalimbali ambayo tunaamini kwamba Wizara ya Kazi na Ajira inayo taarifa hivyo Waziri anapaswa kutoa majibu bungeni ni hatua gani ambazo amechukua mpaka sasa kwa upande wake kwa kushirikiana na Mawaziri wenzake wenye dhamana.

4.4 FIDIA KWA WAFANYAKAZI

Mheshimiwa spika, mwaka 2008 bunge lako tukufu lilitunga sheria ya fidia ya wafanyakazi (workers comensation act). malengo ya sheria hii yalikua ni pamoja na kuweka utaratibu wa kulipa fidia fanyakazi kulipwa fidia wanapopata ajali na kukumbwa na majanga wakiwa kazini.aaisha sheria inalenga kuunda mfuko wa fidia kwa wafanyakazi ambao utachangiwa na waajiri wote wa sekta za umma na sekta binafsi. Majukumu ya mfuko huo ni kutathmini na kuboresha viwango vya fidia vinavyotakiwa kulipwa kwa fanyakazi wanaoumia, kupata magonjwa, kupata madhara ya kiafya au kufariki wakiwa kazini.

Mheshimiwa spika, katiba hotuba yake kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 , waziri aliliambia bunge lako tukufu kwamba "maandalizi ya kuanzisha mfuko huu yamekamilika...." Aidha waziri aliliambia bunge lako tukufu kwamba kanuni za utekelezaji wa sheria hiyo zilikwisha kupitishwa.Na licha ya kauli ya waziri hadi leo hii mfuko wa fidia ya wafanyakazi haujaanzishwa. Hii inathibitishwa na maelezo ya waziri juu ya utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa mwaka 2013/2014 ambako waziri amerudia kauli yake ya mwaka 2011 kwamba taratibu za kuanzisha mfuko zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Serikali ya hii ya CCM ya kutotekelezwa kwa matakwa ya Sheria hii ya Fidia kwa wafanyakazi toka mwaka 2008 ni kwamba wafanyakazi wa Tanzania wanaoumia, kupata ajali, kupata madhara ya kiafya au kufariki wakiwa kazini wameendelea kulipwa fidia kwa utaratibu uliowekwa kwenye shria ya fidia kwa wafanyakazi (Workmens Compensation Ordinance) iliyotungwa na dola la kikoloni katika miaka ya mwanzo ya 50. Sheria hiyo iliweka kiwango cha juu cha fidia kwa mfanyakazi anayeumia aukufariki a kiwa

kazini kuwa ni sh. 108,000. Ndio maana kwa mujibu wa taarifa ya kituo cha sheria na msaada wa haki za binaadamu ya mwaka 2013ndugu akida athman aliyekua mfanyakazi wa mamlaka ya bandari Tanznai amjini Tanga na liyepata madhara ya kupofuka akiwa kazini alilipwa sh. 108000 kama fidia. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inaitaka Serikali hii sikivu ya CCM ilieleze Bunge lako tukufu wafanyakazi wa Tanzania wataendelea kudhulumiwa haki zao kama bwana Akida Athman mpaka lini?

4.5 KODI YA PATO LA MSHAHARA (PAY AS YOU EARN)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utaratibu uliopo sasa ya kodi ya mapato ya wafanyakazi ni kati ya asilimia14.5 na 35 ya mshahara wa mfanyakazi. Kwa mujibu wa CAG katika mwaka huu wa fedha, mamlaka ya kodi ta Tanzania imekusanya kodi kutoka kwa wafanyakazi jumla ya trilioni 1.5. Aidha, mdhibiti na mkaguzi mkuu wa serikali anaonesha kwamba katika kipindi hicho, serikali ilitoa msamaha kwa walipa kodi wakubwa na makampuni ya nje liliyofikiwa kiasi cha shilingi trilioni 1.5 sawa na kodi iliyokusanywa na Serikali kutoka kwa wafanyakazi. Misamaha hiyo ya kodi ni sawa asilimia 3.1 ya pato la taifa kwa mwaka huu. Hii ina maana kwamba kama Serikali isingetoa misamaha hiyo ya kodi, mapato ya serikali kutokana na kodi ya walipa kodi wakubwa yangeongezeka maradufu.

Mheshimiwa spika, kutokana na ukuaji mbaya wa uchumi, ongezeko la mfumuko wa bei pamoja na kupanda kwa gharama za maisha, kodi ya mapato ya wafanyakazi imekuwa mzigo mkubwa na maumivu kwa wafanyakazi wa Tanzania waliopo katika ajira rasmi. Katika maoni yake ya mwaka jana, Kambi rasmi ya Upinzani, ilipendekeza kwamba viwango vya kodi ya mapato ya wafanyakazi vipunguzwe kufikia asilimia 9 hadi 27. Pendekezo hili bado lina nguvu leo. Na kwa takwimu za misamaha ya kodi zilizotolewa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa serikali kuna uwezekano wa pendekezo hili kutekelezwa bila kuathiri mapato ya serikali endapo serikali itapunguza au kufuta misamaha ya kodi kwa walipa kodi wakubwa na makampuni ya nje. Kambi rasmi ya upinzani bungeni inataka kujua kwa nini serikali ya CCM inaendelea kuwabebesha watanzania mzigo mkubwa wa kodi wakati ikitoa misamaha ya kodi kwa makampuni makubwa matajiri ya nje na walipa kodi?

4.6 ONGEZEKO LA MSHAHARA

Mheshimiwa Spika, Kwa muda mrefu Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) limependekeza shilingi 315,000 kama kima cha chini cha mshahara kwa sekta zote. Hata hivyo, tarehe 07 Februari 2014 katibu mkuu wa TUCTA, Nicholaus Mgaya aliwaambia mkutano wa viongozi wa shirikisho hilo kwamba kiwango cha chini cha mshahara ambacho TUCTA imekipendekeza

kwa miaka ya nyuma kimepitwa na wakati. kwa mujibu wa Bwana Mgaya kima cha chini cha mshahara kinachoweza kukidhi mahitaji halisi ya wafanyakazi kutoka na hali haliis ya kupanda kwa gharam za maisha kwa sasa ni shilingi 720,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, mara kwa mara wakati wa sherehe za Mei Mosi za kila mwaka, Rais Kikwete ametoa ahadi za kuongeza kima cha chini cha mishahara ya wafanyakazi wa sekta binafsi. Hata hivyo, takwimu za serikali zinaonyesha kwamba mishahara ya wafanyakazi wa sekta binafsi bado ni ya chini sana. Hivyo, kwa mfano, taarifa zilizoko kwenye website ya Wizara zinaonyesha kwamba kima cha chini cha mishahara kwa sekta binafsi kilichowekwa na serikali hii ya CCM katika kipindi cha kati ya mwaka 2013 ni kati ya shilingi 40,000 hadi shilingi laki nne kutegemeana na sekta au aina ya ajira. Kiwango hiki cha mishahara ni dogo mno kwa kulinganisha na ughali wa maisha kwa sasa na kiko chini ya kima kilichopendekezwa na TUCTA tangu mwaka 2006. Ni wazi, kwa hiyo, kwamba serikali hii ya CCM haina mpango wowote wa kuwawezesha wafanyakazi wa sekta binafsi kupata mishahara itakayoendana na hali halisi ya gharama za maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa watumishi wa umma, katika sherehe za Mei Mosi za mwaka 2011, Rais Kikwete alitangaza kuwa serikali yake imeongeza kima cha chini kwa watumishi wa umma kutoka shilingi 65,000 hadi shilingi 135,000 kwa mwezi kati ya mwaka 2006 na 2010. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 38.5 ya mapendekezo ya vyama vya wafanyakazi kwa kipindi hicho hicho. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na gazeti la Mwananchi la tarehe 27 Julai, 2013, kima cha chini cha mishahara ya watumishi wa serikali kuu na serikali za mitaa sasa kimepanda hadi shilingi 240,000 kwa mwezi. Hata hivyo, ongezeko hili nalo halikidhi mahitaji halisi ya wafanyakazi wa Tanzania kwa kuzingatia kupanda kwa gharama za maisha. Kwa vyovyote vile, ongezeko hili liko chini ya mapendekezo ya TUCTA ya tangu mwaka 2006 na hata ya mwaka huu. Ni wazi vile vile kwamba serikali hii haina mpango wowote wa kuwapatia watumishi wa umma wa ngazi za chini kipato kitakachowawezesha kukabiliana na kupanda kwa gharama za maisha yao.

4.7 UDHIBITI NA UKAGUZI WA VIBALI VYA AJIRA ZA WAGENI

Mheshimiwa Spika, kumekua na malalamiko ya muda mrefu juu ya baadhi ya raia wa kigeni kuwepo nchini bila ya vibali vya kazi. Vilevile, wizara ya kazi haijaweka wazi mikakati yake kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 juu ya ukaguzi wa vibali kwa ajira za kigeni katika maeneo ya kazi. Pamoja na taarifa kuwa, kuna watu wengi nchini ambao wamejiriwa katika mahoteli makubwa, migodi, makampuni makubwa, shule za watu binafsi, saluni na migahawa mikubwa nchini ambao hawana vibali vya kufanyia kazi nchini, Serikali haijaonesha kwa vitendo ari yake katika kukabiliana na changamoto hii na ndio

maana mpaka sasa, Serikali inapoteza mapato kwa kushindwa kukusanya fedha za vibali vya wageni nchini. Ni jukumu la wizara ya kazi na ajira kuhakikisha kuwa kaguzi za mara kwa mara zinafanyika ili kuwanasa wale wote ambao wanafanya kazi nchini kinyume cha taratibu.

Mheshimiwa Spika, aidha, kumekua na mazoea ya baadhi ya makampuni ya kigeni ambayo yamewekeza nchini kutofuata sheria na taratibu za kazi hasa katika kuweka uwiano wa ajira baina ya raia wa kigeni na wazawa. Na pengine hii inatokana na kauli za baadhi ya viongozi wa Serikali za kuwabeza wazawa ndizo zinazowapa jeuri wawekezaji nchini katika kutoa nafasi za ajira kwa kigezo kuwa watanzania hawana uwezo, ujuzi na taaluma za kushika nafasi hizo. Kauli za Waziri wa Nishati na Madini ambazo amekua akizirudia mara kwa mara kuwa watanzania hawana uwezo wa kuwekeza kwenye nishati na gesi, imekua ni mtaji kwa makampuni ya uwekezaji katika kuwanyima Watanzania fursa za ajira katika makampuni yao nchini.

Mheshimiwa Spika, hata vivyo kumekua na malalamiko kuwa baadhi ya makampuni ya Kigeni yanayofanya shughuli zake nchini yamekua yakitoa nafasi za juu na zenye staha kwa raia wa nje ambazo hata wazawa wanaweza kuzifanya. Kwa mujibu wa taarifa ya kituo cha Sheria na Haki za Binaadamu kwa mwaka 2013, makampuni ya Strabag (inayojihusha na ujenzi wa Barabara mkoani Dar Es Salaam) asilimia 47 ya ngazi za juu za utawala zilikuwa zikishikiliwa na raia wa kigeni hata kwa nafasi ambazo watanzania wanaweza kufanya. Vilevile katika kiwanda cha Sukari cha Mtibwa kinachomilikiwa na wahindi, kimejaa wafanyakazi wa kigeni ambao wanawanyima fursa pia watanzania wenye uwezo wa kufanya kazi katika nafasi hizo.

5.0 TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

5.1 TUME YA USULUHISHI NA UAMUZI (CMA)

Mheshimiwa Spika, Lengo kuu la kuanzishwa Tume hii ya Uamuzi na Usuluhisi ilikuwa ni kuondoa urasimu uliokuwepo wa rufaa za wafanyakazi kwenda kwa Waziri jambo ambalo lilikuwa linachukua mda mrefu sana na haki kucheleweshwa.

Mheshimiwa Spika, Tume hii inawajibika kutatua migogoro sehemu za kazi kwa ufanisi, usawa na kwa haraka. Hatahivyo kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Kazi na Ajira migogoro 4,620 ilipokelewa na kusajiliwa hadi tarehe 31 Machi, 2014. Migogoro 2,159 ilishughulikiwa na kumalizika sawa na asilimia 46.7 hatahivyo migogoro 1,341 ilisuluhishwa sawa na asilimia 62.1 na migogoro 818 ilitolewa uamuzi sawa na asilimia 37.9.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa hiyo ya wizara, tume hii imefanya kazi ya kusuluhisha na kutoa maamuzi kwa kiwango cha chini ya asilimia 50, jambo linaloashiria kuwa migogoro ya kazi ambayo inahitaji kutolewa maamuzi na kusuluhishwa huchukua muda mrefu hivyo malalamiko mendi dhidi ya tume yamegusia kuwa kesi nyingi huchukua muda mrefu na kuahirishwa mara kwa mara jambo linalopelekea kuwakatisha tamaa walalamikaji kwakuwa wahusika hutumia muda na fedha nyingi kwa katika kufuatilia mashauri husika. Aidha, Tume imelalamikiwa katika utoaji wa haki sawa baina ya mwajiri na mfanyakazi au baina ya wafanyakazi na vyama vyao,hii ni kutokana na waajiri wengi kuwa na nguvu ya kifedha na kuwatumia wanasheria katika hatua za usuluhishi jambo ambalo limeendelea kuwakandamiza wafanyakazi walio wengi ambao hawana uelewa wa masuala ya sheria hivyo haki zao kupotea.

Mheshimiwa Spika, Kambi rasmi ya upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuiwezesha Tume hii kwa kutenga bajeti ya kutosha, kuhakikisha uwepo wa rasilimali watu wa kutosha ili kuhakikisha maamuzi na usuluhishi unafanyika kwa haraka bila kucheleweshwa. Vilevile, tunaitaka Tume kuzingatia weledi katika kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua maafisa ambao hawazingatii taratibu za kazi na kutoa haki kwa haraka pale inapostahili kwani "*Haki iliyocheleweshwa ni Haki iliyonyimwa*".

5.2 WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALA PA KAZI (OSHA)

Mheshimiwa Spika, Wajibu Mkuu wa OSHA chini ya Wizara ya Kazi ni kuhakikisha uwepo wa usalama na afya maeneo ya kazi kwa kusimamia na kuhakikisha Sheria za kazi na kanuni zake mahala pa kazi zinazingatiwa na waajiri maeneo yote ya kazi. OSHA inawajibika kufanya usajili na kutunza kitabu cha usajili katika maeneo ya kazi, kufanya ukaguzi wa maeneo ya kazi,kufanya ukaguzi wa afya na usalama kazini, kuendesha mafunzo kuhusu afya na usalama maeneo ya kazi, kufanya uchunguzi wa ajali na majanga kazini, kuhakikisha kuwa usalama wa afya kazini unazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya kazi hapa nchini yanakidiriwa kufikia 27,500 kwa takwimu za mwaka 2012, hata hivyo OSHA imefanikiwa kusajili maeneo ya kazi yapatayo 6,599 sawa na asilimia 24 hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Januari 2013. Sababu kuu zinazopelekea usajili huu kufanyika kwa kiwango kidogo ni pamoja na kutokuwepo kwa malengo ya wazi ya usajili katika maeneo ya kazi,udhaifu katika kutoa adhabu kwa waajiri ambao hawajafanya usajili maeneo ya kazi, kukosekana kwa mipango madhubuti ya kutoa elimu kwa umma juu ya usajili wa maeneo ya kazi nchini,fedha kidogo zinazotengwa kwa kazi za usajili wa maeneo ya kazi na kukosekana kwa uratibu kati ya wadau wakuu wa OSHA kama Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Brela, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na Ofisi ya Takwimu ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa OSHA inatekeleza majukumu yake na kuhakikisha waajiri wanatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria na kanuni za usalama na afya maeneo ya kazi na pia tunapendekeza OSHA kujikita katika sekta isiyo rasmi ili kuhakikisha usalama na afya ya watanzania vinalindwa. Vilevile, tunaitaka Serikali kutenga fungu la kutosha li kuiwezesha OSHA kutimiza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

5.3 SHIRIKA LA TIJA LA TAIFA (NIP)

Mheshimiwa Spika, Shirika la Tija la Taifa (NIP) ni chombo muhimu kinachoweza kulisaidia Taifa katika kuhakisha shughuli zinafanyika kwa tija ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika ya Umma Na. 17 ya mwaka 1969.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza umuhimu wa Serikali kuliwezesha Shirika hili vizuri kiuwezo na kiundeshaji ili liweze kuandaa na kufanya kazi zake kwa ufanisi. Kw kuwa kwa miaka 20, huduma za Shirika zimekua zikichukua sura ya biashara zaidi kuliko kuchangia mikakati ya Serikali kutokana na kujiendesha lenyewe. Hii imepelekea kuingia katika soko na kushindana na taasisi nyengine za umma kama vyuo vikuu, chuo cha utumishi wa umma na makampuni binafsi ya ushauri ili kupata fedha za kujiendesha lenyewe. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliwezesha Shirika hili kwa kutoa ruzuku ili liweze kuajiri wataalmu wa kutosha na kutekeleza majukumu yake kutokana na Sheria iliyoianzsihwa. Kwa mfano, Mashirika/Taasisi za tija ulimwenguni hupata ruzuku kutoka Serikali zao lakini Shirika hili halipati ruzuku kutoka Serikalini kunakosababisha ushindani kuwa mkubwa ukilinganisha na taasisi binafsi.

Aidha, tunajiuliza ni nini dhamira ya Serikali kuliacha Shirika hili likifanya kazi bila kuwepo na Bodi kwa muda wa miaka 3 sasa tangu Machi 2011? Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuteua mara moja Bodi ya Wakurugenzi haraka iwezekanavyo ili masuala ya msingi yapate kuamuliwa na kutekelezwa. Vilevile, tunaitaka Serikali iandae sera ya taifa ya Tija na Ushindani itakayosimamia utekelezaji wa majukumu ya Shirika.

5.4 WAKALA WA HUDUMA ZA AJIRA TANZANIA (TaESA)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania ni chombo muhimu sana katika ustawi wa watafuta ajira nchini. Chombo hiki kimekuwa kikiwezeshwa na Serikali kila mwaka tangu kuanzishwa kwake ili kufanya kazi kwa ufanisi na tija. Lakini tangu kuanzishwa kwake TaESA kumekuwa na malalamiko juu ya upatikanaji wa nafasi za kazi na uwazi wa taasisi hii kwa

watafuta ajira. Lakini ni dhahiri kuwa chombo hiki hakijawezeshwa ipasavyo na hivyo kukumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo kutokuwa na rasilimali za kutosha kuiwezesha kufikia malengo ya wakala, watafuta kazi wengi kuwa na matarajio makubwa kuliko hali halisi ya soko la ajira, pia baadhi ya waajiri na watafuta kazi kutotumia huduma za wakala nchini. Aidha, changamoto kubwa kuliko zote ni pamoja na wahitimu na watafuta ajira kuwa ni wengi kulinganisha na nafasi za kazi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuiwezesha taasisi hii ili iweze kukabiliana na mahitaji ya soko la ajira pamoja na kupanua wigo wa huduma za ajira katika mikoa mbalimbali nchini na kukabiliana na changamoto tulizoziorodhesha awali.

6.0 MAPITIO YA BAJETI YA WIZARAKWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mheshimiwa Spika, Mwaka wa fedha 2013/14 Serikali ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 13.034 kwa wizara ya kazi fungu 65 kama matumizi ya kawaida, lakini hadi April 30, Serikali ilikuwa imetoa jumla ya shilingi bilioni 13.034 kama matumizi ya kawaida, lakini hadi hadi April, 30 zilikuwa zimetumika jumla ya shilingi bilioni 7.108 ambazo n sawa na asilimia 55 tu. Aidha, kwa Tume ya Usuluhishi (fungu 15) iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 2.275, kati ya hizo shilingi bilioni 1.35 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Lakini hadi tarehe 30 April, 2014 jumla ya shilingi bilioni 1.19 sawa na asilimia 52.2 ya maombi yote ya Tume zilikuwa zimetolewa.
Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Wizara fungu 65 imepanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 15.28 kama fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3 ikiwa ni fedha za ndani ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, kwa fungu 15 imetengewa jumla ya shilingi bilioni 5.29 kati ya hizo matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 2.85.

Mheshimiwa Spika, Ukiangalia bajeti ya Tume kwa mwaka huu imeongezeka karibu ni mara mbili ya mwaka jana. Kambi Rasmi inataka kuelewa ni mogogoro mingapi ya kazi imetatuliwa kwa mwaka wa fedha uliomalizika na hivyo, kutokana na kazi nzuri ya Tume imeongezewa fedha. Mwaka 2013/14 OC ilikuwa ni shilingi bilioni 1.35 na mwaka huu wa fedha 2014/15 imekuwa ni shilingi bilioni 2.85. Hali halisi ni kwamba kuna malalamiko mengi sana kuwa Tume inashindwa kutatua migogoro badala yake inakuwa upande wa wale wanaolalamikiwa.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha Nelson Mandela tarehe 21 Septemba 1953 katika hotuba yake ya ‘ No Easy Walk to Freedom’ alisema,

"Hatari na magumu havijawahi kutuzuia katika harakati zetu huko nyuma, na havitaweza kutuzuia hata sasa. Lakini ni lazima tujiandae vilivyo kukabiliana navyo hata sasa kama wafanyavyo walio katika biashara ambao hawapotezi nguvu katika maneno matupu au matendo yasiyotekelezeka. Njia ya kujiandaa (katika matendo) vimejikita katika mizizi yetu ya kukataa uonevu na kukosekana kwa nidhamu katika taasisi zetu ambazo tunazisimamia katika kuleta mwanga na ubora kuelekea katika mafanikio ya uhuru."

Kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha.

……..
Cecilia Daniel Paresso (MB)
Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni
Wizara ya Kazi na Ajira
24.05.2014

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa nitatangaza wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali, Watendaji Wakuu, Makamishna, Mameneja, Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Maafisa Waandamizi wa Wizara ya Kazi na Ajira, wakiongozwa na Ndg. Erick Shitindi, Katibu Mkuu wa Wizara. Karibuni. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Dkt. Ramadhani Dau, Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF*. Karibu. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, ambao ni Wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha St. John's na Wanafunzi 20 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Pindi Chana, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, kutoka *Girls Guide* wakiongozwa na Ndg. Siamo Mohammed Mdhamini.

Wageni wa Mheshimiwa Meshack Opulukwa, ambao ni Ndg. Geofrey Mitanda, Mwenyekiti wa BAVICHA Jimbo la Meatu na Ndg. Peter Lyimo, Kamanda wa Chama, Meatu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 63 kutoka Chuo cha Mipango Dodoma. Karibuni Dodoma.

Wanafunzi 21 kutoka Chuo cha Biashara *(CBE)* Dodoma, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wanafunzi 50 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi Zuzu, Dodoma. Karibuni sana Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza ratiba yetu ya kuchangia. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Zainab Rashidi Kawawa na Mheshimiwa Kigola ajiandae.

MHE. ZAINAB. R. KAWAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupunguza mzigo mkubwa wa kodi kwa wafanyakazi. Ni matumaini yangu sasa kwamba Serikali itatekeleza agizo ambalo Mheshimiwa Rais alilitoa la kupunguza kodi kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe msukumo leo katika Wizara hii, niendelee kuiomba iongeze juhudi katika kuhakikisha kwamba tatizo la ajira nchini linaendelea kutatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa sababu gani? Leo hatuwezi kujivuna hapa kwamba ajira imeongezeka nchini wakati bado tunazo sekta binafsi ambazo zinaweza zikazalisha ajira kwa wingi, zikiwa zinalegalega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara, kutoa msukumo ili kuweza kuzalisha ajira kwa wingi. Asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Kama tukitoa msukumo katika haya maeneo, ni dhahiri kwamba vijana wengi watapata ajira na pia viwanda vingi vitaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya madini na simu hayatoi ajira za kutosha. Ukienda kwenye madini, ajira hazifiki hata 15,000. Hivyo, hatuwezi kujivunia hapa kwamba tuna ajira au tumekuza ajira kwa haya maeneo ambayo tunajua, kwanza siyo sekta rasmi lakini pia hazikuzi ajira kwa kiasi cha kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia nizungumzie sekta binafsi. Baadhi ya sekta binafsi zimekuwa zikiendelea kuwaonea wafanyakazi. Serikali ilikwishatangaza kima cha chini cha mshahara kwa kila sekta, lakini ni ajabu leo na nitoe tu mfano mmoja; Mgodi wa Mwadui, Wafanyakazi wamekuwa wakilia kwamba mpaka leo bado watu wanalipwa Sh.100,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya kima cha chini cha mshahara ambacho sekta binafsi zimeshindwa kukitekeleza, wafanyakazi wamekuwa wakipuuzwa katika baadhi ya hizi sekta binafsi. Waajiri wanauza viwanda na makampuni yao bila kuwashirikisha wafanyakazi, wakati mfanyakazi ndio mdau mkubwa katika hii sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali isimamie hizi sekta binafsi ambazo zimeshindwa kutatua kero za wafanyakazi, hazilipi kima cha chini cha mshahara, nyingine waajiri wanauza Makampuni bila kuwashirikisha wafanyakazi na mfano mzuri ni *Shoprite;* kampuni nyingine hazitoi maslahi ya kutosha kwa wafanyakazi na mfano mzuri ni wale wanaojenga barabara za mabasi yaendayo kwa speed *(DARTS)* na zenyewe wafanyakazi wake wamekuwa wakilalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui kama muda unaniruhusu, lakini nadhani niishie hapo hapo. Naunga mkono hoja na ninaomba Mheshimiwa Waziri aje na majibu kwamba ni namni Serikali itatoa msukumo wa kukuza ajira katika sekta binafsi hususan sekta za kilimo na viwanda. Pia ni namna gani Serikali itahakikisha inasimamia hizi sekta binafsi ambazo waajiri wake wameshindwa kutatua kero za wafanyakazi? Maana waajiri wa sekta binafsi wamekuwa wakimtumia mfanyakazi kama mtaji wao, lakini wao wenyewe wanashindwa kuwaweka katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu, ahsante. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Kigola na Mheshimiwa Ali Juma Haji ajiandae.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Idara hii nyeti sana kwa Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiongelea masuala ya ajira kwa wafanyakazi maana yake tunaongelea maisha ya watu ambao wanafanya kazi. Wizara hii ni muhimu sana hasa kwa watu wanaotafuta kazi na haki za wafanyakazi. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri wakati anatoa majibu hapa, anieleze Wizara imeshughulikia vipi matatizo ya wafanyakazi hasa wale ambao hawakulipwa na Serikali wakati viwanda vinabinafsishwa? Kwa mfano, sasa hivi kuna kiwanda kile cha Mgololo, wafanyakazi muda mrefu sana hawajalipwa malipo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Wizara iniambie, lile suala yenyewe kama Wizara, kwa wale wafanyakazi ambao hawajalipwa mpaka leo imechukua hatua gani ya kuwasaidia na imefanya Mikutano mingapi na wale wafanyakazi ambao mpaka leo hii wanapata shida sana pale Mgololo? Hilo

nitamwomba Mheshimiwa Waziri aniambie wakati anajibu hoja za Wabunge hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, kuna tatizo la fidia kwa Wafanyakazi. Wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye Kampuni za watu binafsi, wakiumia kazini hawalipwi fidia, na kama wanalipwa tutamwomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni wafanyakazi wangapi katika Tanzania wanaofanya kazi katika kampuni binafsi ambao wamelipwa fidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria zimetungwa kwa mfano ile ya Sheria ya mwaka 2008, lakini nimesoma kwenye kitabu hapa Mheshimiwa Waziri anasema utekelezaji unaanza mwaka 2014/2015. Sheria ya mwaka 2008 ilianza utekelezaji wake leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaiomba Wizara iniambie inachukua jukumu gani kuhakikisha kwamba wafanyakazi ambao hawakulipwa fidia mpaka leo na wameumia wakiwa kazini watalipwa fidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala ni la muhimu sana, sisi Wabunge ambao kwenye Majimbo yetu tuna Kampuni nyingi sana, wafanyakazi wengi sana wanakuja kwetu, tunashindwa kutoa majibu. Sasa leo Mheshimiwa Waziri ni wakati wake kutoa majibu awaambie Wabunge jinsi ya kuwasaidia wale Wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamwomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni kampuni ngapi za watu binafsi ameweza kuzitembelea na kufanya Mikutano? Kwa sababu tuna kampuni nyingi sana ambapo wafanyakazi wanashindwa hata kuuliza maswali kwa Waziri wao. Kuna matatizo mengi, lakini wanashindwa kupata nafasi. Kama hajapita kwenye kampuni hizo, leo namwomba Mheshimiwa Waziri aende kwenye kampuni ya *MPM*, *Uniliver Company*, na afanye Mkutano na wafanyakazi na siyo Menejementi, ili wamwambie kero za pale jinsi ya kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, kuna suala la pensheni. Hili suala la pensheni bado limegubikwa. Kuna watu wamekufa miaka mingi sana. Watu waliokufa hawalipwi pensheni yao, watoto yatima wanabaki, hawaendi hata shule kwani wanashindwa kulipa ada. Ukimwuliza mtoto, anakwambia baba yangu alikuwa mfanyakazi wa kampuni Fulani, lakini hana ada. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, atuambie ile fedha ya pensheni ya watu waliokufa, tuachane na pensheni ya watu waliopo; ya watu waliokufa. Ni watu wangapi mpaka leo hawajalipwa pensheni yao? Kule vijijini tunapata shida sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, ile pensheni ya watu ambao wapo haina *increment*. Kwa mfano, sasa hivi walio wengi wanalipwa Sh. 50,000/=,

iwango ambacho kwa maisha ya sasa hivi ya Mtanzania, haitoshi. Kwa hiyo, hilo nalo naomba Wizara iangalie uwezekano wa kuongeza pensheni kwa watu waliostaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ajira kwa wageni. Hatukatai wageni kuajiriwa, lakini tumeona wageni wanachukua *positions* zote kubwa. Vijana wetu wamemaliza masomo ya Vyuo Vikuu, wana *Degrees, Masters* na *Ph.D* lakini hawapati *positions* kubwa. Sasa naomba Waziri aniambie mikakati aliyoiweka kuhakikisha vijana wetu wanaomaliza Vyuo Vikuu wanapata *positions* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukakuta kwenye *top management* yote ni wageni tupu, vijana wetu ni wasomi lakini wanapewa nafasi ndogo za ukarani tu. Haiwezekani mtu kuwa na *Degree* au *Masters* lakini anapewa kazi ya ukarani tu. Hii haiwezekani kabisa! Lazima tuwe na mikakati, Wizara ituambie inawasaidiaje hawa vijana? Kwa sababu hatuwezi kuwatupa tu! Sasa hivi kuna vijana wengi sana hawajaajiriwa, mpaka wengine wamefikia hatua ya kukata tamaa. Huwezi ukamwajiri mtu ana *Masters* unamwambia awe anauza vocha. Tunaona vijana wanauza vocha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumesoma hapa Mheshimiwa Waziri anasema kuna ajira karibu 1,000 na mia ngapi na kwamba kila mwaka wanaajiri. Ni watu gani hawa wanaoajiriwa? Mbona vijana wetu, kwa mfano kwenye Jimbo langu wapo pale hawana ajira! Kesho nitamwandikia Mheshimiwa Waziri majina ya vijana katika Jimbo la Mufindi Kusini ambao waliomaliza *Degrees* na wamemaliza zaidi ya miaka miwili hawana kazi na ni wasomi na wana sifa zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa tuhangaika wakati kuna makampuni makubwa, nchi hii imeshawaita wawekezaji, wamewekeza lakini vijana wetu hawaajiriwi matokeo yake wanaajiriwa wageni. Hii haiwezi kukubalika kabisa! Ni lazima vijana wetu tuhakikishe kwamba wanaajiriwa, wanafanya kazi na wanapata mshahara.

La mwisho, mwaka jana mmeongeza mishahara, nakushukuru sana uliongeza mishahara kwa makampuni binafsi, lakini kwenye makampuni makubwa umesababisha migomo mikubwa kwasababu bado hawajafikia…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ali Juma Ali na Dkt. Kigwangalla ajiandae.

MHE. ALI JUMA ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema kusimama hapa na kuweza kuchangia hoja hii ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Msemaji aliyekaa kuhusu ajira kwa vijana wetu ambao wana maliza Vyuo Vikuu na wanakaa wanakosa ajira. Mimi hili ningelisemea pia kwa upande mwingine; sijui kama ni mkakati wa makusudi unafanywa hasa kwa baadhi ya hizi sekta binafsi kwamba wakati mwingine wanatoa matangazo lakini wanatoa na masharti kwamba mfanyakazi wanayemtaka ni lazima awe na uzoefu wa miaka mitano, miaka miwili, miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni kikwazo kwa vijana wetu ambao wanamaliza elimu zao za Vyuo Vikuu na kwa kweli mimi nina wasiwasi kwamba hili linafanywa kwa makusudi katika sekta hizi kwasababu tu hawa vijana wanakosa sifa hii na badala yake wachukuliwe wale ambao wanawahitaji wao kwa madhumuni ya kwamba vijana wetu wazurure.

Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia Waziri kwamba ikiwezekana mkakati huu uondolewe au ukiwepo basi pawepo na sharti kwamba kama wanatakiwa vijana watano mmoja awe ni mwenye uzoefu wa miaka hiyo mitano na wengine wachukuliwe wale ambao wamemaliza Chuo Kikuu ambao wana elimu ile kwa kazi inayotakiwa. Naomba Serikali iliangalie hili kwa makini. Vijana wetu wanakosa kazi, wanakosa ajira kwasababu ya uzoefu wa miaka fulani inayotakiwa na Taasisi zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie suala la pili, kuhusu Taasisi binafsi. Mwaka juzi nilichangia hapa Wizara hii hii na nikakilaumu sana Chama kile cha Wafanyakazi wa Mahoteli na wa Majumbani *CHODAU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama hiki sioni kama kinafanya kazi ipasavyo kama vile kinavyofanya kazi Chama cha Walimu ambapo watu wote, Serikali wakati mwingine inatetereka Chama cha Walimu kinaposimama kutetea Wadau wake. Lakini Chama hiki *CHODAU* hatukioni utetezi wake. Wafanyakazi wa Mahoteli wanadhalilika, wafanyakazi wa majumbani wanadhalilika, wafanyakazi wa sehemu mbalimbali wa sekta hizi binafsi wanadhalilika. Ni kwa sababu hawana elimu ya kwamba labda kuna Chombo chao kinaweza kuwatetea.

Sasa mimi ningekiomba hiki Chama kama kipo, basi kwa nini hakitoi elimu kama vile Vyama vingine vinavyotoa kwa wadau wao? Mimi ningekiomba Chama hiki kijitahidi na tukione kwamba kinafanya kazi. Mahoteli yapo, yanajulikana, majumba yapo lakini hawajui wafanyakazi wa Mahoteli na

majumbani kwamba kuna Chama chao au mtetezi wao, kwa hiyo ni lazima wasimame kidete hawa kuwaelimisha wafanyakzi wa mahoteli na majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nimewahi kuona mfanyakazi anapigwa ngumi na Meneja wa Hoteli fulani. Anapigwa kabisa, mimi namwona! Lakini mfanyakazi yule nilipomwuliza wewe mbona unapigwa? Kwa nini hujitetei? Anasema, niende wapi? Sijui popote! Hawaelewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wafanyakazi wa Mahoteli hawaelewi chochote! Halafu mishahara yao ni duni. Wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu, wanakuwa na masharti magumu. Akivunja chombo, unakatwa mshahara; kama vile yule Meneja yeye hawezi kupata bahati mbaya; chombo kile kitafanya kazi mpaka mwisho wa dunia kisivunjike? Lakini watakatwa mishahara bila ya ridhaa zao. Kwa kweli huu ni unyanyasaji na uonevu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee wafanyakazi wa majumbani. Kwa kweli sisi akina baba, akina mama wapo baadhi yao wanawadhalilisha sana wafanyakazi wa majumbani. Utakuta kama baba ana mfanyakazi wa nyumbani msichana, anamtaka kwa njia nyingine. Asipomkubalia, kisago na kumfukuza kazi. Hata akina mama wengine ni hivyo hivyo, wanawalazimisha wavulana wanaofanya kazi majumbani; asipomkubalia anamchongea kwa baba mwenye nyumba.

Kwa hiyo, haya mambo yapo. Hiki Chama kama kipo kiwaelimishe ni wapi pa kukimbilia na kutetea haki zao. Vinginevyo, wanaumia sana hawa watu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kuendelea sana, lakini ningemwomba Mheshimiwa Waziri atueleze Chama hiki msimamo wake kinavyoweka na utetezi wake kinavyofanya kwa wafanyakazi hawa wa Mahoteli na majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Chiku Abwao ajiandae.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, naomba nianze kwa utangulizi kwamba sitaunga mkono hoja ya Wizara ya Kazi na Ajira kwasababu ambazo ziko wazi. Sababu zenyewe ni hizi, mwaka 1Februari, 2013, mimi binafsi nilileta hoja binafsi ya kukuza ajira kwa vijana na kuondoa umasikini.

Hoja ile ilichangiwa na Wabunge walio wengi humu Bungeni na kwa umoja wetu tulipitisha maazimio ambayo niliyapendekeza katika hoja ile. Maazimio yakiwa ni kuanzisha programu ya kukuza ajira kwa vijana ambayo ndani yake itakuwa na Mfuko Maalumu wa kutoa mikopo kwa vijana ili waweze kujiajiri katika shughuli mbalimbali za kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ndani ya programu ile kulipaswa kuwe na uanzishwaji wa Benki ya Vijana ambayo pia ingekuwa ni mwendelezo wa ule Mfuko wa Kukuza Ajira kwa Vijana. Mwaka 2013 zilitengwa Shilingi bilioni sita, mwaka huu zimetengwa Shilingi ilioni tatu tu. Utaona kwamba japokuwa *program* yenyewe inaanza mwaka huu, lakini imetengenezwa toka katika hatua za wali ili ife. Kwa sababu mwaka jana Shilingi bilioni sita, mwaka huu ni Shilingi bilioni tatu, maana yake ni nini?

Kwa hiyo, ili kuisadia Serikali na kuisaidia nchi na kuwakomboa vijana walio wengi katika Taifa letu, mimi siungi mkono hoja hii ili Serikali ijipange upya kuja na mapendekezo ya bajeti ambayo itaenda walau kwa kiasi fulani kutatua tatizo la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu za *Intergrated Labor Force Survey* kwa maana ya takwimu za utafiti wa hali ya nguvukazi nchini ziko wazi na zinaonyesha kwamba vijana wanaoingia katika soko la ajira kwa mwaka huu tulionao ni taribani 850,000 lakini mwakani kwa mujibu wa takwimu za makisio za Benki ya Dunia watafikia 1,300,000. Lakini ajira zilizozalishwa katika taarifa ya Waziri ukurasa wa 12, ziko 630,616 tu. Ukitazama takwimu hizi ambazo ameziwasilisha Waziri hapa mbele yetu utaona kwamba sekta binafsi na kilimo inazalisha ajira takribani asilimia 60.

Hoja yangu ilikuwa inaongelea namna ya kukuza sekta binafsi lakini pia namna ya kuongeza ajira zinazohusiana na kilimo na viwanda vyenye *backward linkage* na kilimo, lakini sasa hoja ile haitekelezwi kama ambavyo tuliwasilisha na matokeo yake tunaletewa hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa ambayo inaelezea mikakati ya mafunzo na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mara ya kwanza siungi mkono hoja ya mama yangu Gaudentia Kabaka kwa sababu hizo. Sababu ziko wazi tu, asilimia 40 ya watu ambao wanakosa ajira kila mwaka ni vijana wanaomaliza Kidato cha Nne na wanafeli mitihani yao. Hili ni janga la Kitaifa na ni bomu la wakati. Ukosefu wa ajira kwa vijana hawa ni bomu la wakati na ipo siku litalipuka.

Sisi Wabunge leo tunaongea hapa na wataalamu huko nje, Watumishi wa Umma, sote kwa pamoja tunawatimulia vumbi vijana hawa ambao angalau wamepata mwanga kidogo na hatukai chini tukafikiria ni namna gani

tutawajengea uwezo wa wao kushiriki katika uchumi mpana wa Taifa letu. Tunajijengea kaburi bila sisi wenyewe kujua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri Kabaka aje na mapendekezo mapya ya namna ambayo watatekeleza programu ya kukuza ajira kwa vijana kama ambavyo tuliwasilisha kwa hoja binafsi niliyoitoa katika Bunge lako Tukufu mwaka 2013 Februari Mosi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema tu kwamba sisi wengine tunatarajiwa na Taifa letu kuiongoza nchi hii, kwa hiyo tusingependa kuibuka siku moja na kukuta kuna vijana wanaoandamana kila siku, kuna vijana wanaohangaika, wanaofukuzwa na Polisi kila siku kwa kuwa hawana ajira lakini pia wamesoma na hivyo tunaomba sana tatizo hili la ukosefu wa ajira kwa vijana lipatiwe ufumbuzi mapema hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwenye Nishati na Madini zimezalishwa 453 tu kwa mwaka uliopita. Lakini pale Nzega vijana waligundua mgodi wa kuchimba dhahabu na katika mgodi ule watu 10,000 walikuwa wapate ajira pale lakini leo hii…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Namwita Mheshimiwa Chiku Abwao na Mheshimiwa Zaynabu Vullu ajiandae.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuwepo hapa siku hii ya leo ili kuchangia katika Wizara hii. Pia nashukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba kuchangia Wizara hii, lengo langu kubwa ni kujaribu kuangalia ni namna gani Serikali itaweza kuwasaidia vijana ambao sasa hivi imekuwa ni changamoto kubwa. Vijana sasa hivi wanahangaika sana, ajira zimekuwa hazipatikani, kila wanapojaribu kushika hapashikiki.

Sasa hivi vijana wengi baada ya kukosa ajira, wameamua kujiajiri wenyewe, na ajira waliyoona inafaa ni kufanya biashara ndogo ndogo. Lakini vijana kila wanapojaribu kushika eneo wakafanya biashara, wanazuiwa. Vijana wanatafuta biashara kwa kuwafuata watu maeneo ambayo biashara inachanganya, wakifika mahali wakazoea kufanya biashara, wanazuiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iringa walidiriki mpaka kuchoma gari la Zimamoto, wamepambana na Askari baada ya kuchanganyikiwa. Eneo wanapewa wafanye biashara, wakizoea tu, biashara yao inapozidi kushika kasi, Serikali inaingilia kati. Kibaya zaidi Serikali imekuwa ikiwajali zaidi wafanyabiashara wakubwa, wanawasahau hawa vijana wadogo ambao wanahangaika. Wamesoma lakini ajira hazipatikani; wanafanya biashara wanaingiliwa kati kwamba wanaleta uchafu. Mimi nafikiri ni wajibu wa Serikali kuangalia, kama vijana biashara imechanganya kwa eneo hilo na wanafuata watu, watafutiwe eneo zuri pale pale Mjini.

Kama Iringa walikuwa wameamua kwamba kila Jumapili, ni biashara ya Jumapili tu mpaka Jumapili ambapo inafungwa barabara katikati ya Mji vijana wanafanya biashara mpaka jioni na usiku ukifika wanafunga biashara ile, mambo mengine wiki nzima yanaendelea. Lakini hata hii siku moja kijana kupewa nafasi ili aweze kufanya biashara yake kwa uhuru, anashindwa kuwekewa mazingira mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vinjana wengi wanalalamika. Toka juzi, wiki nzima iliyopita napokea *message* toka kwa vijana wa Dar es Salaam; naambiwa Kariakoo imechafuka. Kila siku Askari wanavaa mabomu kupambana na vijana pale wanaofanya biashara. Vijana hao kila siku wanapigwa mabomu, lakini kesho wanarudi, kwasababu njaa inawasumbua, maisha ni magumu, hawana la kufanya, wajitolea hata kufa. Maana wanavyopambana na Askari wenye mabomu, ujue kwamba hawa vijana wako tayari hata kufa. Wameamua hata ni bora wafe kuliko wakae bila ajira. *(Makofi)*

Sasa Serikali inaangalia tu, badala ya kupambana kuona ni namna gani waweke mkakati wa makusudi kuhakikisha vijana wanafanya biashara zao waweze kuwa na uhakika wa kuishi, wanatumia nguvu kubwa sana kuleta mabomu na kuleta Askari ambao kila siku wanapambana na vijana.

Mheshimiwa Waziri, nataka kujua hivi ni gharama ngapi ambazo mnatumia kwa mabomu ambayo yanawekwa kwa makusudi kabisa kupambana na vijana ambao wanahangaika kutafuta riziki? Mwisho wa kupambana na hawa vijana itakuwa ni lini? Kwa sababu imeshindana! Mimi nakubali kusema kwamba Serikali imeshindwa kutatua tatizo hili, sasa hivi inatumia nguvu. Tatizo la nguvu kutumika kupita kiasi na Serikali hii iliyoko madarakani, linazidi kuota sugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hawa vijana wahamie wapi? Waendewapi? Wafanye nini? Wamejiingiza kwenye biashara ya boda boda ambapo mlishikia bango kabisa, mkatetea sana ndani ya Bunge hili.

Kuna watu ambao tulisema kwamba hizi boda boda mnazotetea kwa ajili ya hao vijana siyo za vijana ni za matajiri wachache ambao wamenunua boda boda hizo wamewaajiri hao vijana wafanye kazi. Mkasema hapana, hizi ni za vijana mkawafutia na kodi, kwamba tunataka vijana wetu wapate ajira na vijana wakalipokea hilo suala kwa nguvu zao zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wamehangaika na hizo boda boda, sasa hivi biashara imechanganya, mnawazuia wasifike mjini. Watu wanaotumia boda boda zaidi ni wafanyakazi ambao wanataka kuwahi makazini, wanataka kuwahi majumbani, wanataka kuharakisha katika kazi zao mbalimbali kwasababu msongamano wa barabarani ukiwa una haraka onaona ni bora uchukue boda boda ukimbie ukafanye shughuli, au kwa mtoto wa kike anayenyonyesha, akimbie atoroke hata kazini kidogo akanyonyeshe mtoto. Anajua nikipanda boda boda nitakwenda mara moja na kurudi. Yote hayo yanafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mnataka vijana wafanye nini? Kwasababu hata kijana kama ameajiriwa na analea, ana mtoto mdogo kwake inakuwa shida. Usafiri nao mnawabana! Pamoja na kwamba kuwabana vijana ambao walikuwa wameshatulia na kazi ya boda boda wakawa wanajua kwamba wamepata ajira, mimi Mheshimiwa Waziri sitaiunga mkono bajeti hii, nataka mtuambie, hivi hawa vijana mwisho wake wafanye nini?

Serikali mnawajibika ni kwa vijana kuhakikisha kuwa wanawekewa mazingira mazuri? Mimi nazungumzia hasa vijana ambao wanajiajiri, vijana ambao wanahangaika na maisha wala siyo wasomi isipokuwa wanatafuta mbinu za wao kuishi ili wasiwe majambazi au wezi. Kwa hiyo, tunataka tujue Serikali mnawasaidia nini hawa vijana mabo wameishia tu *Form Four,* hawana elimu kubwa, lakini wamejipa uwezo wao wenyewe wa kujiajiri, mnawawekea utaratibu gani?

Mtasema kwamba mlijenga *Machinga Complex* sijui vijana waende huko, mkiwatayarishia maeneo ya biashara hawaendi, hilo ndiyo jibu mtanipa; na hilo jibu silikubali, nalikataa kwasababu maeneo mnayowapeleka vijana hawawezi kufanya hizo biashara. Vijana wanatafuta maeneo ya kufanya biashara kwa kuwafuata watu, na biashara zipo Mijini.

Kwa hiyo, nataka kusikia Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba hawa vijana ambao wamejiajiri kwa biashara ndogo ndogo, vijana ambao wamejiajiri kupitia hizo boda boda mnawawekea utaratibu upi kama mnawazuia wasifanye biashara hizo maeneo ambayo watapata...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Zaynabu Vullu jiandae Mheshimiwa Bukwimba na ajiandae Mheshimiwa Munde.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, lakini awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na mimi kuweza kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi zangu kwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu wake wote na Watendaji wote katika Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya. Lakini naomba waangalie suala la ajira kwa vijana. Wamesema wametenga ajira au watatoa ajira laki nane na nusu kwa maana ya 850,000, ukiangalia idadi ya Vyuo tulivyonavyo nchini, ukiangalia wahitimu wa Vyuo nchi nzima, hali kadhalika ukiangalia wale ambao wanakwenda kwenye sekta binafsi; wakulima, wafugaji na kadhalika, bado hii idadi haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mkiangalia hiki chombo cha *TAESA* inaonekana kama kimeshindwa mpaka watu binafsi wameingia.

Kwa hiyo, niishauri sekta binafsi ambayo imeingia katika suala la kutafuta ajira, iangalie uwezekano wa kutoa ajira ambazo zitalinda afya zao, maslahi yao na kuwapa mshahara ambao utawasaidia katika kuendesha maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuamua kuweka katika Sera yake kwamba kuwepo na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikiwemo *PPF, LAPF, PSPF* na *NSSF*. Mashirika haya yamefanya kazi kubwa sana kwa kujali maslahi ya wananchi, kwa kujali afya na ajira za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza *NSSF* kuanzia Mkurugenzi wake Mkuu Dkt. Ramadhani Dau na Wasaidizi wake wote. *NSSF* imefanya kazi kubwa sana chini ya uongozi wa Dkt. Dau, imeendesha miradi.

Waswahili wana msemo wao unasema hivi: "*unachonga mwiko ili mkono usiungue*."

Kwa hiyo, Serikali kwa kuweka Mashirika haya, nichukulie Shirika la *NSSF,* kwa kweli limekidhi na linatimiza wajibu wake. Hatujasikia malalamiko yoyote ya wanaomaliza kazi zao wanapolipwa pensheni. Kila mtu analipwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona madaraja, nyumba za bei nafuu, sasa hivi wameingia kwenye SACCOs na VICOBA nani anaweza kufanya hivyo? Bima ya Afya ipo, nani anaweza? Ndiyo maana Serikali imesema llani yake ifanye kazi hiyo, maisha bora kwa kila Mtanzania yanapita katika njia hiyo. Kwa hiyo, niwapongeze, wanaowakebehi msiwasikilize, ninyi chapeni kazi. Chama cha Mapinduzi tunajidai na Mashirika yetu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila niwaombe, sekta binafsi, mimi natoka Mkoa wa Pwani, wengi wa watu wa Mkoa wa Pwani ni wakulima, tufuateni kule na sisi mje muone mtatufanyia kitu gani? Serikali imetoa agizo la afya ya mama na mtoto kupunguza vifo, karibuni sana Mkoa wa Pwani mje mtusaidie tupunguze vifo vya mama na watoto.

MBUNGE FULANI: Hasa Mafia.

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Ukizingatia Mkoa wa Pwani una Wilaya saba, mimi nina imani kubwa na jahazi hili linaloongozwa na Dokta Dau hawana dogo watafika, watawaona, wanaotaka kwenye SACCOs ya aina yoyote na zipo nyingi kule kina mama, kina baba tunawakaribisha. Waliokopa warudishe ili Shirika au Mashirika yaweze kuwapa na wengine wafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiharibu huu mchuzi, nataka watu wale chakula kizuri, nawaombea kila la kheri *NSSF, PPF, PSPF* na Mashirika mengine yote wafanye kazi zao kwa ufanisi, watuletee maendeleo Watanzania kwa sababu miradi ya nchi haiwezi ikaendeshwa na Serikali peke yake, tumeona nchi mbalimbali sekta binafsi zinajenga barabara, zinakusanya *road tall* na kadhalika. Kwa hiyo, si ajabu wao kujenga madaraja na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bukwimba ajiandae Mheshimiwa Munde.

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika bajeti hii muhimu kabisa ya Wizara ya Kazi na Ajira. Kwanza nianze kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya na ndio maana tunaona matunda makubwa sana katika Wizara hii kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kuzungumzia ajira migodini. Naanza hivyo kutokana na kwamba mimi natoka katika Mkoa ambao shughuli kubwa ni shughuli za migodi. Kuna mgodi mkubwa sana wa *GGM* ambao umeajiri wafanyakazi wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi kweli napenda kuipongeza *GGM* kwa sababu inafanya kazi nzuri na imeajiri wafanyakazi wengi. Pamoja na pongezi hizo, kuna changamoto kwa wafanyakazi wetu wanaofanya kazi migodini. Kwa hiyo, nitumie fursa hii kumuomba Mheshimiwa Waziri watenge muda kwa ajili ya kwenda kutembelea migodini kuangalia changamoto hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa migodini wanazo changamoto nyingi sana. Kuna kipindi tulikwenda Geita tukakutana nao, wakaelezea changamoto kubwa walionayo migodini. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri kweli tuweke muda mzuri kuweza kuangalia changamoto hizi za wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wafanyakazi wa migodini pia hasa *casual labour* wale wanaoajiriwa hasa kutoka kwenye vijiji, wamenitumia meseji kusema kwamba wakati mwingine miezi mitatu inapita hawajapata mishahara yao. Ndio maana nasema Mheshimiwa Waziri hebu tutenge muda ili tuweze kuwasikiliza watumishi hawa waliopo migodini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme pia kwamba ajira kwa nchi yetu ya Tanzania ni vema tukaongeza wigo wa ajira. Tutaongezaje wigo wa ajira? Napenda kuishauri Serikali iangalie sekta muhimu ambazo zina uwezo wa kuajiri watu wengi zaidi kwa mfano, sekta ya madini. Kutokana na taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwa mwaka uliopita ajira zilizopatikana ni 453 tu, ni ajira kidogo sana kwa sekta ile. Naomba Wizara hii iungane na Wizara ya Nishati na Madini kuangalia uwezekano mzuri wa kuweza kuwasaidia vijana wetu hasa katika maeneo yenye migodi na hasa wachimbaji wadogo wadogo. Tutaweza kuongeza ajira kwa kiasi kikubwa sana kwa sababu vijana wengi sana hasa katika maeneo ya wachimbaji wadogo kwa kweli wamebobea sana katika shughuli za uchimbaji madini lakini wamekosa mitaji na elimu iliyo bora ya kuweza kuwasaidia. Kwa hiyo, Wizara ikishirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, nina uhakika tutaweza kuongeza ajira kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la kodi, kodi hizi za *Pay As You Earn,* kwa kweli kodi hizi ni kubwa sana. Naomba Serikali pia iendelee kuangalia wafanyakazi wetu wanalalamikia sana hizi kodi ni kubwa mno. Kwa hiyo, niombe Wizara iendelee kuangalia namna bora ya kuweza kupunguza kodi kwa ajili ya wafanyakazi maana ikiongezeka mshahara kidogo tu kodi pia inaongezeka, kwa hiyo, wanashindwa kumudu maisha yao kwa sababu ya kodi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusu pensheni hasa kwa wazee ambao wamestaafu mara nyingi wanapofuatilia kupata pensheni zao wanapata shida kubwa sana. Niombe Serikali iendelee kuwekeza katika utaratibu ulio bora ili wazee hawa waweze kupata pensheni zao vizuri. Mme-*improve* kwa kweli ukilinganisha na siku za nyuma lakini naomba muongeze zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iangalie uwezekano wa kutoa pensheni kwa wale waliojiajiri katika kilimo hasa wazee waliopo Vijijni. Hii ni kero kubwa, wananchi wengi wanaulizia hasa wazee ambao wamejiajiri kwa miaka mingi katika sekta ya kilimo, wao kwa nini hawapati pensheni? Kwa hiyo, Serikali iangalie namna bora ya kuweza hata kuweka utaratibu mzuri wazee hawa pia wapate pensheni kwa sababu wamelitumikia Taifa, wamefanya shughuli za kilimo kwa miaka mingi na wanahitaji kuenziwa na kupewa pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie kuhusu ajira kwa vijana wetu. Vijana wetu wengi wanamaliza vyuo lakini wengi hawapati ajira. Niombe Serikali iangalie utaratibu mzuri wa kuweza kuwapa vijana wetu ajira, Kwa mfano, kuna vijana wangu ambao wapo *UDOM*, wengine St. John wapo hapa wanasilikiliza lakini wakimaliza wanakosa ajira. Kwa hiyo, niombe Serikali iongeze wigo kwenye suala la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna vijana wetu wanaomaliza vyuo mbalimbali, vyuo vya ufundi, vya kilimo, wengi kwa kweli! Kuna vijana wangu fulani kwa kweli walivyokosa ajira walisikitika sana, ni kilio kikubwa sana. Kwa hiyo, niombe Serikali iangalie namna ya kuweza kuajiri vijana hawa wanaomaliza vyuo vikuu na vyuo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi niombe Serikali iwekeze kwenye vyuo vya *VETA*. Sera ya Taifa ni *VETA* kila Wilaya, Wilaya ya Geita tupate chuo cha *VETA* ili vijana wengi wapate elimu ya kuweza kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo napenda kuzungumzia ajira kwenye Halmashauri. Siku za zilizopita ajira zilikuwa zinafanyika Kitaifa lakini sasa hivi tunashukuru sheria ililetwa hapa tukairekebisha, sasa hivi Halmashauri zina uwezo wa kuajiri kada ya chini. Niombe sasa Serikali itoe vibali vya kutosha kwa sababu Halmashauri nyingi hazina wale wafanyakazi wa kada ya chini kwenye Vijiji na Kata. Niombe Serikali iangalie uwezekano wa kutoa vibali kwa mwaka huu ili tuweze kuajiri watumishi katika Halmashauri zetu wale ambao wanahitajika, tuna mahitaji makubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana, naunga mkono hoja ili Mheshimiwa Waziri aendelee kutekeleza wajibu wake. Ahsante sana! *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Munde, ajiandae Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri pamoja na Watendaji wake kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini kubwa zaidi niwapongeze kwa kutenga ajira 840,000 lakini niwaambie kwamba tunahitaji ajira zingine. Kwa jinsi watoto wetu wanavyomaliza vyuo, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imeweka vyuo vingi, elimu ni kubwa sasa watu wengi wanamaliza vyuo kila mwaka, naamini ajira 840,000 bado hazitoshi. Nashauri Wizara ishirikiane na wadau wakiwepo ma-*RC*, ma-*DC* kuhakikisha tunapata ajira za sekta binafsi pamoja na ajira zisizo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linawezekana, kule kwetu Igunga Mheshimiwa wetu Mkuu wa Mkoa wa Tabora Fatma Mwasa, Mheshimiwa *DC* wa Igunga walikusanya watoto wa vyuo vikuu wakawafungulia shamba kubwa sana la vitunguu ambalo waliuza kwa mara ya kwanza wakapata milioni 470. Vijana wale zilitoka ajira, Mkuu wa Mkoa akawaambia sasa tunawatafutieni ajira wakagoma, wakasema sisi tunaendelea na kilimo. Kwa hiyo, naamini Wizara kwa kushirikiana na ma-*DC* wetu na Wakuu wa Mikoa tunaweza tukafanya vitu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze tena Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kutenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya vijana. Nimuombe Waziri anisikilize vizuri, tunaomba katika mgao wa shilingi bilioni tatu kule Tabora tupate mgao huu kwa sababu zifuatazo. Tumefungua shamba kubwa sana la vijana Kijiji cha Vijana kiko Skonge, Waziri Mkuu alienda kukagua alishangaa sana, hajawahi kuona! Tumewajengea vijana wale nyumba za kudumu pale, wanatengeneza asali, wana mashamba makubwa ya tumbaku na wana mashamba makubwa ya alizeti. Tunaamini mkituongezea katika mashamba yetu yale hizi shilingi bilioni tatu, kidogo tukapata na sisi vijana hawa wataendelea zaidi. Pia tuna mashamba makubwa ya alizeti, Tabora pale kuna shamba kubwa sana la vijana la mahindi na kuna mashamba ya pamba tumeyaanzisha. Kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali mara nyingi mnakuwa mnatusahau kwenye hii migao, tunaomba Tabora mtukumbuke kwenye hizi shilingi bilioni tatu na sisi tupate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kuongelea migogoro ya wafanyakazi. Naipongeza Serikali imejitahidi kupunguza migogoro kwa kiasi fulani lakini niseme kwenye sekta binafsi na zisizo rasmi migogoro bado ipo, watumishi wanaogopa kusema ukweli wakisema watafukuzwa. Hali sio nzuri kwenye migodi kama alivyosema Mheshimiwa aliyetangulia. Watu wale hawapati mafao ya afya, pesa za matibabu lakini kwenye makampuni ya ulinzi tunashuhudia hawapati haki zao stahiki. Mheshimiwa Waziri, inabidi utafute njia mbadala ya kukutana na hawa watu. Hawa watu ukikutana nao *official* au wafanyakazi wako wa Wizara wakutane nao *official,* watu hawa wanafukuzwa kazi, watu hawa wanapata matatizo, mtafute njia mbadala ya kukutana na hawa watu. Mnaweza mkaviandikia Vyama vya Wafanyakazi barua, mkakutana nao hata *weekend* sehemu nyingine sio kwenye ofisi zao, ili waweze kuwa huru kuwaeleza matatizo wanayoyapata. Matatizo ni makubwa sana, wafanyakazi wa gesti wanapata shida, wafanyakazi wa baa hawana *overtime*, wanafanya kazi mpaka saa tisa za usiku, akivunja chupa moja ya bia anakatwa mshahara! Mheshimiwa Waziri naomba mtusaidie sana na kwenye hotelini pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baya zaidi ni mashambani. Kule kwetu tunalima tumbaku, mtoto mdogo anaajiriwa kwa msimu mzima analipwa shilingi laki mbili baada ya msimu kuisha. Kalima, kaimbua, kachoma na kadhalika, tafuteni jinsi ya kupita kwenye mashamba, ajira za kule zinawaumiza na wananyonywa sana, tunaomba Serikali ifuatilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipongeze Shirika la *NSSF* pamoja na menejimenti yake yote lakini Mkurugenzi wake Ndugu Ramadhani Dau kwa kazi nzuri wanazozifanya. Hakuna Mtanzania asiyelijua hili labda tu kama hakutaka kuongea lakini wamefanya uwekezaji mkubwa sana wanastahili sifa na pongezi kubwa. Wamejenga nyumba, wanakopesha kwa muda wa miaka 15 kitu ambacho kilikuwa hakipo kwenye nchi yetu. Sasa hivi hata maskini anaweza akakaa kwenye nzuri, akalipa kidogo kidogo, mtumishi wa chini akakaa kwenye nzuri akalipa kidogo kidogo kwa miaka 15. Kwa kweli tunawapongeza *NSSF,* endeleeni kufanya hivyo lakini punguzeni masharti kidogo jamani, hata kama mtu anaajiriwa leo kama ni ajira ya kudumu mpeni nyumba, mtashika pensheni yake ama kitu kingine chake angalau vijana wetu waweze kupata makazi ya kukaa. Naipongeza sana *NSSF*. Pia tunapongeza kwa mafao mazuri, tunapongeza kwa kutozungusha sana wanachama wao wakati wa kudai mafao yao, tunaomba waendelee na kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa nilikuwa ziara Mkoani kwangu Tabora, nimekwenda Igunga nikakuta SACCOs moja ikaisifia sana *NSSF*, wameingia nao mkataba, wamewasaidia mambo mengi. Tunaomba *NSSF* sasa mshuke kabisa kwenye *private sector* na sekta zisizo rasmi. Tunajua hata kwa

wafanyakazi bado mnao lakini katika Watanzania wote, asilimia sita tu ya Watanzania ndio wapo kwenye mifuko mbalimbali. Kwa hiyo, mimi nadhani bado uhamasishaji unatakiwa ili Watanzania wengine wajiunge. Naamini mkihamasisha Watanzania wengi watajiunga wakijua mazuri ya *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Tabora mna ofisi lakini tunaomba mje kwa nguvu zaidi kwa sababu kule tuna bodaboda. Mimi niliwahi kufuatilia ofisini kwenu *NSSF* Tabora ili bodaboda wetu waingie *NSSF*. Mimi naona masharti yanakuwa mengi, kama kitu kinawezekana masharti kwa nini yanakuwa mengi? Jaribuni kupunguza masharti yaani mtu anakwenda leo, anakwenda kesho, mambo hayo yamepitwa na wakati. Kama kitu kinawezekana, kila kitu kipo sawa mnaweza kumpa huyo mtu nafasi ya kuwa mwanachama wenu, mpeni! Hamna haja ya kesho, kesho kutwa njoo sijui lini! Yaani kila kitu wanasema ngoja tupeleke barua Makao Makuu ama tumuulize nani Makao Makuu, wapeni *authority* watu wenu wafanye kazi. Kama mmewaamini kuwapa Umeneja wapeni *authority* wafanye kazi sio kila kitu Makao Makuu, naomba sana hilo mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niipongeze Mifuko yote kwa kuwa inafanya kazi vizuri, lakini *PPF* wanafao lao moja linaitwa fao la elimu. Kwa kweli nitoe rai kwa mifuko mengine na yenyewe iweze kuwa na fao hili la elimu. Fao hili linasaidia sana pale mzazi unapofariki, watoto wanasomeshwa. Nilishuhudia siku moja kwenye TV, mama Salma Kikwete alikuwa mgeni rasmi, watoto wale walitoa ushuhuda, nilikuwa naangalia nililia machozi. Mama Salma alilia, alikuwepo Mheshimiwa Saada Mkuya, Mheshimiwa Angellah Kairuki watu wote iliwaliza.

(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Namuita Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar ajiandae Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura na Mheshimiwa Rose Kamili Sukum.

MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba samahani leo sauti yangu haitokuwa nzuri, nina *flu*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Mimi siafiki hoja za Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengine ambao wanaona kana kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijafanya lolote kwenye ajira kwa vijana.

Tuseme tu kwamba haijafikia kile kiwango tunachokitaka lakini inajitahidi jamani tuipongeze Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchochezi si mzuri, ushawishi si mzuri, vijana hawashawishiki, vijana wa Tanzania hawashawishiki, tusiwashawishi. Mheshimiwa Chiku Abwao nakushangaa sana, unasimama hapa unasema mambo ambayo hata Kigwaangalla pia kasema vijana ni bomu, si vizuri jamani tuitetee Serikali yetu inajitahidi, Rais wetu anajitahidi, viongozi wetu wanajitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii - *NSSF*, Shirika hili ni namba moja, naipongeza Serikali, Mashirika yote nayapongeza lakini hilo ni namba moja Tanzania halina mfano. Shirika hili linaloongozwa na Mkurugenzi Ramadhani Dau na watendaji wenzake, watendaji wote wanafanya kazi vizuri, miradi mbalimbali imeboreshwa katika maeneo mbalimbali ya Tanzania, leo Tanzania inang'ara kutokana na *NSSF,* tuipongeze Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Mkurugenzi mzalendo kama huyu katika Tanzania yetu, hiyo ndio sifa yake ya kwanza. Mkurugenzi huyu Dau ni mstahimilivu, mchapakazi na mwaminifu. Kama ingekuwa tumepata watu 20 tu katika Tanzania kama Mkurugenzi Dau na wafanyakazi wake basi ufisadi huu ungekimbilia nchi nyingine Tanzania usingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila naishauri Serikali irejeshe fedha ambazo *NSSF* inawajengea miradi ili kuifanya *NSSF* isonge mbele isije ikaanguka, ikianguka *NSSF* na wafanyakazi wameporomoka. Naishauri sana Serikali ifanye hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la mikataba kwa wafanyakazi wa sekta binafsi kwenye hoteli, wenzangu wengine wameongea hapa, tunayajua fika na kila siku tunasema, sekta hizi binafsi hawawapi wafanyakazi wao mikataba, wanawafanyisha kazi kwa vibarua. Mfanyakazi akikosea kidogo atafukuzwa kazi kesho anaingizwa mfanyakazi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali ifuatilie sehemu hizi za hoteli kubwa Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Mbeya na kila sehemu Tanzania ili wafanyakazi wapate haki zao. Wafanyakazi wa hotelini hususani wanawake wanadhalilishwa, tunaomba Serikali ifuatilie, kila siku tukisema mnasema mnafuatilia lakini tunaona bado. Wanatupigia simu wanasema jamani tusaidieni kwenye bajeti hii, tunaishauri sana Serikali ishughulikie suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia unyanyaswaji wa wafanyakazi wa majumbani, tuweze kutambua sisi binadamu wote ni wamoja na wale wafanyakazi tunaowachukua tukawafanyisha kazi za majumbani wao pia ni binadamu kama sisi. Hivyo wafanyakazi wa majumbani nao wana haki zao, tuwapatie haki zao za upendo, ulinzi, elimu, huduma zote na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inafikia watu wengine wanachukua watoto wa watu wadogo, wanawafanyisha kazi za majumbani bila kuwapa mishahara, bila kuwapa posho yoyote, hawapewi fursa watoto hao na vilevile hata chakula, kama ni ubwabwa wanapewa makombo, wengine wanawadhalilisha watoto kama hawa, siyo vizuri. Wale ni watoto na wao wanatafuta ajira kama vijana wengine, tusiwadhalilishe vijana. Naishauri Serikali ifuatilie suala la wafanyakazi wa majumbani, wengi wao wanadhalilishwa wanaonekana kwamba siyo chochote na siyo lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza ajira ndiyo pale niliposema Serikali inaajiri. Siyo lazima mtu kuajiriwa ofisini jamani Waheshimiwa wenzangu, ajira ziko za aina nyingi, kama mtu amemaliza kusoma anajiajiri mwenyewe kama Mheshimiwa Munde alivyosema, wengine hawataki hata kuajiriwa wanasema wanataka kujiajiri wenyewe kwa sababu Serikali inawapatia mikopo na vifaa mbalimbali vya kufanyia biashara zao au kazi zao. Naiomba sana Serikali iongeze ajira kwa sababu najua kwamba ajira zipo za vijana ilimradi vijana hawa wawe wengi katika kuajiriwa na siyo lazima kazi za ofisini, kazi za kujiajiri wenyewe lakini iwafuatilie vijana hawa na vilevile kuwapatia mikopo mbalimbali, kuwapatia elimu mbalimbali jinsi ya kuendesha miradi yao na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nampongeza sana Mheshimiwa Kabaka, wanawake tunaweza, nampongeza Mheshimiwa Dokta Makongoro Mahanga na wanaume wanaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sabreena atafuatiwa na Mheshimiwa Rose.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kupongeza hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni na naiunga mkono. Pili, napenda kuchangia kwenye Wizara hii kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza na suala zima la mawakala wa ajira. Mwaka jana katika bajeti hii niliishauri Serikali na nilimshauri Waziri kwamba kumekuwa kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu kupitia wakala wa ajira nchini, wananchi wengi wamekuwa hawapati haki za wafanyakazi kama vile *bonus, overtime*, likizo na kadhalika. Tulipiga kelele na Waziri kwa upande wake alijaribu kuchukua jitihada za kukemea suala hili lakini mpaka dakika hii kuna watu wamegoma kufuata amri za Waziri. Ili kuwathibitishia Watanzania kwamba hii nchi siyo Taifa la Kambale kwamba kila mtu sharubu ni lazima Serikali ionekane inachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii tunaambiwa ni Serikali Sikivu, Serikali hii inashughulikia mikutano ya UKAWA huko Kigoma kwa sababu za kiusalama lakini Serikali hii ama wana usalama haohao wanashindwa kugundua makampuni yanafanya kazi ndani ya miaka mitatu kwenye nchi hii bila kulipa kodi, halafu tunasema Serikali ni sikivu, Serikali iko makini, ni umakini gani huo? Tumeona makampuni kadhaa hapa baada ya tamko la Waziri mwaka jana yameenda kujisajili kwamba na wao wawe wakala wa ajira. Nchi iko wapi, Serikali imelala miaka 52 ya Uhuru, tunasema Serikali ni sikivu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri aje na majibu, kwanza aangalie Sheria zake za Kazi, je, hawa watu wanaoitwa mawakala wa ajira ambacho ni kitu kipya nchini kwetu wako *included*? Kwa sababu umesema umetengeneza Kanuni ambazo hazijatoka bado kwa *AG* lakini Kanuni hizo zitafuatana na sheria, kwa sababu huwezi kuweka Kanuni ambazo hazina sheria. Wale mawakala wengine wamegoma wanasema kwamba matamko ya Waziri hayana nguvu ya kisheria. Kwa hiyo, timu yake ijaribu kuangalia Sheria za Kazi tulizonazo, mawakala hawa wameingizwa humo, kama hawapo basi Mheshimiwa Waziri uweze kuleta Muswada wa Sheria hapa ili Wabunge waweze kuamua na kuwatetea Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiacha hilo suala lingine ambalo nataka kuchangia ni *issue* ya Bulyankulu. Waziri kumekuwa kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu katika migodi mbalimbali hapa nchini na *case study* ni mgodi wa Bulyankhulu. Mgodi ule unaingia chini kilomita moja, unasambaa kilomita kumi na mbili kwenda *underground*. Hali iliyopo kule joto ni kali, maradhi ni mengi lakini kinachoendelea kule mfanyakazi anafanya kazi kwa muda wa miaka miwili *underground,* akitoka hapo wanamhamisha kwenye kazi za nje. Baada ya miaka minne yule mfanyakazi anaachishwa kazi, mwaka wa tano wafanyakazi wale wanakufa. Mheshimiwa Maige amefanya *research* nzuri sana kule Bulyankulu na imeonekana kuna watu zaidi ya 300 wamefariki. Sasa hivi ninavyoongea kuna wagonjwa karibia 80 wako Durban *hotel* huko Dar es Salaam wanasubiri kutibiwa ndani ya nchi, wagonjwa wale wanahitaji rufaa za kwenda nje ya nchi, lakini makampuni yameshindwa kuwapeleka. Kwa nini tunatengeneza matanuru ya kutengeneza marehemu na maiti watarajiwa

kwenye nchi hii, Serikali sikivu imekaa kimya? Ni lini Waziri mtachukua hatua, Watanzania wanaumia, Watanzania wanakufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri aje na majibu ya kutosheleza kuhusiana na wafanyakazi ambao wanapata shida katika migodi yetu na atuambie hawa wanaojiita OSHA, mawakala na taasisi zingine zinazosimamia haki za wafanyakazi, kwa nini haziendi huko? Namwomba Waziri mara moja moja awe anaenda huko chini migodini kwa sababu ndiyo kazi ambayo ameikubali, akaone hali halisi, akaone Taifa linavyozalisha marehemu watarajiwa kila baada ya miaka mitano, watu wanatoka *underground* miaka miwili ile wanafariki, kwa nini Serikali ipo kimya na haichukui hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuongelea ni suala la *Jambo Plastic*. Mwaka juzi Kamati yako ilitembelea kiwanda kile na baada ya ziara hiyo tu wafanyakazi takribani 400 walifukuzwa na wafanyakazi hao walifukuzwa kwa sababu walidai haki zao za msingi hawana *protective gear,* hawapewi *overtime*, haki zote za wafanyakazi walikuwa hawapewi. Baada ya kudai haki zao wafanyakazi wale 400 walifukuzwa lakini mpaka sasa hivi Serikali haijatoa karipio lolote kwa watendaji wa makampuni kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuliongelea ni kuhusu mafao ya Wazee. Najua kabisa kwamba sisi sote tuliopo hapa ni wazee watarajiwa lakini ukiangalia kwenye ripoti hii ambayo imewasilishwa hapa inaonekana kabisa timu mbalimbali za Wabunge zilienda nchi mbalimbali ikiwemo Indonesia, China na nchi nyingine kufanya utafiti kuhusiana na Mfuko wa Pensheni ya Wazee. Kwa kuwa sisi wote ni wazee watarajiwa na wazee ni haki yetu kuwatunza, kwa nini Serikali inakuja na majibu kwamba kwa kuzingatia hitaji hilo la msingi tumeendelea kujadiliana na wadau mbalimbali kwa lengo la kubaini vyanzo sahihi vya mapato ya Mfuko ambavyo ni muhimu katika kuhakikisha kuwa fao la pensheni kwa wazee litakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania sasa hivi hatutaki kusikiliza kwamba kitu gani kitakuwa endelevu ama mpango unaendelea. Tunataka kujua Mfuko wa Wazee utaanzishwa lini? Kauli kama hizi za kwenda kutembea wapi na wapi haiwezekani, hatuwezi kujifunza kuhusu kuhudumia wazee kwa sababu kuhudumia wazee ni sadaka. Basi tukatafute viongozi wa dini wakatufundishe jinsi ya kutoa sadaka kuliko kupoteza pesa za Serikali kupeleka watu nchi zaidi ya tano eti wakajifunze kuhudumia wazee. Hii ni aibu, ni lazima tu-*act,* Mfuko huu wa *pension* ya wazee utaanzishwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusu uwakilishi wa wafanyakazi katika Bodi za Wakurugenzi katika makampuni na taasisi mbalimbali za Serikali. Kumekuwa kuna kilio kikubwa na

Mheshimiwa Rais alikiri katika maazimisho ya Mei Mosi mwaka huu, akasema ni lazima sheria iletwe ifanyiwe marekebisho. Kwa kuwa Rais anateua Mwenyekiti wa Bodi na Mawaziri wanachagua Wajumbe wa Bodi, basi mlete marekebisho ili wafanyakazi na wao wawe sehemu ya Wajumbe wa Bodi ili wafanyakazi hao waweze kutetea haki zao. Nataka jibu lini sheria hiyo italetwa hapa? *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu amemteua Mheshimiwa Samuel Sitta kukaimu nafasi ya Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Bungeni. Naomba muwe na taarifa hiyo. Mheshimiwa Rose Kamili. *(Makofi)*

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Kazi, Ajira na Vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba mimi ni Mjumbe kwenye Kamati ya Maendeleo ya Jamii kuhusu Wizara hii lakini leo napenda kuchangia maeneo mawili kama nitapata nafasi vizuri na nianze na ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa vijana imetengwa shilingi bilioni tatu lakini hizo shilingi bilioni tatu si kwa vijana wote wa Tanzania ambao wamemaliza vyuo au wanaohitaji ajira kwa kujiajiri wenyewe. Hizo shilingi bilioni tatu zimetengwa kwa ajili ya vijana 200 walio tayari kujiajiri. Swali la kwanza linaanzia hapohapo, wale wengine mamilioni ya vijana ambao wanataka kujiajiri wanafanyaje na wanaishije hapa nchini? Je, mnapowaambia vijana wakajiajiri wenyewe kwa jinsi gani, maana yake Serikali yenyewe ndiyo iliyowalipia fedha labda asilimia 80 kwenye vyuo vyao kwa mikopo, hiyo mikopo watairejeshaje endapo hawa vijana mpaka sasa hivi hawajaajiriwa? Ni lazima Wizara iangalie sasa ni jinsi gani hawa vijana wote wa Tanzania wanawezeshwa ambao wanahitaji hiyo ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo fedha ambazo zimetengwa pia zinaonesha zaidi kwa hawa vijana kupewa mafunzo ya biashara. Unawapa mafunzo ya nini, endapo wanaajiriwa Wizarani wanapewa mafunzo kwanza au wanaenda moja kwa moja kufanya kazi? Mimi nadhani hakuna sababu ya kumaliza hizi fedha kwa ajili ya kuwapa elimu vijana, wameshasoma na wana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaeleze, hotuba ya Mheshimiwa Waziri kila wakati inajirudiarudia, takwimu zake hazieleweki. Tunaomba sasa badilikeni takwimu za kujirudia kila wakati, hotuba hiyohiyo, taarifa hiyohiyo tunaomba sasa ifutike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa ajira unasababisha umaskini kwa vijana na tatizo linazidi kuwa kubwa hasa katika nchi yetu. Mheshimiwa Kigwangalla amesema ni bomu na mimi ninamuunga mkono Mheshimiwa Kigwangalla kwamba vijana ni bomu linalosubiri kulipuka. Kwa sababu kama vijana hawana ajira ni wazi kabisa kwamba hilo bomu litalipuka saa yoyote na wakati wowote. Sasa ni jinsi gani Serikali inaangalia suala la ajira kwa vijana nchini na vijana wengine wote hata ambao hawakuenda shule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la nchi yetu ni kuwa, viwanda vyote vilivyobinafsishwa haviajiri vijana wetu wakati enzi zile za zamani za Mheshimiwa Rais Nyerere walikuwa wanaajiri vijana kutokana na viwanda vilivyopo, vyote vimebinafsishwa na havifanyi ile kazi. Hivyo turudi na sisi Wizara hii tuangalie ni jinsi gani tunawawezesha vijana wetu kuajiriwa kwenye hivyo viwanda au tuwatafutie kazi. Aidha, ikiwezekana *NSSF* kwa kuwa iko chini yetu basi *NSSF* watafute namna yoyote ya kuwawezesha vijana wetu waweze kujiajiri na kuajiriwa kwa mikopo bila kuangalia utaratibu wao wa kusema kwamba ni lazima uwe mwanachama wa *NSSF* kwa kuwa vijana hawana ajira. Hilo naliomba na nalisemea kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie sasa wazee. Kundi la wazee tangu mwaka juzi tunazungumzia suala la Muswada wa Sheria wa Uanzishwaji wa Mfuko wa Pensheni ya Wazee. Imekuwa ni wimbo, kwenye Kamati ni wimbo na tunaambiwa kwamba tayari Muswada umefikishwa kwenye Baraza la Mawaziri, mimi najua hiyo ni hadithi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba naye ni mzee mtarajiwa. Saa yoyote akikosa kura yeye ni mzee mtarajiwa. Je, tunafanyaje kumhusu yeye mwenyewe wakati hana Ubunge? Je, tunawafanyaje wazee wenzetu ambao wapo huko? Kwa kuwa sisi ni wazee watarajiwa, namwomba atoe kauli leo hapa kwamba Muswada unakwenda lini ili tujue wazee wanapata hiyo pensheni au laa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge ametupeleka India, Malyasia, China yote ni kwenda kujifunza ni jinsi gani wenzetu wameweza kuwalipa wazee. Hivyo basi na mimi naomba nikuambie hakuna sababu ya sisi kwenda kujifunza tu halafu hatujaanza utekelezaji. Inatosha, sasa tunataka kujua wazee tunawafikisha wapi? Hili ni tatizo, Waziri akumbuke kwamba yeye mwenyewe anapotaka kuomba kura Wabunge ndivyo tunavyofanya, tunawatafuta

wazee, tunaongea nao ili waweze kukunyooshea mambo yako. Sasa mambo yako yananyooka kutokana na wazee halafu hawa wazee tumewaacha, tumewasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tuambiwe je, kuna ugumu gani kuweza kuleta Muswada huo Bungeni? Kama siyo tatizo, je kwa nini tunawahadaa hawa wazee na tutawahadaa mpaka lini wazee kila siku wanapiga *mark time* hapa Bungeni, wanatumia hiyo nauli ndogo wanakuja kuuliza jamani vipi Muswada wetu kwa ajili ya kulipwa pensheni. Mheshimiwa Waziri tunaomba majibu kuhusu suala la wazee siyo utani tena hiyo imepitwa na wakati, tunataka wazee wetu waishi maisha mazuri, wazee wasihangaike pamoja na wale wazee wanaodai madai yao pia walipwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri wa Kazi ameambatana vilevile na Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi TUCTA, Ndugu Hezron Kaaya na ameandamana na Wawakilishi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO). Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Sanya.

MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kidogo kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba sana Wizara iangalie mambo matatu, ajira, wanaoajiriwa wakiwa kazini na wanapostaafu. Hii idadi tuliyopewa ya miaka mitatu ya ajira ya 630,000 ni ndogo sana yaani kutoka mwaka 2008 - 2014. Nataka niseme kwamba Serikali yoyote duniani haiwezi ikatoa ajira za kutosha kwa raia wake, wawe vijana au watu wazima. Kitu cha kuangalia zaidi ni kujenga mazingira ya kiuchumi yatakayowafanya vijana kuajiriwa katika sekta binafsi au kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Mapinduzi kule Zanzibar, Marehemu Mzee Karume alifungua vyuo vya kuwasomesha vijana kazi za amali. Chuo kimoja kilikuwa Gulioni kikisomesha mambo ya kutengeneza bomba za maji na umeme, kingine cha fenicha *Mikunguni Trade School* na kilitoa *product* nzuri sana mpaka hii leo hao wazee wamejiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini cha kufanya sisi? Tuongezeni vyuo vya amali kwa sababu Mwalimu Nyerere, Baba wa Taifa yeye kwa upande wa Bara akaanzisha *Folk Development Colleges* ambazo baadaye ndiyo tumezi-*convert* zikawa ni *VETA*. Hata hivyo, tuangalie Tanzania hii kwa asilimia ya vijana

tuliyonayo ni vyuo vingapi vya *VETA* ambavyo vinatoa nafasi kwa vijana hawa kuweza kufundishwa hizi kazi za amali yaani kazi za mikono?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, ukiangalia hata hawa ndugu zetu wa *NSSF* tunaowasifia sana hapa, ni wajibu wetu sisi tuwaelekeze washirikiane na Shirika la Nyumba kujenga *malls* katika Miji Mikuu ili kupunguza ongezeko la vijana barabarani na badala yake wajiajiri kwa biashara zao ndogondogo katika *malls* hizo. Mifano mizuri ipo, *congestion* ya Dar es Salaam itapungua na kama mtakwenda Malyasia mtaona ni namna gani Serikali ya Malyasia ilivyowajengea vijana maeneo kama haya na Thailand, Vietnam, Zimbabwe mkienda mtaona ni namna gani *free market* zao zinavyoajiri vijana wao wanaita *Sunday Market* wanapakuwa wanapata fedha kwa kufanya biashara zao ndogondogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma wale Walimu wa Vyuo Vikuu waliokuwa wakifundisha Vyuo Vikuu walikuwa na chombo kinaitwa SSS *(Senior Staff Superannuation Scheme)*. Bahati mbaya Walimu hawa hawakutakiwa au hawakupewa nafasi ya kujiunga na Mfuko wa *PPF* ulioanzishwa mwaka 1978. Baada ya kuvunjika *East African Community* wakaomba kujiunga wakakataliwa, wakastaafu wale waliostaafu wakapata *only one gratuity* yaani mkupuo mmoja tu wa fedha. Shirika la Kazi Duniani linasema kwamba *pension* ni haki ya kila mfanyakazi hawa hawakupewa pensheni. Matokeo yake mpaka Machi, 2011 waliobakia ambapo wengine walishastaafu wakajiunga huku, wao wakapata nafasi wanapomaliza wanapata fedha zao na wanapomaliza wanapata pensheni zao. Hawa Walimu ni Watanzania, ni *product* yetu na walijitahidi sana kuwafundisha Watanzania na wengine wamo humuhumu ndani ya Bunge. Inawezekana hata Mheshimiwa Waziri pengine kapitia katika vyuo hivi na Walimu hawa ndio waliomsomesha. Naomba muwafikirie walau na wao wapate pensheni waweze kujikimu katika kipindi chao cha maisha kilichobakia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la kuchekesha kwamba sisi Wabunge tunapitisha Miswada ya Sheria humu ndani, hapo nje kuna vijana wetu wa Magereza wanajenga jengo letu la Bunge zuri sana lakini pita uwaone, hawana *mask,* hawana *gloves* na wanajenga jengo la wanasheria, sisi tunapindisha Sheria hizo. Nakutaka Mheshimiwa Waziri leo ukitoka na wataalam wako jaribu kupita na gari uwaone vijana wetu wanavyofanya kazi bila vifaa husika au hawapewi haki zile kwa sababu wao ni wafungwa lakini wanazalisha, wanajenga jengo letu, wanacheza na vumbi, hawana *mask,* wanacheza na vitu vizito hawana *gloves,* tunasema nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi Mheshimiwa Waziri sina matatizo na wewe leo, isipokuwa nakuomba uongeze vyuo na ndiyo ukaona China imeinuka ghafla kwa sababu Mao Tse Tung alikuwa na mpango kabambe wa

muda mrefu wa kusomesha vijana wake. Mfumo wa kibiashara wa dunia ulivyogeuka ghafla akawa na *manpower* ya kutosha na leo China inaongoza kiuchumi kwa sababu vijana wao wamefundishwa namna ya kufanya kazi bora na namna ya kujifunza kutengeneza vifaa ambavyo leo vimeenea dunia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Kuruthum ajiandaye Mheshimiwa Lissu, Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Mtanda.

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama hapa nikiwa na afya nzuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunatambua mchango mkubwa sana unaofanywa na Mashirika ya Hifadhi katika nchi yetu. Hata hivyo, ilio kikubwa na hata hotuba ya Kambi ya Upinzani imesema kwamba Serikali imekuwa na tabia ya kutumia vibaya pesa za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CAG* anatukumbusha kwa mfano, Serikali ilitoa dhamana kupitia *NSSF* kwenda Kiwira takribani shilingi bilioni 6.65 lakini ziko wapi? Pia dhamana ilitolewa kupitia Mfuko wa *NSSF, PSPF* na *CRDB* kwa jumla takribani shilingi bilioni 28 kwenda Kiwira na Serikali ndiyo ilitoa dhamana katika Shirika au ile Kampuni ambayo ingekuwa haikopesheki, lakini pesa zile zimekwenda, za wananchi ambazo waliwekeza kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na hazina tija mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfano mwingine katika Jimbo lako wa *Machinga Complex* zimekopwa fedha kutoka kwenye Mifuko lakini zimetumika pale mpaka leo hazina tija. Ule ni mkopo, unalipika vipi na tija kwa wananchi ikoje? Kwa hiyo, nakubali kabisa kwamba Mashirika ya Hifadhi ni muhimu sana lakini pesa zake zinatumiwa vibaya na Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekti, katika ukurasa wa 12 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri anazungumzia suala la ukuzaji wa ajira nchini. Tumekuwa mabingwa sana hapa kwa Serikali kutuletea matamko, maazimio na vitu vingine wakisema kwamba tunaboresha suala la ajira kwa vijana. Mheshimiwa Waziri kama unakumbuka mwaka jana Wizara ya Kilimo ilikuja na mpango kabambe hapa kwa ajili ya kuwezesha ajira kwa vijana kupata mkopo kupitia Benki ya *CRDB* ili vijana wapate mikopo, wafanye kilimo cha kibiashara. Kaka yangu Kigwangalla kasema ni kweli. Sasa zimekuwa ni kama kanyaboya, maneno, chengesha bwege, maneno ambayo kwa kweli hayana tija. Hatuwezi kuwavumilia kwa kuja na mipango mizuri, tunafanya maazimio mazuri,

lakini hayatekelezeki. Tulisema vijana tutawakopesha kupitia *CRDB* waweze kujiajiri kwa sababu ajira kwenye sekta zilizo rasmi zimekuwa finyu. Mpaka sasa Mheshimiwa Waziri niambie ni vijana wangapi wamenufaika kupitia *CRDB* kwenda kujiajiri katika sekta ya kilimo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Wizara nyingine kuhakikisha kwamba masuala ya ajira kwa vijana yanatekelezeka. Kwa mfano, Maliasili, kwangu kule Rufiji vijana wengi ni wachongaji, wanachonga vitanda, viti na vitu vingine kuleta Dar es Salaam lakini Maliasili sasa wamepitisha, kwa mfano kijana akichonga kitanda chake pale Rufiji, kijana wa Ikwiriri, kijana wa Muhoro, kijana wa Utete, zamani alikuwa anatoa shilingi elfu sita kwa ajili ya kupeleka kitanda Dar es Salaam anakileta sokoni lakini sasa kitanda kinapelekwa kwa Sh.120,000/=. Sasa vijana wengi walichukua mikopo kwenye *VICOBA*, kwenye *SACCOs* kwa ajili ya kufanya kazi zile, sasa mikopo hailipiki, vijana wanashindwa kufanya ile kazi. Halafu tunasema tunahamasisha ajira kwa vijana, vijana watapata ajira kutoka wapi? Mheshimiwa Waziri vijana hawa hawajasoma, hawana hizo digrii zenu lakini vijana hawa wana nguvu zao na fani zao, sasa mnawabana, hawawezi kufanya chochote hivi mnategemea vijana hawa ambao tunawazalisha kila siku kukosa ajira watafanya shughuli gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ndiyo haya sasa Dar es Salaam tunasikia kuna 'panya *road'*, vijana hao, Zanzibar kuna vijana wanaitwa 'ubaya ubaya'. Sasa inakuwa ni kazi ya kupora, kuingia mtaani, Polisi watawachukua watawaweka ndani, lakini sasa kama Serikali mmefanya juhudi gani za kuhakikisha vijana hawa wanaachana na mambo hayo ya uporaji na vitendo ambavyo havifai, kwa sababu ninyi wenyewe ndiyo mnawagandamiza. Naomba namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze Wizara yake ina mkakati gani wa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Kilimo kuhakikisha kama vijana hawa wanapata ajira kama tulivyokusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengi wameongelea suala la pensheni kwa wazee. Imekuwa ni hadithi, Serikali hii sikivu kila siku inasisitiza kwamba wataleta, hawaleti. Wazee wetu wanateseka na maisha ni magumu kule vijijini. Tunaomba suala la pensheni kwa wazee lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira mabaya kazini, vijana, watoto wetu, kazi katika migodi, kazi katika kampuni hasa hizi za ujenzi. Kwa mfano, vijana wa *Strabag* pale. Hivi kweli kijana anafanya kazi kwenye Kampuni analipwa Sh.5,000/=, Sh.3,000/- inamsaidia nini katika maisha ya sasa? Cha kusangaza sehemu zilezile za kazi kwa mfano *Strabag* na sehemu nyingine, wageni wenye uwezo sawa na vijana wa Kitanzania wanalipwa pesa nyingi kuliko vijana wa Kitanzania, nini tatizo? Mheshimiwa Waziri naomba utuambie leo kwa nini

wageni wanaokuja hapa nchini na wengine hawana hata huo ujuzi wanafanya kazi zilezile ambazo zinafanywa na vijana wetu wa Kitanzania, vijana wetu wananyanyasika, vijana wanapata pesa nyingi, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tunawekeza tunapata makampuni ili vijana wapate ajira, mbona vijana wananyanyasika? Mimi naomba Mheshimiwa Waziri atupe majibu kwa nini wageni wanaokuja katika nchi yetu wanathaminika na kupata pesa nyingi kuliko wazawa ambao wana elimu ileile na ujuzi uleule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Sanya kasema hapa mfumo wa elimu tulionao kwa kweli hauwajengei vijana wetu uwezo wa kujiajiri. Kila siku tunalalamika mfumo wa elimu hauruhusu vijana wetu kujiajiri. Vijana wanakariri elimu ambayo hawana tija nao. Sasa je, Mheshimiwa Waziri tunawasaidiaje vijana hawa kuwa na mfumo wa elimu ambao utawawezesha vijana kuweza kujiajiri, kuacha ile akili kwamba wao lazima wataajiriwa. Tunaona ajira katika Serikali zimekuwa finyu. Sasa tunawasadiaje vijana hasa katika mfumo wa elimu ili wajue kwamba wanapomaliza masomo yao moja kwa moja wataweza kujiajiri badala ya kutegemea tu kuajiriwa. Mheshimiwa Waziri naomba utupe jibu hasa katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naendelea kusisitiza suala la mikopo kwa vijana.

(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lissu jiandae Mheshimiwa Jafo.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kusema kwamba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni Ofisi ya Kikatiba kwani imeundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na majukumu yake vilevile ni majukumu ya Kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na kila anapofanya ukaguzi wa hesabu za Serikali, za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma anapeleka ripoti yake kwanza kwa Rais halafu ndiyo inaletwa Bungeni. Taarifa ya Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaletwa Bungeni kwa sababu jukumu nambari moja la Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kulipa Bunge taarifa muhimu juu ya matumizi ya fedha za umma ili Bunge litimize wajibu wake wa kuisimamia Serikali, wa kuishauri Serikali na wa kuiwajibisha Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka Mdhibiti na Mkuu wa Hesabu za Serikali analeta taarifa humu Bungeni na kwa miaka mitatu mfululizo ambayo tumekaa humu Bungeni tangu mwaka 2010, kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali analalamika kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii inatumia fedha zake kuwekeza katika miradi ambayo haina tija kwa Mifuko, haina tija kwa wafanyakazi ambao ndiyo fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu ni za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, shilingi bilioni 661 ambazo mifuko imewekeza katika miradi mbalimbali mpaka sasa hivi hazijalipika. Hizi ni fedha za wafanyakazi, zilipaswa ziwekezwe katika miradi halafu zirudishwe na zirudishwe kwa riba. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anasema hazijalipwa, hizo fedha hazilipiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anasema kwenye taarifa yake ya mwaka huu, iliyoletwa humu mwezi huu kwamba *PSPF* peke yao nakisi ya uwezo wa kulipa wanachama wao ya shilingi trilioni 6.49 fedha za wafanyakazi ambazo zimewekezwa katika mambo mbalimbali na haya siyo maneno ya sisi Wabunge, maneno ya aliyepewa jukumu la kutueleza matumizi ya fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hizi taarifa za miaka mitatu mfululizo za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya matumizi mabaya ya fedha za Mifuko kwenye miradi ambayo inafanya hela hazilipiki ni za kweli au si za kweli? Mdhibiti anatudanganya au Serikali ndiyo inatudanganya? Haiwezekani wote wawili wakawa sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amesema mwaka huu, tatizo ni Serikali kuingilia kazi na maamuzi ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii ndiyo maana hali ya kifedha ya Mifuko hii imezorota. Haya ni maneno siyo yangu ni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mheshimiwa Waziri atusaidie hii kauli ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Mkuu wa Hesabu za Serikali yeye anaionaje? Ni ya kweli au ni porojo tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za wafanyakazi wetu, mimi ni Mheshimiwa Mbunge na wote humu ndani ni Wabunge. Nafikiri sitasema uwongo nikisema kila mmoja wetu amelalamikiwa na wapiga kura wetu hatujalipwa fedha *NSSF, PSPF,* wastaafu wetu wanataabika, hawalipwi mafia yao, ni shida tupu kwa sababu kwa mujibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali fedha

za Mifuko zimepelekwa katika miradi ambayo kwa maneno ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu *they are none performing, they are none performing* kwa maana ipi? *They are none performing* kwa sababu fedha hizo hazijarudishwa, tuleteeni majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi baadhi yetu humu ndani ni wanachama wa *NSSF*, ni wanachama wa Mifuko hii. Tusidhani kwamba kuwasifusifu, basi hela zetu zitakuwa salama sana. Kesho na keshokutwa hatutakuwa Wabunge, tumewekeza huko, hela zetu ziko salama kiasi gani? Mheshimiwa Mwenyekiti,

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa hizi, *finally* sifa hizi zina sababu yake. Nina nyaraka hapa na barua zinazoonyesha Wabunge mbalimbali wa Bunge hilihili ambao wamechukua fedha za Mifuko hii kwa sababu mbalimbali. Tunaomba baadaye Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili liunde Kamati Teule tuchunguze hii Mifuko na … *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Lissu. Sasa namwita Mheshimiwa Jafo, jiandaye Mheshimiwa Mtanda na Mheshimiwa Ridhiwani.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata fursa hii japo na mimi niweze kuongea machache sana katika mchana huu wa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza napenda kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa sana inayofanya, hilo ni la jambo msingi. Sambamba na hilo nipende kupongeza sana Taasisi zote za Wizara hasa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kazi kubwa wanayofanya kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipa changamoto Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu wako na Timu yako mna kazi kubwa sana ya kufanya kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu hili. Tukizungumzia suala la kazi, hivi sasa tuna vijana wengi wanaomaliza Vyuo Vikuu, tunaomba sasa msikae maofisini, tunaomba mfanye kazi kutafakari jinsi gani mtalinusuru Taifa letu letu hili. Maana sisi kama Wabunge hapa haturidhiki kuona Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wenu mnakaa Ofisini bila kutafuta jibu muafaka kwa ajili ya mustakabali wa Taifa letu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana wengi wanapata taabu. Sasa hivi wengine ni *graduates* wamemaliza miaka mitatu, minne hawana kazi wako mtaani. Mimi nina imani kwamba Timu yako ikifanya kazi vizuri itaweza

kututatulia tatizo hili. Mheshimiwa Waziri nakujua, ni kiongozi shupavu sana, naomba uongeze juhudi katika hilo. Naomba uangalie ni jinsi gani uwekezaji wetu katika nchi na ikiwezekana Wizara yako ishirikiane na Wizara zingine hasa Wizara ya Kilimo ili tuweze kutatua fumbo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina imani, tutakapopata wafanyakazi wengi, hata hii Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii itakuwa na wanachama wengi wa kuweza kuchangia. Hata hii miradi ambayo inaelekezwa moja kwa moja katika kukwamua nchi yetu itaweza kupata tija kubwa sana kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hii ni changamoto tunaomba tuifanyie kazi kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapojisifu kwamba Dodoma tuna Chuo Kikuu cha *Dodoma University* ambacho ni Chuo cha mfano Tanzania na *East Africa,* jambo hili limefanywa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuona kwamba Mifuko hii inafanya kazi na kuweza kuwa na wanachama wengi ili iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia daraja la Kigamboni ina maana kwamba hatuna mtaji mwingine isipokuwa ni Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii inafanya hivyo. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kusema kwamba Tanzania hii tunataka tupate wafanyakazi wengi ambao watachangia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naliomba sana, tulikuwa tunasubiri toka muda mrefu, Sheria ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, tulikuwa na changamoto kubwa sana hapa katikati. Nina imani ule Muswada utakuja Bungeni. Lengo letu tuweze kuufanyia kazi kwa pamoja kwa ajili ya mustakabali wa wafanyakazi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kuishauri Mifuko. Sasa hivi Tanzania tuna Balozi zetu nyingi sana nchi za nje ambazo hali zake ni mbaya. Tuna viwanja vya Serikali nje ya nchi, tuna majengo yetu yaliyochakaa huko nje, kwa mfano ukienda Ubalozi wa Maputo peke yake *apartment* moja ukijenga pale Maputo kwa mwezi mmoja siyo chini ya dola 10,000 na tuna viwanja vingi sana nje ya nchi hii. Sasa mimi naona kama ikiwezekana Serikali iangalie jinsi gani itatumia Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii katika viwanja mbalimbali vilivyoko Ofisi za Mabalozi nchi za nje kwenda kuwekeza na kujenga huko. Inawezekana Balozi hizo ambazo kila mwaka hapa tunazitengea pesa inawezekana kumbe pesa zingekuwa zinajitengeneza zenyewe huko huko. Naiomba sana Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii iangalie jinsi gani itafanya utaratibu mzuri kwa ajili ya kuwekeza katika Ofisi za Mabalozi hasa kujenga Maofisi ya Mabalozi na sehemu mbalimbali za kibiashara. Ninaamini tutakuwa tumepata mafanikio makubwa sana katika nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala zima la wafanyakazi hasa wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Nataka niwaguse wafanyakazi wa migodini. Naomba sana Wizara, wengine wameshazungumza, upitie huko migodini. Kuna wafanyakazi wengine ambao wako katika mazingira magumu kweli kweli hasa wanaofanya kazi katika Sekta ya Migodi. Wafanyakazi wale wengine hali zao sio nzuri wanaumwa na wakishaumwa tu wanaachishwa kazi. Naomba Waziri uende kulifanyia kazi jambo hili, ni kero sana kwa vijana wetu wa Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kuna sekta zingine wakienda kufanya kazi, wanakuwa *black listed* kwamba mtu huyo akiachishwa kazi hawezi kupata kazi sehemu nyingine yoyote. Hii inanyima haki Watanzania wa Taifa letu hili. Waziri ukiangalia katika maeneo hayo itasaidia sana hasa kuhakikisha kama vijana wa Kitanzania wanapata kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa sababu mimi mwenyewe nimeshatembelea migodi mingi. Kule utakuta wafanyakazi wengi wa Tanzania wanalalamika. Naamini tukienda kulifanya vizuri hili tutakuwa na vijana wetu ambao wanafanya kazi kwa ajili ya mustakabali wa nchi yao na tukijua kwamba hawa watu lazima tuwalinde pindi wanapotumikishwa na haya makampuni na wanapoachwa wakiwa wagonjwa na bila kuhudumiwa maana yake tunapoteza nguvu kazi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nawaomba sana, tunajua kwamba, kuna kazi kubwa inafanyika huko, tunajua kwamba tunajivunia kila sababu tunayoiona huko, naomba ikiwezekana ule uwekezaji wenye tija uzidi kuendelea kama kawaida. Mwisho wa siku ni kwamba watu wote wa Tanzania tuweze kunufaika. Mimi kama Mbunge kwa kweli lazima nisifie kwamba Mifuko hii yetu inafanya kazi kubwa sana kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu. Leo hii kama mtu anasema kwamba kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma sio jambo la msingi, basi nadhani mtu huyo atakuwa na matatizo katika Taifa letu hili. Leo hii mtu akisema kwamba kujenga daraja la Kigamboni sio jambo mwafaka, naamini Mtanzania huyo atakuwa na matatizo katika Taifa letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina imani kwamba inatakiwa sasa Wakurugenzi Wakuu waangalie jinsi gani *investment* zao zitasaidia katika suala zima la kuijenga nchi yetu lakini halikadhalika kuhakikisha Mifuko hiyo inasimama imara kwa ajili ya kuleta mustakabali wa Taifa letu na haki za wafanyakazi ambao wanachangia michango yao, mwisho wa siku wanapostaafu waweze kupata michango yao. Mheshimiwa Waziri, kuna wafanyakazi ambao waliachishwa kazi katika mashirika mbalimbali. Wafanyakazi wale waliambiwa mpaka wafike muda wao wa kustaafu ndio wapewe mafao yao; watu wale sasa hivi mtaani wanahangaika, wengine

walifanya *TTCL* na mashirika mbalimbali. Wengine waliachishwa kazi wanasubiri mpaka wafikishe ule muda wa kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba alifanyie kazi suala hili, kipindi kilichopita tumelizungumza, kero ile bado inaendelea; hawa ni Watanzania na wengine wamekufa kabla ya kupata haki zao. Hatutakuwa Wabunge imara kama kuona kwamba kuna Watanzania wengine wameachishwa kazi wanasubiri kwanza mpaka muda wao wa kustaafu ufike ndio walipwe mafao yao na wanazidi kupoteza maisha yao na maisha yao yanakuwa katika mazingira magumu. Hatutakuwa radhi katika hilo. Mheshimiwa Waziri tunakuamini sana, chapa kazi tuko nyuma yako kwa ajili ya mustakabali wa Tanzania yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtanda, Mheshimiwa Ridhiwani na Mheshimiwa Hokororo.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ili na mimi niweze kujadili hoja hii ya Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwa mujibu wa Kanuni zetu naomba ku-*declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii ambayo Wizara hii ni miongoni mwa Wizara ninazozisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia moja hoja hii na ningeomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuunge mkono hoja ya Wizara hii kwa sababu mipango ambayo imo kwenye Kitabu cha Bajeti mwaka huu, sisi Kamati tumeridhika kwamba inaweza kusaidia ingawa ziko changamoto nyingi ambazo tunataka Serikali iziangalie ili mambo yaweze kwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uwasilishaji wa ripoti yangu tumeelezea mambo mengi, ikiwemo *pension* kwa wazee, fedha za Mfuko wa Vijana hizo shilingi bilioni tatu na mambo mengine. Nimepata pia fursa ya kusoma ripoti ya Kambi ya Upinzani; ukiiangalia *theoretically* ina mambo mazuri na nampongeza Waziri Kivuli kwa kuibua changamoto nyingi isipokuwa upungufu mkubwa upo katika kushauri kwa sababu nia kubwa ya Bunge ni kuishauri Serikali nini kifanywe ili tuweze kwenda mbele zaidi. Kwa hivyo, ripoti hii ya Upinzani imejaa malalamiko na manung'uniko lakini haitoi *solution* kwa matatizo ya ajira kwa vijana. Sasa kama viongozi nia yetu kubwa ni kuisimamia na kuishauri Serikali, sio kulalamikalalamika. Kwa hiyo, naamini Waziri Kivuli, Rafiki

yangu Pareso ni mtu mwenye uwezo, awamu ijayo ataboresha taarifa yake na itakuwa bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze mambo machache sasa baada ya kueleza juu ya hali hii ya ripoti ya Upinzani. Kwanza niwapongeze sana wenzetu wa *HelpAge International* wakiongozwa na Ndugu Smart kwa kuwa wamekuwa mstari wa mbele sana kupigania haki na maslahi ya wazee nchini. Mimi pia kama Mwenyekiti, tumekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba wazee wanajengewa mazingira bora na salama kwa ajili ya maisha yao. Wazee ni watu muhimu, tunawatambua na nimepata fursa ya kukutana na wazee mara kwa mara. Ushauri wao ndio unaonifanya niwe kiongozi mzuri leo hii, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mkoani Lindi yuko Mzee Majumba ambaye kwa kiasi kikubwa anatusaidia katika kukabiliana na changamoto za wazee. Nampongeza na kumwomba aendelee na kazi hiyo na sisi tutaendelea kuwasaidia wazee kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa Wabunge wenzangu, yako maeneo na yako mambo tunaweza kuyafanya katika maeneo yetu na kuinua hali za wazee. Kwa mfano, Halmashauri yangu ya Lindi, tayari tumeandaa vitambulisho kwa ajili ya wazee hawa wanapokwenda Hospitali kutibiwa bure, tuisimamie hii Waheshimiwa Wabunge kwenye maeneo yetu. Wale wazee ambao bado hawajapata vitambulisho hivi wapatiwe ili wasipate usumbufu wanapokwenda kutibiwa. Changamoto kubwa ni kwamba tunaomba Serikali ikija na Mfuko huu wa Pensheni kwa Wazee, wazee wale wenye umri mkubwa kwa sababu sasa hawajiwezi, tuwatambue na hatimaye tuanzishe Mfuko huu ili waweze kuneemeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia juu ya tatizo la ajira. Wako vijana maeneo mengi ya vijijini wanahangaika huku na kule, wanaweka mkazo katika kilimo. Tunaomba Serikali kupitia Wizara hii na Wizara ya Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi, kuona sasa iko haja ya kuwekeza kwenye maeneo ya vijiji hasa katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Jimboni kwangu Mchinga, tumefanya *training* ya vijana waendesha Bodaboda. Nilivyofanya sensa nikapata vijana 500, tumehakikisha wamepata *training* ya mafunzo ya usalama barabarani na vijana wale wote 500 wamepata leseni, wengine wakitoka Lindi Mjini kwa Mheshimiwa Barwany. Changamoto kubwa sasa ajira ile si ya kudumu, tunawataka sasa wajiunge kwenye vikundi vidogovidogo vya uzalishaji mali na hasa wawekeze nguvu zao kwenye kilimo. Mkoa wa Lindi ni maarufu kwa kilimo cha ufuta kwa hivyo, Serikali tunaiomba sasa iwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii kwa mfano *NSSF,* kupitia huu mpango wa *Suplimentary Scheme* hasa *Mkulima Scheme* kwenda Lindi, kwenda Mchinga, maeneo ya Nangaru, Rutamba, Milola, Kiwawa, Mvuleni, Mipingo mpaka Kitomanga ili wakulima wale waweze kuandikishwa kwenye Mifuko hii ya *Suplementary Scheme* hasa inayomhusu mkulima ili waanze kupata pembejeo. Mpaka Mpigamiti, Liwale huko waje tu, hakuna tatizo, ili waanze kupata pembejeo, waanze kupata vitambulisho kwa ajili ya matibabu, nadhani hii itatusaidia sana. Wale vijana ambao wako pale Rutamba, wako kule Milola, wanaojihusisha na uendeshaji wa Bodaboda, ajira ya kudumu ni katika sekta ya kilimo lakini vijana hawawezi kulima kama hawajawezeshwa matrekta.

(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Namwita Mheshimiwa Ridhiwani, ajiandae Mheshimiwa Hokororo na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Nassib Omar.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pia nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya yeye pamoja na Wakuu wake wa Mifuko ya Jamii, akina bwana Dau, akina bwana Erio, kazi nzuri sana tunaiona. Sisi ndani ya Jimbo la Chalinze tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na hayo, nataka nizungumzie sana jambo la ajira kwa vijana. Ziko Taasisi zilizo chini ya Wizara hii, kwa mfano wenzetu wa *OSHA,* wanafanya kazi nzuri kwa kweli, lakini katika maeneo mengi ambayo mimi nimepata bahati ya kwenda kuyafikia, nachokiona wale *OSHA* wanatoa taarifa kwamba, kesho nakuja, basi ndani ya ofisi ile wanajiandaa; ukitaka *helmet* utapewa, ukitaka *gear* za kufanyia kazi viatu, *gloves,* zote utapewa lakini si mazingira yanayofanyika bada ya wakaguzi wale kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwangu nilikuwa nataka nitoe rai kwa wenzetu hawa wa *OSHA* waendelee kufanya ukaguzi huu na hata wakati mwingine bila ya kutoa taarifa ili waweze kubaini upungufu huu. Haya tunayaona katika maeneo kama ya migodini kule, tunapoona vijana wetu wanazidi kuharibikiwa, wengine wanakosa *gear* za kuwasaidia kuwalinda, haya yote naamini kwamba yanawezekana utaratibu mzuri ukipangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Chalinze imeendelea kukua na katika ukuzi wake yako maeneo muhimu sana ambayo mimi ningependa kuyazungumza hapa mbele ya Mheshimiwa Waziri. Kwa mfano, tumeshuhudia jinsi wenzetu wa *NSSF, PSPF* na *PPF* wanavyoendelea kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Ni imani yangu kwamba sasa muda umefika wa kuanza kuangalia jicho la pili la utatuzi wa matatizo ya ajira. Waje wajenge Kituo kikubwa pale cha biashara Chalinze kwa sababu Chalinze ndio sehemu inayounganisha watu wote wanaotoka njia ya Kaskazini na watu wote wanaotoka njia ya Nyanda za Juu Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakuja tukawekeza pale Kituo Kikubwa cha Biashara hakutakuwa na sababu ya mtu anayetoka Mbeya kwenda mpaka Dar-es-Salaam kufuata simenti. Hakutakuwa na sababu ya mtu anayetoka Arusha na Moshi kwenda Dar-es-Salaam kufuata nondo, vitu vyote vitapatikana Chalinze. Pia hii kwa upande wa pili itatusaidia pia kuendelea kulinda barabara zetu ambazo kwa namna moja au nyingine zimeendelea kuzidiwa kutokana na wingi wa mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumeshuhudia juzijuzi hapa juu ya suala zima la ajira lilivyokuwa ni tatizo. Leo hii mtu ametoka shuleni, ametoka Chuoni ana *First Class, Second Class* nzuri tu, anaambiwa kwamba kwenye ajira anatakiwa uzoefu wa miaka mitano, hili jambo si sawa. Hawa vijana au hawa wafanyakazi wanapata *experience* baada ya kufanya kazi; mtu hujaampa kazi, leo hii unamwambia eti alete *experience* ya miaka mitano, ataitoa wapi Mheshimiwa Waziri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo si sawa, muda mumefika sasa tuanze kuangalia. Watu wapewe ajira ili waweze kujenga uzoefu, waweze kupata maarifa ya kuona jinsi gani wanaweza kuitumikia nchi yao. *Otherwise* tutakuwa kila siku tunaendelea kupiga kelele hapa, vijana wametoka vyuoni hawana ajira, atapata wapi ajira kama vigezo vyenyewe vya kupata ajira ni uzoefu wa kipindi cha miaka miwili, mitatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ziko baadhi ya Ofisi za Serikali na Mifuko hii ya Jamii utaona ajira zimetangazwa kwenye magazeti nzuri tu na kijana anaona kabisa ana-*qualify,* lakini ukienda pale tayari mtu keshapewa ajira. Lazima sasa ajira hizi ziwe wazi, haiwezi kufikia sehemu Mheshimiwa Waziri ikawa kwamba tunafanya mchezo wa vijana wetu kujaza makaratasi wakati watu ajira tayari mmeshawapa. Tumeyaona haya yanatokea katika maeneo ya *TRA* na hili ni jambo ambalo lazima tulikemee. Tuna imani kwamba sasa mambo yatakaa vizuri na vijana wetu wataanza kupata ajira na tukija humu hakutakuwa tena na malalamiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nirudie tena suala la Chalinze. Tunayo miradi mizuri pale ya kufanyika, tunataka Chalinze sasa ipanuke Mheshimiwa Waziri. Tunayo shida kubwa pale ya stendi ya malori, tunayo shida kubwa pale ya stendi ya mabasi, Chalinze ndio kiunganishi. Leo hii mtu anayetoka Mbeya hawezi kwenda Dar-es-Salaam kufuata mahitaji yake kama hakupita Chalinze; mtu anayetoka Mwanza, Arusha, Tanga, hawezi kufika Dar es Salaam bila kupita Chalinze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kwamba kazi hii nzuri inayoendelea kufanywa na *PSPF, PPF* na *NSSF* sasa mtaangalia Chalinze kama sehemu ambayo mnaweza mkaiweka vizuri. Hata na ninyi wenzangu mnapotoka Dodoma kabla hamjafika Dar-es-Salaam mnapita Chalize kwa hiyo pia mtaingalia Chalinze kwa namna hiyo. Tuondoe malori pale barabarani, tuweke mazingira vizuri. Mimi nina imani Mifuko hii ya Jamii inaweza kutusaidia sisi pale na hata wenzetu wa Mlandizi pale nao mkawawekea vizuri, mambo yakakaa vizuri pale, ili biashara iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana, naunga mkono hoja, lakini Mheshimiwa Waziri, haya mambo ukiyaangalia basi nchi yetu hii nayo itakaa vizuri, hata mipango ya maendeleo nayo itaweza kusimamiwa vizuri. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Hokororo ajiandae Mheshimiwa Nassib Omar, ndiye mchangiaji wetu wa mwisho.

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko Mezani. Kwanza naomba niipongeze Wizara inayoongozwa na mama mwenzetu, anaweza na kwa kweli, amekuwa akiitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Watendaji wengine na hasa Taasisi zote zilizopo katika Wizara hii. Ukiangalia kwenye Wizara hii ina Taasisi nyingi za Umma, wapo *OSHA, TaESA, NIP, NSSF, SSRA* na *CMA*. Zote hizi zimekuwa zikifanya kazi zake vizuri bila kujali mazingira yao ya kazi kama ni magumu pamoja na kwamba kwa kipindi cha miaka minne sasa Kamati ya Maendeleo ya Jamii imekuwa ikisisitiza na kuiomba Serikali kuongeza tengo la bajeti kwa sababu bajeti ya Wizara hii kwa kweli, ukilinganisha na majukumu waliyonayo bado imeendelea kuwa ndogo. Niiombe na niishauri Serikali, ni vema kulinganisha majukumu yaliyopo katika Wizara hii, tukiangalia kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama hapa anaona na hata Taarifa ile ya Kamati yetu na ya Kambi ya Upinzani, kwa kweli majukumu waliyonayo Wizara hii ni mazito, hayalingani na bajeti ambayo inatengwa mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wanahusika na ukuzaji wa ajira, haki, Sheria, Kanuni na Taratibu za Kazi na hasa pale tunapotaka sasa kuwatetea hata watoto wetu wanaokumbana na ajira zile hatarishi. Kwa hiyo, niombe na nisisitize kwamba ni vema Serikali ikaona namna ya kuongeza bajeti ili ikatekeleze majukumu yao kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati na naomba pia nisisitize mambo machache. Katika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 13, ameonesha pale namna ambavyo Wizara yake imefanya au inatarajia kutekeleza suala zima la kuwajengea uwezo vijana. Mimi naishauri Serikali na hasa Wizara hii, ilitekeleze jambo hili kwa kushirikiana na Wizara nyingine kama vile Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Fedha. Hili naliomba hususan katika Mkoa wa Mtwara. Mkoa wa Mtwara kuna gesi, sekta hii hapa nchini ni mpya lakini tunaweza tukaona na tukaendelea kuchekelea bila kuwanufaisha vijana wa Mkoa wa Mtwara, itakuwa pia haina tija kwa hao vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba, Mheshimiwa Kabaka Wizara yako katika kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo vijana wa Mkoa wa Mtwara ni vema ukashirikiana na hizo Wizara nyingine. Suala kubwa kwa kweli naloliomba ni kuwawezesha vijana wa Mkoa wa Mtwara waweze kupata elimu na mafunzo katika kutoa huduma mbalimbali katika Mkoa wa Mtwara. Pia waweze kupata ujuzi wa kuajiriwa na kujiajiri katika sekta mbalimbali na lingine vijana wa Mkoa wa Mtwara wanahitaji kuwezeshwa shughuli za vijana wanazozifanya wao kwa asili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa tukihusika na kilimo cha korosho. Tumekuwa tukifanya uvuvi, kama tunavyojua kwamba kule kuna bahari, lakini tumekuwa tukilima karanga na mazao mengine. Ni vema Wizara ikawawezesha vijana katika vitu vyao vya asili ili waweze kutumia hizo fursa walizonazo kwa umakini na zikawaletea tija. Naomba katika uwezeshaji huu wa vijana isiangaliwe tu vijana wa Mtwara Mjini, waangaliwe vijana wa Masasi, wa Nanyumbu, wa Newala, wa Tandahimba, Mtwara Vijijini na Mjini na hao wawezeshwe kwa kiasi cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, naomba nizungumzie kidogo suala la Mfuko wa Pensheni kwa Wazee. Naunga mkono mawazo yaliyotolewa na Kamati na Wabunge wengine na hasa tukisisitiza kwamba suala hili ni muhimu. Upo usemi unaosema kwamba chezea ujana fainali ni uzeeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa mtazamo wangu sikubaliani na ule mtazamo unaoonekana kwamba wazee ambao hawakushiriki katika mfumo rasmi wa uchangiaji wa pensheni wao wasihusike. Kwa sababu, wazee wa Mtwara wanalima korosho na wazee wengine katika Mikoa mbalimbali yapo

mazao kwa mfano kahawa, pamba, wamekuwa wakiliingizia Taifa hili fedha za kigeni. Je, hawahusiki na kuongeza pato la taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vema wazee hawa wote kwa umoja wao kwa nchi nzima, Watanzania, wakulima, wale masikini vijijini, Mikoa yote, utaratibu huu ukaharakishwa kama ambavyo Serikali iliahidi kwa wazee wa Tanzania. Mimi naomba huu mchakato uharakishwe kwa sababu wazee wamekuwa wakiendelea kukata tamaa mwaka hadi mwaka. Ni jambo jema ili wazee nao waone wao ni sehemu muhimu katika nchi yao na katika Taifa lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona pia kwenye Kitabu hiki kwamba utaratibu mzuri unaoendelea kufanywa na hasa kutengeneza ajira ambazo zimeonekana hapa takribani laki saba. Mimi niiombe Wizara, kwa takwimu tulizonazo vijana wa nchi hii ni wengi na kama ambavyo Wabunge wameendelea kuchangia hapa kwamba lipo tatizo kubwa lakini tuone sasa kufanya kazi pamoja. Zipo Wizara nyingine ambazo na wao wakifanya kazi huko kwenye Wizara zao na Wizara hii ikawa inaendelea kuratibu, hili jambo litaendelea kupungua siku hadi siku. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. AGNESS E. HOKORORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Nassib Omar?

MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, tumshukuru Mungu kwa neema zake nyingi sana juu yetu. La pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Mwisho, nasema naunga mkono bajeti hii ya Wizara ya kazi kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitaanza na ajira kwa vijana. Tatizo la ajira ni kubwa sana na kila siku linaongezeka. Kwa mfano, tuangalie vijana ambao hivi sasa wanamaliza darasa la saba kila mwaka, darasa la 10, 12, 14 na chuo kikuu, lakini vilevile tuwaangalie wale ambao wanamaliza vyuo kama *VETA* wote hawa wanaingia kutafuta ajira na katika wao ni kidogo sana ambao wanapata ajira. Kwa hiyo, tutaona tatizo hili linaongezeka mwaka hadi mwaka. Lazima hatua thabiti zichukuliwe ili kuli-*adress* suala hili.

Mhshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hapa kubwa zaidi la kusaidia ni elimu ya ujasiriamali na biashara. Ikiwa hawa wote watapatiwa elimu wataweza

kufungua *VICOBA*, wataweza kufungua *SACCOs* na wengine kuweza kupata mikopo midogomidogo kutoka benki na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara imepangiwa kupatiwa shilingi bilioni nne kwa ajili ya ajira ya vijana. Hizi ni pesa nyingi na kama zitatumika vizuri, basi suala la tatizo la ajira kwa vijana litapungua sana. Katika ripoti yake ya mwanzo ya Mheshimiwa Waziri ambayo ninayo hapa, iliyokuja katika Kamati, Mheshimiwa Waziri amepanga kutumia shilingi bilioni tatu kwa kuwapatia vijana 200 waliomaliza vyuo vikuu katika mwaka huu, vijana 200 kwa shilingi bilioni tatu? Kwa hivyo, nafikiri Mheshimiwa aliangalie tena suala hili ili kuhakikisha kwamba vijana hawa wanaongezwa wanafikia hata 5,000 au 10,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika amesema katika ripoti hii kwamba atatumia shilingi milioni 700 kwa kuwapatia elimu vijana 200. Shilingi milioni 700 kwa elimu? Yaani ni sawasawa na shilingi milioni 3.4 kwa kila kijana mmoja. Sasa hizi ni pesa nyingi, lazima wakae, waangalie na wahakikishe pesa hizi shilingi milioni 700 wanapatiwa elimu vijana wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, harakaharaka nizungumzie *Work Permit;* vibali kwa wale wafanyakazi wageni ambao wanataka kufanya kazi katika nchi yetu. Vibali hivi hutolewa na Wizara hii ya Kazi na hutolewa bure. Katika mwaka 2013/2014, waombaji walikuwa 7,432, waliokubaliwa walikuwa watu 6,237; wote hawa wamepatiwa vibali hivi bure. Mfano hapa tungekuwa tumechaji shilingi laki moja moja kwa kila kibali utaona Wizara hii ingeweza kupata zaidi ya shilingi milioni 600. Nchi za wenzetu na hasa majirani zetu wanafanya hivihiv, wanatoa vibali lakini hawatoi bure. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili na atakapokuja hapa baadaye atuambie ni nini mwelekeo wake yeye katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama mahali pa kazi. Kazi hii inafanywa na Shirika la *OSHA*. Wao hukagua umeme, hukagua *boiler* na mitungi ya hewa. Katika ripoti yake ileile ambayo nimeionesha hapa amesema kwamba ukaguzi ulikuwa ni 90%. Vifaa kama *boiler* ambavyo vinatumia mvuke wenye joto kali na *temperature* kubwa na *pressure* lazima vikaguliwe kila mwaka; huwezi kukagua nusunusu, majanga yake ni makubwa. Siku zilizopita tumeona hapa kumetokea *accident* ya *boilers* na watu wengi wakafariki na wengine majeruhi. Tumesikia nchi za jirani vilevile kumetokea *accident* ya *boiler* na watu wengi sana wameathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kazi hii ya *inspection* huwa haifanywi bure, inafanywa kwa pesa. Sasa tatizo liko wapi kwamba hamuwezi kukagua *boilers* na vifaa vyote, ni nini tatizo? Hamna *Inspectors* wakutosha au vitendea

kazi vya kutosha? Nafikiri Waziri atakapokuja hapa atueleze nini msimamo wake juu ya suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine kubwa zaidi ni kwamba, viwanda sasa hivi vinaongezeka. Mtwara huko viwanda vya saruji, vyote hivi vinatumia ma-*boiler* makubwa makubwa, mitungi ya gesi na kadhalika lazima Waziri akija hapa atuambie ana *inspectors* wangapi? Je, kapanga vipi kulitatua suala hili? Je, ni kiasi gani cha pesa ambayo ana-*charge* kwa *inspection* hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa kuwa Wizara hii ndiyo msimamizi mkubwa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa *NSSF,* ningependa alieleze Bunge hili Tukufu mpaka mwaka 2014, Mfuko wa *NSSF* umefikia hatua gani katika kurejesha fedha za Mfuko zilizowekwa katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma; *General Tyre;* Kiwira na *Machinga Complex*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Usuluhishi na Maamuzi *(CMA)* imetelekezwa. Vituo vya Mikoani na Watumishi wake hawajawahi kupewa fedha za kuendeshea ofisi, hali iliyopelekea huduma kudorora! Wimbi la wafanyakazi kuacha kazi kutokana na kukatishwa tamaa lipo juu sana lakini hakuna anayejali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atuambie kama Wizara yake inayajua haya na ina mpango wa kuchukua hatua gani hasa ikizingatiwa umuhimu wa chombo hiki.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha bajeti hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Serikali inipatie ufafanuzi wa baadhi ya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuridhia mikataba mbalimbali. Nchi yetu ilisaini Mkataba wa 189 wa Shirika la Kazi Duniani. Mkataba huu ulisainiwa toka Juni, 2011 na ulitakiwa toka uliposainiwa uwe umesharidhiwa na Bunge ndani ya mwaka mmoja, sasa imeshapita miaka mitatu tangu uliposainiwa kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge. Tulitegemea Mkataba huo kama ungeridhiwa ungeweza kutetea masilahi yao.

Je, ni lini sasa Mkataba huu wa Wafanyakazi wa Majumbani utaletwa hapa Bungeni ili tuuridhie na ni tatizo gani ambalo limesababisha kuchelewesha Mkataba huo?

Sambamba na hilo, Mkataba wa 183, *Maternity Porotection,* pia ulisainiwa Juni, 2011. Mkataba huu unahusu haki mbalimbali ya likizo ya uzazi, pia umekuwa ukiulizwa sana hapa Bungeni nao ni lini utaridhiwa hapa Bungeni ili wafanyakazi wapatiwe haki zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wazee ni kundi muhimu sana katika jamii yoyote Duniani. Wazee wa Tanzania wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu sana ukilinganisha na nchi nyingine. Wazee wengi wamekuwa ndiyo wakulima na wafanyakazi, lakini wakishastaafu basi ndiyo mwisho wa maisha. Tumeshuhudia wengi wao wakipata presha au kupoteza maisha na wengine kuuawa hata na watoto wao wakiambiwa wachawi. Ni vyema sasa Serikali iwe hata na mpango wa kuweka mpango wa pensheni kwa ajili ya Wazee. Je, ni lini Mfuko wa Pensheni kwa Wazee utaanzishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe katika Kamati ya Miundombinu. Tulipofanya ziara katika Mradi ya Ujenzi tulikumbana na malalamiko mengi sana kuhusu malipo kidogo kwa vibarua na wafanyakazi wazawa. Pia zipo kazi za utaalam ambazo hata Watanzania wengi wangeweza kuajiriwa, lakini tumekuta makampuni ya kigeni wameleta wafanyakazi kutoka nje wanaajiriwa. Je, ni chombo gani kinasimamia wafanyakazi hao kwa sababu athari inayotokea kutokana na posho hizo kidogo wafanyakazi wamekuwa wakifanya hujuma mbalimbali za wizi wa mafuta, wizi wa vyuma vya madaraja, maruma, mishahara na posho zao zinapangwa na nani kwa sababu kila kampuni ya kigeni inajipangia itakavyo yenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa vijana ni kilio kikubwa sana kwa nchi yetu. Pamoja na Serikali kuwa na mkakati wa kuanzisha Vyuo vingi vya Elimu ya Juu, lakini bado hatujaweza kuweka mitaala itakayowawezesha vijana wetu wanapomaliza masomo yao waweze kujiajiri. Je, Wizara hii inasaidia vipi kuhakikisha elimu inayotolewa inawasaidia vijana kujiajiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nayapongeza pia Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Wakala wa Usalama wa Afya Mahali pa Kazi *(OSHA),* inafanya kazi nzuri ya kuelimisha na kusimamia maswala ya afya na usalama kazini. Ninao ushauri ufuatao:-

Isukumeni Wizara iharakishe kuleta Bungeni Mkataba Namba 155 wa *Occupational Safety Health Convention, 1981*, ili uridhiwe na ule wa *Occupational Safety in Construction, 1988.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hivi sasa iko katika harakati nyingi za ujenzi majumba ya ghorofa. Yapo matukio kadhaa ya kuanguka au kuporomoka kwa baadhi ya majengo kutokana na sababu mbalimbali na katika matukio hayo waathirika wa karibu ni wafanyakazi katika Sekta hiyo. Wengi ni vibarua hawana *insuarance* na hawana *guarantee* yoyote. Hivyo, upo umuhimu sasa kwa *OSHA* kuangalia sekta binafsi ya ujenzi kwa lengo la kutoa elimu ya usalama mahala pa kazi. Naamini sekta binafsi ya ujenzi ikihamasishwa, kushirikishwa na kuelimishwa, itaweza kuchangia katika kufanikisha ili elimu hiyo itolewe maeneo yote ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati za Afya na Usalama Mahala pa Kazi: Kutokana na Serikali kutoa nafasi kwa sekta binafsi kuwekeza katika kutoa huduma mbalimbali, sasa tumepata bahati ya kuwa na Hospitali Binafsi na Vituo vya Afya vingi, lakini ni kwa kiasi gani Watendaji wa Sekta hii wanafuata taratibu za afya na usalama mahala pa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Afya ni nyeti na inashughulikia magonjwa mbalimbali mengine ya kuambukiza. Inakusanya takataka zinazotokana na tiba ya wagonjwa mbalimbali. Ni kwa kiasi gani wafanyakazi katika sekta binafsi za afya wanatoa kipaumbele kwa afya na usalama wao pahala pa kazi hasa wale wanaoshughulikia ubebaji takataka hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji madini wadogo na hata wakubwa, wana uwezekano mkubwa wa kuvuta tani nyingi za vumbi ndani ya mapafu yao na kuwapelekea kupata maradhi. Je, wawekezaji katika Sekta hii wanafikiriwa na kuangaliwa huduma zao wanazozitoa na ni kwa vipi wanawajali wafanyakazi wao?

Je, kwa kiasi gani tutawafikia wachimbaji wadogo kupata elimu ya afya na usalama katika maeneo yao wanayofanyia kazi na kupata riziki zao? Lengo kuu ni elimu ya kinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mionzi na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, wakae pamoja na kuja na mkakati thabiti wa kuuelimisha umma na hususan wale ambao wanachimba

madini hayo. Elimu hiyo itasaidia sana na kuwaelimisha wao na jamii zao na matatizo yatokanayo na madini ya urani pindipo hifadhi hazitochukuliwa.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mosi, ajira kwa vijana lazima ziongezwe kwani nchi yetu inaruhusu kuwepo ajira za kutosha; kwa mfano, Mkoa wa Rukwa na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ina hali nzuri ya hewa kuendeleza kilimo. Skimu za Kilimo cha Umwagiliaji kikianzishwa katika Mikoa hii tatizo la ajira linaweza kuisha au kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazawa wenye elimu na ujuzi lazima waongoze Taasisi zinazoongozwa na wageni. Kazi yoyote inayoweza kufanywa na Mtanzania isifanywe na mgeni yeyote. Fedha iliyotengwa ni kidogo sana, lazima kutafuta nje na ndani namna ya kuongeza kifungu hiki kwa mwaka huu kuwawezesha vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo kwa wastaafu yanasumbua hasa wale waliostaafu hapo nyuma kidogo. Serikali ilijitahidi kuleta mageuzi katika changamoto hii. Wazee wasio watumishi wanateseka, tunataka wazee walipwe kuanzia bajeti hii au ijayo, tafadhali wapewe vitambulisho vya matibabu bila kusumbuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali iache kukopa fedha kwenye Mifuko ya Jamii ili kuiwezesha itune kwa manufaa ya wastaafu wetu nchini.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua Wizara hii inawasaidiaje wafanyakazi waliostaafu ambao wanahangaika kufuatilia mafao yao bila mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata majibu ya Serikali kuhusu wawekezaji wa kigeni hasa waliopo Dar es Salaam hasa Wachina wanaofungua biashara za viwanda ndani ya nyumba wanazopanga, kwenye magodauni na kwenye karakana za magari ambapo wameajiri Wachina au Wahindi na huwa wanawafungia kwenye maeneo hayo na mara kadhaa huonekana wakitoka nje usiku. Je, kwa nini Wizara hii haiweki mpango wa muda mrefu kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kubaini na kuchukua hatua stahiki?

Mwaka 2013 katika Kiwanda cha Sukari Kilombero II – Ruaha Kata, katika ujenzi wa Kiwanda cha Konyagi mwekezaji alileta Wahindi na Wakenya takribani 260 ambao walikuwa wanafanya kazi za ujenzi kwa mfano,

kuchanganya mchanga na *cement*, kubeba matofali, kazi ambazo zingefanywa na wazawa. Nilitoa taarifa kwenye Kikao cha *briefing* hapo Ukumbi wa Msekwa. Naibu Waziri Mambo ya Ndani, alipofuatilia aliwakuta Wahindi 80 na Wakenya 8 na wengine walishaondoka na walikuwa hawana vibali vya kuishi nchini, lakini hadi leo Wizara yako haijatoa adhabu yoyote kwa mwekezaji huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini pamoja na kuwa na matatizo mengi ya ukatili, unyanyasaji, upunjaji wa stahili za wafanyakazi maeneo tofauti, Wizara hii haijawahi kukemea au kuwachukulia hatua wanaofanya vitendo hivyo na katika Hotuba yake hatujaona orodha ya wavunja sheria hao na hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ajira binafsi kama mama lishe, waendesha pikipiki (bodaboda) na wauzaji vifaa na nafaka mijini na vijijini, kwa muda mrefu sasa Serikali inawanyanyasa, kuua mitaji na kadhalika, lakini Wizara hii haijawahi kutoa kauli wala kuwa na mpango madhubuti kulinda ajira hizo. Je, Wizara inasema nini kuhusu hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaposema kwenye Hotuba yake kuwa inatoa mafunzo ya afya kazini; ni maeneo gani ya kazi mafunzo hayo yanatolewa na kama Serikali inatambua ajira binafsi kama bodaboda, wazoa taka, wafanya usafi; je, ni kwa vipi Wizara imetoa mafunzo kwa makundi hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inabagua aina ya ajira kwani idadi ya ajira rasmi ina watumishi wachache kuliko walioko kwenye ajira zisizo rasmi. Sasa basi wakati umefika wa Wizara kuja na mpango madhubuti wa kuboresha na kutoa mafunzo kwa watu walioko kwenye ajira zisizo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ndiyo Wizara inayowalinda wafanyakazi nchi hii ili wapate haki zao. Je, ni kwa vipi Wizara hii imefuatilia matatizo wanayoyapata wafanyakazi yanayosababishwa na waajiri wao; kwa mfano, matatizo wanayoyapata Wafanyakazi wa *TAZARA* mara kwa mara na kusababisha maisha magumu kwao na familia zao pia kwa wasafiri wanaotumia usafiri wa Reli ya *TAZARA*? Je, Wizara imefanya jitihada gani kwa kushirikiana na Wizara ya Uchukuzi ili kulinda masilahi ya wafanyakazi inaowasimamia na kulinda masilahi na stahiki zao?

MHE. JOYCE J. MUKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda na mimi kuchangia katika Hotuba hii ya Wizara ya Kazi na Ajira kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahudumu wa ndani *(Housegirls* na *Houseboys*), wamekuwa katika wakati mgumu sana katika ajira zao kutokana na manyanyaso na uonevu mkubwa wanaoupata kutoka kwa mabosi wao. Kibaya zaidi, wengi hawana elimu ya kutosha, umri mdogo na uwoga,

vinawaponza kwani hawana uwezo wa kushtaki popote na hawawezi kujisimamia katika kupata haki zao za msingi. Mateso hayo wanayopata matokeo wamekuwa wakipeleka chuki kwa watoto wa familia kwa sababu ndiyo wanaokaa nao kwa muda mrefu na hata kupelekea kuwafanyia matendo ya kutisha watoto hao kama mauaji, kuwapiga na kadhalika; na hii yote inajengwa na chuki inayotokana na wahudumu hao kuteswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi hawa pia wamekuwa wakilipwa mishahara midogo sana tofauti na kazi wanazofanya, kwani wanafanya kazi zaidi ya saa 16 kwa siku. Mimi naomba Wizara hii iweke Sheria ya Kazi ya kuwasaidia wafanyakazi hawa wa majumbani kwani hali yao ya usalama siyo nzuri kabisa. Pia kuwekwe kiwango cha ulipwaji wa mishahara kwa hawa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na uzamiaji mkubwa wa wageni kutoka nje ambao wamefanya kazi hapa nchini bila vibali vya kufanyia kazi kisheria; kwa mfano, wafanyakazi wa ndani wanaotoka nchi za nje kama Malawi, kumekuwepo na wahudumu wengi sana wa ndani wanaotoka nchini Malawi na hawana vibali vya kufanya kazi kisheria. Je, wakipata tatizo itakuwaje? Serikali naomba sana ilisimamie hili ili kulinda masilahi ya nchi na hao wageni wanaotoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za migodi zimekuwa za kudhalilishana sana na inatia huruma sana. Kwanza, kipato ni kidogo sana na pia wakati madini yanapopatikana wamekuwa wakipekuliwa kila mahali katika miili yao na kibaya zaidi ni maeneo ya siri, sehemu za haja kubwa, eti kwa kuhisi tu mfanyakazi katoka na madini na kuyaingiza katika sehemu za siri. Hili limetokea katika maeneo ya Mererani huko Wilaya Simanjoro - Manyara. Hii ni fedheha sana na inapelekea hata wafanyakazi hao kujifunza mchezo wa kufanya mapenzi kinyume cha maumbile kutokana na kuingizwa vidole wakati wa ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ilizungumzie hili wakati Mheshimiwa Waziri anajibu kwani wahusika watasikia na kupunguza kuwafanyia unyama huu watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. GOSBERT B. BLANDES: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na pongezi hizo, naomba nilete maombi ya Vijana wa Wilaya ya Karagwe kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe, wameleta maombi yao ya mkopo kwa *SACCOS* ya Vijana. Tunaomba Wizara

hii isaidie upatikanaji wa mkopo huu ili vijana wetu waweze kupata mkopo huo na kuinua uchumi wa vijana na kuwapatia ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri awasiliane na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe kupitia namba hii ili ampe hali halisi ya mahitaji ya vijana nayo ni 0782-050 028, Mheshimiwa Wallace Mashanda. Kuongea naye ni muhimu sana kabla ya kuhitimisha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Workers Compensation Act*, *2008* (Sheria ya Fidia ya Wafanyakazi), iliyotungwa na Bunge hili ilikuwa na malengo mema sana ya kuweka utaratibu wa kuwalipa fidia wafanyakazi pindi wanapoumia wakiwa kazini. Serikali iliahidi kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi haraka iwezekanavyo. Mwaka 2012 niliuliza swali hapa Bungeni lini Mfuko huu utaanzishwa na nilijibiwa kwamba, mchakato uko katika hatua za mwisho. Ni nini kimekwamisha uanzishwaji wa Mfuko huu? Kwa nini Serikali inaendelea kutoona umuhimu wa kuanzisha Mfuko huu ili wafanyakazi wanaoumia kazini nao waweze kupata haki yao? Serikali itoe kauli yake na lini (kwa tarehe) Muswada wa kuanzishwa Mfuko huu utaletwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* kuendelea hasa na utaratibu wa kutoa mikopo katika sekta isiyo rasmi kwa Wanachama wake katika Vikundi vya *SACCOs* na *VICOBA,* ni muhimu sasa kwa Shirika hili kugeukia na sekta iliyo rasmi kwa kutoa mikopo kwa Wanachama wake hasa wale wa muda mrefu. Wanachama binafsi ambao hawajajiunga katika vikundi ambao ni wengi nao wana mahitaji yao binafsi na wanahitaji kujiandaa na maisha pindi wanapostaafu. Ni jambo jema mtu kupewa mkopo, kwa mfano, kujenga nyumba yake mwenyewe wakati anapokuwa kazini ili anapostaafu kazi asiwe tena na kazi ya kujenga pale anapomaliza muda wa utumishi wake kazini. Muda wa kustaafu ni muda wa kumalizia maisha ya amani na si muda wa mtumishi mstaafu kuanza kutangatanga na maisha.

Naomba *NSSF* iangalie utaratibu wa kuanza kutoa mikopo kwa mtu mmoja mmoja ambao ni Wanachama wa muda mrefu ili nao wapate kufurahia michango yao na kujiandaa kwa maisha ya baadaye ya uzeeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. ROSE K. SUKUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, inashangaza kuona programu ya kukuza ajira kwa vijana imetengewa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya sekta isiyo rasmi ambayo hutoa asilimia 10.1 ya ajira zote nchini, badala ya kuwekeza fedha hizo katika Sekta ya Kilimo kwa vijana ambayo inaajiri asilimia 75.1 ya ajira zote nchini. Aidha, bajeti inaonesha kuwa programu ya ukuzaji wa ajira kwa vijana nchini inatarajia kutambua vijana 200 ambao wapo tayari kujiajiri na Shs. 3,000,000,000 zimetengwa kuwapa mafunzo ya biashara na ujasiriamali. Kati ya hizo, shilingi 702,000,000 ndizo zitakazotumika katika mafunzo hayo. Wakati shilingi 2,001,325,000 zitawekwa katika mabenki kama dhamana ili vijana hao wakopeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inamaanisha kuwa kati ya vijana hao 200, kati ya shilingi 702,000,000 kila kijana atatumia jumla ya shilingi 3,510.000 kwa ajili ya mafunzo ya biashara na ujasiriamali kwa mwaka. Jumla ya fedha hizo sawa na karo ya mwanafunzi *(tuition fee)* wa Chuo Kikuu cha Umma kwa muda wa miaka miwili hadi mitatu, wakati Wizara ya Kazi na Ajira imepanga kuzitumia kugharimia mafunzo kwa kijana mmoja tu ndani ya mwaka mmoja wa fedha 2014/2015, jambo ambalo linatoa taswira ya matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kukosa uhalisia. Fedha hizi zikitolewa hazitawafikia vijana wanaojiajiri katika Sekta ya Kilimo ambayo hutoa asilimia 75.1 ya ajira zote nchini na Sekta ya Shughuli za Kiuchumi za Kaya *(Household Economic Activity Sector)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napendekeza kuwa, idadi ya vijana walengwa wa Mradi iongezeke kutoka 200 iliyowekwa hivi sasa mpaka vijana 600 na kutumia shilingi 1,170,000 kwa kila kijana badala ya shilingi 3,510,000 zilizotengwa hivi sasa. Kati ya vijana 600, vijana 200 wapewe mafunzo ya biashara na ujasiriamali katika sekta isiyo rasmi. Vijana wengine 200 wapewe mafunzo ya utafutaji wa masoko ya mazao ya biashara na chakula na ufungaji wa bidhaa za mazao hayo *(packaging & branding)* katika Sekta ya Kilimo. Vijana 200 wapewe mafunzo ya kuongeza thamani ya huduma na bidhaa katika Sekta ya Shughuli za Kiuchumi za Kaya *(Household Economic Activity Sector*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya kukuza ajira kwa vijana imetenga shilingi bilioni mbili kati ya bilioni tatu ambazo zitawekwa katika Taasisi za Fedha zinazokopesha vijana kama dhamana kwa ajili ya ukopeshaji wa vijana katika kukuza ajira zao. Aidha, bajeti ya Wizara hii ya Kazi na Ajira inaeleza kuwa Programu ya Kukuza Ajira kwa Vijana imetenga jumla ya shilingi 2,001,325,000, ambazo ni sawa na asilimia 67 ya fedha zote za programu zimetengwa kama dhamana katika Taasisi za Fedha zinazokopesha vijana nchini.

Hii inaamaanisha kuwa, jumla ya shilingi bilioni mbili pekee zitawekwa kama dhamana katika Taasisi za Fedha zinazokopeshwa vijana kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Hii ni bila kujali kama vijana watakwenda kukopa ama la na bila kujua vijana wangapi watanufaika na mikopo itakayotolewa kama matokeo ya dhamana hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, napendekeza; mosi, Wizara ya Ajira na Kazi iweke bayana idadi ya vijana inayotarajia watanufaika na mikopo inayotokana na uwekezaji wa dhamana hiyo katika Taasisi za Fedha. Pili, uwekezaji wa shilingi bilioni mbili kama dhamana katika Taasisi za Fedha ili vijana wakopeshwe upunguzwe kutoka shilingi 2,001,325,000 mpaka shilingi 500,000,000 ili fedha zinazobaki, shilingi 1,00,325,000 zipelekwe katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana uliopo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ambayo imetenga shilingi 4,000,000,000 Mwaka wa Fedha 2014/2015; hivyo, kufanya fedha hizo kuongezeka kuwa shilingi 5,000,000,000 ili vijana wengi zaidi wanufaike na fedha za Mfuko huo. Aidha, napendekeza kuwa shilingi 500,000,000 zitakazopunguzwa kati ya shilingi bilioni mbili za dhamana katika Taasisi za Fedha zitengwe kama fedha za kianzio *(Seed Funding*) kwa Miradi ya vijana 600 watakaonufaika na mafunzo ya kukuza ajira.

MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu MKuu na Uongozi wote wa Wizara hii, pamoja na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia yafuatayo:-

Je, ni lini sasa utafiti wa hali ya nguvu kazi nchini *(Intergrated Labour Force Survey)* utakamilika?

Naipongeza Wizara kwa kuandaa Rasimu ya Muswada wa Sheria ya Ajira kwani zipo nyingi zikiwemo zingine za Kimataifa ambapo wageni wamekuwa wakiingia nchini na kufanya kazi bila kufuata utaratibu na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Huduma za Ajira *(TaESA),* uandae Mpango Mkakati Maalum wa Kutafuta Ajira na Kuunganisha Watafuta Kazi na Waajiri. Aidha, *TAESA* ifanye vikao na Balozi zetu za nje ili kuhamasisha ajira mbalimbali ili tuongeze fursa za ajira ya nchi kwa Watanzania wanaotafuta kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara iweke utaratibu wa malalamiko maana yako malalamiko ya watafuta kazi kudaiwa rushwa ya ngono. Hivyo, ni vyema uongozi ukafuatilia, ili waomba kazi wasidhalilishwe kwa namna yoyote katika hali yao ya kutafuta kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kwa niaba ya Wizara ya Katiba kwa *NSSF,* kwa ubia katika ujenzi wa Jengo la Ofisi za *RITA (RITA TOWER)*. Mradi huu utasaidia sana *RITA* kupata ofisi za kisiasa na pia kuwapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iongeze wigo wa kutoa elimu kuhusu Sheria za Kazi hususan kwa wafanyakazi. Aidha, iandae vipindi mbalimbali vya elimu kwa umma ili wafanyakazi waelimishwe kuhusu Sheria za Kazi na Kanuni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuulizia kuhusu hatua iliyofikiwa kuhusiana na Mikataba mbalimbali ya Shirika la Kazi Duniani kuridhiwa na Bunge lako Tukufu hususan Mkataba Namba 189, unaohusu wafanyakazi wa majumbani na Mkataba unaohusu *Martenity Perfection Number 183.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine napenda kuwapongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri na Naibu wake, kwa utendaji mzuri na makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na tatizo kubwa la wageni kuingia katika soko la ajira nchini. Naishauri Serikali kuwa, Wizara zote na Mamlaka zote, waweke mfumo mzuri ambao utadhibiti uvamizi huu ambao unahatarisha ustawi wa ajira nchini.

Kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, waangalie wimbi kubwa la utoaji leseni za biashara ndogondogo kwa wageni.

MHE. DKT. LUCY S. NKYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wao wote, kwa Hotuba nzuri ya Bajeti ya 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia machache kwa nia ya kuboresha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauari Wizara iangalie namna ya kuongeza ajira kwa katika Sekta ya Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi wamejiajiri katika Sekta hizi mbili; hivyo, Wizara hii iwatambue na iwapatie huduma za hifadhi ya jamii ili

wakistaafu waweze kupata pensheni. Kama hili litafanikiwa, suala la pensheni ya wazee litakuwa limepata suluhisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwakaribisha *NSSF* katika Wilaya ya Morogoro Vijijini ili waanzishe *Pilot Project* ya kuandikisha Wanachama; Wakulima na Wafugaji.

Je, Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii wanafaidi nini kutokana na faida zinazotokana na vitega uchumi vilivyowekezwa kwa michango yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie ni kwa namna gani waliochangia kwenye Mashirika haya mpaka wakaweza kuwekeza watapata nao mgao kama wanahisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ikae na Mfuko wa Bima ya Afya ili wachambue wateja wao kwani kuna wateja ambao wanahudumiwa kiafya kwa pamoja na Mashirika haya mawili. Ni vyema wakatengeneza mfumo ambao utaundwa hii fursa ya mtu mmoja kuhudumiwa na mashirika haya kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naomba Serikali ituambie ni Watanzania wangapi wamepelekwa nje kufanya kazi za majumbani. Je, ni nani anayesimamia *welfare* yao? Nauliza hili kwa sababu kumekuwepo na minong'ono ya unyanyasaji hususan kwa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ninaomba sana Mkurugenzi wa *NSSF* anikubalie ombi langu la kuendesha *Pilot Project* ya kuwasajili Wakulima na Wafugaji wa Tarafa ya Ngerengere kuwa Wanachama wake kwani ndiyo ajira zilizopo vijijini.

Nawatakia mafanikio makubwa katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira kwa vijana wetu wanaomaliza vyuo ni kubwa sana, ningependa kujua Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijana hawa ambao ni nguvu kazi kubwa ya nchi yetu, wanapata ajira hata kama ni za kujiajiri wenyewe; nini mkakati wa Serikali wa kuondoa tatizo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna asiyejua kuwa gharama za maisha zimepanda kwa kasi kubwa na kiasi wanachopata wastaafu hawa cha shilingi elfu hamsini hakiwezi kutosha kumudu gharama hizi. Tukumbuke kuwa, wastaafu hawa walifanya kazi kwa kufuata maadili ya utumishi wa umma.

Ningependa kujua Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ina mpango gani wa kuongeza kiasi hicho cha fedha ili kiendane na gharama za sasa za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua Wakala Binafsi wa Ajira unasaidiaje, yako malalamiko toka kwa wafanyakzi kuwa wamekuwa wakikosa mishahara yao kwa wakati, wengine kunyimwa likizo wakati likizo ni haki ya mtumishi na wengine kufanyishwa kazi hata muda wa kazi ukiwa umekwisha. Ningependa kujua Serikali inachukua hatua gani za kuwasaidia watu hawa ili waweze kupata haki zao za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko toka kwa wafanyakazi wa migodini kuwa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, lakini wanapoachishwa kazi hawapimwi afya zao kama sheria inavyoelekeza. Naomba Serikali iisimamie sheria hii ili wafanyakazi hawa waweze kupata haki zao kama afya zao zitakuwa zimeathirika maana wamekuwa wakitendewa ndivyo sivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la ajira kwa watoto. Wamiliki wa mashamba na migodi wanatumia watoto wetu na kuwafanyisha kazi ambazo haziendani na umri wao na hii ni kinyume na haki za mtoto. Naomba Serikali ichukue hatua kali kwa watu wanaotumia watoto wetu kujinufaisha wao na familia zao, huku watoto hao wakiendelea kuumia na kukosa haki zao za kusoma na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia.

MHE. REBECCA M. MNGODO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 5, kuna maelezo kwamba, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imetekeleza majukumu yake katika kusimamia viwango vya kazi, ukuzaji wa ajira, ushirikishwaji wa wafanyakazi sehemu ya kazi, kuboresha hifadhi ya jamii na kushughulikia migogoro ya kazi na usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Jambo Plastics kiliwafukuza wafanyakazi wake wote mwaka 2011 baada ya Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kutembelea kiwanda hicho. Wafanyakazi zaidi ya 400 walifukuzwa kwa mpigo baada ya kufanya kazi katika kiwanda hicho zaidi ya miaka saba bila ya mwajiri kuwawekea akiba katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na hiyo ilikuwa mwezi mmoja baada ya Kamati kukitembelea kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Waziri na Wizara yake wana jukumu la kushughulikia migogoro ya kazi na wafanyakazi na usalama wao kiafya, ningependa kufahamu Wizara imechukuliaje mgogoro huo ambao kimsingi wafanyakazi walikuwa na haki ya kuwekewa akiba katika hifadhi ya jamii,

kulipwa *overtime* pale walipofanya kazi kwa saa za ziada, kupewa *protective gears* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Jambo Plastics ni kimoja tu ambacho nakitolea mfano, lakini nina hakika kuna wafanyakzi wengi zaidi katika viwanda vilivyopo hapa nchini, hususan vinavyomilikiwa na wageni kama Jambo Plastics, ambao wananyanyaswa na waajiri wao kwa kunyimwa haki zao za msingi za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara iendelee kutoa elimu kuhusu sheria za kazi au vyombo vya habari ili kuwafikia watu wengi zaidi badala ya ilivyo sasa kwamba, elimu imetolewa kwa wafanyakazi 8,201 na waajiri 412 wa Sekta za Viwanda na Biashara, Afya, Kilimo, Ujenzi, Huduma za Hoteli, Ulinzi Binafsi, Madini na Usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri suala la pensheni kwa wazee liharakishwe. Mwaka uliopita Mheshimiwa Waziri aliwahi kusema kwamba, angependa akumbukwe kwa kuanzishwa kwa Mfuko wa Wazee. Ni kweli vyanzo vya mapato ya Mfuko huu inawezekana havijapatikana kama Mheshimiwa Waziri alivyoelezea katika Hotuba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Mashirika haya ya Hifadhi ya Jamii yanafanya biashara kubwa kubwa, kwa mfano, *NSSF* napendekeza ile faida wanayoipata kutokana na biashara wanazofanya basi watenge asilimia fulani kwa mfano, asilimia kumi au chini ya hapo ili kuchangi Mfuko wa Pensheni ya Wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, wazee wengi waliotumikia Taifa hili kwa uaminifu mkubwa wanaishi kwa tabu sana. Wengi waishio katika mazingira magumu na hasa huko vijijini hupata malipo ya mafao yao kila baada ya miezi mitatu mitatu. Napendekeza walipwe kila mwezi, kwani hata hivyo kiwango chenyewe ni kidogo sana. Serikali iangalie jinsi ya kuongeza kiwango cha pensheni kwa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira kwa watoto bado ni tatizo kubwa. Badala ya kuendelea na masomo kutokana na usimamizi, inabidi wajiingize katika ajira ya utotoni. Aidha, katika Mashamba ya Maua Arusha watoto huajiriwa kwa ujira mdogo sana, lakini baada ya miaka kadhaa huachishwa kazi kwani huwa wameathirika na madawa yanayopigwa katika mashamba ya maua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze kasi katika kufuta kabisa ajira kwa watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni za wastaafu imekuwa ni kero kubwa na hivyo naoimba Serikali kuyafanyia utafiti malalamiko hayo ili katoa ufumbuzi wa kero hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa utoaji Pensheni na hasa kiasi cha malipo yanayolipwa kinakuwa kilekile kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali kila wakati mshahara ukipanda pensheni haiongezeki? Pensheni ya shilingi 50,000 ni ya muda mrefu hata kama mshahara umekuwa ukiongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iweke msukumo wa utendaji wa kazi. Watu wakifika kazini wanaanza na porojo kwanza na muda wa kazi unapotea bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza hasa Waziri, Naibu wake na Katibu Mkuu pamoja na Timu yote ya Wizara, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuunga mkono hoja.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kazi nzuri na kubwa inayofanyika. Naomba kushauri yafuatayo:-

Kusimamia utetezi kwa wafanyakazi wanaoachishwa kazi migodini, baada ya kupata maradhi wakiwa kazini.

Serikali ifanye mpango wa haraka kwa kuleta Muswada wa Hifadhi za Jamii ili kuwezesha Wanachama kuhama kutoka Mfuko mmoja hadi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. FATUMA A. MIKIDADI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa bajeti nzuri. Kusudi langu ni kuomba kutungwa kwa Sera ya Wazee. Inabidi tuwasaidie, tuwathamini wazee, kwani wazee ni chanzo cha maendeleo yote. Uzee hakuna atakaeukwepa, wote tunakwenda huko; nani atakwepa kuzeeka? Tuwasaidie wazee.

La mwisho ni pongezi kwa *NSSF* kwa kazi nzuri. Ahsante.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Kazi na Ajira. Napenda kuunga mkono Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu Mifuko ya Hifadhi za Jamii hasa *NSSF* kuhusu kucheleweshwa kwa mafao ya wafanyakazi. Hii inatokana na ukweli kuwa, Mifuko hii imewekeza katika Miradi mikubwa bila ridhaa ya wenye amana na hivyo kupelekea kusuasua kwa malipo hayo kama Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali inavyoonesha. Ni vipi Wizara kwa kupitia *SSRA,* inasimamia uwekezaji wa Mifuko hii ambayo inchangia kwa ucheleweshaji wa malipo ya pensheni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wamekuwa wakikumbana na adha mbalimbali katika mazingira ya kazi hasa kutumikishwa muda mrefu kinyume na Sheria ya Kazi ya Mwaka 2004 bila ya kupewa malipo ya ziada. Asilimia kubwa ya wafanyakazi wa hotelini, majumbani na migodini, huwa wanatumikishwa tofauti na muda wanaostahili kufanyia kazi lakini hawalipwi. Huu ni unyonyaji wa nguvu za wafanyakzi ambao wanajituma kukabiliana na ugumu wa maisha. Serikali inatoa kauli gani kwa waajiri wanaowatumikisha wafanyakazi na vibarua bila kuwalipa masaa zinazozidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko kuwa wafanyakazi wengi hawana mikataba ya ajira inayoeleweka, hali inayochangia kwa waajiri kuwanyima haki na stahili zao ikiwemo mishahara yenye staha, likizo za malipo, mafunzo na kadhalika. Ni dhahiri kuwa, bila mikataba inayoeleweka haki za wafanyakazi zitaendelea kuminywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda mrefu Kambi ya Upinzani tumekuwa tunaelezea umuhimu wa Wizara hii kusimamia haki za Wafanyakazi wa Sekta mbalimbali ambao hucheleweshewa mishahara ikiwemo *TAZARA*. Kumekuwa na migogoro na migomo ya Wafanyakazi wa *TAZARA* ambayo inasababishwa na menejimenti mbovu. Sote tunaelewa jinsi ambavyo gharama za maisha zimepanda, inakuwaje kwa wafanyakazi kuishi bila mishahara kwa miezi mitatu na mishahara yenyewe bado ni duni? Wizara itueleze, ina mkakati gani wa kuhakikisha Wafanyakazi wa *TAZARA* hawanyanyasiki mara kwa mara hasa kwa kucheleweshewa mishahara ukizingatia kuwa hii si mara ya kwanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangazwa na Wizara hii kuweka mikakati yake yenye kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, wakati yenyewe

haina uratibu mzuri wa masilahi ya wafanyakazi. Hii inajidhihirisha kwa mazingira mabovu ya maeneo ya kazi ambayo yanaambatana na ajali kazini. Tumezungumza sana hapa Bungeni juu ya wajibu wa Wizara kufanya kaguzi za mara kwa mara maeneo ya kazi, lakini kaguzi hizi hazifanywi kwa kiwango kinachoridhisha, hali inayopelekea ajali mbalimbali makazini. Inasikitisha kuona kuwa wakati ujenzi na ukarabati wa maeneo ya Bunge kwa maandalizi ya Bunge Maalum la Katiba, wafungwa waliokuwa wakijenga na kufanya kazi za ujenzi walipigwa picha na vyombo vya habari wakiwa hawana vifaa vya kinga vya kazi. Inasikitisha kuona kuwa, Taasisi ambayo ndiyo inayotunga Sheria za Kazi na AJIRA inashindwa kuzisimamia kwa uadilifu. Wizara ya Kazi ina majibu gani kuhusiana na upungufu huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuitaka Serikali kupitia Wizara hii, kusimamia kwa ufasaha nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi itakayoendana na hali halisi ya maisha na kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. HAMOUD ABUU JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mungu, kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kazi na Ajira ya Mwaka 2014/2015 iliyopo mbele yetu. Kwa nafasi hii ya kipekee, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na jopo la wataalam wake kwa kutuandalia bajeti nzuri, yenye kuonesha dhahiri kutaka kutatua matatizo ya kazi na ajira nchini na kuweka sheria nzuri zitakazomlinda mfanyakazi pamoja na kuweka suala la ajira kuwa wazi na kuwanufaisha Watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo *(UNCTAD),* limetoa ripoti ya nchi zinazoendelea yenye kaulimbiu, ustawi na ajira kwa maendeleo jumuishi na endelevu. Ripoti hiyo inayobainisha kwamba, watu milioni 170 wataingia sekta ya ajira katika nchi zinazoendelea kufikia mwaka 2020, imeangalia uchumi wa nchi zinazoendelea na uhusiano wake na ajira ambapo inapendekeza sera mbazo zitawezesha kuongeza nafasi za kubuni ajira. Ajira bado ni changamoto inayokumba Mataifa yanayostawi.

Jambo la kusikitisha ni kwamba, Mataifa yanayokabiliana na ukosefu wa ajira, yanaongoza katika viwango vya watoto wanaozaliwa, hali ambayo inaendelea kugharimu sekta ya ajira sasa na kwa siku za usoni hali inaonekana itazidi kuwa tata kama hapajatafutwa ufumbuzi wa tatizo hili. Ongezeko la watu wasiokuwa na ajira hususan vijana limekuwa linaongezeka siku hadi siku na hivyo kutishia hali ya baadaye ikizingatiwa pia ongezeko la watoto wanaozaliwa limekuwa kubwa nalo.

Ukosefu wa ajira kwa vijana ni tishio duniani kote kwani vijana ndiyo nguvu ya Taifa lolote, sasa inapotokea vijana hawa kukosa fursa za ajira, inawawia vigumu kuweza kumudu maisha ya kila siku. Wasomi wamekuwa wengi na kila mwaka tumekuwa tukijionea vijana wengi wakimaliza elimu zao za vyuo vikuu na kukosa ajira. Wasomi hawa wakizidi kuwa wengi mtaani kwa kukosa kazi ni hatari kwani ni sawa na *timing bomb* ambalo siku likilipuka tutakosa pa kukimbilia.

Naipongeza Serikali kwa juhudi zake za kuongeza Vyuo Vikuu ili kukidhi mahitaji ya Taifa na watu wake, kuhakikisha vijana wetu wanapata elimu bora. Nawakumbusha Serikali inapoongeza kasi ya kuongeza Vyuo Vikuu basi isisahau na kuongeza kasi ya kuwandaa vijana hawa kupata ajira au kujiajiri wenyewe ili kuondokana na ongezeko la fursa za ajira kuwa ngumu nchini. Sasa hivi imejengeka na kuonekana ni kitu cha kawaida kwa vijana wetu kutokuwa na matumaini pindi wanapomaliza elimu zao za juu kupata ajira, tofauti na miaka ya zamani, mtu akimaliza elimu tu anakutana na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mambo yote hayo, lakini pia kuna changamoto zinazowakabili wahitimu wa vyuo ambao ni vijana wetu; kwanza, ni ubora wa wahitimu wenyewe umekuwa wa mashaka mpaka ninajiuliza hivi kijana huyu miaka mitatu Chuo Kikuu alipitaje pitaje katika mitihani yake mpaka akafanikiwa kumaliza elimu yake. Rasilimali watu yenye sifa ni nguzo muhimu katika utendaji kazi ulio bora na wenye kufikia malengo katika sehemu yoyote iwe ya huduma au uzalishaji. Nchi nyingi Duniani na hususan kwenye Utumishi wa Umma zimeweza kuendelea kwa kasi kubwa kutokana na kuwa na rasilimali watu yenye kukidhi viwango vya hali ya juu (rasilimali watu yenye weledi).

Upatikanaji wa rasilimali watu bora unategemea sana uwepo wa wahitimu bora toka kwenye vyuo au taasisi za elimu na elimu ya juu zilizopo katika nchi husika. Naishauri Serikali kuweka mkakati wa muda mrefu kutilia mkazo suala zima la elimu ikiwemo kuwekeza katika sekta hiyo pamoja na kutoa fursa kwa watu binafsi, mashirika na taasisi mbalimbali kuanzia shule na vyuo ambavyo vimechangia kwa kiasi kikubwa kutoa wahitimu wenye ubora, wanaoweza kukabiliana na ushindani ulioko kwenye soko la ajira ndani na nje ya nchi. Pamoja na ushauri huo ambao utaleta mafanikio, bado kuna changamoto kubwa kwa baadhi ya wahitimu kumaliza ngazi mbalimbali za elimu wakiwa wamemaliza na kupata vyeti, lakini hawana uelewa wa kutosha wa kile walichokisomea (taaluma husika), pamoja na ufahamu wa mambo mbalimbali yanayoendelea kwenye mazingira husika. Matarajio ya wahitimu walio wengi pindi wamalizapo masomo yao ni kuwa na uwezo wa kuajiri ama kuajiriwa katika sekta binafsi au za umma kutokana na weledi wa kitaaluma pamoja na uelewa mpana wa mambo yanayowazunguka ili kuweza kuendana na soko la ajira katika karne hii ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ndicho chombo kinachopewa jukumu la kuhakikisha kuwa, Utumishi wa Umma unakuwa na watumishi wenye weledi wa hali ya juu kupitia mchakato wa ajira. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa, inapata waombaji wenye sifa kitaaluma, uwezo na ujuzi ili kuufanya Utumishi wa Umma kuendeshwa na watumishi wenye weledi na maadili mema katika kuiwezesha Serikali kutimiza malengo yake kwa ufanisi.

Katika kipindi cha miaka minne ya kutekeleza wa jukumu hilo, Sekretarieti ya Ajira imekabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo ubora wa wahitimu wanaowasilisha maombi ya kazi Serikalini, kuanzia waombaji wenye elimu ya ngazi ya sekondari, astashahada, stashahada, shahada ya juu, shahada ya uzamili, pamoja na shahada ya uzamivu. Katika tathmini yangu niliyoifanya, nimebaini upungufu mbalimbali utokanao na ubora wa wahitimu wanaoomba kazi kupitia chombo hiki ambao wamehitimu ngazi mbalimbali za elimu ikiwemo wanaotokea kazini. Aidha, tofauti ya upungufu huo hutofautiana kutoka ngazi moja na nyingine, uwezo wa kitaaluma, ufahamu, kuamini vyeti peke yake vinaweza kuwapa kazi pasipokuwa na uelewa mpana wa kile walichoombea kazi, kutotilia maanani sifa au vigezo na masharti ya tangazo husika, kutokujiamini, kukosa uzoefu kwa kazi inayohitaji uzoefu, uwezo mdogo wa mawasiliano ikiwemo matumizi ya lugha sahihi, uwezo mdogo wa kutumia nyenzo za utendaji kazi hususan vifaa vya kielektroniki, kutokujiandaa vya kutosha, kukosa mbinu za usaili na kutozingatia muda.

Changamoto nyingine ni kutokujitambua, kusoma kwa kufuata mkumbo, kukosa sifa halali za kitaaluma, kutokujua namna ya kuandika barua za maombi ya kazi, namna ya kuandika wasifu wao *(CV)*, kutokuwa na maandalizi sahihi pamoja na kughushi baadhi ya sifa kwa lengo la kujipatia ajira. Kwa upande wa wahitimu wanaoomba kazi wakitokea kazini, baadhi yao wameonesha udhaifu wa kutokuwa na uwezo wa kukabiliana na changamoto hiyo kuona ni bora atafute kazi nyingine, kutokupitisha barua kwa waajiri, kukosa uelewa mpana unaoendana na uzoefu wake kazini ili kuweza kuonesha tofauti yake na waajiriwa wapya, kukimbilia Serikalini ili kupata fursa ya kusomeshwa lakini si kwa lengo la kwenda kuongeza tija kiutendaji. Hali hii inadhihirisha kwamba, wapo waombaji kazi ambao wanasoma ili kuhitimu au kufaulu na siyo kuelewa kwa ufasaha fani wanazozisomea ili kuweza kuleta utaalam wao katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Jambo ambalo limekuwa likichangia wengi wao kushindwa kufikia hatua ya kuitwa kwenye usaili kutokana na kukosa baadhi ya vigezo na wengine kufikia hatua ya usaili na kushindwa kufaulu usaili husika kutokana na kutojiandaa ipasavyo.

Katika kukabiliana na changamoto ya upungufu unaotokana na ubora wa wahitimu kabla ya kuingia katika mfumo wa kutumia maombi kwa njia ya kielektroniki, ni bora kuweka upungufu huu kwa uwazi ili kusaidia wahitimu husika na wadau mbalimbali wa elimu katika kuzitatua changamoto hizo na kuboresha. Aidha, naishauri Serikali kutembelea Sekta za Elimu ikiwemo kushauriana na mamlaka na wadau mbalimbali wa elimu kuhusu namna ya kukabiliana na changamoto hizo kwa pamoja ikiwemo kuandaa programu ya elimu kwa umma ili kuwezesha waombaji wa kazi kuweza kutimiza vigezo vinavyohitajika ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kupata kazi husika wanazoomba.

Kumekuwepo na utaratibu usiofaa kwa baadhi ya mashirika na makampuni pindi wanapotangaza nafasi za kazi kuweka kipengele cha uzoefu ambacho mimi nakiona kwa baadhi ya nafasi za kazi hakina tija. Hivi unapoweka kipengele cha uzoefu; je, hawa vijana wetu waliomaliza elimu zao za juu na hawakuwahi kuajiriwa wanatoa wapi huo uzoefu ilhali kila mwajiri anataka mtu mwenye uzoefu?

Naishauri Serikali kuwawezesha vijana wetu kwa kuwaajiri ili waweze kupata uzoefu wakiwa kazini kwani kufanya hivyo kutasaidia sana vijana wetu kupata ajira. Kingine, kumekuwepo na mawakala wa kuwatafutia kazi watu. Mawakala hawa wamekuwa wakijipatia fedha nyingi pasipo kihalali kupitia vijana wetu pindi wanapowapatia nafasi hizo za kazi. Huo ni unyonyaji mkubwa, kwani vijana hawa wamekuwa wakikosa haki zao za msingi kwa waajiri wao, kwani mikataba yao imekuwa ikisainiwa baina yao na hawa mawakala; hivyo, mwajiri anakuwa hahusiki na mishahara yao imekuwa ikikatwa kwa riba kubwa sana, pia wamekuwa hawawezi kujiunga na mfuko wa pensheni; hiyo yote ni kuwakosesha haki zao za msingi.

Naiomba Serikali kuchukua hatua kali dhidi ya walaghai hao kwa kuwafungia makampuni hayo usajili wao na kuwafikisha mahakamani. Makampuni hayo yamekuwa yakijulikana; hivyo, sidhani kama itakuwa ni jambo gumu sana kwa Serikali kuwashughulikia na ikiwezekana Serikali iyaamuru makampuni hayo kuwalipa fidia vijana wote ambao walipata ajira zao kupitia makampuni hayo. Nayasema haya kwa kuwa Serikali ikiyaacha makampuni haya yaendelee na utaratibu huu, inapelekea kwa wale vijana wote ambao walisomeshwa na Serikali kutokukatwa fedha za mkopo walizokopeshwa na Serikali katika mishahara yao; hivyo, Serikali kupata hasara na kupelekea vijana wengine kutokupata nafasi ya kupata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale fursa za ajira zinapokosekana, utu na heshima ya mwanadamu vinawekwa rehani. Ukosefu wa fursa za ajira, mazingira duni ya kazi, athari za myumbo wa uchumi kimataifa, kazi za suluba zinazofanywa na watoto, ubaguzi wa rangi na ukosefu wa usawa katika utoaji wa mishahara pamoja na mazingira mabaya ya kazi ni mambo ambayo

yanasababisha madonda makubwa katika utu na heshima ya wafanyakazi, kiasi kwamba, athari zake pia zinajionesha kwenye familia kwa kushindwa kutekeleza wajibu wake barabara.

Hatuna budi kuonesha upendo na mshikamano wa dhati na wafanyakazi wanaokumbana na athari za myumbo wa uchumi kimataifa, kiasi kwamba, hawana tena matumaini kwa kesho iliyo bora zaidi. Vilevile tutakuwa wakosaji kama hatutawakumbuka wafanyakazi waliopoteza maisha yao wakiwa wanatoa huduma kwa jamii, matukio ambayo kimsingi yanasababishwa na ukosefu wa usalama kazini na maelezo ya kina. Vifo na ajali kazini ni matukio ambayo yanaacha madonda makubwa kwa familia na wafanyakazi na taifa kwa ujumla wake. Kumbe, kuna haja ya kuhakikisha kwamba, usalama kazini unapewa pia kipaumble cha kutosha.

Vyama vya Wafanyakazi visipoteze dhamana na wajibu wake, wafanyakazi wataendelea kupoteza maisha, kupata vilema vya kudumu na hatimaye watatumbukia kwenye umaskini wa hali na kipato! Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani, iwe ni fursa kwa wafanyakazi kutekeleza wajibu wao kimiliki kwa kutambua kwamba, kazi ni utimilifu wa utu na heshima ya binadamu. Kazi ambayo mtu ameichagua kwa hiari yake mwenyewe inachangia kwa kiasi kikubwa mchakato wa maendeleo ya jamii inayomzunguka, kwa kukidhi mahitaji ya familia pamoja na kuacha chapa ya kudumu katika maisha ya mtu binafsi, kifamilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika, migodi inachangia Pato la Taifa na ajira, lakini utabaini kuwa, mchango huu unakuja na ulemavu, maradhi yasiyotibika na umaskini mkubwa. Mazingira hatarishi ya kiafya na vifaa duni vya kujikinga na madhara ya kiafya yanayosababishwa na shughuli za uchimbaji dhahabu migodini, udhaifu wa sheria zinazosimamia usalama wa afya mahali pa kazi na fidia, uwezo mdogo wa mamlaka zinazosimamia usalama wa afya za wafanyakazi, ni miongoni mwa mambo yanayosababisha madhara ya kiafya na kupoteza uwezo wa kufanya kazi tena kwa waliokuwa wafanyakazi migodini bila kulipwa fidia stahiki kutokana na athari wanazopata, ambao unatuhumiwa na baadhi ya waliokuwa wafanyakazi wake kutengeneza wagonjwa zaidi ya 300, wengine wakiwa wamepoteza uwezo wa kufanya kazi yoyote tena kutokana na athari za maradhi yanayotokana na kazi *(Occupational Diseases)* na kisha kuwatelekeza.

Kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani *(ILO), silicosis* ni ugonjwa wa mapafu usiokuwa na tiba unaosababishwa na vumbi linalotokana na miamba yenye *cystaline silica* na unaweza kumpata mtu yeyote anayefanya kazi muda mrefu kwenye maeneo ya vumbi hilo. *Silicosis* huathiri uwezo wa mapafu kufanya kazi na kumfanya mgonjwa ashindwe kupumua vizuri. Mgonjwa wa *silicosis* ana uwezekano mara tatu kupata Ugonjwa wa Kifua Kikuu *(TB),* hali ambayo wakati

mwingine wataalamu huiita *silicotuberculosis*, huambukiza kirahisi magonjwa ya mapafu na magonjwa ya kushindwa kupumua *(respiratory failure)*. Hivyo basi, naishauri Serikali kuweka sheria kali katika sekta nzima ya waajiri migodini ili kupunguza athari ambazo kwa kiasi kikubwa, zimekuwa zikiwaacha wafanyakazi na vilema vya maisha bila kuwa na msaada wowote kutoka kwa waajiri wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Wizara hii katika maeneo machache sana, lakini ni muhimu katika ukuzaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ametueleza kuwa, hadi kufikia Aprili, 2014 ni ajira 630,616 tu ndizo zimezalishwa. Napenda kujua hizi ajira ni kipindi cha mwaka mmoja tu au?

Pili, hii ni takwimu ndogo sana hasa katika Sekta ya Kilimo ambayo Watanzania zaidi ya asilimia 80 ni wakulima na hapa namaanisha kuwa ni ajira 130,974 tu ndiyo zilizozalishwa. Napenda kupata majibu ni katika kada zipi za kilimo hizi ajira zimezalishwa? Je, ni kuajiri au kuajiriwa?

Wizara itueleze bayana ni mikakati gani waliyonayo ili kukuza ajira hasa kwenye kilimo na hili litafanikiwa kwa kushindana na sekta zingine mtambuka au Wizara na katika Sekta ya Madini, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuhusu takwimu za ujuzi sambamba na hatua ya kuhakikisha Watanzania wenye sifa mbalimbali wanapata ajira ndani ya nchi na hata nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri tuna vijana wenye sifa na uzoefu katika sekta mbalimbali, lakini wapo mtaani hawana kazi kabisa. Ningependa Wizara ituambie hadi sasa hii *Labour Market Information System* imeweza kuwa na idadi ya Watanzania wangapi wenye ujuzi katika kada tofauti na kati ya hao wangapi wamefanikiwa kupata ajira?

Tunahitaji kuwa *aggressive* katika kuchangamkia fursa mbalimbali nje ya nchi na hata ndani kuliko kuwakumbatia wageni tu huku wazawa wakisota mtaani. Kwa muktadha huu, kumkwamua Mwananchi ni ndoto na uchumi wetu kukua hautaakisi uhalisia wowote. Naomba tuwe *serious* katika kukuza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kumalizia hoja hii ya ukuzaji ajira, napenda kujua ni lini Muswada wa Sheria ya Ajira kwa wageni utaletwa humu

Bungeni ili tuujadili na kuweza kuupitisha. Nashauri Muswada huu uletwe kwa dharura ili tukomeshe wimbi la wageni kutoa ajira ambazo zingeweza kufanywa na wazawa. Utashangaa hata kazi ya ufagizi au ulinzi zinafanywa na wageni? Hii siyo haki na ni kuua uchumi wa nchi na kupata au kutengeneza Taifa la wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nizungumzie pia suala zima la kodi ya kipato, yaani *Pay As You Earn (PAYE)*. Hii tozo ya kodi bado ni kubwa mno, pamoja na agizo la Rais, nashauri *PAYE* walau iwe asilimia 10 au 12 tu ili tuweze kuwasaidia hawa Watanzania walio katika ajira. Ikumbukwe wafanyakazi ndiyo walipaji kodi waaminifu kwa maana kila mwezi wanalipa kodi. Vilevile mwaka jana kwenye Wizara hii nilishauri wafanyakazi wanaolipwa chini ya shilingi laki tatu wasilipe kodi ili tuwatendee haki kama ilivyo kwa wafanyabiashara wenye kipato chini ya milioni nne kwa mwaka haliwalipi kodi, basi tufanye hivyo na kwa wafanyakazi wanaopata mshahara wa 300,000/= au 330,000/=, ambayo inakuwa ni 3.6 ml au 3.96 ml kwa mwaka wasilipe kodi ya *PAYE*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana mlifanyie hili kazi pamoja na kupata majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni juu ya unyanyasaji wa wafanyakazi wa ndani. Kiukweli hawa watu wananyanyasika sana. Kwanza, unakuta wanaosajiliwa ni watoto chini ya umri wa miaka 18. Utakuta mtoto wa miaka 13 hadi 17 ameajiriwa na anafanyishwa kazi masaa mengi na kazi ngumu kulingana na umri wao pia ujira kwa maana ya mshahara mdogo sana. Haishii hapo tu, hawa watoto hasa wa kike wanapata *sexual harassment*, ambapo kuna kesi za wasichana wa ndani kuambukizwa magonjwa ya *HIV* na waajiri wao; maana wanakuwa hawana jinsi bali kukubali. Hivyo, iwepo sheria kali sana ambapo wanaokiuka utu na kuwanyanyasa wachukuliwe hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia sasa naomba Serikali ituambie imefikia wapi kwenye suala zima la *pension* ya wazee. Nakiri tulitembelea nchi mbalimbali na kuona vipi wao wanafanya katika kuhakikisha Wananchi wanapata huduma bora ya afya, elimu, malazi na makazi kupitia Mashirika ya Hifadhi.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi nachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwajiri mkubwa ni sekta binafsi, nashauri *OSHA* ipangiwe fedha na watumishi wa kutosha ili kutekeleza kazi za ukaguzi wa usalama katika sehemu za kazi. Ninazungumzia viwanda na karakana *(garage)*.

Je, Wizara haioni mlundikano wa majalada kwenye Masjala za Mahakama na za Halmashauri za Wilaya kama ni hatari kiafya *(Health Hazard)?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Tume za Usuluhishi ziwepo kila Mkoa na ziwe na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe elimu ya Sheria ya Kazi hasa kwa sekta binafsi wasiachiwe Vyama vya Wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kazi ijue ni nini *living wage,* hata kama Serikali haina fedha za kulipa kwa ajili ya wafanyakazi wa sekta binafsi, wanaweza kupatana *(negotiation)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa mwelekeo mzuri wa kazi kwa Wizara hii ya Kazi na Ajira na mvuto wake mkubwa katika kuwezesha Taasisi zilizopo chini, kufanya kazi na kutoa huduma nyingi kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo, ushauri na maombi maalum kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Hifadhi ya Jamii *(NSSF)* limeanzisha mpango mzuri wa mikopo katika Vikundi vya *SACCOS* na *VICOBA* na Wilaya ya Muheza imenufaika kupitia *TCCIA SACCOs.* Wastani wa mikopo iliyotolewa inafikia shilingi milioni kumi, baadhi ya Wanachama hasa vijana wameanza kutumia fursa hizo kwa ajili ya mikopo ya pikipiki (bodaboda) na hivyo kuanzisha ajira binafsi badala ya kuendesha bodaboda za wamiliki wengine.

NSSF ifanye uratibu wa mpango huo ili kuwa na orodha kamilifu na kuweza kutoa taarifa za kitaifa jinsi mpango huo unavyochangia kutengeneza ajira katika Taifa letu la Tanzania kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NSSF* itoe elimu kwa vijana nchini juu ya fursa hiyo na pia elimu juu ya usalama wa uendeshaji wa bodaboda (madereva na abiria).

NSSF, ianzishe na kujenga maeneo maalum ya kazi za akina mama *(Mama Ntilie Site)* ili kuwezesha akina mama kupata maeneo maalum ya kufanyia kazi na kuepuka adha ya kuvunjiwa maeneo yao yasiyo rasmi.

NSSF ianzishe na kuboresha maeneo ya viwanda vidogo vidogo kuongeza uwezo wa *SIDO* na hivyo kuwezesha vijana kujijengea uwezo wa kujiajiri kama vile ufundi wa kazi za umeme, magari, useremala, upigaji rangi, upishi na ujenzi. Pamoja na ushauri huo, *NSSF* ijenge mfumo wa kujiwezesha kwa uwiano wa mapato na matumizi ili isijifikishe katika hali mbaya ya kuelemewa na majukumu. Kila Mradi watakaouanzisha kuwepo na rejesho la mapato ya wastani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isaidie Serikali kutekeleza na kuondoa malalamiko ya madeni na mafao ya walimu na wafanyakazi wengine. Moja ya jukumu la Wizara ya Kazi na Ajira ni pamoja na kusimamia Sheria za Kazi na masilahi halali ya ajira. Kwa msingi huo, Wizara ya Elimu inapolalamikiwa na walimu kuhusu malimbikizo ya madeni ya mishahara, marupurupu ya utendaji na mafao, Wizara hii inapaswa kuwa mshauri kwa Serikali ili kuondoa kero hizo. Wizara ijipange kama sehemu ya Serikali na kuchukua jukumu hilo kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Taasisi ya *NSSF* isaidie Wilaya ya Muheza katika ujenzi wa Jengo la Maabara katika Shule ya Sekondari ya Shebomeza iliyopo Tarafa ya Amani. Shule hii imeteuliwa kuwa *High School* na ndiyo itakuwa *High school* ya kwanza kwa upande wa Serikali. *High School* iliyopo, *Muheza High School* ilijengwa kwa msaada wa Chama cha Wananchi wa Muheza wanaoishi Dar es Salaam, *Muheza Development Trust Fund,* miaka mitano iliyopita na kukabidhiwa Serikalini kati ya Tarafa nne katika Wilaya ya Muheza, *Muheza High School* ipo Tarafa ya Muheza na *Shebomeza High School* iko Tarafa ya Amani. Tarafa mbili zilizobaki, yaani Tarafa ya Ngomeni na Tarafa ya Bwembera bado hazina *high schools*.

Kihistoraia Muheza eneo la Mgila ndiyo ilijengwa shule ya kwanza hapa Tanganyika chini ya Wamisionari na kujenga Tanganyika kielimu. Hata hivyo, Muheza wala Mkoa wa Tanga hazijajaliwa kuwa na Vyuo Vikuu wala taasisi kubwa za kielimu, wala Muheza kuwa hata na Sekondari ya Serikali hadi sasa ambapo ndiyo zimeanzishwa Shule za Sekondari za Kata. Huo ndiyo msingi wa ombi hilo maalum kwa *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ABDULSALAAM S. AMER: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote kwa juhudi zao katika kutekeleza majukumu magumu ya Wizara hii. Pia nawapongeza Watendaji wote kwa utendaji wao wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapongeza kwa Hotuba yao nzuri na yenye changamoto nyingi, naomba sana Wizara hii ijielekeze katika

kuwapatia vijana uwezo wa kujiajiri wenyewe kutokana na taaluma waliyonayo au kwa uzoefu wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwawezesha vijana ni jukumu la Serikali na sisi Viongozi, pamoja na Serikali kujipanga kwa kuwawezesha vijana kujiajiri. Tatizo linakuja katika utekelezaji ngazi za chini kuanzia Mikoani, Wilayani hadi ngazi ya kijiji. Ngazi hizo ndiyo zenye ukiritimba mkubwa katika kuwafikia walengwa.Dhana waliyonayo vijana wa vijijini ni kuwa wa kuwezeshwa ni vijana wa mijini tu ni dhana potofu, ingawa kiukweli ndiyo wanaopewa kipaumbele katika kupata mitaji. Ningeomba Wizara ifuatilie sana miradi hiyo kwa ngazi za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbushia juu ya suala la wafanyakazi wa iliyokuwa Kampuni ya Sukari ya Kilombero kabla ya kubinafsishwa; wafanyakazi hao hadi leo wanaendelea kufuatilia mafao yao lakini hakuna hatua inayochukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kukumbushia suala hili, namwomba sana Waziri angeagiza mtendaji wake mmoja tuongozane ili akae na hao waliokuwa wafanyakazi wa kampuni hiyo ambao wako katika hali ngumu sana kimaisha. Naamini Waziri atalielewa ombi langu hili na kuwasaidia na kuwakomboa waliokuwa wafanyakazi hao ambao wanaishi maisha magumu. Namalizia kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake nzuri na namtegemea kulipa kipaumbele ombi langu na Mungu atambariki.

MHE. MARIAM N. KISANGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara, kwa jinsi wanavyoendesha Wizara hii kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe pongezi zangu za dhati kwa *NSSF* jinsi wanavyoendelea vizuri na ujenzi wa Daraja la Kigamboni; hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingine ziende kwa Mifuko ya Serikali; *NSSF, PSPF, PPF,* jinsi wanavyosaidia Serikali katika ujenzi wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo. Mifuko hii inatoa fedha nyingi kama mkopo. Je, fedha hizi zinarudishwa? Fedha hizi zisiporudi Mifuko itaanguka mwisho ishindwe kulipa wateja wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezwa kwa mishahara ya wafanyakazi na kulipwa kwa madeni ya walimu ni ya Mheshimiwa Rais, ambaye tunampongeza sana. Sasa itekelezwe kwa wakati, madeni ya walimu ni jambo ambalo limesemwa sana, naomba sasa walipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Walimu (CWT), kiwatendee haki walimu kwa kuwafanyia kazi za kutafuta masilahi ya walimu kwa kuwatengenezea mazingira mazuri, maisha bora kwa walimu siyo kujiingiza kwenye mambo ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Klongozi wa Chama cha Walimu anayetaka kuingia kwenye siasa atoke katika Chama cha Walimu aende kwenye siasa asivuruge walimu. Kwa mfano, Mwalimu Oluoch, amekuwa na tabia ya kuhamasisha walimu wagomee Serikali. Je, *Mwalimu House* inawanufaishaje walimu?

Viongozi wa CWT kama hawataki kujirekebisha basi tutoe uhuru wa Mwalimu kujiunga na Chama anachotaka na kukatwa mshahara kwenda kwa CWT iwe si jambo la lazima bali la hiari. Chama cha CWT kiwe na ubunifu wa njia mbalimbali za kuwasaidia walimu bila kutegemea Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ajira zinatolewa kwa watu wale wale tu bila kuwa na mzunguko? Mtu mmoja anatoka *NSSF* anakwenda kufanya *interview TRA* anapata, anatoka *TRA* anakwend *Barrick; why?* Serikali idhibiti hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia 100.

MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC: Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa na ndiyo asilimia kubwa ya watu nchini, lakini ajira imekuwa tatizo kubwa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hii ni tatizo la mfumo mbaya wa elimu nchini ambao umelenga zaidi kuwaandaa kwa kuajiriwa na si kujiajiri wenyewe. Kibaya zaidi, hata wakijiajiri wenyewe kwa biashara ndogondogo, Serikali imekuwa haina muundo mzuri wa kuwaendeleza vijana hao; mfano, Wamachinga. Wamachinga wakemuwa wakifukuzwa kama hawamo nchini kwao. Naiomba Serikali kuheshimu biashara ndogondogo kwani ndizo zinawafanya Watanzania walio wengi kuishi, kusomesha watoto wao na kulipa kodi kuiinua Serikali. Serikali iwatafutie maeneo ya kufanyia biashara zao kwa amani na siyo kuwahamisha kwa kuwanyang'anya biashara na kuharibu kwani hiyo ndiyo ajira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijitahidi kulipa pensheni za wastaafu bila kuwacheleweshea mpaka wastaafu wengine wanapoteza maisha na kuacha pesa zao zifuatiliwe na familia zao kwa usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naishauri Serikali kupitia Wizara hii, kukagua somo la ujasiriamali wanalojifunza mashuleni ili kuondoa tatizo la ajira

wamalizapo shule. Je, linamwandaa mtoto kwa maisha ya baadaye amalizapo shule? Tofauti na sasa ambapo mwanafunzi alikuwa anaambiwa epeleke fagio shuleni ndiyo anapewa *marks* za somo la maarifa ya stadi za kazi. Huo ni utapeli wa maisha ya vijana katika ajira yake ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Gaundentia Mugosi Kabaka, Waziri wa Kazi na Ajira na Mheshimiwa Dkt. Makongoro Mahanga, Naibu Waziri wa Kazi na Ajira na Katibu Mkuu pamoja na Wataalamu walioko katika Wizara hii, kwa Hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iendelee kuweka mazingira mujarabu ambayo yatasaidia kuongezeka kwa wigo wa ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iliambie Bunge lako Tukufu mkakati ilionao kuhakikisha vijana wetu wanaohitimu Vyuo Vikuu watakavyonufaika na ajira hapa nchini. Pili, napenda kujua Serikali kupitia Wizara hii imefikia hatua gani kuanzisha Mfuko wa Vijana ambao utatumika kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu na hivyo kuwapunguzia au kuwaondolea madhara ya kutokuwa na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujua Wizara ina mkakati gani kushirikiana na Wizara za Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Elimu na Ufundi ili kuja na mkakati ambao utakuza ajira kwa vijana wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara ya Kazi na Ajira ndiyo mratibu wa masuala yote ya kazi na ajira hapa nchini, naomba nijulishwe ni ajira ngapi zimetengenezwa, aidha moja kwa moja na Wizara hii au kwa kushirikiana na Taasisi zingine za Umma au za binafsi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Mataifa yaliyoendelea zimewekeza sana katika miundombinu ya kiuchumi na sekta binafsi kwamba; mazingira mazuri yaliyowekwa na Serikali hizo za Mataifa yaliyoendelea yamepelekea kuvutia uwekezaji na hivyo ajira nyingi zimetengenezwa na kupunguza matatizo yanayowakabili vijana na makundi mbalimbali kutokana na kutokuwepo kwa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishauri Serikali yangu kwamba, kutokana na tatizo la ajira kwa vijana na makundi mengine, hali hiyo yaweza

kuwalazimisha watu hao kujiingiza kwenye ujambazi na hivyo kuhatarisha amani ya nchi yetu. Hali ya kutokuwa na ajira ya uhakika yaweza kuwashawishi vijana kujiunga na makundi ya kigaidi kama Alshabab, Alqaida na kadhalika. Hivyo, ni muhimu Serikali yetu kupitia Wizara hii, iwekeze zaidi kupanua wigo wa ajira ili kuondoa hali niliyoieleza hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze uamuzi wa Serikali kuanzisha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi *(The Workers Compensation Fund*). Natumai Mfuko huu utasimamiwa vizuri na hivyo kutekeleza malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Napenda kuishauri Serikali kwamba, mafao ya Wanachama katika Mifuko hii yapatikane wakati wowote Mwanachama anapohitaji kwani hiyo ni haki yake. Mifuko iache kuwazungusha kwa kisingizio cha umri. Waziri akija kufanya majumuisho aniambie ni lini utaratibu huu utaachwa.

Nakusudia kutoa shilingi iwapo sitapewa maelezo ya kina kwa nini Wananchi wetu ambao wamejiunga na Mifuko hii huteseka sana wanapotaka mafao yao hasa baada ya wao kupoteza ajira katika taasisi walizokuwa wakizifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba kujua hatima ya mafao ya waliokuwa Wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki; ni lini watalipwa mafao yao kwani wenzao huko Kenya na Uganda walishalipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaunga mkono hoja baada ya maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua ni kwa nini na sababu zipi za kimsingi ambazo mara nyingi zimekuwa zikiwazuia Makatibu Muhtasi *(Secretaries) k*ujiendeleza kimasomo hasa katika ngazi ya juu ya *degree?* Kada hii imekuwa ikidharauliwa na upeo wa kujiendeleza kielimu mwisho wake ni ngazi ya *diploma* tu na pindi anapojiendeleza kielimu katika ngazi ya *degree*, mtumishi wa kada hii atalazimika kuhamia kada nyingine na kuanza kazi kwa mshahara mpya, yaani mshahara wa kwanza.

(a) Je, ni kwa nini Serikali isianzishe kozi zinazoendana na kada hii kwa ngazi za juu yaani *degree*?

(b) Kwa nini Serikali hairekebishi ngazi ya mishahara katika kada hii?

(c) Kwa nini Serikali haiangalii upya namna mtumishi wa kada hii pindi anapohamia *department* nyingine asiende na ngazi yake ileile apande daraja kwa mshahara mpya wa kada hiyo nyingine atakayohamia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi kuhusu pensheni kwa wazee. Pensheni ya aina gani hiyo kwa kuwa pensheni lazima uchangie?

Naulizia hivi kwa sababu suala hili limekuwa likileta utata sana katika jamii hasa kwa upande wa wazee kwani ni vyema suala hili likatolewa ufafanuzi wa kutosha ili liweze kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Timu yake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara na hasa kuongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mfumo wa pensheni kwa wazee ni muhimu sana, naiomba Serikali iharakishe mpango huu ili kuwaondolea wazee wetu suluba za uzeeni. Kwa kweli wazee wengi wanapoteza maisha kutokana na umaskini na kukosa faraja. Pia wapo wazee wastaafu wengi ambao hawapati pensheni kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kutokujua utaratibu na pengine taasisi husika kutokuwajali. Sisi sote Mungu akitujalia maisha marefu, tutakuwa wazee wasio na nguvu siku zijazo. Je, tutajisikia vipi iwapo jamii itatutelekeza? Naiomba sasa Serikali ifuatilie wazee wastaafu na kuwaingiza katika Mfuko wa Pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iendelee na utatuzi wa migogoro ya kazi iliyobaki zaidi ya 2,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira katika makampuni ya gesi na madini katika sehemu mbalimbali za nchi yetu zisiwe za ubaguzi. Waangalie na kuzingatia sana vijana wa maeneo husika kabla ya kuajiri watu kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, semina za ujasiriamali kwa akina mama na vijana ziongezeke ili kuyawezesha makundi haya kujiajiri kirahisi baada ya kupatiwa elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa kuyaelewa masuala ya wafanyakazi. Jitahidini kupunguza migogoro 2,296 iliyobaki inayoendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kazi njema.

MHE. MESHACK J. OPULUKWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inajitahidi sana na ninawaombea kwa Mwenyezi Mungu, afya njema na mafanikio katika kutumikia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia zile nafasi kubwa Serikalini wapewe pia watu wenye ulemavu. Mfano, sijawahi kuona Waziri albino, Mkuu wa Wilaya albino, Mkuu wa Mkoa albino, Rais albino, Wakurugenzi na Wenyeviti wa Bodi mbalimbali walemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliangalie hili kwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawatafutia ajira wanaohitimu vyuo mbalimbali, lakini bado Serikali imetoa kazi kwa walio na kazi tayari, kwa mfano, Wabunge kuwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa hili liangaliwe.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Shirika la *NSSF* kwa jinsi linavyofanya kazi nzuri. Sasa hivi unaweza kabisa kupata mafao yako ndani ya siku moja tu, hatua hii ni maalumu sana katika kuwahudumia Wananchi au Wanachama. *NSSF* ni mfano wa kuigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira kwa vijana wetu bado ni kitendawili, hakuna uwazi kwenye sekta ya ajira nchini, bado kuna upendeleo, kujuana, kufahamiana, rushwa na *nepotism* (ukabila).

Mheshimiwa Mwenyekiti nashauri Wizara hii isimamie kwa karibu ajira za vijana wanaomaliza vyuo kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuwe na uwazi zaidi katika ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Umma chini ya Wizara ya Kazi na Ajira zina dhima ya kuchangia katika kuwezesha mazingira bora ya utekelezaji mzuri na viwango vya kazi usawa na kazi za staha na kuongeza nafasi za ajira. Kwa nyakati mbalimbali kati ya mwaka 2011, 2012 na 2013, nimetoa mapendekezo kwa Taasisi mbalimbali za Wizara ya Kazi na Ajira, hata hivyo sijawahi kupata majibu ya maandishi juu ya utekelezaji uliokamilika.

Hivyo, katika majumuisho naomba Waziri na Wizara inipe mrejesho wa utekelezaji kutoka kwa Taasisi zifuatazo:-

Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi *(OSHA)* ni maeneo na mahali gani kwa kazi katika Jimbo la Ubungo imefanya ukaguzi? Nini matokeo ya ukaguzi huo na hatua gani imefikiwa katika utekelezaji wa mapendekezo? Na ni maeneo gani *OSHA* inakusudia kufanya utafiti katika Mwaka wa Fedha 2014/2015?

Kwa nini mpaka sasa haijaleta Bungeni Mikataba mitatu ya Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* ili iridhiwe? Mikataba hiyo ni Na. 155, 167 na 187 ambayo ni ya muda mrefu toka 1981, 1988 na 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Huduma za Ajira *(TAESA)* imefanya uhamasishaji gani kwa upande wa Jimbo la Ubungo kuhamasisha na kusajili watafuta kazi? Katika orodha ya vyuo ambao *TaESA* imevitembelea hakuna hata kimoja cha Jimbo la Ubungo pamoja na eneo hilo kuwa na Vyuo vingi vya Elimu ya Juu.

Je, ni lini *TaESA* itatembelea Vyuo vya Elimu ya Juu vilivyopo Jimboni Ubungo ikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Usafirishaji, Chuo cha Maji, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha St. Joseph Kibamba na vyuo mbalimbali vya binafsi vya Ualimu, Uuguzi, Uandishi wa Habari na fani nyingine mbalimbali? Naomba pia *TAESA* inishirikishe katika ziara hizo kuweza kuhamasisha vijana namna ya kukabiliana na soko la ajira na kutumia fursa zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati mbalimbali nimetoa mapendekezo kuhusu Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* hili juu ya mipango yake ya mafunzo na tafiti, kutazama pia washiriki kutoka Jimbo la Ubungo na Taasisi za Umma na za Binafsi nilizozipendekeza mwaka 2011, 2012 na 2013. Ni mapendekezo gani ambayo imeyatekeleza mpaka sasa na katika mwaka 2013/2014? Je, *NIP* iko tayari tukutane mara baada ya makadirio ya mapato na matumizi ya 2014/2015 kuangalia ni mapendekezo yapi yanaweza kutekelezwa kwa mwaka unaoanzia Julai, 2014?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti Hifadhi za Jamii *(SSRA)* ilete Bungeni Ripoti ya Ukaguzi iliyofanya katika maeneo 16 ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili Wabunge tuzitumie kufuatilia utekelezaji wa sheria zilizounda Mifuko husika. Aidha, *SSRA* itoe taarifa Bungeni juu ya ahadi ya kupatia ufumbuzi endelevu mgogoro wa fao la kujitoa.

MHE. MARGARET A. MKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Watendaji wote wa Wizara kuanzia Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu

Mkuu na Wakurugenzi wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara hii, kwa kufanya kazi nzuri ingawa wana changamoto ya bajeti ndogo sana ikilinganishwa na majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuiuliza Wizara ni kwa kiasi gani inahakikisha kuwa, watu wenye ulemavu waliobahatika kusoma wanapata ajira Serikalini na kadhalika kama Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inavyoelekeza?

Nauliza hivi kwa sababu wengi wanaomaliza kwa mfano, Vyuo Vikuu wamekuwa wakiniomba kuwatafutia kazi Serikalini lakini nashindwa kuwasaidia. Hivyo, nashauri Serikali iweke utaratibu maalum wa kuhakikisha wenye ulemavu walio na vigezo vya kuajiriwa sehemu wanazoomba kazi wapewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuhimiza na kuratibu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Nchini. Mifuko hiyo inajitahidi kutimiza wajibu wao, lakini nashauri deni la Serikali kwa Mifuko hii mbalimbali lilipwe ili Mifuko hii isidhoofike kirasilimali fedha, kwa sababu imewekeza katika maeneo mbalimbali kwa miradi ya majengo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira ni uwekwe utaratibu unaeleweka kwamba, ajira zozote zinazotokana na uwekezaji wa wageni, makampuni hayo yahakikishe katika shughuli za kitaalamu lazima wafanyakazi wazawa wanafundishwa ili wageni hao waweze kuzalisha wataalamu wa humu nchini. Zaidi, nataka kufahamu Serikali imepunguza asilimia ngapi ya kodi ya mishahara yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio machache ambayo Waziri ameeleza katika Hotuba yake, Wizara hii inakabiliwa na changamoto nyingi na hapa nitataja chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto kubwa zinazoikabili Wizara hii ni kuwa Uchumi wa Taifa haukui kwa kasi inayowezesha uzalishaji wa ajira za kutosha na hasa katika Sekta za Kilimo, Ufugaji na Uvuvi. Jumla ya ajira 630,616 ambazo Waziri amezitaja katika ukurasa wa 12 wa Hotuba yake kuwa zimezalishwa kati ya 2008 na Aprili, 2014, hazitoshi kwa kulinganisha na vijana lukuki wanaozurura mijini na vijijini bila ajira. Ajira haziwezi kufanywa na watu wasio na ujuzi. Serikali katika hili imezembea imeshindwa hata kutekeleza mpango wake wa kujenga vyuo vya ufundi, ambavyo ndivyo vingekuwa mkombozi wa vijana. Kila wakati Serikali imekuwa ikitoa sababu ya ukosefu wa fedha; kwa nini isikope kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama ilivyokopa katika kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma? Ni rai yangu kwamba, Serikali ichukue

hatua thabiti ya kukopa ili ijenge vyuo vya ufundi katika kila Wilaya ili viwasaidie vijana wetu waweze kuajirika na kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mafao ya waliokuwa Wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, SUA na *MUHAS* ambao walikuwa kwenye utaratibu wa *SSSS* uliofutwa Machi, 2011; ulipofutwa wale waliokuwa bado hawajastaafu walihamishiwa *PPF*. Tatizo ni kuwa wale waliokuwa wamestaafu hawakupata haki ya Pensheni ya mwezi, wanachodai ni haki sawa na wenzao waliohamishiwa *PPF* hasa kwa sababu kubaki *SSSS* ulikuwa siyo uamuzi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pensheni za watu waliostaafu zamani ni ndogo sana. Pensheni hizi ziboreshwe.

MHE. ABASI Z. MTEMVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba nzuri sana Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kuhusu *TaESA* kuwajengea uwezo vijana ili waweze kusafiri nje ya nchi kama Oman, Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE),* Saudi Arabia na Qatar, kuwatafutia kazi Watanzania, kuna kazi nyingi sana nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Wizara ya Kazi na Ajira na *NSSF*, kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Je, ni lini Daraja hilo litakuwa limekwisha na kuanza kutumika?

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu ya wachangiaji imekwisha; kwa maana jioni Mheshimiwa Waziri mtaanza moja kwa moja saa 10 kujibu na badaye tutaingia kwenye Kamati ya Matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, Wizara hii ni kubwa sana na ndio watu wengi wanaitegemea na hasa vijana. Mngejaribu kutizama vilevile mkakati wa kufanya vijana wapende kilimo, muwe na *program* hizo. Wenzetu wa Ethiopia wamefanikiwa sana kuwafanya vijana wapende kilimo.

Vilevile mngejitahidi katika vikao vyenu kuwa na bajeti maalum, hii siyo ya kwenu lakini Serikali ikubali kutenga kama shilingi bilioni 200 uwe mtaji kwa vijana waliomaliza vyuo waweze kujiajiri, waweze kutoa huduma Serikalini. Serikali ikitaka *procurement* inakwenda kwa hawa na hawa waweze kutoa huduma hizo kwenye Uwakili, *Engineers, Consultancy* na mambo mengine. Ni vitu vya kufanya maamuzi tu *otherwise* kutakuwa na matatizo makubwa sana siku za usoni. *(Makofi)*

Hata hii sekta ambayo siyo rasmi, wenzetu nchi ya jirani sekta isiyo rasmi, hawa Machinga, Bodaboda, Daladala, wanachangia shilingi trilioni nane kwa

mwaka kwenye kodi, lakini sisi tunafukuzana nao tu mitaani. Kwa hiyo, ningeomba mjaribu kulitizama hilo.

Kuna mgeni hapa mahsusi wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mwanri; Ndugu Jonathan Nassari ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha. Karibu sana Dodoma. *(Makofi)*

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 6.48 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye hoja ya Waziri wa Kazi na Ajira kuhusu Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia baadhi ya maoni, maswali na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia, nichukue fursa hii, kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia uhai na afya kuweza kuwa mbele yako na mbele ya Wabunge siku ya leo. Nawashukuru sana Wapigakura wangu wa Jimbo la Segerea, ambao wameendelea kuniamini na kunirudisha Bungeni na kuweza kupata nafasi hii ambayo sasa naitumia. Nimshukuru vilevile Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Ajira, Mama Gaudentia Kabaka, kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa na kuniongoza katika kutumikia nchi hii kupitia Wizara ya Kazi na Ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingi zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge na kwa muda tulionao mimi na Mheshimiwa Waziri, inawezekana tusiweze kumaliza kuzijibu zote. Tunaahidi tu kwamba, majibu yatatolewa kwa hoja zote zilizotolewa kwa maandishi ili Wabunge wapate maelezo kutoka Serikalini kuhusu hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kama Wizara ya Kazi na Ajira, ina shughuli za Wizara lakini ina Taasisi mbalimbali katika Wizara hii ambazo zinawajibika kwa Wizara; na kwa maana hiyo hoja zilizotolewa, zipo zile

zinazohusu Wizara kama Wizara na zipo zinazohusu Taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na hoja chache za Taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara hii na zinafanya kazi kwa maelekezo ya Wizara kisera. Labda nianze na hoja zinazohusu Sera za Hifadhi za Jamii zinazosimamiwa na *SSRA*, ambao ndiyo wadhibiti wa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii nchini. Kama tunavyojua, liko hili suala la pensheni ya wazee, ambalo limeulizwa na Wabunge wengi sana na sina haja hata kuwataja watatajwa kwenye *Hansard*. Sasa tunajua kabisa kwamba, Sera ya Wazee nadhani toka mwaka 2006 ilitoka kwenye Wizara yetu na kwenda kwenye Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa hiyo, Sera ya Wazee na masuala yote yanayohusu wazee na watu wenye ulemavu na watu wanaoishi kwenye mazingira magumu, Kisera yako kwenye Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Kwa kuwa masuala ya pensheni yako Wizarani kwetu kupitia *SSRA*, hili suala la kuandaa pensheni kwa wazee lililetwa Wizarani kwetu ili *SSRA* na Wizara iweze kulisimamia. *SSRA* ukweli wamefanya hiyo kazi kwa hatua za mwanzo na tumekutana na changamoto nyingi sana; ni kweli Viongozi wa Kitaifa waliahidi suala hili kwamba, litaanza kuangaliwa na *SSRA* imekuwa ikifanya hii kazi.

Waheshimiwa Wabunge wa Kamati yetu ya Maendeleo ya Jamii, watakumbuka namna ambavyo tumekuwa tukilijadili kwenye vikao vyetu kwa undani na hata tukatoa ratiba au mpango kazi wa kushughulikia suala hili Mara ya mwisho tulikuwa kwenye suala la kupata uzoefu kutoka nchi mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wa Wizara, tulipita kuona wenyewe wanafanyaje hasa kwenye suala hili la pensheni ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ripoti imetoka, nchi mbalimbali ambazo tumezitembelea na kwa kweli Wajumbe wa Kamati ambao wote wamepata nafasi ya kutembelea nchi mbalimbali na mimi nilikuwa nao kwenye maeneo mengi katika hizo nchi, wataniunga mkono kwamba, tulipata changamoto hata kwenye hizo nchi ambazo zingine zimeendelea sana; kwa maana kwamba, hatukukuta maeneo mengi, labda kama eneo moja hivi ambao wanatoa ile *universal pension* kwa wazee. Kwa maana wale wazee ambao hawakuwahi kuchangia kwenye Mifuko yoyote ya Hifadhi ya Jamii, lakini sasa wanalipwa na Serikali kutokana na Bajeti ya Serikali yenyewe na siyo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Nchi nyingi zilituambia hilo ni gumu kutokana na suala la uendelevu *(sustainability),* kwa sababu linahitaji bajeti na kodi za Wananchi. Kwa hiyo, kwa nchi kama ya kwetu walituambia tuwe waangalifu kama ambavyo Viongozi wamekuwa wakituambia. Tuwe waangalifu katika kuliendea suala hili, tuwe na uhakika wa vyanzo vyetu vya mapato kama nchi kama Serikali, ili tutakapoanza

kutoa basi tuwe na uhakika kwamba, utoaji huo wa pensheni kwa wazee utakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi suala hilo la uendelevu na kuangalia vyanzo vya mapato ndiyo itakuwa hatua tunayotakiwa tuangalie, tukishirikiana na Wizara ambazo zinahusika kushughulikia mapato ya nchi, kwa maana Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha; kuona kwamba je, tukianza kutoa pensheni hii tutakuwa na uwezo kama nchi kuendelea kutoa kwa miaka mingi ijayo?

Kwa hiyo, siyo suala tu la kurukia kuleta Muswada wa Pensheni ya Wazee hapa Bungeni, lakini tujiridhishe kwanza na wenzetu hawa ambao ndiyo wanatafuta vyanzo vya mapato hapa nchini, kama tutaweza kulipa pensheni kwa wazee, ndipo baada ya hapo tulete sasa Muswada na mambo mengine ambayo yanaendelea. Mpango Kazi huo tunao, tunaendelea nao na kila baada ya muda tutakapokuwa tunakuja Bungeni, tutaweza kutoa taarifa tumefika wapi katika ule Mpango Kazi wa kuona kwamba, tufike mahali tuanze kutoa pensheni hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kukopesha fedha na hazirudishwi na Serikali, wengi wamezungumza, ndugu yangu Mariam Kisangi na wengine na hata Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Faida Bakari, Mheshimiwa Mipata; niseme tu kwamba, *SSRA* wana jukumu vilevile la kuangalia jinsi ambavyo Mifuko hii inatoa mikopo. Kwa upande wa mikopo ambayo inatolewa kwa Serikali, kwa mfano, ujenzi wa *UDOM* au ujenzi wa Jengo hili na daraja kwa mfano la Kigamboni, nyumba za Watumishi wa Serikali kama Polisi na kadhalika, inaonekana kabisa kwa ukaguzi wa *SSRA* kwamba, Serikali inaendelea kulipa mikopo hiyo. Sasa ukiona mkopo umebaki inategemea mkataba kwamba, mikopo hiyo ingelipwa kwa miaka mingapi. Kusema Serikali hawalipi, hii si kweli kabisa na Serikali inajitahidi kulipa. Pale inapokuwa imekwama kidogo inakumbushwa kama ambavyo mtu yeyote hata sisi tunavyokopa ukichelewa kidogo unakumbushwa.

Kwa sasa kwa sababu *SSRA* ipo, uwekezaji unafanywa kwa kuzingatia Miongozo ya Uwekezaji ya Mwaka 2012 ambayo imeandaliwa kwa pamoja na *SSRA* pamoja na Benki Kuu ya Nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kwa upande wa uwekezaji na ukopaji, mimi nadhani Mifuko yetu inafanya vizuri, faida imekuwa ikionekana na ndiyo maana Mifuko yetu yote inatoa taarifa za faida zinazopatikana na inaendelea kukua.

Kuhusu Wanachama kuruhusiwa kuhama kutoka Mfuko mmoja kwenda mwingine, alizungumza ndugu yangu Mheshimiwa Jafo; suala hili linaendelea

kushughulikiwa na kwenye maboresho ambayo tunaendelea kuyafanya katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii, ushauri huu umezingatiwa. Baada ya muda tutaona matokeo yake, Wanachama wanaweza kuruhusiwa kuhama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililotolewa na Profesa Kahigi ni kuwarudisha Wanachama wa *SSS* ambao waliondoka kabla ya kuhamisha Mfuko huo kutoka Shirika la Bima kwenda *PPF*. Hivi sasa Serikali kwa kupitia Mfuko wa *PPF*, inalipa pensheni kwa Wanachama waliokuwa wa SSS ambao walikuwa bado wapo kwenye Utumishi wa Umma wakati Serikali inahamisha Mfuko huo kutoka Bima kwenda *PPF* na ambao walikuwa bado hawajachukua mafao yao kutoka Mfuko huo wa *SSS*.

Mhehimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa John Mnyika, aliomba Kaguzi za Mifuko kupelekwa Bungeni. Kwa mujibu wa Kifungu cha 39(9) cha Sheria Namba 8 ya Mwaka 2008, kaguzi zinazofanywa na mamlaka kuhusu utendaji wa Mifuko, zinawasilishwa na Wenyeviti wa Bodi kwa ajili ya kufanyia kazi maagizo ya mamlaka. Kwa hiyo, zipo mamlaka ambazo zinakagua ripoti hizi na wala hazina tatizo lolote na ukizingatia kwamba, *CAG* naye anakagua Mifuko hiyo. Wabunge kadhaa vilevile walilalamikia pensheni ndogo ya shilingi hamsini elfu kwa Watumishi wa Serikali. Niseme tu kwamba, hili tunalichukua na litawasilishwa Wizara ya Fedha ili lifanyiwe kazi kwa uzito wake.

Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya, alizungumzia faida kwa Wanachama kutokana na uwekezaji wa Mifuko hii. Mifuko hii ni ya pensheni ambayo inatumia utaratibu wa Kibima; hivyo, mafao anayoyapata Mwanachama yanajumuisha michango pamoja na faida inayotokana na uwekezaji. Ikumbukwe kwamba, Mwanachama anachangia jumla ya asilimia ishirini ya mshahara wake, lakini anapostaafu mkipiga mahesabu anapata pensheni ambayo ni kiwango cha si chini ya asilimia 67, *replacement rate* ya mshahara wake baada ya kupata malipo ya mkupuo au *lump sum*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo hoja zilikuwa za Kisera ambazo zilielekezwa kwenye Taasisi yetu ya *SSRA*.

Kulikuwa na hoja vilevile kwa Taasisi yetu ya *TAESA*, ambapo Mheshimiwa Angellah Kairuki na Mheshimiwa John Mnyika, walizungumzia masuala ya *TAESA*. Niseme tu kwamba, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka huu unaokuja kama ambavyo Mheshimiwa Waziri alivyosema, *TAESA* imepanga kutekeleza mengi tu kama ambavyo imefanya; kutembelea waajiri kwa mfano 1,000 kwa lengo la kubaini idadi ya aina ya fursa za ajira katika sekta mbalimbali; kutembelea vyuo vya elimu ya juu ishirini kwa lengo la kutoa mafunzo ya jinsi ya kukabiliana na soko la ajira; vilevile kuweza kuboresha mifumo ya TEHAMA; na imepanga kufanya makongamano mawili makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutembelea maeneo ya kazi ni gharama na *TAESA* wamekuwa wakijitahidi. Inawezekana kwenye Majimbo yetu ikiwemo Ubungo, kuna maeneo ambayo hayajatembelewa, lakini katika mipango ya Taasisi hii wataendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa John Mnyika, alizungumzia vilevile suala la mkopo la Kiwira kuwa haina tija na deni halijalipwa. Niseme tu kwamba, mkopo wa *NSSF* kwa Kiwira ulitolewa kwa nia ya kufufua kiwanda kizalishe makaa ya mawe na umeme. Siyo kweli kwamba, mkopo huu haujalipwa. Mkopo uliotolewa ni shilingi bilioni tisa mwaka 2007 Julai, ambapo hadi kufikia mwaka 2012 zilishapanda na kufika bilioni 18. Shilingi bilioni 14.25 zililipwa na Serikali mwezi Septemba, 2012 na shilingi bilioni tatu zililipwa mwezi Julai mwaka 2013. Kwa hiyo, kiasi kilichobaki cha milioni 742 kitalipwa na Serikali kabla ya mwisho wa Mwaka wa Fedha huu ambao tunaumaliza mwezi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *PSPF* kwamba kuna *actuarial deficit* ya shilingi trilioni 6.49; niseme tu kwamba, Serikali imepanga na inatekeleza mpango wa kuipa *PSPF* fedha za kuondoa *deficit* hiyo, inayotokana na kulipa mafao ya wastaafu ambao walikuwa hawachangii katika Mfuko huu wakati huo. Tunaelewa kwamba, Serikali kila mwaka imepanga kulipa, kwa sasa wanalipa bilioni kumi, lakini uwezo ukiongezeka watakuwa wanalipa zaidi kwa mwaka. Nikuhakikishie tu kwamba, *PSPF* haipo katika hali mbaya. Kwa hiyo, hizi bilioni 58 ambazo zimekopesha Bodi ya Mikopo, nayo ilifanywa katika mpango ule ule wa Sera ya Vitega Uchumi na mkopo utalipwa kutokana na makubaliano ya mkopo huo.

Mheshimiwa Tundu Lissu naye aliuliza kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, inayotumia shilingi bilioni 662 kutekeleza Miradi ya Serikali isiyo na tija, hadi sasa fedha hazijalipwa. Kwa kweli sina hakika kama Wabunge watakubaliana na Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba, Miradi hii inayowekezwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii haina tija kwa Taifa. Mifano ni mingi na mimi nadhani Wajumbe wengi walizungumzia faida hizo. Niseme tu kwamba, maamuzi yote ya uwekezaji hufanywa na Bodi za Wadhamini za Mifuko hii na zinaangalia tija kabla ya kukubali uwekezaji wa aina hiyo. Kwa hiyo, nadhani kusiwe na wasiwasi wowote kuhusu tatizo hilo. Kusema kwamba, Bunge liunde Tume, mimi nadhani hakuna sababu ya kuunda Tume kwa sababu Mifuko hii inafanyiwa kaguzi za mara kwa mara na *actuarial valuation* na hali inaonesha kwamba ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza kuhusu mikopo inayorudishwa ya ujenzi wa *UDOM* na hata *General Tyre*. Kuhusu *General Tyre*, kwanza, kama mnavyojua, tatizo la kampuni ile, baadaye *NSSF* ilianza taratibu za kuitaka Serikali iilipe *NSSF* fedha zake kufuatia udhamimni wa Serikali kwa sababu Serikali

ndiyo ilidhamini. Hata hivyo, Kamati ya Bunge Iliishauri *NSSF* iache kufanya hivyo ili kiwanda kifufuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Machinga Complex* umeshindwa kulipa, ni kweli lakini *NSSF* inaendelea kufanya mazungumzo na Serikali ili mkopo huo ulipwe kwa njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo hoja nyingi zilitolewa kuhusu *NSSF* na nyingine labda atazijibu Mheshimiwa Waziri, kwamba, *NSSF* iwekeze kwenye maeneo yaliyo nyuma kimaendeleo. Hilo linazingatiwa lakini tukumbuke tu kwamba, lazima iangalie ifanye upembuzi yakinifu ili kila Mradi unaoanzishwa uwe kwa manufaa ya wenye *NSSF* ambao ni Wanachama.

Hili la kuangalia namna ya kuboresha mafao ya Wanachama, limekuwa likiendelea kufanywa na Shirika la *NSSF* limeanzisha mafao ya ziada kwa Wanachama. Mafao hayo ya ziada ni pamoja na mikopo kwenye *SACCOS* na *VICOBA* kama ambavyo imeelezwa, ujenzi wa nyumba za Wanachama na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ofisi za Wabunge Majimboni; majadiliano kati ya Ofisi ya Bunge na *NSSF* kwa upande mwingine yamekaribia kukamiliza, kwa hiyo, tusubiri hili litakwenda vizuri.

Kambi ya Upinzani vilevile ilizungumzia kuhusu *NSSF* kukiuka Waraka wa Serikali unaotaka Watumishi wa Mikataba kulipa kiinua mgongo. Hili nalo kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi, mwenye mkataba anatakiwa kulipa *gratuity* ya asilimia 25 watumishi waliopo katika ajira ya mkataba, wakurugenzi wa mikataba ya miaka mitatu mitatu hulipwa kiinua mgongo. Hivyo, hakuna malipo ambayo yanalipwa mara mbili kulitia hasara shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua muda wangu umekwisha, yapo mambo mengi ambayo Mheshimiwa Waziri atakuja kuyajibu, nashukuru sana kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa tena nafasi mchana huu hasa kwa nia ya kutoa majibu kulingana na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuwasilisha hoja yangu asubuhi.

Hoja hii imevutia wachangiaji wengi na kwetu hii ni furaha kwa sababu inaonesha Wizara hii inavyofahamika, wanavyojua majukumu yake na hivyo wangependa majukumu haya yaboreshwe. Kwa hiyo, kwetu michango hii itatusaidia sana katika kujipanga upya kwa kipindi cha mwaka ujao wa fedha ilimradi hizo pesa mtusaidie kuzipata.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi wako 37 na waliochangia kwa kuongea wako 18, akiwemo Mheshimiwa Makongoro Mahanga, kwa hiyo, jumla wako wachangiaji 55. Naomba niwashukuru sana kwa michango yenu na yote ni michango ambayo ina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idadi hiyo michango, siahidi kama tutaweza kutoa majibu hapa niliposimama kwa dakika zilizobaki. Kama ilivyo ada, sisi tutatoa majibu kwa kutumia bango kitita na tutampa kila Mbunge ili iwe rejea kwake kwa baadaye. Naomba nijitahidi sasa hivi kuendelea na majibu ya hoja zilizotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine yaliyoongelewa sana ni suala zima la ukosefu wa ajira na kukuza ajira. Hapa naomba nianze kwa rai kwamba, ukosefu wa ajira kama tunavyofahamu upo Dunia nzima, Afrika nzima, Afrika Mashariki pamoja na Tanzania. Kwa hiyo, ni suala ambalo linaumiza Serikali nyingi na hasa ajira kwa vijana. Tunapozungumza hasa tujikite kwenye ajira kwa vijana. Natoa rai na kusema kwamba, kazi yetu kubwa pamoja na kuizungumza Serikali, pamoja na michango mizuri iliyotolewa, mimi naomba nitoe aina moja au hali moja ambayo inasaidia au inakwamisha kuwapa vijana wetu ajira kama tunavyotegemea.

Kwanza, mimi niwashukuru sana akina Mheshimiwa Faida Bakar, pamoja na Mheshimiwa Munde, kwa kueleza na kuonesha mtazamo uliopo wavijana wengi kuhusu suala zima la ajira. Kwa hali ya kawaida, vijana wengi wa Tanzania na nchi nyingine, wanapohitimu elimu yao hasa elimu ya juu, wazo lao kubwa ni kupata ajira Serikalini. Akikosa hiyo ajira Serikalini basi atatafuta kwenye makampuni binafsi ikiwemo viwandani, kwenye *NGOs* na kwa watu binafsi. Akiikosa hiyo ajira Serikalini na kwenye Sekta Binafsi, kinachofuata ni kuilaumu Serikali kama wengi tunavyofanya kwamba, Serikali imenisomesha lakini imeshindwa kunipatia ajira.

Naomba niwapongeze sana Vijana wa Tanzania ambao kwao dhana ya ajira imeanza kupanuka, wameanza kuondokana na *traditional thinking* ya ajira kama kazi ya kuajiriwa ofisini, Serikalini au viwandani kwa kutumia vyeti walivyotoka navyo Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hapa nitoe taarifa kwamba, Jumapili iliyopita tarehe 18 Mei, 2014 nilisoma Gazeti la Mwananchi, ukurasa wa 13,

kulikuwa na stori ya kijana mmoja ambaye alijiita kwa jina la Nick wa 11. Kichwa cha habari cha hiyo stori kilikuwa kimeandikwa; "*Rapper* wa *hip hop* mwenye *Masters* ambaye hataki kazi." Kama Waziri wa Kazi na ambaye nilitarajia kutoa kusoma bajeti, ilibidi niwe na hamu ya kujua kinachojiri katika hii stori.

Huyu kijana ana Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Huyu kijana pamoja na kwamba, ana Shahada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika fani ya Uongozi, yeye ameamua kuwa mwimbaji wa *hip hop*. Katika kuimba kwake ametunga wimbo na wimbo alioutunga karibuni maneno aliyozungumza aliwalenga vijana waliohitimu elimu ya juu kama yeye mwenyewe. Wimbo huo unasema sitaki kazi; sina hakika kama mmeshausikia?

Anasema nanukuu: "Niliimba wimbo huu kutokana na kuwaona vijana wengi wenye elimu ya juu wanahangaika kupita huku huku na vyeti vyao wakitafuta ajira. Kwangu mimi naona ni utumwa kwa msomi kutegemea kufanya kazi za watu wengine badala ya kuibua cha kwako ili utoe ajira kwa wengine." Mwisho wa kunukuu.

Kwenye gazeti la leo niliendelea kusoma kwamba, kwenye wimbo huo ameelezea pia namna yeye mwenyewe au kijana mwingine anavyoweza kutatua tatizo la ajira kwa kubuni vitu mbalimbali ambavyo vitazalisha pato na kuweza kuajiri maelfu ya vijana wenzie waliohitimu mwaka hadi mwaka. Jina lake ni Nickson Simon, kama nilivyosema wala hakusomea uimbaji amesomea Shahada ya Uzamili katika Maendeleo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kutoa mfano huu si kwamba, nabeza vijana ambao wanatafuta ajira, hapana; lakini nilitaka tu nitoe mfano kwamba, kuna vijana ambao wameshaanza kupanua dhana zima ya ajira kwamba si kuajiriwa, kwamba siyo watafuta kazi, vijana wasiwe watafuta kazi bali wawe watengeneza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine kama ilivyoeleza Sera yetu ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008, tumeanza na tunahamasisha vijana wengi, wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vingine vya elimu ya juu, kuwa wabunifu na kutumia ubunifu huo na mazingira waliyomo ili kujiari na kuajiri wengine. Tunafahamu vijana wanapomaliza vyuo vikuu hawana taaluma ya kujiari, hili tumeligundua, hawana mtaji wa kujiajiri, hawana maeneo ya kazi kwa maana ya ardhi, ili watimize azma hii ya kujiri.

Serikali yangu kama nilivyosoma kwa mwaka huu fedha, tumeamua angalau kuanza na hili kwa kujaribu, tulitaka tupate angalau bilioni 36 lakini kutokana na Sungura mdogo tumepata bilioni tatu tulizotengewa, tutajitahidi kadiri tutakavyoweza kuwasaidia vijana ambao wako tayari kujiari. Narudia, ambao wako tayari kujiajiri. Kwa sababu Waswahili wanasema huwezi

kumlazimisha punda kunywa maji, lazima punda huyo awe tayari kunywa maji. Kwa kutumia hao vijana walioko tayari kujiajiri, nafikiri tunaweza sasa kuhamasisha wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kuna vijana wameshahamasika na tunawatambua, wamemaliza vyuo vikuu, hasa Chuo Kikuu cha *SUA,* ambao kwa kutumia ubunifu wao na kwa kuongozwa na Viongozi wao, wameanza kujiari. Kama nilivyosema, siyo Serikali peke yake inayowasaidia vijana hawa, lakini kwa kushirikiana na wadau na wadau wetu kama nilivyosema mwanzoni ni hiki Chuo Kikuu cha *SUA*, lakini benki zetu Benki ya *CRDB* ikiwa mojawapo. Tuna Shirika la Kazi la *ILO* ambao pamoja na Wizara ya Kazi, tunao Mradi tunaouendesha unaoendesha shughuli za ajira unaoitwa kazi nje nje na kuna aina pia ya Mradi unaoitwa moto wa nyika. Ukiona majina yote haya yanaashiria kwamba, ajira ni shughuli, ni dhana ya ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwamba, tunao Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ambao tuko nao bega kwa bega katika kuhakikisha kwamba, dhana ya ajira kama shughuli ya ambayo anafanya Mwananchi ili kujikwamua na umaskini, inaenda na shughuli nyingine kama hizo za kilimo. Nitoe mfano wa mikoa hiyo; tunaye Mkuu wa Mkoa wa Tabora ambaye kupitia Wilaya ya Sikonge na Igunga, wametumia kilimo kuhakikisha vijana wanajiajiri. Tunaye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mkuu wa Wilaya ya Iramba, ambapo vijana wanajiajiri kupitia Sekta ya Madini. Mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Iringa, ambapo vijana wanajiajiri kupitia kilimo, tuna Mkoa wa Dodoma vijana wanajiajiri kupitia kilimo, tunao Mkoa wa Shinyanga vijana wanajiajiri kupitia madini, lakini tunao Mkoa wa Pwani, ambapo vijana wanajiajiri kupitia stadi mbalimbali zikiwemo za kilimo, ufugaji, ujenzi na upandaji miti. Mikoa yote hii imeonesha kuwa inawezekana. Inawezakana kabisa kubadilisha mtazamo wa vijana kuhusiana na dhana ya ajira, badala ya vijana kuwa watafuta ajira sasa wanakuwa watengeneza ajira, yaani *from job seekers to job creators*.

Naomba niwaalike wadau wengine tusaidiane katika hili na tusiwe wa kwanza kuilaumu Serikali kwa ukosefu wa ajira hasa kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nianze na hili kama *preamble* ya kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge, ambao wamezungumzia ukuzaji wa ajira kwa kirefu na kwa uchungu, ikiwemo pia Hotuba ya Kambi ya Upinzani, ambayo imezungumzia suala hili la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi wameulizia mkakati katika kutatua tatizo la ajira kwa vijana, nafikiri nimeshausema lakini labda niwataje tu ni wengi, yupo Mheshimiwa Juma Sululu Juma, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimwa Eng. Ramo, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa,

Mheshimiwa Said Mussa Zuberi, Mheshimiwa Gosbert Blandes; ni wengi, naomba wote mwamini kwamba, tumewatambua. Kama nilivyosema, suala hili la ukuzaji wa ajira linahusisha wadau. Wadau wote, Serikali ikiwa mdau mmojawapo, sekta binafsi ikiwa mdau, mashirika ya kijamii yakiwa wadau, mashirika ya kidini, jukumu kubwa la Serikali katika hili ni kuweka mazingira wezeshi ya kisera, sheria na miundombinu na hii ndiyo tunafanya. Aidha, katika kukabiliana na tatizo hili la ukosefu wa ajira, Serikali imekuwa ikitoa mafunzo na miongozo ya namna ya kuingiza masuala ya ukuzaji ajira katika bajeti na programu za Wizara mbalimbali, Idara za Serikali za Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wizara imehamasisha wadau wengine wa sekta binafsi kama nilivyowataja, kuona umuhimu wa kuzingatia masuala ya ukuzaji ajira kupitia makongamano na mafunzo mbalimbali. Nafikiri mmekuwa mashahidi katika kuwasikia vijana, *NGO* zinavyoendesha makongamano mbalimbali, yote hayo yakiwa na lengo la kusaidia vijana kukuza ajira na kujiajiri.

Wizara yangu kama nilivyosema, tumeandaa programu, tumeitaja katika bajeti iliyopita, tulifikiri tungetengewa pesa lakini haikuwezekana. Kama nilivyosema, mwaka huu tulikuwa tumeomba bilioni 36, lakini tumepata bilioni tatu, tutaanza nayo. Hii tutawapa vijana mikopo ya masharti ya nafuu, lakini tutawafundisha pia stadi za ujasiriamali na kuwasaidia kupata maeneo ya kufanyia shughuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la maeneo la kufanyia kazi, labda niunganishe nalo kwa kujibu suala ambalo limezungumzwa kuhusu Wamachinga. Nafikiri wote ni mashahidi hasa tunaokaa Dar es Salaam, tunaopita Dar es Salaam, sidhani kama kuna mtu anapendezwa kila mahali unapopita hasa mnapoendesha magari unakutana na vijana wametandika nguo, wametandika sufuria, vikombe, *glass, socks;* sidhani kama inatija. Hakuna nchi Duniani, ninyi mnaenda sana nje ya nchi, hamna mahali mnakuta kila mahali pamezagaa bidhaa za wajasiriamali wadogo. Kwa hali hiyo, siyo kwamba Serikali ya CCM imeamua kukimbizana na Wamachinga; hapana, lazima kuwe na *orderly work,* lazima kuwe na taratibu za kufanya biashara na ndiyo maana kuna maeneo.

Mheshimiwa Chiku Abwao amesema nisizungumzie suala la *Machinga Complex,* lakini ujenzi wa *Machinga Complex* ilikuwa ni moja ya hatua za kutatua maeneo ya Wamachinga kufanyia biashara zao. Shirika la *NSSF* kwa dhati waliamua kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, lakini ilikuwa tayari kujenga majengo kama yale Kinondoni na Temeke, kwa hiyo, kwa Mkoa mzima wa Dar es Salaam na baadaye wangeenda katika mikoa mingine.

Lile Jengo la *Machinga Complex* kama tungesaidiana wadau kuwaweka vijana wote pale, mimi nafikiri hao wanaotembeza nguo kwenye magari,

kwenye msururu wa magari, wote wangekuwa pale na miji yetu ingekuwa safi, tungeweza kupita bila kubughudhiwa na bila kuibiwa. Kwa hiyo, mimi nafikiri Waheshimiwa tusitetee suala hili kama vile hatuoni madhara yake.

Mimi nafikiri tukubaliane, kwa sababu mtu anapotaka kufanya biashara, Serikali siyo ya kwenda kumtafutia maeneo. Sema hivi Serikali ipange iweke maeneo ya kufanyia shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, kila anayetaka kufanya shughuli yake, anaenda kuomba kwamba nataka kufanya shughuli yangu. Serikali haimtamfutii mtu mahali pa kujenga nyumba, Serikali inapima maeneo, unapotaka kujenga nyumba au unataka kujenga jengo la biashara, unaenda kuiomba Serikali wanakupa kwa kibali kwa maandishi. Kwa hiyo, nafikiri hili tuliongelee kwa hali hiyo na wala tusiilamu sana Serikali, kwa sababu hakuna Serikali ambayo inapenda kunyanyasa watu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha na kuongeza ufanisi katika kusimamia ajira za wageni nchini, suala ambalo limechangiwa na Waheshimiwa wengi; Mheshimiwa Suzan Limbweni Kiwanga, Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Mheshimiwa Joyce Mukya, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Nassib, kwamba, vibali vya wageni wanapokuja kufanya kazi katika nchi hii wanamaliza nafasi za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwa kifupi kwamba, hili tumeliona siku nyingi, lakini kutokana na hali halisi ya utoaji vibali iliyokuwepo kwa muda mrefu tunafanya nini? Wizara imeamua sasa kuhakikisha vibali vya ajira za wageni vinatolewa na Mamlaka moja. Tumekamilisha mapendekezo ya Muswada na ninaamini Muswada huu utakapokuja hapa Bungeni hata kama ni kwa Hati ya Dharura, naomba mtukubalie. Sheria itakayotungwa itawezesha kuwepo kwa mamlaka moja ya kutoa vibali na kuondoa mkanganyiko wa kisheria uliopo, unaozipa mamlaka zaidi ya moja katika kutoa vibali vya ajira kwa pamoja. Pamoja na mambo mengine, sheria itaainisha shughuli ambazo wageni hawapaswi kufanya hapa nchini na shughuli wanazopaswa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tarifa ni kwamba, kibali kikitoka *TIC, Class A,* hakimzuii huyo mwekezaji kuanzisha biashara ya kuuza maua. Sasa katika Muswada huu, katika Sheria hii tunasema hivi, tumeainisha shughuli ambazo mgeni akiingia nchini haruhusiwi tena kuzifanya ikiwemo na hizo. Sheria pia itazingatia utozaji wa tozo wa vibali vya ajira. Kwa hivi sasa hatutozi vibali vya ajira isipokuwa mgeni anatozwa pesa na uhamiaji kwa maana ya kibali cha ukaazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, alitoa hoja kwamba, kuna hali hatarishi zilizopo Mgodi wa Bulyanhulu, kwa mfano, vumbi la *silica,* hewa pungufu mgodini, kelele kutokana na *jakhammer* na

mengine. Suala hili pia lililetwa na Mheshimiwa Maige, ambaye alilalamika sana kwamba, *OSHA* hawasaidii Wafanyakazi wa Mgodi wa Bulyanhulu.

Naomba tu nisaidie kumjibu Mheshimiwa Sabreena Sungura kwa kusema hivi; ni lazima ifahamike kwamba, hayo ndiyo mazingira halisi ya mgodi hasa mgodi wa chini ya ardhi. Mwajiri analifahamu hili na vihatarishi hivyo vilivyopo na Sheria ya *OSHA* inamtaka mwajiri amweleweshe mfanyakazi hali hiyo; kwamba, mgodi huu ni wa chini ya ardhi. Mwajiri pia anapaswa kuhakikisha kwamba, vihatarishi tajwa vinadhibitiwa ili visilete madhara kwa wafanyakazi, mfano, kuweka mitambo ya hewa ya ziada kutoka nje ili kuongeza hewa ya *oxygen* huko ndani, kunyunyizia maji wakati wa kutoboa miamba ili kupunguza vumvi la *silica,* kupunguza saa za kufanya kazi ili kupunguza muda wa kuwa kwenye vihatarishi, kutumia vifaa vya kukinga masikio ili kupunguza athari za kelele na kadhalika. Kwa maana nyingine, kuhakikisha wafanyakazi wake wana vitendea kazi vinavyozuia madhara yatakayotokana na aina ya kazi wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia *OSHA* imekuwa ikikagua migodi na hasa Mgodi huu wa Bulyanhulu na kuhakikisha kuwa, mikakati hiyo imetekelezwa kama ilivyopasa ili kulinda afya za wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini, alieleza matukio ya wafanyakazi kuugua ugonjwa wa *silicosis* na hata kufa. Mimi siyo Daktari, lakini kupitia Wakala wa Afya na Usalama Mahala pa Kazi *(OSHA),* naomba mtusaidie kuthibitisha au kutuambia mtu yeyote ambaye ana orodha ya majina ya watu waliokufa na kuumia kazini kutokana na huo ugonjwa wa *silicosis,* maana yake unatokana vumbi la *silicone*. Hata hivyo, mpaka sasa *OSHA* imepima wafanyakazi wapatao 6,427 katika migodi minane ambayo ni Tulawaka, Mwadui, *Kambanga Nickel*, *Shantamining*, *Tanico Energy,* Ruvuma, Buzwagi na *Geita Gold Mine*. Hata hivyo, hakuna mfanyakazi hata mmoja aliyepatikana na *silicosis,* isipokuwa kuna baadhi wamepatikana na matatizo ya kifua cha kawaida na matatizo ya mgongo. Kwa hiyo, hayo ni maelezo ya kitaalam na kama kuna mtu ana orodha ya watu waliokufa au waliougua *silicosis,* basi tupate taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari na Mheshimiwa John Mnyika, walipenda kujua ni lini Mikataba Namba 155, 167 na 187 italetwa Bungeni. Mikataba hiyo imeshafanyiwa uchambuzi wa kitaalam, wa mwisho umefanyika na waraka upo katika hatua za mwisho ili kupelekwa katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, ipo katika hatua za mwisho. Nashukuru kuona kwamba mnaifahamu Mikataba yote hiyo.

Mheshimiwa Nassib Omary alisema, ufanyike ukaguzi wa vyombo vyote vya mvuke na kukabiliana na ongezeko la viwanda. Tunaposema tumefanya

kazi au ukaguzi asilimia 90 au pungufu, tuna maana ni kati ya kaguzi zote za aina mbalimbali. Isipokuwa kwa kaguzi ya vyombo vya mvuke, upepo na kunyanyulia mzigo, kaguzi hizi zinafanyika kwa asilimia 100. Kwa hiyo, unaposema tumefanya asilimia kadhaa ya kaguzi, maana yake ni kaguzi zote kwa jumla; lakini *specifically* ni kwa ajili ya hivi vyombo vya upepo wa kunyanyulia mizigo, hizi zimefanyika kwa 100% kama Sheria inavyotaka.

Pia, kaguzi hizo zinatozwa gharama kidogo ili kugharamia kaguzi zenyewe. Ili kukabiliana na ongezeko la viwanda, Wizara inafanya juhudi za kuongeza idadi ya Wakaguzi wakiwemo Wakaguzi wa Serikali, Wakaguzi wa Muda na Wakaguzi wa Mikataba.

Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, kwanza, nakushukuru sana kwa mifano, maana umechangia lakini umejaribu kutueleza nchi nyingine zinavyofanya, kwanza, katika kuzalisha ajira. Vilevile umezungumzia kuhusu kufanya kaguzi katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama likiwemo Jeshi la Magereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutoa huduma za afya na usalama mahali pa kazi, ikiwemo ukaguzi katika Majeshi ya Ulinzi na Usalama, inahitaji mawasiliano maalum yafanyike kati ya Vyombo hivyo na Wziara yangu. Hiyo ni kutokana na unyeti wa Vyombo vyenyewe. Wizara yangu itafanya mawasiliano na Jeshi la Magereza, kuona namna ambavyo itafaa ili kulinda afya na usalama wa wafanyakazi walioko magerezani.

Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, amezungumzia kuhusu kutoa taarifa ya ukaguzi kwa waajiri kabla ya kwenda kwenye ukaguzi. Kwamba, tunatoa taarifa, kwa hiyo, tunawakuta wameshajiandaa, wameshatoa vitendea kazi ambavyo labda havikuwepo wanavitoa stoo wanawapa wafanyakazi. Mimi nakubaliana naye, lakini mara nyingine siyo vizuri kumvizia kwa sababu unaweza usimkute. Kwa kawaida kaguzi nyingi za afya na usalama mahali pa kazi hasa zile za kawaida, zinafanyika bila kutoa taarifa kwa mwajiri. Lengo la kutotoa taarifa ni kutaka kujua hali halisi ya mazingira ya kazi na hata hivyo, ni kweli kwamba, kuna baadhi ya kaguzi tunazifanya baada ya kutoa taarifa kwa mwajiri na hizi ni zile zinazohitaji maandalizi ili kaguzi hizo ziweze kufanyika ipasavyo. Kaguzi hizo ni kama vile kaguzi za vyombo vya mvuke, upepo wa kunyanyulia mizigo na *boiler inspection*. Kwa hiyo, sisi tunakubali inapowezekana ni vuzuri kwenda kwa vizia vizia ili tuwakute katika hali halisi

Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari amesema, *OSHA* iangalie sekta binafsi ya ujenzi, majumba ya ghorofa, hospitali binafsi na Sekta ya Madini, wachimbaji wadogo wapewe elimu na afya ya usalama. Ndiyo, Wizara kupitia Wakala wa Afya na Usalama Mahala pa Kazi hufanya hivyo na hasa kutoa mafunzo mbalimbali ikiwemo kuongeza uelewa wa masuala ya afya na usalama kwa

wafanyakazi wa Sekta ya Ujenzi, kozi ya ujenzi, namna ya kuwa salama kazini na vifaa salama kama majukwaa au hizo *scaffolds*. kozi ya kuunda Kamati za Afya na Usalama Mahala pa Kazi, kozi ya huduma ya kwanza mahala pa kazi, mafunzo maalum kwa sehemu zisizo rasmi ukijumuisha wachimbaji wadogo, ambao kwa kiwango kikubwa washiriki wakubwa wa kozi hizo wanatoka kwenye sekta binafsi na wahitimu hao hupewa vyeti vya kuhitimu mafunzo. Zaidi ya wafanyakazi 1,000 wa kada mbalimbali walipatiwa mafunzo hayo katika kipindi cha mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia kutoka kwa Mheshimiwa John Mnyika, ambaye anauliza ni maeneo mangapi yaliyokaguliwa na *OSHA* katika Jimbo la Ubungo. Amekuwa *very specific* katika mwaka uliopita na matokeo ya ukaguzi yalikuwa yapi na hatua gani zilichukuliwa. Pia ameuliza *OSHA* inatarajia kufanya kaguzi ngapi katika Jimbo lake. Yeye zaidi yuko kwenye Jimbo la Ubungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa uliopita, *OSHA* imefanikiwa kufanya kaguzi 15,916 katika Kanda zake zote sita zilizotapakaa nchini. Zaidi ya asilimia 70 ya maeneo hayo yaliyokaguliwa yanapatikana katika Kanda ya Pwani ambapo Jimbo la Mheshimiwa Mnyika lipo. Matokeo ya Kaguzi hizo ni kwamba, kwa upande wa Kanda ya Pwani, waajiri 112 walipatiwa vyeti vya kukidhi ubora wa huduma za usalama na afya, *compliance license* na waajiri 173 walipewa adhabu mbalimbali, *compounding* na Mwajiri mmoja alifungiwa na mmoja alipelekwa mahakamani. Hayo ndiyo matokeo ya kaguzi. Aidha, kwa vile kaguzi za *OSHA* hurudiwa kila mwaka, kwa mwaka ujao maeneo yote yaliyokaguliwa yatakaguliwa tena kwa maana ya *follow-up inspection* na maeneo mengine yote yatakayosajiliwa katika Jimbo hilo yatakaguliwa pia, kwa sababu kabla hujasajili huwezi kukagua.

Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Waziri Kivuli, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, amezungumzia kuhusu kuiwezesha *OSHA* iweze kutekeleza majukumu yake, kwa mfano, kuongeza idadi ya usajili sehemu ya kazi ikiwemo sekta isiyo rasmi, tunakubaliana kabisa na wewe. Tunashukuru kwa maoni hayo na Wizara itaendelea kuiongezea *OSHA* uwezo wa kutekeleza majukumu yake kadiri hali itakavyoruhusu. Mfano, Wizara inaendelea kiwezesha *OSHA* ili kupata wakaguzi wapya watakaoongeza nguvu kazi na Wizara imeongeza pia fedha za matumizi ya kawaida kutoka shilingi milioni 100 katika mwaka huu wa fedha hadi kufikia shilingi milioni 300 katika mwaka ujao wa fedha. Hali hiyo, itaiwezesha *OSHA* kuongeza usajili wa sehemu za kazi, ambapo mwaka jana ulikuwa asilimia 24 labda itafikia sasa asilimia 30 au zaidi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya Miradi ya Serikali na *NSSF,* Mheshimiwa Mahanga ameijibu vizuri. Kuhusu suala la Mheshimiwa Tundu Lissu kwamba, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii wanatumia shilingi 6662.2 bilioni kutekeleza

Miradi ya Serikali isiyokuwa na tija hadi sasa. Ningefurahi kama Mheshimiwa Tundu Lissu kidogo angekuwa *fair* kwamba kuna Miradi, siyo kuna Miradi, Miradi yote ambayo imetekelezwa na *NSSF* jamani, kwa kweli ukisema haina tija inaleta picha ambayo siyo nzuri. *Why don't you say the truth* jamani, *why don't you give credit where due?*

Miradi ambayo haina tija maana yake ni *hopeless*. Mradi mmojawapo ni huu ambao Bunge hili tulilokalia, sijui kama ni *hopeless,* hauna tija, Wabunge tumekaa kwa raha, Wajumbe wa Bunge la Katiba wamekuja tumekaa nao vizuri watu 600, kama Wabunge wataongezeka miaka ijayo watakaa nafasi ipo. Sina haja ya kutaja Miradi mingine, lakini ni ile kusema haina tija; kwa kipengele kipi haina tija? Afadhali kama kijana msomi angetusaidia tujue haina tija kwa sababu gani. Hapa tunasema Miradi hii ina tija na inasaidia utendaji kazi, inajenga uchumi na hivyo inaongeza na inakuza ajira. Sina haja ya kuitaja yote na hapa nitakuwa napoteza muda kwa sababu inafahamika.

Kamati yetu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii imesema *NSSF* iwekezwe katika maeneo ambayo yako nyuma kimaendeleo; hili limeshajibiwa. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, unajua wanapowekeza lazima wahakikishe kwamba pale ambapo wanawekeza pesa yao itarudi. Nadhani ndiyo hii mnayoizungumza kwamba, wahakikishe hawafilisiki. Sasa wakiwekeza maeneo mengine ambayo hayana tija kama inavyosemekana, maana yake pesa haitarudi. Kwa hiyo, kwa kupitia Bodi yao watahakikisha kwamba, kwanza, maeneo hayo yanaangaliwa kama yatatoa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuboresha mafao ya Wanachama. Kwa kweli zaidi ya mafao mazuri ya Kisheria yanayotolewa na *NSSF,* Shirika pia limeanzisha mafao ya ziada kwa wale waliohudhuria mkutano wa mwisho wa juzi wa wadau, wameona na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati alikuwepo; kwa hiyo, nafikiri alikuwa anatumia uzoefu huo kwamba, waongeze na akawa ametaja maeneo yake ya Mchinga. Nafikiri awasiliane na Shirika ili wakikubali basi waweze kwenda Mchinga.

Kambi ya Upinzani inasema Serikali itoe kauli kama *NSSF* haipo hatarini kufilisika. *For heaven's sake NSSF* haipo hata karibu kufilisika, kwa sababu tathmini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama ina afya nzuri, inafilisika tu kutokana na taarifa za *actuarial valuation* na si vinginevyo; si taarifa ya *CAG,* kwa sababu Taarifa ya *CAG* ni ya mwaka mmoja, *actual valuation* inachukua miaka minne, mitano, inaonesha tathmini ya Mfuko ikiwemo wachangiaji, mwelekeo na jinsi wanavyowekeza. Kwa hiyo, ndiyo inatoa tathmini kamili kuhusu Mfuko. Tathmini ya Mtaalam George Langis kutoka Canada, aliyeteuliwa na Shirika la Kazi Duniani, ambayo imekagua *NSSF* hiyo *actual valuation* inasema, *NSSF* inaweza kujiendesha kwa usalama bila matatizo yoyote kwa miaka 50 ijayo. Aidha, tathmini ya Mtaalam kutoka Afrika ya Kusini aliyeteuliwa na *SSRA* kufanya tathmini ya Mifuko yote, inaonesha *NSSF* inaweza kutekeleza majukumu yake

yote pamoja na kulipa Wanachama kwa asilimia 78 wakati kiwango cha Kimataifa huwa ni asilimia 60. Kwa hiyo, haipo karibu kabisa na kufilisika na niwahakikishie hilo. Kwa hiyo, kama mwenye dhamana ya Mfuko, naomba mjiunge na *NSSF* mahali ambapo ni salama kwa pesa yenu na kwa mafao yenu ya baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msemaji wa Kambi ya Upinzani pia nafikiri anataka kujua, anasema *NSSF* imenunua vipooza hewa kwa bei shilingi hiyo ukilinganisha na makadirio ya Wahandisi, yaani *Engineers*. Makadirio ya Mradi wa *ACs* kwa Mradi wa Arusha yalifanywa na washauri mwaka 2009, kwa bei za wakati ule ilikuwa shilingi 230.10 milioni. Ununuzi wa *ACs* ulifanyika mwaka 2012 kwa kushindanisha wazabuni kwa uwazi. Labda niseme hivi; kwa wale tuliokuwa kwenye mkutano ule, *NSSF* wamepata Cheti Bora kutoka Wakala wetu wa Manunuzi *PPRA, the best* katika nchi kwa matumizi bora na manunuzi bora. Kwa hiyo, mimi nafikiri ni vizuri tukazingatia hilo. *(Makofi)*

Uwekezaji wa *NSSF* hauwashirikishi wadau; siyo kweli. Maagizo ya uwekezaji yamefanywa na Bodi ya Wadhamini inayohusu utatu, kwa maana ya Wafanyakazi, Waajiri na Serikali na Jumuiya. Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii kupitia *SSRA* na Benki Kuu, inawapa *guidelines* za kuwekeza na hamna njia yoyote ambayo wanaweza kufanya bila kupitia kwenye maeneo hayo.

NSSF itoe mikopo kwa Wanachama binafsi ambao hawako kwenye vikundi maalum; kwa mfano, mikopo ya kujenga nyumba wakati bado wako kazini. Ni vyema Wanachama kujiunga katika vikundi rasmi ili kurahisisha utoaji na ulipaji wa mikopo. Hata hivyo, Sheria mpya ya mabadiliko ya *SSRA* inamruhusu Mwanachama kutumia hadi asilimia 50 ya akiba ya dhamana kwa ajili ya mikopo ya kujengea nyumba. Kwa hiyo, Wanachama watafaidika na Mifuko hii. Nawaomba mjiunge muwe Wanachama ili muweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi na sasa naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Hoja hiyo imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Uchukuzi, ambao ni Wenyeviti wa Bodi, Wakurugenzi na Wajumbe wa Bodi zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi wakiongozwa na Ndugu Salim Msoma.

Wapo pia Watendaji Wakuu wa Wizara, Wakuu wa Idara, Vitengo, Wakuu wa Idara Wasaidizi, Wakuu wa Vyuo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Maafisa wengine kutoka Wizarani wakiongozwa na Dokta Shaban Mwinjaka, Katibu Mkuu wa Wizara na Bi Monica Mwamunyange, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara. Karibuni Dodoma.

Yupo pia Bi Lina Mwakyembe, mke wa Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ambaye ameambatana na marafiki; karibuni sana Dodoma.

Katibu, hatua inayofuata!

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 15 – Tume ya Usuluhishi na Uamuzi

Kif. 1001-*Administration and HR Management* … … Sh.4,683,837,000

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Sina dhamira ya kuondoa shilingi kwenye kifungu hiki, nahitaji tu kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri. Nashukuru safari hii fedha za Tume hii zimeongezeka kutoka jumla ya bilioni 2.2 za mwaka jana mpaka bilioni 4.6 za mwaka huu na Tume hii ni muhimu sana kwa ajili ya usuluhishi na uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hii inashughulikia mashauri inayopelekewa, kwa maana ya mashtaka yanayofunguliwa *CMA*, lakini vilevile nayo huwa inafanya uchunguzi na inafuatilia migogoro makazini, ikisimamia Sheria ya Kazi Namba 204 na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini. Sasa ningependa kupata ufafanuzi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwenye maandiko yangu kwamba, *CMA* ifanye uchunguzi wa migogoro inayojirudia mara kwa mara kwenye Kampuni ya *STRABERG*, kwenye Mradi wa Mabasi ya Haraka, pamoja na Kiwanda cha Urafiki.

Sasa ningependa kupata *commitment* ya Waziri, iwapo katika mwaka huu wa fedha unaoanza, kwa nyongeza hii, kwa sababu kwenye posho ya vikao peke yake zimeongezeka kutoka milioni 389 mpaka 670. Ukiangalia kwenye mafungu mbalimbali, fedha za kazi zimeongezeka. Ningependa kupata *commitment* ya Waziri, iwapo *CMA* itachunguza hii migogoro ya maeneo haya mawili. Naomba ufafanuzi kutokana na nyongeza hii ya fedha iliyoongezeka.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, *CMA* ina jukumu kubwa sana la kufanya kaguzi na kutatua migogoro mbalimbali kwenye maeneo ya kazi. Nashukuru kwamba, Mheshimiwa Mnyika ameona fedha zilikuwa kidogo na sasa angalau wameongezewa mwaka huu wa fedha tunaouombea.

Sasa kutokana na fedha zilivyokuwa ndogo kabla, ni kweli kwamba, maeneo mengi hawakufika. Tuahidi tu kwamba, baada ya kuongezewa fedha na kuwa na uwezo sasa, mwaka huu ujao wa fedha *CMA* itafanya kaguzi nyingi zaidi, ikiwemo na maeneo hayo ya *STRABERG* katika Jimbo la Ubungo.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba sina nia ya kukamata shilingi kwa dada yangu, lakini ninahitaji ufafanuzi wa kina kwenye Kasma 230100, ambayo inahusu *Routine Maintenance and Repair of Roads and Bridges,* kuna milioni 14. Sasa nilikuwa najiuliza, kama hii ni Tume ya kusuluhisha migogoro, ni kwa kiasi gani tena wanajishughulisha na kukarabati barabara na madaraja? Sasa naomba ufafanuzi wa kina hizi barabara na madaraja yako wapi katika Tume hii? *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *term* ambayo imewekwa hapa na Wizara ya Fedha kwa maana ya *Maintenance and Repair of Roads and Bridges,* ni *term* ambayo ipo kwenye kila Wizara na ina mambo mengi. Pale ambapo Wizara husika haina mambo ya barabara na madaraja, lakini angalau kuna *pavements*, kuna barabara zinazopita karibu na maofisi yao, inaingia kwenye fungu hili. Kwa hiyo, fedha hizo zimewekwa kwa ajili hiyo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi nipo kwenye *vote* hiyo hiyo ya *CMA*. Mimi ni mdau, suala langu hapa, kumekuwa kuna malalamiko sana kutoka kwenye Ofisi za Mikoani kwamba, hakuna fedha zinazopelekwa za kuendeshea ofisi, hali iliyopelekea Maafisa kukata tamaa na wengi sana kuacha kazi.

Sasa nataka *commitment* ya Waziri, kwa sababu fedha imeongezeka karibu mara mbili; ni Ofisi gani za Mikoa ambazo zimepata nyongeza ya fedha kwa ajili ya uendeshwaji wa ofisi? Naomba nipate hiyo *commitment*, kwa sababu malalamiko yamekuwa mengi na watu wanaacha kazi kwa wingi na tunajua hizi ofisi zikiwa hazina ufanisi, tafsiri yake ni kwamba, watumishi ambao wanategemea kupata haki katika hizo ofisi, hali zao zitakuwa mbaya sana.

Kwa hiyo, naomba nipate tu *commitment* na nijue ni ofisi gani ambazo *at least* mafungu yao kwa mwaka huu yamekumbukwa, ukiachia kutelekezwa kwa kipindi kirefu sana.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya bajeti ya mwaka huu, Ofisi za Mikoa za Wizara ya Kazi na Ajira, zilikuwa hazina *subvotes*. Kwa mwaka huu angalau kwa Idara ya Kazi, kumekuwepo *na subvotes* ambazo zimeoneshwa kwenye bajeti kwa hizo Ofisi za Kazi za Mikoa. *(Makofi)*

Kwa upande wa *CMA*, inategemea fedha zimekuwa zikitoka tu Makao Makuu kupelekwa kwenye ofisi hizo. Kama alivyosema, katika miaka iliyopita, kwa kweli ilikuwa inapata fedha kidogo. Mwaka huu fedha zimeongezeka kwenye *CMA* na tunategemea watapeleka sasa mikoani. Kwa vyovyote tunaamini watapeleka mikoani fedha zaidi ili kuondoa matatizo hayo ambayo ameyazungumza ya wafanyakazi kuacha kazi. Lilikuwa ni tatizo kubwa, lakini kwa nyongeza hii, sasa ni ofisi gani za mikoa gani zitapelekwa, wao wenyewe wataangalia kwa sababu hakuna *subvotes* za *CMA* za Mikoa. Wataangalia tu ofisi ambazo zinahitaji fedha zaidi ili kazi ziendelee vizuri katika Ofisi hizi za Mikoa.

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi nipo *subvote* 411000, nimeona mwaka jana ilitengewa shilingi milioni kumi, sasa imetengewa shilingi *60 million*. Naomba maelezo kwa nini imeongezeka zaidi ya mara tano.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni lilelile la fedha, katika miaka iliyopita na hata mwaka jana. *CMA* hawakufanya matengenezo kwenye maeneo yao au kwenye nyumba zao kutokana na matatizo hayo ya fedha. Kwa waliopita pale wangeona kulikuwa na uvujaji wa jengo lao, lakini kwa fedha hizi sasa tunategemea matengenezo yatafanyika katika mwaka huu wa fedha ili kuweka ofisi ile katika hali nzuri zaidi, ikiwemo na Ofisi za Mikoani.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 65 – Wizara ya Kazi na Ajira

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* … … .... Sh. 3,746,297,000

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida, tuna orodha ambayo tumeshaipata kutoka kwenye Vyama; Mheshimiwa Dkt. Augustino Mrema!

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naomba nimpongeze Waziri na Naibu

wake, kwa kazi nzuri wanayofanya. Nami nataka *ku-declare* kwamba, zamani nilikuwa Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana, kwa hiyo, ilikuwa Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, swali langu ni kutaka ufafanuzi; Serikali imetangaza maeneo kama matatu ambayo watu wanahitaji huduma za bure. Watoto wadogo chini ya miaka mitano, linatekelezwa, sijui limefanikiwa kwa kiwango gani lakini ni tangazo la Serikali kwamba kila mtoto mdogo, chini ya miaka mitano ahudumiwe bure. Pili, wanawake wajawazito, wakienda hospitalini wasidaiwe nyembe, nyuzi, *gloves,* wahudumiwe na Serikali. Sasa ngoma ipo kwa tatizo la wazee, shahidi yangu atakuwa Mheshimiwa Samuel Sitta, alipofika Kiraracha, wakati namzika ndugu yangu Anselm Mrema; nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kufika pale, lakini nataka nitamke kama shahidi, uliwaona wale Wazee wa Kiraracha, Wanaume na Wanawake, ambao wanawawakilisha Watanzania wote, hali zao ni duni, hali zao ni mbaya.

Mimi ninachoogopa kama huu Mfuko wa Kuangalia Wazee, tutatumia visingizio mbalimbali, mnaona ninyi Maafisa wa Wizara ya Kazi na Ajira, mliweza kusafiri Duniani kote, eti mnafanya utafiti. Fedha mlipata za kufanya utafiti, lakini inapokuja kuwapa pensheni hao wazee, kwanza, nataka niwasemee, siyo lazima tuanze nchi nzima, tutafute maeneo ambayo wazee walichangia. Kwa mfano, Kilimanjaro, kule Jimbo la Vunjo, wakulima wazuri wa kahawa. Wakati ule wa mgogoro mkubwa wa mafuta, sisi tuliweka kahawa yetu rehani, tukaiokoa nchi ikapata mafuta na Wakulima wa Pamba kwa Mheshimiwa Cheyo.

Mimi ninashangaa mnapozungumza jambo hili kijumla jumla! Sasa wale wazee Mheshimiwa Sita uliowaona wale, wenzetu Ulaya wana utaratibu wa kuwahudumia hao wazee na sisi kule kwetu vijana wengi unakuta wako Dar es Salaam, wako Tanga, wako wapi, wale wazee kule Vunjo wametelekezwa wameachwa. Sasa kama Serikali haitaanzisha huo utaratibu wa Mfuko wa Pensheni kwa ajili ya wazee, hawa wazee watafia barabarani na wengi wao wakifikia umri wangu, utakuta wana kisukari, wana *pressure*, wana magonjwa mbalimbali. Wakienda hospitalini, hawana fedha za kulipa, ingawa mnasema wazee wahudumiwe bure. Sijui kama Serikali inaweza kunipa orodha ya Wazee wa Vunjo wanaohudumiwa bure hospitalini? Wanahangaika.

Kwa hiyo, ninachotaka kusema, kama huu Mfuko ni gharama kubwa mnaona mtatumia fedha nyingi, kwa nini tusiende hatua kwa hatua tukaanzia Vunjo, kule Kilimanjaro, tukaona hilo jaribio lifanyike pale, kama litafanikiwa tuendelee. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mrema, ahsante, umeeleweka.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimeeleweka nakushukuru. Haya jibu wewe Waziri hapo. *(Kicheko)*

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mrema, Mstaafu wa Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Vijana, kwa rai yake ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejaribu kueleza na ninaomba nirudie kwamba, kulingana na tafsiri ya Sera ya Hifadhi ya Jamii, Pensheni ya Wazee ni sehemu ya hifadhi ya jamii. Kwa maana ya huduma wanazopata, tayari katika Sera yao na Katika Sera ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wazee hawa wanapaswa kupata dirisha maalum kwa ajili ya matibabu.

Pensheni inayozungumzwa hapa Mheshimiwa Mrema, ni *universal pension,* kwa maana mzee kama mimi Mama Kabaka, kama wewe na wengine wazee wa umri wangu, tuendelee kupata pensheni pamoja na wale wazee ambao wako majumbani, wote tupewe pensheni kwa maana ya *cash transfer, cash* mfukoni, kila mwezi bila kukosa kama wanavyopata watumishi wengine walioajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosema ni hivi; hiyo pensheni tunaweza kuamua tukasema tutenge mwaka huu kwenye bajeti, tukatoa mwaka mmoja. Bahati nzuri kama ilikiwa ya mwaka mmoja na mimi mzee nikapata, lakini Mkosamali atakapokuwa amefikia uzee, hiyo pensheni atakuwa anaisikia kama historia kwa sababu tutakuwa hatujaifanyia maandalizi ya kuhakikisha kwamba hiyo pensheni ni endelevu.

Kwa hiyo, tunachofanya sasa hivi Serikali, ni kuhakikisha kwamba, pensheni tunayotaka sasa tuwape wazee wetu tunaowapenda, tunaowathamini, tuna deni nao kwa kuitumikia nchi hii katika eneo lolote lile hata kama hawakuwa kwenye ajira, tunataka tuifanye kisayansi, kiuhakika, kwa utulivu na kwa kufuata taratibu. Kama walivyosema Kamati ya Maendeleo ya Jamii, tuendelee na mchakato huo na mchakato huo tunaendelea nao. Tuliwahi kupeleka Waraka kwenye Baraza la Mawaziri, ukarudishwa, kwa sababu ilionekana siyo endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwamba, hakuna anayesema pensheni ya wazee haitakaa itolewe na wala haifai na wala msituchonganishe kwa wazee, maana mimi ni mzee mwenzao. Tunachosema ni hivi, nikianza kupata mimi na wajukuu zangu wakija waikute

hiyo pensheni ikiwa inaendele; na hii ndiyo ilikuwa maana ya kuwapeleka Waheshimiwa Wabunge kwenda kujifunza nchi zilizoendelea wamefanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, China, wamechukua miaka tisa, kabla hawajatoa Pensheni ya Wazee. Kabla hawajatoa hiyo pensheni, walihakikisha wazee wale wamechangiwa; Serikali imewachangia na wao wamechangiwa, kwa namna ya kipato chochote walichokuwa nacho. Sisi tunataka kutoa pensheni, hakuna hata mchango mmoja, lakini tumesema tutatoa, iwapo tutakuwa tumeiandaa kwa hali ambayo tuna uhakika kwamba, kila mwezi pensheni hiyo itatolewa bila kukosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni afadhali usianze, kuliko ukaanza halafu ukaisimamisha baada ya mwaka mmoja au miwili, itakuwa *chaos,* itakuwa ni siasa na watakaokuwa wanatuhangaisha ni wale ambao wanatulazimisha kutoa bila kwanza kukaa chini na kufikiria hiyo pensheni itolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bukwimba!

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nimwulize Mheshimiwa Waziri. Mimi ninahitaji tu ufafanuzi.

Katika mchango wangu kwa kuzungumza nilijaribu kuelezea jinsi ambavyo ajira kwa vijana ni kitu muhimu sana, hasa hasa vijana ambao wamejiajiri katika shughuli za uchimbaji wa madini. Katika mchango wangu nilijaribu kuelezea kwamba vijana hawa wanahitaji kusaidiwa na Serikali hasa katika upande wa mitaji, na Wizara hii ya ajira ni Wizara muhimu ambayo ni kiungo kikubwa kwa Wizara zingine muhimu kuwawezesha vijana hawa kujiajiri katika shughuli mbalimbali za uchimbaji wa madini na shughuli nyingine.

Kwa hiyo sasa ningependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, sasa ni namna gani Serikali hasa Wizara hii ina mkakati kwa ajiri ya vijana hawa katika ajira ndogondogo hasa za kwa wachimbaji wadogo wadogo wa madini. Ahsante.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaongelea mkakati wa ajira kwa vijana, siyo mahsusi kwa ajili ya wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu hao nafikiri Wizara husika ya Nishati na Madini itakapokuja itatoa mikakati ya wachimbaji wadogo wadogo.

Mkakati niliozungumza pale wakati najibu ndiyo huo kwamba tunajaribu kuanza programu ambayo itatusaidia, itatupa kama *eye opener* kuona jinsi tunavyoweza kuwasaidia vijana, kwanza kwa kuwapa taaluma ya ujasiriamali ambayo tuna hakika hawana. Hata kama amesoma kilimo, hana taaluma ya ujasiriamali, yeye amesoma tu taaluma inayohusu *animal husbandry* na mambo kama hayo. Kwa hiyo, tumpe taaluma ya kutunza vitabu vya mahesabu, taaluma ya kuangalia masoko na mambo mengine kama hayo kwa kutumia wataalam. Pia tumsaidie kumpa mtaji mdogo kwa kuona kwamba ana uwezo baada ya kutuandikia ka-*concept paper* kake tuone kwamba anajua anachotaka kufanya. Pia tusaidie kumpatia eneo la kufanyia kazi zake.

Kwa hiyo huo ndiyo mkakati tulionao na nafikiri ni mkakati mkubwa, tunachoomba mtupitishie hii pesa kidogo angalau itusaidie kuona kama tunaweza angalau kuanza. Vile vile niwaomba, Waheshimiwa ninyi ni wadau, tumesema sera yetu ya ajira inashirikisha wadau, siyo Serikali peke yake, kwenye majimbo yetu sisi ni wadau, NGOs tulizonazo ni wadau, kwa hiyo tusaidiane katika hili la kutatua ajira ya vijana.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilizungumzia suala zima la haki za wafanyakazi hasa vijana wenzangu walioko katika sekta ya madini, sekta ya viwanda vya kutengeneza dawa katika mashamba mbalimbali ambapo watu hawa wanatumia *chemicals* na *especially* hata mimi nina mfano mzuri, kule kwangu Kisarawe katika lile zao la jatropha, baadhi ya vijana walikuwa wameathirika sana na dawa.

Vile vile nilipotembelea katika sekta ya madini nimekuta baadhi ya vijana ambao wameathirika, lakini mara baada ya kuathirika watu hao wanaachishwa kazi, watu hao wanakuwa hawana ulinzi. Kwa hiyo maana yake tunapoteza nguvu kazi kubwa sana ya taifa letu. Lakini kubwa zaidi, sijaona mkakati wa Wizara unafanyaje kulinusuru taifa hili la vijana katika sekta mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza hapa kuna watu hivi sasa wako hospitalini wanakosa huduma, familia zao zimekosa mwelekeo kabisa. Sasa nataka majibu kutoka Serikalini, jinsi gani imefanya na itafanya kuhakikisha kwamba inawanusuru vijana hawa na nisipopata majibu sawasawa, kwa kweil nakusudia kutoa shilingi. *(Makofi)*

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Jafo kama ifuatavyo:- Nimeeleza, Wakala wetu wa Afya na Usalama Mahali pa kazi (OSHA) hiyo ndiyo kazi yao, kukagua na kuangalia kwamba mazingira ya kazi yana usalama na hayaharibu afya ya wale wanaofanya kazi. Sasa mpaka waende pale, kwa sababu siyo rahisi wakakaa, wakalala, wakaamka wakaota kwamba eneo fulani kuna ukiukwaji wa

masuala ya afya na usalama mahali pa kazi. Lakini wanapokagua na kukuta kwamba kuna ukiukwaji huu, wanachukua hatua na nimesoma hapa hatua zilizochukuliwa, ikiwemo kuwatoza faini, lakini na wengine wanawaambia wanafunga maeneo ya kazi. Kwa hiyo mimi nizungumze tu kwa ujumla kwamba wanapokuwa wanaenda kukagua hivi ndivyo vitu wanavyoviangalia na kuwashauri, ikiwemo migodini, kuwashauri waajiri kwamba hapa mnapaswa kutumia vifaa kadhaa, mnapaswa kuwanunulia wafanyakazi wenu vifaa kadhaa, na wanajua.

Nafikiri mnapokuwa mnazunguka mnatembelea, mkipata hii taarifa kwamba mahali fulani kuna ukiukwaji wa vifaa vya mazingira ya afya. Kwa nini msiniambie hata mimi na mimi nikampa taarifa Mkurugenzi wa OSHA, wataenda mara moja. Maeneo ambayo tumepata taarifa, wakaguzi wameenda na wame-*establish* na wamechukua hatua.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli sijaridhika, kwa sababu hata katika majibu ya Mheshimiwa Waziri inaonekana kwamba…

MWENYEKITI: *No*, sema kabisa unatoa shilingi.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti mimi natoa shilingi.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika kwa sababu majibu yanayotolewa na Mheshimiwa Waziri wakati huku kuna taifa la vijana linateketea. Mnakumbuka mwaka juzi hapa nilikuwa nauliza maswali moja kwa moja kwa Waziri Mkuu jinsi vijana wa Kisarawe walivyokuwa wakiathirika katika lile zao la jatropha, ambalo nimesema mpaka kuna vijana wengine walipoteza u-rijali wao kwa ajili ya kutumia *chemicals*, na watu hawa nikizungumza hiyo ni sehemu moja. Lakini sasa hivi ukiangalia katika sekta ya madini, kuna watu ambao hali zao ziko tete na wengine wako hospitalini, lakini hata jinsi gani vijana hawa wanahudumiwa kupewa hata lile fungu lao la kuwahudumia na familia yao, kwa kweli hali imekuwa ni mbaya, watu hawa wanaachwa kabisa wanapotea mtaani, na ina maana tunapoteza taifa kubwa sana ambao hawa ndiyo wanaokwenda kuchangia hii mifuko ya hifadhi ya jamii, ambapo ukiangalia kuna mifuko mingine ya hifadhi ya jamii inaathirika kwa sababu wale wafanyakazi wenyewe ambao wanatakiwa wachangie wengi wanaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hoja hii ijadiliwe na Wabunge ilimradi ionekane kwamba ni jinsi gani jambo hili lina *interest* ya taifa hili. Ahsante. Naomba Wabunge wenzangu waniunge mkono katika hili.

MHE: CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naungana na Mheshimiwa Jafo juu ya madhara yanayowapata watendakazi katika maeneo ya kazi kutokana na kutopata stahiki za kulinda usalama wao. Suala la afya, suala la mazingira ya kazi.

Katika mchango wangu huo naona upungufu katika hiyo taasisi ya OSHA, kwamba OSHA suala lenu siyo kumpiga mtu faini, haina maslahi kwetu. Ningependa kusikika kutoka kwa Serikali kwamba hiyo mamlaka ya OSHA ni majukumu gani zaidi inapewa ya kuwashawishi watu, ya kuhamasisha watu kwamba mlete ripoti kwetu kama mnaonewa. Yaani kisionekane ni chombo cha kutoza faini. Kinaweza kuwa ni chombo cha kutoza faini, yule anayetozwa faini akakiona akakiweka sawa.

Sasa tungependa tuelezwe kwamba itangazwe hata kwenye magazeti, hata kwenye *television* pale inapokuwa mtu kaonewa aje OSHA na ahakikishiwe kwamba utapewa fidia hizi na hizi, si kwamba wanatoza faini. Kutoza faini, kuna mtu anaweza akatumia nguvu kazi ikafa na akalipa faini ya shilingi 2,000. Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ndiyo huo.

MHE ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia sikuridhika kabisa na ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri, na ninaunga mkono moja kwa moja hoja ya Mheshimiwa Jafo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama mahali pa kazi ni jambo muhimu sana na hususan migodini na kwenye viwanda mbalimbali vya hapa nchini. Mimi nikiwa kwenye Kamati ya POAC wakati ule, Wabunge tuliwahi kwenda kwenye kiwanda cha ngozi pale Morogoro na Mheshimiwa Esther Bulaya alikuwepo, tuliwakuta hususan akina mama ndiyo waliokuwa wengi, wanapekua hawana hata buti, hawana hata *gloves*; na tukamwambia yule mwenye kiwanda kwa nini anafanya mambo kama haya!

Mheshimiwa Mwenyekiki, kama alivyosema Mheshimiwa Mwijage, hawa OSHA hawa wamekuwa ni watu wa kushauri, wa kumshauri kwamba tumekukuta ukiwa na upungufu huu, uufanyie kazi. Tunataka watu hawa wakikutwa wamefanya makosa, wakikutwa wafanyakazi hawana vifaa vya usalama wachukuliwe hatua za kufikishwa mahakamani. Sheria ile inaruhusu kabisa wafikishwe mahakamani na waadhibiwe. Kwa sababu watu wa migodini wana pesa nyingi, kwa hiyo kama ni masuala ya faini wana uwezo wa kulipa faini na kuendelea kukaidi sheria za nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunataka utupe maelezo ya kina ni makampuni mangapi ambao wamefikishwa mahakamani, ni matajiri wangapi wamefikishwa mahakamani na hatua zilizochukuliwa. Haya mambo ya sijui OSHA…

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kwenye migodi, Waziri amesema hapa kwamba wanafanya ukaguzi wa kushitukiza. Sasa katika mazingira ya kushitukiza, ukienda kwenye migodi ambako kuna ulinzi mkali, kuna udhibiti wa kuingia mgodini. Kuna wakati hata Mheshimiwa Ngeleja kule Geita alipata taabu ya kuingia mgodini. Kwa hiyo, ni wakati gani sasa wanawakagua wakati hawaruhusiwi kuingia migodini? Huu ni uongo. Tunataka maelezo ya kina. *(Makofi)*

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jafo kwa sababu inahusu jimbo langu la vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyoongea kuna vijana ambao hawana mikono, hivi tunavyoongea kuna vijana ambao wamepoteza maisha, hivi tinavyoongea kuna vijana ambao wamepoteza viungo vyao mbalimbali kutokana na kukosa usalama mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, mama yangu namuheshimu sana, lakini kwa majibu ambayo ametupa hajawatendea haki vijana wa taifa hili. Unapozungumzia OSHA, wanapotoa taarifa wanakwenda kukagua wanapewa vifaa watu wachache kwa ajili ya kudanganya tu, kwa ajili tu ya kupaka mafuta kwenye mgongo sijui wa nini ili watu wakienda kukaguliwa waonekane kiwanda kina vifaa kumbe hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemuomba pia Mheshimiwa Waziri, mbali ya kutegemea OSHA na yeye awe na utaratibu wa kufanya ziara kwa kushitukiza, kama ambavyo alikuwa akifanya Baba wa Taifa na viongozi wengine ndipo utaona hali halisi. Lakini, hivi tunavyoongea na mikakati mliyonayo, bado vijana wa taifa hili wataendelea kupata matatizo mahala pa kazi. Tunaomba muwe mna mikakati ya kuturidhisha sisi Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi wanaopata taabu, hasa vijana wa taifa hili ambao wanategemea kujenga taifa lao, wanakosa viungo watajenga na nini!

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naungana na Mheshimiwa Jafo kwa sababu kule Tabora kuna vijana walikuwa wanafanya kazi kwenye *quarry plant* za wachina, wamekatika mikono, wengine wamevunjika miguu, lakini fidia zao wanazopata ni za ajabu kabisa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tafadhali, tupate maelezo ya kina. Na hata wiki ya jana nimepita kukagua barabara za Tabora, nimekuta vijana bado wanapasua

mawe, hawana viatu vya maana, hawana *gloves*, hawana *masks* kwenye uso wao, ni hatari sana na wengi wameishaanza kuugua kifua kikuu. Kwa hiyo, kwa kweli tulikuwa tunaomba Mhesimiwa Waziri atupe majibu ya kuridhisha.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Wiki moja nilipokuwa Mwanza, kuna kundi la watu walikuja kwangu walikuwa na kesi na OSHA. Wakasema kwamba walikuwa wanafanya kazi migodini wakafukuzwa, lakini wakati wanafukuzwa hawakupimwa afya. Sasa kesi ikaenda OSHA. Kesi ilipoenda OSHA, yule mwajiri akaja akakiri kwamba kweli kipindi hawa watu hawa wanaachishwa kazi hawakupimwa. Sasa baada ya hapo wale watu wakataka sasa wapewe barua, yaani OSHA itoe barua inayothibitisha kwamba mwajiri alikiri kwamba wale watu kweli hawakupimwa kipindi wanaachishwa kazi kule mgodini. Barua hiyo imechukua muda mrefu sana, na kila wakienda OSHA wanapigwa chenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninachohisi ni kwamba mtu akishafanya kazi sehemu moja muda mrefu anaanza kufanya kazi kwa mazoea, anazoea wadau ambao anatakiwa awasimamie kwa namna kwamba inawezakana kuna vitu anapewa.

Kwa hiyo mimi naungana na Mheshimiwa Jafo kwamba Waziri atoe tamko, na ikiwezekana wanaoshughulikia OSHA leo, na Mkuu huyo wa OSHA abadilishwe kwa sababu ameanza kufanya kazi kwa mazoea na hatimaye hatendei wananchi wetu haki.

MWENYEKITI: Nakushukuru. Mheshimiwa Waziri Majibu!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba niseme hivi, kwa *specific* suala la Mheshimiwa Jafo, mimi nafikiri kama angekuwa ametuletea taarifa hiyo, tungeishatuma wakaguzi. Lakini nilichosema hapa ni kwamba, wakaguzi hawa wa OSHA wanaenda, wanakagua, wakikuta kuna matatizo si kwamba wanatoza faini tu, wanapeleka mahakamani, na hapa nimesoma taarifa ya mahakamani ya maeneo ambayo yalikaguliwa na Mahakama watu walikopelekwa.

Sasa hivi siwezi kutoa idadi kamili ya watu waliokwenda mahakamani kwa sababu lazima niwe nimeletewa takwimu hizo, siwezi kuzitoa kichwani, lakini wanapelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili; Suala la fidia kwa wale wanaoumia nimesoma hapa. Mwaka huu tunaanzisha Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi wote wa Serikali, sekta ya umma na sekta binafsi. Mfuko huu utachangiwa na sekta hiyo ya umma, sekta binafsi, Serikali za Mitaa, Serikali kuu na makampuni ya watu bianfsi. Kanuni zimeshatoka nimeishazisaini.

Kwa hiyo mfuko utakapoanza, fidia ya hawa watakaokuwa wanaumia haitegemei tena mwajiri mwenyewe kwa sababu mwajiri atakuwa ameshachangia, na ndiyo maana tumeanzisha mfuko huu. Sheria hii imeanza toka 2008, lakini tulikuwa tunashindwa kupata hela, sasa hivi tumepata hela ya kuanzisha mfuko huo, kwa hiyo suala la fidia halipo tena kwa maeneo ya waajiri.

Suala hili la wafanyakazi walioachishwa kazi 2007 ni suala ambalo mimi mwenyewe nimelishughulikia ofisini, ni suala ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelishughulikia tukiwa na Mheshimiwa Maige, lakini ni suala ambalo OSHA wamelishughulikia kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nina taarifa. Tarehe 30/10/2013 OSHA iliwaandikia barua Bulyankhulu kuonesha kusudio la kutaka kuwashitaki kwa kufukuza wafanyakazi bila kupima afya zao, lakini ilipofika tarehe 5 Juni, OSHA ilimtuma afisa kwenda Shinyanga kufungua mashitaka hayo, ni Shinyanga hiyo, kwenda kufungua mashitaka hayo. Inawezekana wengine ndiyo hao wanakuja Mwanza, lakini ilipeleka mtu Shinyanga akafungue mashitaka. Na kama ulivyosema, Mgodi wa Bulyankhulu uliandika barua OSHA kwamba hilo suala walifanye nje ya Mahakama.

Kwa hiyo, waliandika barua tarehe 27/06/2013, barua ya kuomba kikao kati ya OSHA, mwajiri pamoja na mwakilishi wa hao wafanyakazi ambaye ni chama cha wafanyakazi TAMICO. Tarehe 10 Julai, OSHA ilikubali ombi, na ilipofika tarehe 15 Julai, kikao kilifanyika kati ya mwajiri ambaye ni mgodi, chama cha wafanyakazi pamoja na OSHA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo walikubaliana kwamba sasa OSHA itawaandikia barua mwajiri ili aweze kuleta sasa majina ya hao walioumia ili waweze kupimwa, kwa sababu bila kupimwa utajuaje kwamba huyu amepata ugonjwa kutokana na kazi?

Kinachogomba mpaka sasa ni kwamba majina ya wale wanaotaka kupimwa hayajafika kwenye ofisi ya OSHA, utampima nani? Na ndiyo maana hawajapimwa; lakini la barua, juzi nimepata *message*, *in fact* nashangaa kwa nini nimeifuta, ya kijana mmoja ambaye alikuwa anafuatilia, anaitwa Makene, akaniambia OSHA wameshawapa barua. Kwa hiyo barua unayosema Mheshimiwa Mbunge wameshaipata, tunachosubiri ni majina ya wale walioathirika wakapimwe. Kwa hiyo hilo ndilo suala la hawa waliofukuzwa.

Lakini hili la Mheshimiwa Jafo nasema hivi, Mheshimiwa Jafo rudisha Shilingi yangu. Mimi nisaidie kunipa majina ya eneo hilo, hicho kituo *immediately* baada ya bajeti hii na mimi ninatuma wakaguzi wa OSHA waende huko

wakapime na watakuletea nakala ya taarifa na kilichotokea. Ukitaka ongozana nao, na mara nyingi huwa wanaongozana na wawakilishi wao wa vyama vya wafanyakazi.

Kwa hiyo, hilo si tataizo, ni kwamba tu hatuna *movement* ya kutosha OSHA siyo wengi kiasi hicho hasa kutoka makao makuu ambako ndiko kuna madaktari. Kwa hiyo Mheshimiwa Jafo, Chonde chonde nirudishie hiyo shilingi na uniletee majina na maeneo niwatume OSHA *immediately* wakapime.

MWENYEKITI: Na wanasema kutia mkazo, barua hizo uzibebe mwenyewe uende nazo, siyo OSHA. Mheshimiwa Jafo!

MHE. SELEMANI SAIDI JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri kuonesha kwamba kuna tatizo lipo ndani ya nchi, hilo ni jambo la msingi. Jambo lingine ni kwamba ninaomba Wizara yako isitegemee sana kuwabeba waajiri, tuangalie jinsi gani wafanyakazi wa Tanzania watalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mama namuamini na timu yake, naomba sana lisimamie jambo hili, narudisha shilingi yako bila mashaka. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Moses Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kimsingi nasimama hapa kuulizia kuhusiana na suala la fao la kujitoa *(withdrawal benefits)*. Mwaka jana wakati Muswada wa *GEPF* umeletwa hapa katika Bunge hili Waziri wa Kazi na ajira Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, alieleza kwamba wataenda kulifanyia kazi suala hili. Lakini, katika hotuba yake sijasikia mahali popote pale ambapo ameweza kuzungumzia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipate kauli ya Serikali, na kama nitakuwa sikuridhika nakusudia kutoa shilingi. Kwa sababu haiwezekani mtu anfanyakazi, *let us say* labda ni miaka mitatu au ni miaka mitano, anataka aweze kurejeshewa michango yake ambayo alichangia katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, azuiwe, ili hali sheria ya pensheni inamtaka mtumishi au mtu ili aweze kuwa *pensionable* baadaye awe amefanya kazi kwa takriban miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali linakuja, huyu mtu aliyefanya kazi kwa miaka mitatu au miaka mitano, kesho unasema kuwa atakuja kuwa *pensionable,* utampa pensheni kwa kutumia utaratibu upi wakati haja-*contribute* kwa miaka 15?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakasema kwamba wamefanya utafiti kwenye nchi nyingine, hakuna fao hili. Upo ushahidi kuna nchi kama za Uingereza, wana fao la kujitoa. Nilikuwa naomba nipate kauli ya Serikali, suala hili limefikia wapi kuhusiana na suala zima la watu ambao wanafanyakazi kwa muda mfupi, na pengine baadaye hawana mpango wa kuweza kuchangia. Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na suala hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa shilingi.

MWENYEKITI: Ahsante. Umeeleweka Mheshimiwa Machali. Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sijamuelewa, amesema katika nchi nyingine hakuna fao la kujitoa, lakini hapa ni kama ametetea fao la kujitoa liwepo. Kwa hiyo sijaelewa anachotaka hasa ni nini?

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba katika nchi nyingine wana fao la kujitoa. Hapa Tanzania, hamtaki fao la kujitoa kwa misingi gani? Naomba ufafanuzi, na urejee kauli ambayo uliitoa wakati ule kusema kwamba mtalifanyia kazi, kwa hiyo tuliweke *pending,* hiyo *issue* ilibaki *pending*, naomba tuendeleze pale tulipoishia.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mashahidi ni wale tuliozunguuka nao katika zile nchi, hakuna fao la kujitoa, halipo! Hawaruhusu wafanyakazi kujitoa katika mafao. *In fact* hakuna kitu kinachoitwa fao la kujitoa. Maana yake ni kujitoa katika mafao ya muda mfupi, ikiwemo matibabu, ikiwemo masuala ya uzazi, ikiwemo na mambo mengine, ndiyo maana ya kujitoa. Una-*withdraw from the benefits*. Kwa hiyo hilo siyo fao. Hapa limeitwa tu fao, kama tu ni jina la kulielezea kwamba watu wanajitoa, lakini siyo fao. Shirika la Kazi Duniani, halina fao hilo na mafao yetu yanaenda kwenye *standard* hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nieleze, kujitoa au *withdrawal* imekuwepo kutokana na matatizo mbalimbali hasa kwa vijana wetu ambao wamekuwa wakijiajiri, wanaingia kwenye Mifuko wa Hifadhi ya Jamii au wakiajiriwa na mashirika haya ya madini na kampuni za madini au maeneo mengine ajira ambazo siyo za muda mrefu. Baada ya muda wanatoka kwa sababu moja au nyingine. Sasa anaona alichochangia pale akachukue kimsaidie wakati huo anatafuta ajira. *NSSF* wamekuwa wakiwaamba, uje baada ya miezi sita ili kuwaruhusu angalau ndani ya miezi ile sita waweze kutafuta ajira mahali pengine. Kwa sababu unamhurumia huyu mtu atakapokuwa ame-*withdraw*, maana yake kama nilivyosema amejitoa kwenye mafao mengine haya madogo madogo, maana hata matibabu sasa itabidi aende hospitali alipe hela. Akiwa kwenye Mfuko wa Hifadhi, miezi mitatu

analipiwa na mfuko yeye na watoto wake wanne. Kwa hiyo ni nikutu ambacho mifuko imekuwa ikiki-*discourage*, na Serikali tumekuwa tuki-*discourage*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya lile zogo lililotolea katika mgodi ambalo Mheshimiwa Jafo alikwenda, tulichofanya, tumeona na tuliomba hapa wakati ule tunatoa hoja yetu, tunakubaliana na Azimio la Bunge, ni kwamba tulifanyie hili suala *a thorough work,* ili kusudi tunapokuja tunasema *okay,* tunaelewa kuna vijana kama wale wa migodini ambao wana majhitaji ya kupata hizo fedha ili waweze kujikimu wakati wanahangaika kutafuta ajira. Sasa tufanyeje!

Kwa hiyo tunaanda *something, in fact* sasa hivi Muswada uko mbali, kwa sababu Miswada hii haiendi haraka haraka ni mingi ndiyo maana hatujaweza kuileta hapa, suala ambalo tayari tumeishalipeleka mbali. Kwa sababu tunataka tuone sasa badala yake tufanye nini! Lazima utoe njia mbadala sasa, anapo-*withdraw* ataishishije. Na sisi tunataka asi-*withdraw, some how* aendelee kuwa katika mfuko hata kama ni ile pesa yake aliyochangia basi achukue angalau asilimia kidogo kama wanavyofanya China nafikiri, wanachukua asilimia hata mbili ili aendelee kujikimu wakati anatafuta ajira. Nia ni kutotengeneza tena Wazee ambao watakuja kuiomba Serikai *pension*.

MWENYEKITI: Mheshimwia Machali!

MHE. MOSE J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyeiti, natoa shilingi.

MWENEKIKTI: Endelea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Mheshimiwa Waziri, iwapo nitakukeletea ushahidi wa kukuthibitishia kwamba katika nchi nyingine wana kitu kinaitwa *withdrawal benefits,* utakuwa tayari kuweza kuwajibika kwa sababu unazungumza uongo mahali hapa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, aa acha hiyo mikwara sasa. Wewe zingatia tu mambo yako.

MHE. MOSES J.MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naliondoa neno hilo. Labda ni nitumie neno moja kwa kutokuzungumza ukweli.

MWENYEKITI: *No, no, no*. Wewe hujampa huyu *document* yoyote. Sasa hebu…

MHE. MOSES J. MACHALI: *Okay* nashukuru.

MWENYEKITI: Wewe andelea kuchangia tu, ulishatoa shilingi, fursa sasa ni yako.

MHE. MOSES J. MACHALI: *Okay,* ninashukuru. Mheshimiwa Malima, usikasirike sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema ni kwamba. Nimetoa mifano nikasema *let us say* mtu anafanya kazi miaka mitatu, halafu ajira yake inakwisha ama kwa kuugua au vyovyote vile ambavyo inawezekana. Huyo mtu pengine ana chochote anahitaji pesa yake anasema kwamba mimi nakwenda zangu kufanya shughuli zangu binafsi. Inaweza kuwa ni biashara, ha-*contribute* mahali pengine, na sheria imesema kwamba ili mtu aweze kuwa *pensionable* anapaswa kuchangia kwa miaka 15, hakuchangia, itakuwaje hiyo baadaye? Itakuwaje baadaye huyu mtu wanasema kwamba uzeeni watamsaidia kwenye uzee wake, watamsaidiaje?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, omba wengine wakusaidie, muda wakao umeishapita. Tunakwenda kwa muda, sasa waombe wenzio wakuunge mkono.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja, na ninaendelea kutoa shilingi.

MHE. EZEIAH D. WENJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuunga mkono Mheshimwia Moses Machali, kwa sababu *mentality* ya Serikali ni *mentality* ya ku-*create work force forever*. Yaani hii ni *mentality* ya ku-*create* wafanyakazi mpaka mtu unazeeka yaani *forever*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko hivi; Kuna mtu anajiriwa leo akiwa labda ana miaka 28, lakini anakuwa na malengo ya kufanya kazi mpaka miaka 30 au miaka 35 anaacha. Siyo kwamba kila mtu anataka afanye kazi mpaka, kama kuna Wabugne Wazee humu ndani mpaka wanataka kufia ubunge. Hii siyo *mentality* ya kila mtu duniani. Kuna watu, mtu amezaliwa, lakini anayo malengo yake kwenye maisha, anataka aajiriwe afanye kazi miaka 30, anapofikisha miaka 35 anastaafu *formal empoyoment* anakuwa labda ana kazi yake.

Sasa mtu kwa mfano ameajiriwa mgodini, amefanya kazi, amefikisha labda miaka 35. Anana kwamba *savings* alizo-*save* akitoa inao uwezo wa kumsaidia akaanzisha *employment* ili aajiri na watu wengine. Kwa nini mtu kama huyu asiruhusiwe kuchukua?

Kwa hiyo hii *mentality* ya Serikali ni *mentality* ya *create work force forever,* ambayo haina tija. Tunajhitaji tusaidie watu, wao waweze kujiajiri na wajiri watu wengine, na namna pekee ni wanapowezeshwa kutoa pesa kama hizi.

Mheshimiwa Mwenyeiti, nimuunga mkono Mheshimiwa Machali.

MHE. GOOLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa darasa zuri alilotupata sasa hivi juu ya fao la kujitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimwa Mrema aliulizia juu ya Wazee, wakulima wa kahawa ambao walichangia pato la taifa kupitia kilimo katika miaka ya nyuma na ambao leo hii hawana pensheni, na ambao tumekuwa tukipambana hapa, kwamba wazee wale walipwe penshieni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoona mimi Serikali inafanya ni kama mzazi anayemchujua mwanaye mgonjwa anampeleka hospitali hata kama hataki kwa sababu anajua faida za kutibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hifadhi ya jamii, halikomi kwa sababu umeacha kazi, utakapofika umri ambao huwezi kujitegemea huwezi tena kufanya kazi. Unahitaji kutunzwa na jamii na ndipo wakati ambapo utahitaji hiyo hifadhi ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukweli ni kwamba Waheshimiwa Wabunge tujitahidi kuwapenda wapiga kura wetu. Tusiwadanganye kwa kuwaambia ya kwamba tunakuunga mkono unapotaka kujitoa. Tuwashauri na kuwaelimisha umuhimu wa kujiwekea akiba leo, kwa ajili ya maisha yetu hapo uzeeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi mkono hoja hiyo. *(Makofi)*

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi kweli siiungi mkono hoja. Pengine tuchukue mifano tu ya humu ndani kwenye nchi yetu. Mimi nilipokuwa Mbunge au kipindi kile cha nyuma, nilitoa wazo kwamba pensheni Wazee wale waliokuwa wanateseka warejeshewe pensheni. Utaratibu uliokuwepo zamani ni kwamba unapostaafu, unaamua, uchukue pensheni yako kwa fungu zima au ulipwe kidogo kidogo. Hali ilipokuja kubadilika, wazee wale walijikuta kwenye hali mbaya sana. Tukaiomba Serikali irejeshe, na ikakubali Serikali yetu kurejesha mzigo wa kulipa pensheni nyingine.

Kwa hiyo huu ni uzoefu mzuri ambao tumejifunza kwa kuamua kuchukua chote mapema halafu ufike mahala baadaye uwe mzigo kwa Serikali. Mimi nafikiri Serikali inawajibika kwa watu wake ni kama mzazi. *(Makofi)*

Kwa kweli tusiunge mkono wala ndugu zangu tusiseme tu kwa sababu ya kutaka kuonekana. Tuseme mambo ambayo yana kina kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge ambao hawamo katika orodha ya wachangiaji hoja hii walisimama kuomba kuchangia)

MWENYEKITI: Waheshimwia subirini. Inapotoka hoja kutoa shilingi, anapoungwa mkono mtoa hoja ni kipindi kile kile tunapoandika majina. Watu hawasimami tu *at random,* watu hawashabikii tu wakiona sasa m*otion* imekwenda mnaanza kusimama. *No!* Nina majina hapa ya Mheshimwia Shekifu, Mheshimiwa Ezekiah Wenje, Mheshimiwa Msafiri, Mheshimiwa Ole-Medeye na Mheshimiwa Dkt. Kigwangala.

Mheshimiwa samahani sikukuona kweli, *with due respect.* Alisimama huyu, sikukuona. Subiri. Mheshimiwa Kigwangala!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wazo la kuwa na fao la kujitoa lilipoanzishwa lilikuwa na msingi wake na hata siku moja halikuwahi kuwa wazo la hovyo.

Na kwa maana hiyo kwa bahati mbaya sana, hata kama tutadhani kama sisi uwepo wa fao la kujitoa unakuwa haupo katika *profession* zetu za hifadhi ya jamii, lakini wale wananchi wenyewe ambao wanawekeza katika hii mifuko wanaona kwamba fao la kujitoa lina maana kwao.

Kwa maana hiyo sisi humu ndani tukikaa kabisa tukasema tunaweza tukali-*scrape off* fao la kujitoka, maana yake ni kwamba tunakwenda kinyume na matakwa ya wao wenyewe wanaotaka kuwekeza katika hifadhi za jamii. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo mimi siungi mkono kuwa na fao la kujitoa 100%, lakini ninaunga mkono wazo tofauti kwamba Serikali itengeneze utaratibu wa kuigawa ile hifadhi ya jamii katika sehemu mbalimbali. Kidogo iruhusiwe kuingia katika fao la kujitoa, lakini nyingi zaidi iende kwenye uwekezaji, iende kwenye bima za afya na kwenye mambo mengine yanahohusiana na hayo. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo siungi mkono *a hundred percent* hoja ya Mheshimiwa Machali, lakini ningependa pengine Serikali i-*modify* hoja ile ya Mheshimiwa Machali na kwamba fao la kujitoa lisitolewe kwa 100%. Huo ndiyo mchango wangu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msafiri!

Mheshimiwa Lissu, ulisimama baada ya Mheshimiwa Ole- Medeye. Sisi tuna *camera* hapa, tunaona vizuri, ulisimama baada ya yeye kusimama, kwa hiyo hapana. W*ith due respect,* hukusima, kaeni. Mmepigwa bao safari hii. Mheshimiwa Msafiri. *(Kicheko)*

MHE. SARA MSAFIRI ALLY: Mheshimwia Mwenyekiti, asante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Machali kwa sababu hoja hii inataka kuwarudisha nyuma vijana. Msingi wa fao lolote, hasa akiba ya uzeeni, ni kwamba mtu afaye kazi, inapofikia umri kwamba hana uwezo tena wa kushiriki kwenye shughuli za kiuchuki, ndipo aweze kuwezeshwa sasa kwenye miaka ile michache iliyobaka ya kuishi ili aweze kujiwezesha kupata huduma za kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka nitoe mfano, kwa mfano kijana, amefanya kazi miaka mitatu. Baadaye ameacha ile kazi. Siamini kwamba huyu kijana atashindwa kutafuta njia yoyote ile ya kuweza kujiwezesha wakati anatafuta ajira nyingine apewe mafao yake kama yangeliweza kukaa hayo mafao yakajilimbikiza mpaka siku atakapofikia umri wa kustaaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi suala la mafao ya kujitoa kama kwenye nchi nyingine lipo, mimi sikatai, lakini kwa uchumi wa nchi yetu na mazingira ya Kitanzania, suala la fao la kujitoa ni kudanganya vijana waache kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niongezee, suala la mafao siyo kwamba ni kwenye ajira ya utumishi wa umma tu, hata mtu anayejiajiri mwenyewe anatakiwa aingie kwenye masuala ya huduma za kijamii. Kwa hiyo kama uliajiriwa kwenye sekta ya umma, ukaacha kazi, unatakiwa ujiingize kwenye sekta binafsi, na vile vile tuhamasishe vijana wenzetu waingeie kwenye mafao kupitia sekta binafsi. Lakini siyo sawa sawa kwamba mtu afanye kazi miaka mitano akiwa na umri wa miaka 30 au 35, akiacha kazi apewe mafao yake yote. Huyu kijana siku akipoteza nguvu za kufanya kazi ataishije?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Mkofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, kuna hoja imetolewa, kama ulivyosema, hiyo ya China kuna 2% amesema Mheshimiwa Dkt. Kigwangala amesema kuna afya. Re-*consinder* hivi vitu, unatazama kama mnaweza mka-*revisit* haya mambo halafu mrudishie mtoa hoja.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naomba tu nimuelewesheshe Mheshimiwa Machali, kwamba sisi tunaenda

by standards za *ILO* na kwa kila nchi mwanachama wa *ILO,* anajua kuna mafao 9 tu. Fao la pensheni ya uzee, fao la matibabu, fao la kuumia kazini, fao la ulemavu, msaada wa mazishi, *un-employment* ambayo Tanzania hatunayo bado, bali tunajaribu kufanya kitu kama hicho, *family relief,* uzazi na wategemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii, *NSSF,* imeshafikisha mafao saba. Sasa mimi ninaomba uniletee hiyo nchi ambayo ina hicho kitu kinachoitwa fao la kujitoa. Naomba sana tafadhali, ili nielewe kama ni nchi mwanachama wa ILO au imeunda kitu chake tu. Kwa hiyo mimi nafikiri utani… Na hii ni *Convention* ambayo wanachama wote wa ILO tunanapaswa ku-*adhere*. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mimi nafikri maelezo waliyoyatoa Waheshimwia Wabunge, yamenielewesha kwamba wameelewa nini maana ya kujitoa. Na wala Mheshimiwa Wenje, mwanangu, mwanafunzi wangu, hatusemi kwamba mtu aendelee kufanya kazi. Mheshimiwa Sara Msafiri, amelizunguza vizuri. Kufanyakazi katika sekta rasmi ni moja, lakini unaweza bado ukatengeneza utaratibu wako wa kuendelea kuchangia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

MBUNGE FULANI: Kama wanavyotaka kufanya katika sekta ya Kilimo.

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Eee, kama walivyofanya katika sekta ya kilimo. Kuna Mzee alitoka kule, Sheikh, anachangia sekta ya hifadhi ya jamii na ana manufaa yake. Vijana katika uchimbaji wa madini wanachangia sekta, siyo lazima uajiriwe. Kwa hiyo mimi naona labda ni kuelewa.

Mara nyingi sana *SSRA* wametoa hapa semina, naomba muwe mnahudhuria hizi semina, zinatusaidia sana kujielimisha sisi na kuelimisha Wapiga kura wetu. Kwa kweli kama walivyosema wengine, tusiwapake mafuta kwa mgongo wa chupa, tunawaumiza. Kwa sababu kama uko katika Hifadhi ya Jamii na majanga yanakupata, kwa kweli una *fall back position. Una fall back position,* uwe umri mdogo, uwe umri mkubwa kwa sababu majanga haya umri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hii pensheni au katika kuchangia Mfuko wa Jamii, unajiwekea akiba ambayo siyo akiba ambayo umempa mtu akuwekee, ni akiba ya mfuko ambao una mafao mengine ambayo yatakufaa wakati huna pesa mfukoni. Kwa hiyo tunachosema ni nini, tunachosema ni hivi, usiondoke kabisa kwenye mfuko, usiondoke kabisa kwenye Hifadhi ya Jamii.

Hii aliyoisema Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, kwa kweli ndiyo hiyo ambayo tunataka kufanya kwamba kuwe na aina fulani ya kumlinda huyu mfanyakazi, wakati anahangaika kutafuta ajira au kutafuta namna ya kujikimu ili aendelee kuchangia, aweze kujikimu. *So,* tutakapokuwa tumekamilisha nafikiri Wabunge mtatuunga mkono kusudi tuwasaidie vijana wetu, wasiondoke kwenye Hifadhi ya Jamii, na hii ni sera ya nchi kwamba tupanue wigo wa wanachama wa wananchi wanaoingia katika Sera ya Hifadhi ya Jamii.

Leo Kambi ya Upinzani imesema kwamba Hifadhi ya Jamii, bado haijaenea kwa Watanzania, na ninyi mnazungumzia *withdrawal,* kwa kwa kweli ni vitu viwili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekikti, ahsante. *(Makofi)*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti…
MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali, kubali yaishe tu, maana hoja za msingi umeambiwa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nashikilia shilingi, na ninaomba kidogo muda maana ametumia muda mrefu kidogo.

MWENYEKITI: Aha, muda ninapanga mimi, haya endelea.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza sana, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba ni suala la uelewa pia naye. Naomba niseme kwamba kuna mahali ana *gap* kidogo. Katika maelezo yake amezungumza mwenyewe kwamba kuna fao linaitwa *Un-Employment Benefits.* Sasa hebu *imagine* kwamba mwenyewe unazungumza unaji-*contradict* Mheshimiwa Waziri. Mtu amefukuzwa kazi, huyo mtu hana kazi na ndiyo ana *fall* kwenye hiyo *category* ya *unemployment benefits*. Sasa huwezi ukasema kwamba huyu mtu amefukuzwa kazi halafu anabaki anahangaika, lakini ana fedha zake ambazo alikuwa anakatwa, ame-*invest* mahali fulani, asizichukue fedha hizo. Sijui mnazungumza vitu gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu bado *still* wanakwepa hoja ya msingi. Sheria imesema kwamba ili mtu aweze kuwa *pensionable* baadaye anapaswa ku-*contribute* kwa *15 years*, amefanya kazi miaka mitatu pengine anakwenda kufanya kazi na haku-*contribute* tena baada ya kufanya kazi miaka mitatu ambayo alikuwa anachangia. Hivi kesho huyo mtu utakuja kum-*pension* kwa kutumia fedha gani na wakati haja-*contribute* kwa *15 years?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo unakuwa ni wizi wa mchana kweupe, naomba tuzungumze hivyo. Hizo fedha zinapelekwa wapi kama huyo mtu baadaye tena hakuchangia, hakuajiriwa mahali popote, alifanya kazi zake, alichokipata alikuwa anakitumia yeye na watu wake, hizo fedha zake zinakwenda wapi? Naomba watueleze hilo fao, na Mheshimiwa Waziri alisema kwamba watalifanyia kazi, hata ile kusema kwamba wafanye nusu nusu kwamba mtu kama wazo ambalo amelitoa Mheshimiwa Dkt. Kigwangala, hilo suala unasema unampa kidogo, unakatalia nini kuweza kuchukua fedha zake zote wakati haja *qualify* kwenye miaka 15 ya kuchangia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utakuwa ni wizi na kama Bunge hili linakubali matendo haya, kwa kweli ni kutokuwatenda haki wafanyakazi.

MWENYEKITI: Mheshimwia Machali, nakushukuru maana nakuona unarudia hayohayo.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi yangu bado naikamata ni bora tupige kura wananchi wajue.

(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)

(Hoja Iliamualiwa na Kukataliwa)

(Kifungu Kilichopitishwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko Yoyote)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Keissy!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nakusudia kukamata shilingi kama sitapata maelezo ya kutosha.

Nchi katika ulimwengu inaangalia wafanyakazi wanafanyishwa kazi hakuna cha Jumapili, hakuna cha Jumamosi, hakuna cha likizo, wanafanya kazi saa 24 hawalipwi? Wenyeviti wa Vijiji nchi nzima na Wizara ya Kazi na Ajira ipo haiwatetei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo ndiyo hoja yangu, sikubali nitaishikilia shilingi na Wabunge wenzangu mniunge mkono. Haiwezekani, ni dhuluma ya hali ya juu. Nchi gani ulimwenguni inamfanyisha kazi mtu bila kumlipa chochote na Wizara ya Kazi na Ajira imekaa. Hawana Jumapili, hawana Jumamosi, hawana sikukuu wala hawana saa za kupumzika, saa 24 tunawatumia kama vile watumwa, lakini hatuwalipi na Wizara ya Kazi ipo inacheka. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nakusudia kukamata shilingi na Wabunge wenzangu mniunge mkono. Nataka wananchi hawa walipwe na ninyi Wabunge mnawatumia kwenye mikutano yenu, kwenye maendeleo ya kujenga shule, kujenga hospitali na kila kitu mnawatumia Wenyeviti wa Serikali za Vijiji, lakini hawalipwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asiyeniunga mkono wananchi watamjua huko nje hafai na msimpe kura. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria za kazi hasa Sheria Namba 6 ya mwaka 2004 inatoa vigezo vya mtu kuitwa mfanyakazi, na inatoa vilevile muda au saa za kufanya kazi na kwamba akifanya kazi muda wa ziada analipwa, na yote hayo yanawekwa kwenye mkataba wake wa ajira.

Sasa kama kuna mfanyakazi yeyote ambaye anafanya kazi saa 24 kwa siku, lakini mkataba wake unasema saa nane halafu halipwi muda wa nyongeza, aje kwetu na mkataba wake ule wa ajira na sisi tutamtetea. Lakini isije ikawa hawa anaowazungumzia ni watu wa kujitolea, hawana hata mikataba ya ajira, hapo hatuwezi kutetea kama hakuna mikataba ya ajira.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa hiyo Serikali inapoteza mabilioni ya fedha kufanya uchaguzi wa Serikali za Vijiji na hivi inatangaza inafanya uchaguzi kutumia mabilioni ya fedha ili kuwatumikisha wananachi bure katika nchi hii! Na unasema hujui kama wameajiriwa wakati wanafanya kazi na wewe mwenyewe Mheshimiwa huko kwenye Jimbo lako unawatumia katika kujenga shule, kujenga dispensari, kila kitu unawatumia. Leo unasema kwamba hawakuajiriwa, kwani nchi hii mkikuta kwenye shamba la chai au la kahawa wananafanyishwa tu kazi bure, hawana mkataba hamchukui hatua? Jimbo lako wapo watumishi wa namna hiyo!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy hujatoa shilingi bado!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshasema natoa shilingi, tangu mwanzo nimesema.

MWENYEKITI: Sasa ndiyo unatoa?

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Natoa shilingi!

MWENYEKITI: Endelea sasa!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Naomba Wabunge mniunge mkono, nchi gani hii katika ulimwengu gani huu inatumikisha wananchi bure?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa asilimia mia moja siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Keissy, na siungi mkono kwa sababu dhambi hii ni yetu sisi Wabunge ambao ni Madiwani wa Halmashauri zetu. Serikali imetenga 20% ya fedha ambazo zinapeleka katika Halmashauri, 20% ile inatakiwa iende vijijini. Ndani ya 20% ile kuna takribani 3% ambayo wanatakiwa wapewe Wenyeviti wa Vijiji, na hii ni miongozo ambayo TAMISEMI wameitoa. Sasa kama wewe Mheshimiwa Mbunge hili hulifuatilii ni kosa lako mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, singu mkono hiyo hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtutura!

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Natofautiana kwa kiwango fulani na Mheshimiwa Keissy kwa sababu hawa Wenyeviti wetu wa Vijiji si waajiriwa, si waajiriwa, lakini wanastahili kupata posho ambazo Serikali imekuwa ikizitoa kupitia Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu la Mbunge na ni jukumu la Madiwani kuhakikisha kwamba zile fedha 20% kama alivyoeleza mdogo wangu Rajab, ni jukumu letu kuhakikisha kwamba tunafuatilia zile fedha na zikishafika basi hawa Wenyeviti wetu wa Vijiji ndipo stahili zao wanapostahili kupata pale. *(Makofi)*

Lakini kwa upande wa Serikali, mara nyingi fedha hizi huwa zinacheleweshwa na zikicheleweshwa ndipo mianya inapopatikana ya Wenyeviti wetu wa Vijiji kutozipata fedha zile. Lakini ni jukumu la sisi Wabunge pamoja na Madiwani kuhakikisha kwamba fedha hizi zinafika kwenye Vijiji na Mtendaji wa Kijiji ahakikishe kwamba ile sehemu ya Mwenyekiti wa Kijiji inapatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kigola!

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la msingi sana. Ni kweli kwamba Serikali inatenga ile 3% kwa ajili ya Wenyeviti wa Vijiji, lakini tumeona Halmashauri nyingi sana hazifanyi hivyo na kwenye kaguzi nyingi tumeona kwamba Wenyeviti wa Vijiji hawalipwi, ndiyo maana kuna malimbikizo huwa yanatokea.

Mimi nataka niishauri Serikali kwamba suala hili inabidi hata kwenye Katiba mpya liingizwe kisheria, isionekane kwamba mtu anajitolea tu. Haya masuala ya kusema tunajitolea, sasa hivi tunakwenda ulimwengu mwingine, inabidi watu wawe wanalipwa. Sisi kama Wabunge ni kweli Wenyeviti wa Vijiji tunawatumia sana. Kwa hiyo nataka nishauri kwamba kwenye Katiba mpya tunapokuja kulijadili hili suala lazima tuliweke kwenye Katiba mpya tuhakikisha kwamba Wenyeviti wa Vijiji na wenyewe wawe wanalipwa kisheria, kuliko tuseme kwamba kuna asilimia ngapi lakini haijwekwa vizuri kisheria. Hii itakuwa imesaidia sana kwa Wenyeviti wetu wa Vijiji!

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Lugola!

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusikitika namna ambavyo tunataka kupotosha hoja nzuri ya Mheshimiwa Keissy.

Hoja ya Mheshimiwa Keissy ni kwamba wako watu ambao wanafanya kazi Serikalini na inaitwa Serikali ya Kijiji, Serikali ya Kijiji ambako ndiko Serikali inapoanzia. Na Yule Mwenyekiti ndiye anayeongoza Serikali hiyo inayotambulika kisheria. Sasa leo Keissy anaitaarifu Wizara ya Kazi na Ajira kwamba kuna watu wanafanya kazi Serikalini, lakini hawalipwi ujira, wakati ninyi Wizara mpo mnatazama, kuna nini?

Kwa nini mnawaacha watu hawa wanafanya kazi Serikalini, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, lakini wananyonywa hamchukui hatua. Na ndiyo sababu leo hii wako wenzetu wanaofanya kazi kwenye Baa, tuna Ma-*house girl* na wafanyakazi wengine ambao pia Wizara hii hii inahakikisha kwamba watu kama hawa pia hawanyonywi, wanalipwa ujira.

Sasa hoja ya Mheshimiwa Keissy siyo kwamba kwa nini hawalipwi mshahara, kwa nini Wizara hii inawaacha watu hawa wanaonyonywa, wanaotumikishwa Serikalini halafu haichukui hatua? Hiyo ndiyo hoja ya Mheshimiwa Keissy. Na mimi namuunga mkono asilimia mia.

Wamekuwa wakimamatwa na ma-DC, kwa nini hawasimamii maendeleo, wanawekwa ndani saa 48, watu hawa wamekuwa wakifanya kazi kwenye Serikali za Vijiji kwa tuhuma mbalimbali ambazo zinawapa shida wakati

mwingine. Halafu leo Wabunge tunasimama hapa tunasema tujilaumu sisi wenyewe kule, kwa nini sisi Wabunge ndiyo tunaosimamia watu wanaonyonywa waweze kulipwa ujira? Anayesimamia ni Wizara ya Kazi, kwa nini Wizara ya Kazi, dada yangu Mheshimiwa Kabaka mnakaa ilihali kuna Watanzania wanafanya kazi Serikalini hawalipwi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lugola, ahsante. Mheshimiwa Waziri!

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bila shaka baada ya mimi kujibu na mazungumzo yaliyofuatia, imeonekana kwamba suala hili kwa kweli siyo la Wizara ya Kazi na Ajira.

Wizara ya Kazi na Ajira inaangalia kweli maslahi ya wafanyakazi wenye mikataba kwenye maeneo yao ya kazi. Sasa kama utashika shilingi kwenye Wizara ya Kazi kwa kazi ambazo kwa *definition* ya Sheria Namba 6 siyo hizo kazi. Kwa sababu sisi tunaelewa, kwa hizi kazi za kuchaguana ni Wabunge na Mheshimiwa Rais ndiyo wamepangiwa mishahara, lakini Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji, zile ni kazi za kujitolea na kule waajiriwa ambao wakija hapa tutawatetea, ni wale Watendaji wa Vijiji ambao wana mishahara na Watendaji wa Mitaa na Watendaji wa Kata, wale ni waajiriwa na wana mikataba ya ajira ambayo wanaotakiwa kuwalipa wakienda kinyume, sisi Wizara tutawatetea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hatuwezi kutetea kazi ambazo ni za kujitolea ambazo sana sana ni posho na Wabunge tunaweza tukaomba tu jamani Serikali, ongezeni posho kwa Wenyeviti wa Vijiji, na mimi hilo nalitetea na wala hamtakuja kwenye Wizara ya Kazi, tutakwenda kwenye Wizara nyingine au mtu mwingine humu ndani atajibu swali hilo la posho kuongezwa kwa hawa Wenyeviti, lakini siyo suala la mishahara na siyo suala la kazi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy, nafikiri umelielewa vizuri!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika!

MWENYEKITI: Haya, tuendelee!

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Hivi Mheshimiwa Waziri, maafisa wako wa *Labour* wakikuta mtu ametumikisha kwenye shamba lake watumishi 100 hawana mkataba, hawalipi, humchukulii hatua? Utamuacha hivi hivi kwa sababu hana mkataba? Kakaa kijijini analimisha shamba lake watumishi 200/300 kuanzia asubuhi mpaka jioni masaa 24 hawana Jumapili, hawana Jumamosi, wewe utawaacha kwa sababu hawana mkataba?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitakubali nchi hii kusema kweli kutumikisha wananchi saa 24 siku 7, miaka mitano mpaka uchaguzi mpaka uchaguzi

hawana likizo bila chochote, halafu Mheshimiwa pale anasema kwamba 3% Halmashauri imetenga, wapi Halmashauri imetenga? Kuna Halmashauri zingine hazichangii hata 2% kwenye mfuko wa bajeti, leo unaniambia 3%, labda huko Zanzibar ndiyo wanachangia, siyo Tanzania Bara huku.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Keissy, kwa hiyo bado umeshikilia shilingi ya Waziri?

MHE. ALLY KEISSY MOHAMED: Mimi nashikilia shilingi, wananchi wanasikiliza kama kupiga kura tupige kura tuwakatalie, lakini wananchi wanajua Wabunge wao wamewasaliti Wenyeviti wa Vijiji, siwezi kukubali kurudisha shilingi, bora tupige kura ili ieleweke!

MWENYEKITI: Nakushukuru Sana.

(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rajab!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nilitaka maelezo ya kina kutoka kwa Waziri kuhusiana na Waraka wa Serikali ambao ulitoka na namwomba kaka yangu Mheshimiwa Malima anisikilize vizuri kwa sababu hili anahusika nalo zaidi.

Serikali ilitoa Waraka namba CAC.45/257/01/TEMP/26 wa tarehe 1/2/2009 ikiwataka waajiri kwamba watumishi wao wote wa mikataba kulipwa kiinua mgongo baada ya mkataba kuisha. Vilevile wasilipwe mafao ya pensheni, wale waajiriwa ambao wako katika mikataba na unielewe vizuri siyo nkataba ni mikataba. Vilevile kwa wale wafanyakazi wa ajira ya kudumu wanatakiwa kulipwa mafao ya pensheni kwa mujibu wa sheria.

Sasa mbali ya sifa nyingi ambazo tumezitoa kwa ndugu zetu wa NSSF ambazo nyingine mimi nakubaliana nazo, hata hii sasa hivi wanayotaka kutujengea Kijiji cha Wabunge nakubaliana nayo, unaona bwana!

Nataka nijue ni kwa nini NSSF walikiuka waraka ule wa Serikali. Je, ni dharau? Je, ni kutokujua au Serikali mnaiogopa NSSF?

NSSF ililipa milioni 13 kwa watumishi wake wa mkataba, lakini vilevile ikalipa bilioni 1.965 watumishi wa ajira za kudumu kama malipo ya mkataba

yaani *gratuity*. Nataka kupata maelezo ya Serikali, ni kwa nini ukiukwaji huu wa sheria hawakuufanyia kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru! Nitaomba kutoa shilingi…

MWENYEKITI: Umechelewa! Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rajab Mbarouk amejieleza vizuri na nimemwelewa au nimemfahamu kwa lugha ya kule kwao. Sasa kwa mujibu wa waraka huo, mtumishi mwenye mkataba kwa kweli analipwa *gratuity* na siyo pensheni na analipwa *gratuity* ya 25 ya mishahara yake wakati ule wa mkataba.

Sasa kwa upande wa NSSF walivyotekeleza waraka huu siyo kweli kwamba wamelipwa mara mbili au wamelipwa *gratuity* na pensheni. Watumishi wa NSSF wako katika utumishi wa mashirika ya umma na wakati wanaingia kwenye mashirika ya umma wao walijiandikisha katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa PPF kama walivyokuwa watumishi wa umma wa wakati huo.

Sasa kinachofanyika kwa hawa watumishi wa umma wa mkataba ambao ni ma-*director* ambao wako kwa muda wana mikataba ya miaka mitatu mitatu na wakati huo ndani ya miaka mitatu wanachangiwa na NSSF kwa sababu lazima walipe hifadhi ya jamii kule PPF. Kwa hiyo, wanachangiwa na NSSF na wanachangia wenyewe kwa hiyo NSSF inachangia 15% na wao wanachangia 10% ya mshahara wao.

Wanapofikisha miezi mitatu wakati sasa wamemaliza *gratuity* na walipwe *gratuity*, ile 15% NSSF inawakata kwa hiyo, atakapoenda kulipwa pensheni baada ya kumaliza kazi NSSF ataenda na mchango wake wa 10% less 15% ambayo alikuwa anachangiwa na mwajiri wake kwa sababu walishaikata wakati wanamlipa *gratuity*.

MWENYEKITI: Ahsante! Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla.

MHE. DKT. HAMIS A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante!

Mimi napenda kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na hoja ambayo nimeiwasilisha kwa kusema hapa Bungeni lakini pia kwa maandishi kwamba Serikali ni kwa kiasi gani imetekeleza Azimio la Bunge la tarehe 1/2/2013 lililotokana na hoja binafsi niliyoiwasilisha hapa Bungeni siku hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yenyewe kimsingi ilikuwa inaelezea ni namna gani sisi kama taifa tungeweza kupunguza umaskini kwa kuwatumia

vijana wetu kwa kuwekeza kwa vijana wetu ili kuzalisha ajira nyingi zaidi kupitia uanzishwaji wa mfuko wa mikopo ya kukuza ajira kwa vijana lakini pia benki ya vijana ili vijana waweze kujipatia mikopo nafuu.

Katika bajeti hii Serikali wamekuja na wazo la kutekeleza programu ya kukuza ajira kwa vijana na katika program hiyo zimetengwa shilingi bilioni tatu za Kitanzania tu. Katika randama yao inaonekana bilioni hizi tatu zimegwanyika katika mtiririko mbalimbali ikiwemo kuweka *collateral* kama ya bilioni mbili kwenye benki ili vijana waweze kupata mikopo.

Sasa napenda kufahamu, hivi kweli kwa vijana wote wa Tanzania zaidi ya 65%, zaidi ya 65% Watanzania ni vijana, wanawezaje kusaidiwa kupata ajira ama kuwezeshwa kujiajiri kwa shilingi bilioni tatu tu? Ninaomba niweke wazi nia yangu kutoa shilingi endapo sitopata majibu yatakayotoa ufafanuzi wa kutosha juu ya suala hili.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Waziri anaelezea programu ya ajira alichukua muda mrefu sana kuzungumzia tatizo la ajira na mikakati mbalimbali ambayo Wizara na Serikali inachukua na alionesha *concern* kwamba, hili ni jambo ambalo kila mtu analijua.

Sasa ni kweli kulitokea Azimio la Bunge kabla ya bajeti ya mwaka jana na tulikutana Wizara hasa mbili ambazo matatizo ya vijana na ajira ni kubwa; Wizara yetu ya Kazi na Ajira na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Baada ya pale Wizara zote mbili zilitengeneza *programs,* kwa bahati mbaya kutokana na uwezo wa Serikali, Wizara moja kwa maana ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo walipata shilingi bilioni sita, sisi hatukupata kabisa.

Kwa hiyo, nina hakika zile shilingi bilioni sita walizipanga kwenye programu za kukuza ajira na bila shaka kwa sababu nadhani bajeti yao bado watatueleza jinsi zile shilingi bilioni sita zilivyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara yetu mwaka jana hatukupata hata senti tano kwenye programu tuliyoitengeneza. Mwaka huu tulitegemea kupata na Waziri amesema awamu ya kwanza shilingi bilioni 36, hatukuweza kupata kutokana na ufinyu wa bajeti ya Serikali, tumepata shilingi bilioni tatu. Hatuwezi kusema sasa hizi ni kidogo sana haziwezi kusaidia vijana tusianze na ndiyo maana tumeanza na ukiangalia randama yetu tunategemea tuanze na vijana 2,400 kuwapa mafunzo na kutoa mikopo. Kwa sababu tutaweka kama dhamana na ndiyo maana tumebuni hiyo ya kwenda benki, kwamba shilingi bilioni mbili hizi zitakapobaki baada ya mafunzo na mambo mengine, huwezi kuanza kuwakopesha tu hao vijana wakatosheleza, tupeleke benki kama

dhamana ili mikopo itoke mikubwa zaidi ya shilingi bilioni mbili hii. Kama wakitoa mara tatu tunaweza tukapata shilingi bilioni tisa au nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni mwanzo mzuri kwa hizo shilingi bilioni tatu tulizozipata, lakini nategemea kwa kauli yake na *concern* ambayo iko kwa Wabunge na vijana nchini, mwaka kesho tutai-*scale up* hii programu na bila shaka na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha yuko hapa ananisikiliza, watatuongeza kutoka hii tatu tupate hata thelathini, ili ile programu kuanzia mwaka kesho iwe kubwa zaidi kuliko ambayo tumeandaa mwaka huu. (*Makofi*)

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi kwa hoja ifuatayo:- Ni kwamba, nawapongeza kwa hatua hiyo ya awali ya kuanza na hii programu, ni jambo ambalo linapongezwa. Lakini ninaendelea kuhoji ni kwanini Serikali haikutenga walau zile shilingi bilioni 36 ambazo Mheshimiwa Waziri wakati ana-*wind up* hapa hoja ya bajeti yake alisema Wizara yao iliziomba kwa Serikali. Ni kwanini walau hawakutenga zile shilingi bilioni 36? Wangefanya vile walau tungesema sasa hapa kuna nia ya makusudi ya kutatua tatizo la upatikanaji wa ajira kwa vijana wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tukiwasilisha hoja ile mwaka jana tulikuwa tunaongelea shilingi bilioni 200 na hata wewe mwenyewe mchana nafikiri ulikuwa unakumbuka kwa sababu ile hoja ilizua hisia humu Bungeni, ulisema hapa wakati unaahirisha Bunge mchana kwamba, kwanini Serikali isitenge walau shilingi bilioni 200 za kuwawezesha vijana ili waweze kuzalisha ajira. Sasa leo hii Wizara ya Kazi wameomba shilingi bilioni 36 wanapewa shilingi bilioni tatu. Hivi kweli kuna nia mahususi ya makusudi ya kutatua tatizo hili, ama ni namna tu ya kujaribu kuanza kupeleka jambo hili kwa mtindo wa *business as usual* (mtindo tu wa mazoea) bila ya kuwa na nia mahususi? Kwa sababu hoja yangu mwaka jana ilitaka tuwe na nia ya makusudi ya kuanza kutatua tatizo hili kwa kuwekeza kwa vijana wetu, kwa sababu tunaamini kwamba, ni vijana ndiyo watakaoishi miaka mingi kibaiolojia kuliko wazee wetu hawa ambao leo hii wanaelekea kututoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tunajua kwamba vijana ni 65%, pia tunaamini kwamba tukiwekeza kwenye nguvu kazi hii, tutafika mbali. Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kutoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

MWENYEKITI: Asante. Mheshimiwa Nkamia!

NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Nilitaka tu niongezee majibu ya hoja ya Mheshimiwa kaka yangu Dkt. Kigwangalla, kwamba fedha anazozungumza Waziri wa Kazi ni tofauti na zile

zinazotekelezwa na Wizara ya Habari kwenye Mfuko wa Vijana. Zile hazina *collateral* ya benki, ni maombi yanayotoka kwenye vikundi vya vijana kutoka katika Halmashauri zetu nchini na zinapokwenda kwenye Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, ndiyo inatoa zile fedha kwa vikundi ambavyo vimekuwa *approved* kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ya Alhamisi Mungu akijalia tukiwa salama kwenye bajeti yetu hapa tutaelezea. Lakini la nyongeza ni kwamba, na pia nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wahamasishe vikundi vya vijana kwenye majimbo yao ili waweze kupata fedha hizo. Tulishaomba *six billion* tumepata *two billion* na tunaendela sasa kuchambua baadhi ya vikundi ili fedha hizo ziweze kutoka.

Hizi anazozungumza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, ni tofauti na hizi ambazo Mheshimiwa Kigwangalla amezungumza kwenye Mfuko wa Vijana. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza, suala analolizungumza Naibu Waziri, Mheshimiwa Nkamia, hizo fedha za Halmashauri mpaka kuzipata ni *issue* na kwanza hazipo. Kwa hiyo, kama katika vikundi 200 kinapata kikundi kimoja, sijui kama Serikali inaweza ikaja hapa ikasema kuna fedha ambazo zinatengwa kule za maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani hoja ya Kigwangalla ni kwamba, hatutarajii kila kijana ni mfanyabiashara, hoja yake ni kwamba Serikali lazima iangalie kuna utaratibu gani wa kuwajumuisha vijana katika kila sekta muhimu ya nchi yetu, siyo kuja kutoa mikopo ye elfu kumi kumi, elfu ishirini au elifu hamsini. Kwa mfano; Serikali mna mkakati mkubwa wa kilimo wa SAGCOT, yanakuja makampuni makubwa kutoka huko nchi za Magharibi. Huu mkakati vijana ambao tunaambiwa itakapofika mwaka 2050 uhitaji wa chakula duniani utaongezeka kwa asilimia 70 tunatumiaje hiyo fursa kwa vijana wetu ili Tanzania 2050 iwe inailisha Marekani, yaani wakati sisi tunaunua *Ipad* Marekani, Marekani wananunua chakula kwetu, ndiyo hoja ninazozizungumza. (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ninachoomba Wizara msitujibu kwa lugha nyepesi, Wizara yenu ni mtambuka, inaingia katika kila Wizara. Kwa hiyo, tunataka mkija na mpango wa vijana, mnakuja na mpango mpana na msituambie hamna pesa. Kama tunaweza kusamehe kodi, kila siku nasema, tunasamehe kodi *almost* trilioni mbili kwa mwaka kwa wafanyabiashara wakubwa, hivi tunakosa bilioni 200 kuandaa kizazi ambacho kitakuja kuipeleka Tanzania hatua moja mbele? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili suala ni *serious* na tusitengeneze mazingira, kwa sababu dunia ya sasa hivi ni kijiji, vijana wa Tanzania wanaona

vijana wa nchi nyingine wanavyotembea barabarani kudai haki zao, tusifike huko. Kama uwezo tunao tuutumie sasa kuwekeza. CAG kila siku analalamika hapa, trillion 1.2 mishahara hewa. Hivi kwanini mishahara hewa tusiizue siku moja twende tukawekeze kwa vijana! Hatuoni, tutaona lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona mwenzio ananyolewa wewe tia maji. Sasa nyie muanze kutia maji kwa sababu mambo yanaonekana, tuwe *serious* katika hizi *issues*. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri hata kama mwaka huu anaona kwamba amebanwa banwa hana kitu, atoe *commitment* yenye tija, watuletee taarifa mipango mikakati ya maana katika nyanja pana kuweza kuokoa kizazi chetu hiki.

Mmeshaanza kuona bodaboda ndiyo dili, matokeo yake sasa hivi ukienda Muhimbili vijana wamekatika miguu, wanaendesha bodaboda siyo kwa sababu wanapenda, kwa sababu ya umaskini, Serikali hamjatoa fursa. Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja ya Kigwangalla, Waziri atupe majibu ya kina na kama yeye ni mzigo vilevile tujue hapa hapa kwamba yeye pia ni mzigo yaani haeleweki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Asante. Mheshimiwa Bulaya.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilikuwa mmojawapo wa walioleta *amendment* katika hoja ya ndugu yangu, rafiki yangu Dkt. Kigwangalla. Hoja ile ilikuwa hoja maalum, kwa ajili ya Serikali itengeneze mpango maalum kwa ajili ya kukuza ajira kwa vijana, baada ya kugundua hiyo mikakati mingine waliyokuwa nayo imeshindwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua hoja maalum kunakuwa na bajeti maalum. Sitaki kuamini kwamba 61% ya Watanzania ambao ni vijana, wanahangaika katika suala zima la ajira, *either* wajiajiri wenyewe au la, kwamba Serikali haijaona kwamba kulikuwa kuna umuhimu wa kutenga fedha kwa ajili ya kuwasaidia vijana hawa kwenye ku-*invest* kwenye maeneo mbalimbali hasa sekta kilimo na *amendment* yangu ikasema hata wale ambao wanajihusisha kwenye masuala ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja ya maazimio ni kwamba, kutengwe maeneo ya kilimo ya vijana, kutengwe maeneo ya biashara ya vijana. Hili nalo mpaka sasa hivi halijatekelezwa, mbali na kwamba tu zimetoka hizo fedha ndogo.

Mimi nilifanya ziara kwenye Mikoa mitatu, nilikuwa najaribu kuwauliza Halmashauri katika utekelezaji wa hili Azimio, hawajaambiwa na hawajatenga. Sasa sisi Wabunge wa vijana tunapokutana na vijana wenzetu wanatuambia matatizo yao tunakuja kuieleza Serikali, halafu Serikali hatuoni kwamba ina mikakati ya dhati ya kuhakikisha jambo hili linashughulikiwa.

(Kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kumalizika)

MHE. ESTHER A.BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo siyo kengele yangu.

MWENYEKITI: Ahsante sana.

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kigwangala na ninataka maelezo ya kina. Na hizo fedha alizosema Mheshimiwa Nkamia, shilingi bilioni mbili hazifiki, jana nimetoka Bunda, nimeongea na Bunda SACCOS, hakuna hela iliyoenda.

MWENYEKITI: Mheshimiwa kaa chini! Mheshimiwa Mnyika, si usubiri nikuite! Mheshimiwa Mnyika. *(Kicheko)*

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mwaka jana wakati hoja hii inajadiliwa, nilipendekeza maazimio matatu kuingia kwenye maazimio ya Bunge na nilitahadharisha wakati ule kama maazimio haya hayataingia, mwisho wa siku tutafika kwenye bajeti Serikali haitatekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendekeza Tanzania ina Sheria ya Uhamasishaji wa Ajira ya mwaka 1999, ina Sheria ya Uwezeshaji ya mwaka 2004, ilianzisha mifuko ya vijana na wanawake toka mwaka 1994, lakini kumekuwa hakuna utekelezaji. Nikapendekeza kwa Bunge kwamba moja; tuletewe taarifa ya tathmini ya mipango yote hii ambayo haijatekelezeka na pili mkakati maalum sasa ambao bajeti maalum itatengwa na Bunge kufanikisha mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matokeo tunayaona. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kigwangalla hapa kwa sababu kimsingi Serikali haijatekeleza hata yale maazimio kidogo yaliyopitishwa pamoja na kuyakataa maazimio mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaweza kutumia shilingi bilioni 50 kwenye Maadhimisho ya Uhuru, kama tunaweza kutengeneza mkakati maalum wa kunusuru uchumi wa nchi na tukatenga trilioni kwa ajili ya mkakati huo,

tunashindwaje kutenga shilingi bilioni 200 kwa ajili ya mpango maalum wa ajira kwa vijana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukubaliane hapa tusisubiri mwaka ujao, mwaka ujao ni 2015 tunaelekea uchaguzi, mpango ukitengwa utakuwa ni wa kuwapa matumaini hewa vijana kuelekea uchaguzi. Lazima jambo hili lieleweke safari hii, tukubaliane kwamba suala hili lipelekwe kwenye Kamati ya Bajeti sasa hivi, Kamati ya Bajeti kwenye Bunge hili ikaangalie ni mafungu gani mengine yanakwenda kupunguzwa kuongeza pesa kwenye mfuko huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili litawezekana kama wote ama Serikali hapa kupitia Wizara ya Fedha ikatoa *commitment* ya kuongeza pesa au tukapitisha azimio la kutoridhika tukaondoa shilingi ambayo Mheshimiwa Kigwangalla ametoa hoja ya kuiondoa ili Serikali tukienda kwenye Kamati ya Bajeti itajua bayana kwamba tunataka pesa ziongezeke. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ole – Medeye.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kwa sababu baada ya kupitishwa kwa azimio lile kwamba tunaanzisha Mfuko wa Ajira kwa Vijana, mimi nilipita jimboni kwangu nikahamasisha vijana anzisheni vikundi vya kiuchumi ili muweze kuanzisha ajira ninyi wenyewe badala ya kutegemea kwenda kwenye machimbo ambako watu wanafia kule. Nilikuwa na matumaini makubwa sana kwamba, tungepata fedha za kutosha vijana hawa waweze kujiajiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa ni kweli ni shilingi bilioni tatu nimeziona, lakini shaka yangu zaidi siyo wingi wa fedha ambazo labda zingetengwa, zingetengwa nyingi ningefurahi sana kwa sababu zingefika kila kona ya nchi. Tumekuwa na mipango mingi ambayo tunaanzisha nchini zinatengwa fedha, kwa mfano mabilioni ya Kikwete, hatujui ziligawanywaje fedha zile! Tulikuwa na mdororo wa uchumi tukatenga shilingi trilioni moja nukta ngapi, sijui zilivyogawanywa. Tungependa Serikali ituambie fedha hizi za vijana ni utaratibu gani unatumika ili vijana waweze kupata bila upendeleo wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Wabunge wanataka *commitment* na wanataka kama itaweza kwenda kwenye Kamati ya Bajeti kwa sababu *this is a serious thing*, hata mimi mchana niliisema. Kwa hiyo, lazima muitazame kwa upana wake. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge kwamba jambo hili ni jambo kubwa. Lakini, mpaka dakika hii naomba niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwenye utaratibu mzima wa kibajeti hata ule wa mwaka jana yako mambo mengi ambayo tunakuja nayo hapa Serikalini na bado tunagombana nayo katika kujaribu kuyatimiza kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtu anakataa kwamba, ni lazima tuwe na mkakati hasa wa uwezeshaji wa huu mfuko wa vijana, na wenye dhamana tumeongea nao. Labda nilitaka niliweke tu ili lisionekana kwamba, labda Wizara hizi mbili Kazi na Ajira na wale wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo wametofautiana katika hili, hapana! Kimsingi sisi Wizara ya Fedha tunapokaa tunaangalia yale majukumu ya pamoja ambayo ni mtambuka ambayo yanaweza yakafanywa na Wizara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *concept* iliyokuwepo hapa ni kwamba hata tukirejea ule mfano wa mabilioni ya JK, mimi nilikuwa Mjumbe wa Taifa katika Wabunge saba waliotoka humu kwenye Bunge la Muungano ambao tuliteuliwa mwaka 2006, nadhani tulikuwemo mimi na Mheshimiwa Ngeleja naye alikuwemo kwenye ile Kamati na wengine. Jambo moja kubwa lililotukwaza kwenye mabilioni ya JK ni kwamba, hatujajenga tamaduni ya kuchukua na kurudisha. Sasa tuambizane ukweli kwamba, hatujajenga tamaduni ya kuchukua na kurudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika hili tunasema mwaka huu kwa mfumo wa kibajeti tuna majukumu ambayo tunabidi tutoke nayo mwaka huu twende nayo mwaka kesho. Kwa hiyo, tumewaomba wenzetu wa Wizara ya Kazi na Ajira, kwamba katika utaratibu huu waanze na kitu kinaitwa *pilot*. Sasa wataamua wenyewe katika ile bilioni tatu, wameamua kwamba katika ile shilingi bilioni tatu watakwenda kui-*leverage* kwenye mfumo wa benki wapate shilingi bilioni saba au bilioni nane, halafu katika utaratibu ule watengeneze utaratibu wa *select*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla namheshimu sana, lakini huwezi kutengeneza mfumo ukasema 60% ya Watanzania milioni 45, tuwatengenezee mfumo wa kuwakopesha. 60% wale ni Watanzania milioni 27 na nilikuwa najaribu kuangalia hapa kwenye *demographics* kama kweli vijana ambao wako kwenye umri wa kufanya kazi wanafika milioni 27 kwa sababu kwenye ile milioni 27 kuna watoto wako shule na kadhalika na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachosema ni kwamba, hili jambo kwa ukubwa ni tatizo kubwa, lakini tumewaomba Wizara ya Kazi na Ajira walisimamie kwa fikira ya kwamba, katika hizi tumewapa watakwenda kuzisimamia, watakuja na utaratibu wa mfano kwamba walikuwa wamechukua vikundi kwenye maeneo ya Tanzania 40 wamepata vikundi 40, vile vinakuwa ni *pilot*, mwaka kesho tunaweza kusema twende bilioni 10 au twende bilioni 20 kulingana na uwezo wa kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni lazima niseme kwamba siwezi kukaa hapa, tunaongopeana hapa, nikasema tutakwenda kwenye Kamati ya Fedha, tutatoa shilingi bilioni mia mbili, hazipo. Kilimo wanadai bilioni themanini za nyongeza, hakuna, sijui nani hao, *It is just not possible,* niseme ukweli kwamba katika jambo hili, ni lazima tumewa-*commit* wenzetu waanze na hizi bilioni tatu, iwe kama ni sehemu wakazifanyie kazi ili mwakani tuone namna ya kuziongeza, tukitambua kuwa *demographic* za Tanzania vijana wanaongezeka na hili ni jukumu ambalo ni kubwa na tunajipanga kuliangalia, lakini kwa uwezo wa kifedha mwaka huu haiwezekani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri!

WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nawashukuru Wabunge wote mliochangia na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, utakumbuka wakati najumuisha na nilipoelezea hii program nilisema hivi tutakwenda kwa vijana walio tayari na ndiyo hiyo huwezi ukaamka tu ukaanza ku- *dish out money* na *actually* mabilioni ya Kikwete yalitupa fundisho.

Kwa hiyo, tunataka kwenda kwa vijana walio tayari kwa maana ya ku-*identify* na tume-*identify* nchi nzima baada ya lile Azimio hapa, kazi tuliyofanya ni ku-*identify* vikundi, Mikoa yote, Wizara ya Kazi na Ajira ina aina ya vijana na vikundi na shughuli zao. Kwa hiyo, tuna *bank* ya shughuli za vijana. Hivyo, tunajua ni wapi na tumesema katika hii bilioni tatu tutachukua kila Mkoa na tutasambaza kila Mkoa hata kama ni vikundi viwili, basi tuchukue kila Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, *it's a pilot* tuanze na hawa tuone inavyokwenda na tuna uhakika kwa sababu tulishazungumza na *CRDB* watatuongeza maradufu kama *collateral,* kama dhamana na vijana walio tayari watatuonesha sasa njia ya kwenda na *next year* Mungu akijalia, tutakapokuwa tunatoa taarifa hapa na kuomba fedha nyingine na kwenda Serikalini kuelezea zaidi, nina uhakika tutapata fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla alitoa wazo zuri na tuliliunga mkono Azimio lake kwa kuwa ni kijana; tukalichangamkia, tukafanya *mapping* ya vijana, tunao, nia ipo na tunataka kuanza sasa hivi kwa *pilot,* mwaka jana tulikosa pesa kwa nini tena utoe shilingi baada ya kupata pesa hii na kutaka kuanza? Kwa hiyo, Mheshimiwa tunakuomba uturudishie shilingi yetu tuanze na tutaanza *immediately* baada ya bajeti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, hoja yako ni ya msingi na ume-*broadcast* vizuri sana, nchi nzima wamekuelewa na naamini Serikali ina mipango mizuri, *give them time* na wakati huo bado tutawabana ili kuhakikisha *issue* hii inafanikiwa na vijana wawe na Mfuko wao na Serikali hiyo ni muhimu. Karibu Mheshimiwa Kigwangalla!

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niwashukuru kwanza Wabunge wote waliochangia kwenye hoja yangu, Mheshimiwa Malima alikuwa anajibu hoja ambayo siyo iliyoko mezani kwa sababu hoja aliyokuwa anaijibu ni hoja kwamba kuna uhalali kwenye hoja yangu ama hakuna uhalali, lakini ukweli ni kwamba hoja hii ilishajadiliwa mwaka jana na watu wakarekebisha hapa ndani wakiwemo Waheshimiwa Mawaziri wote, tukakaa kwa pamoja kama Kamati ndogo, tukapitisha Maazimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo hoja ile ilikubalika na pande zote za Bunge, upande wa Serikali na upande wa Upinzani. Kwa maana hiyo, hakukuwa na shaka kwenye wazo lenyewe, kwa hiyo majibu ya Mheshimiwa Malima siyakubali, labda kama hakuna fedha angesema kuwa hakuna fedha, lakini siyo kukataa wazo lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kwanza kwa kiasi kikubwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara ya Kazi kwa kuanza kutekeleza wazo hili kwa angalau hatua hiyo ndogo, ninawapongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba ili kuweka heshima ya Bunge, basi Azimio hilo lifanyiwe kazi na naomba uelekeze Serikali wakakae na Kamati ya Bajeti waongeze fedha kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika hata Waziri atafurahia kwa sababu sisi tunachokifanya ni kumsaidia yeye atekeleze mpango wake ambao tayari ameshaanza kuufanyia kazi. Hivyo, nitairudisha hiyo shilingi kwa heshima tu ya Mama kwa sababu ni Mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba sana utoe maelekezo kwenye Kamati yako hii Tukufu ya Matumizi kwamba, hoja hii ichukuliwe, irudishwe kwenye Kamati ya Bajeti kule mwishoni, waje na marekebisho mengine, lakini

sikubaliani kabisa na kwenda mbele na wazo hili ambalo litatekelezwa kwa bilioni tatu, hilo ni jambo nisilolikubali. Narudisha shilingi ya Waziri.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana na hoja yako imekubaliwa. Mheshimiwa Chiku Abwao, Chiku vipi unamfikiria Lukuvi? *(Kicheko)*.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Katika mchango wangu nilikuwa nimejaribu kuzungumzia suala la matatizo ya vijana. Mheshimiwa Waziri amejibu na kurudisha kwamba hili suala ni suala ambalo linahusika na Halmashauri. Ni kweli na mimi najua kuwa hili suala linahusika na Halmashauri, lakini nimeona ni suala ambalo limezidi kuwa kubwa na kwa mtazamo wangu nimeona kana kwamba Halmashauri zimeshindwa kulifanyia kazi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanateseka sana, vijana ninaowazungumzia kama nilivyosema awali siyo wale Maafisa waliosoma wenye *degree,* ni vijana ambao wamesoma elimu yao mpaka *form four* ambao wamejua kabisa kuwa wao hawaajiriki Serikalini, lakini wanatafuta mbinu za kufanya kazi ambapo ndipo wamejiingiza kwenye masuala ya kuendesha bodaboda na wengine wamekuwa Wamachinga ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa kuhangaika bila kuwa na vituo maalum na wamekuwa wakifukuzwa kila maeneo na sasa hivi tunasikia wapo watoto wa mbwa mwitu, wamepewa majina mengi ambapo sasa hivi wanaashiria hatari kubwa ya kuvunja amani katika Taifa letu. Sasa nataka kujua Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakusudia kutoa shilingi kama hatanipa maelezo ya kutosha.

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kushughulikia vijana na hasa kwenye suala zima la ajira kama ambavyo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge hapa wengi ni suala mtambuka. Sisi kama Wizara ya Kazi na Ajira pamoja na kujishughulisha na hizi *programmes* kama hii ambayo tumekuwa tukizungumzia hapa kwa kweli kubwa zaidi ni Sera ya ujumla ya ajira na ku-*coordinate* maeneo mbalimbali ambayo yanakuza ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye hizi fedha ambazo zinakwenda kwenye Halmashauri, sisi tunajua kwamba nadhani hata Wabunge wote wanafahamu kwamba kuna zile 5% kwa vijana na 5% kwa wanawake ambazo zinatengwa na Halmashauri, hizi zinasimamiwa na TAMISEMI. Sana sana sisi ni kupata taarifa kwamba zimeweza kukuza ajira kwa kiasi gani kwa maana ya

takwimu, lakini kuna Mifuko ya Vijana na Mifuko ya Wanawake, Mfuko wa Vijana unasimamiwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na ule wa akinamama na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi Wizara zote zinafanya kazi, hiyo nadhani kama kuna upungufu wowote kwenye mkakati au mpango wa Wizara mojawapo, katika hizo nimesikia tukiwauliza maswali, hapa Wizara ya TAMISEMI tulizungumzia masuala haya, masuala ya biashara yalizungumzwa kwenye Wizara ya Biashara kwa ajili ya Vijana hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli ni suala ambalo kila mmoja ana majukumu yake anayoyafanya, yeye ameona kuwa kule TAMISEMI labda mambo hayaendi vizuri au labda kwenye Wizara zingine, nadhani hiyo ni hoja tofauti. Sisi tuangalie haya majukumu ambayo tunayo na program ambazo sisi tunazo kama Wizara ya Kazi na Ajira, ndiyo tuyaulizie, kama kuna haja ya kuondoa Mifuko mingine kwenye Wizara zingine, hiyo ni hoja ambayo anaweza kutoa kwa namna nyingine.

MHE. CHIKU A. ABWAO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na natoa shilingi. Mheshimiwa Waziri alivyojibu hoja yangu, kwanza hajanielewa nafikiri, yeye anaelezea habari ya Mfuko, mimi naelezea juu ya vijana ambao wala siwaombei fedha hapa. Vijana ambao wameamua kujiajiri wenyewe, vijana ambao wanafanya biashara ndogondogo, lakini wanakosa maeneo ya kufanyia kazi, wamekuwa wakifukuzwa kila wanapokwenda, hiyo ndiyo hoja yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kuitaka Serikali iniambie, kuna mkakati gani ulionao kwa sababu hili ni jopo kubwa la vijana, nazungumzia jopo la vijana nchi nzima, vijana ambao sasa hivi wanachanganyikiwa pamoja na kujituma kufanya kazi, lakini hawapati ushirikiano na Serikali kuhakikisha kwamba wanaheshimika katika shughuli zao za kihalali wanazozifanya Serikali ina mpango gani kuwafanyia utaratibu hawa vijana ambao hawana sehemu ya kufanyia kazi na wamekuwa wakifukuzwa kwa maana ya kuwatafutia maeneo muafaka ama hata kwa siku maalum kwa maeneio fulani kufungwa kama ni barabara au nini wafanye kazi hawa vijana zilizo halali ili kuepukana na jopo hili la vijana ambao wanakata tamaa sasa hivi wanajiingiza katika shughuli za wizi, ujambazi na madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoa shilingi kwa sababu hiyo na naomba maelezo ya kina na nawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mninunge mkono, tuangalie leo vijana wetu hawa watatafutiwa mbinu gani za kuweza kufanya biashara zao kwa njia halali bila ya kutangatanga na kufukuzwa na Serikali.

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Chiku una hoja ya msingi na ndiyo wote tunaisimamia na kwa mujibu wa Kanuni zetu muda wetu umekwisha, tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu!

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*… … …Tshs. 510,706,000/=
Kif.1003 – *Policy and Planning* … … … ...Tshs. 566,771,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit* … … … … Tshs. 199,500,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Management Unit* … … … … … … … … ..Tshs. 263,218,000/=
Kif. 1006 – *Government Communication Unit* … … … … … … … … ..Tshs. 222,076,000/=
Kif. 1007 – *Information and Communication Tech Unit* … … … … … … ... Tshs. 110,015,000/=
Kif. 1008 – *Legal Service Unit*… … … … ...Tshs. 41,010,000/=
Kif. 2001 - *Labour* … … … … … … ...Tshs. 5,386,629,000/=
Kif. 2002 – *Employment Division*… … … Tshs. 2,494,844,000/=
Kif. 2003 – *Registrar of Trade Union* … … ..Tshs.155,331,000/=
Kif. 2004 - *Arusha Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 84,480,000/=
Kif. 2005 - *Dodoma Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 50,688,000/=
Kif. 2006 – *Geita Regional Labour Office* … … … … … … … … Tshs. 50,688,000/=
Kif. 2007 - *Iringa Regional Labour Office* … … … … … … … … Tshs. 53,576,000/=
Kif. 2008 – *Kagera Regional Labour Office*… … … … … … … …Tshs. 53, 280,000/=
Kif. 2009 – *Kigoma Regional Labour Office*… … … … … … … … Tshs. 53,776,000/=
Kif. 2010 – *Kilimanjaro Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 62,888,000/=
Kif. 2011 - *Lindi Regional Labour Office*… … … … … … … … Tshs. 55,488,000/=
Kif. 2012 – *Manyara Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 55,088,000/=
Kif. 2013 – *Mara Regional Labour Office* … … … … … … … … Tshs. 53,688,000/=
Kif. 2014 – *Mbeya Reginal Labour Office* … … … … … … … …Tshs. 66,838,000/=
Kif. 2015 – *Morogoro Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 75,688,000/=

Kif.2016 – *Mtwara Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 65,788,000/=
Kif. 2017 – *Mwanza Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 87,088,000/=
Kif. 2018 – *Njombe Regional Labour Office*… … … … … … … … Tshs. 58,088,000/=
Kif. 2019 – *Pwani Regional Labour Office*… … … … … … … … Tshs. 55,688,000/=
Kif. 2020 – *Rukwa Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs.56,088,000/=
Kif. 2021- *Katavi Regional Labour Office* … … … … … … … … Tshs. 56,916,000/=
Kif. 2022 – *Ruvuma Regional Labour Office*… … … … … … … … Tshs. 55,538,000/=
Kif. 2023 – *Shinyanga Regional Labour Office*… … … … … … … … ..Tshs. 54,888,000/=
Kif. 2024 - *Simiyu - Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 58,788,000/=
Kif. 2025 - *Singida Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 54,888,000/=
Kif. 2026 - *Tabora Regional Labour Office*… … … … … … … … Tshs. 58,838,000/=
Kif. 2027 – Tanga *Regional Labour Office*… … … … … … … … Tshs. 76,400,000/=
Kif. 2028 - *Temeke Regional Labour Office*… … … … … … … … Tshs. 45,600,000/=
Kif. 2029 - *Kinondoni Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 43,088,500/=
Kif. 2030 – *Ilala Regional Labour Office*… … … … … … … … ...Tshs. 39,888,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

FUNGU 65 – WIZARA YA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA

Kif.1002 – *Employment Division*… … … Tshs. 3,000,000,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

TAARIFA

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kuyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kazi na Taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2014/2015, Mafungu kwa Mafungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, basi naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja Ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa mwaka 2014/2015 Yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wewe na timu yako na wote ambao mmeandaa bajeti hii pamoja na Mifuko yenu kwa kazi nzuri, lakini suala la ajira siyo kama funika kombe, ni suala *very serious* na wote tunaliunga mkono. Ni lazima sasa mkae msikilize ushauri wa Wabunge kuhusu umuhimu wa ajira kwa vijana, *this is a very burning issue*. Katibu!

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 – Wizara ya Uchukuzi

MWENYEKITI: Waziri wa Uchukuzi!

Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2014/2015 ya Wizara ya Uchukuzi kama Ilivyosomwa Bungeni

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuchambua bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na kuweka mezani taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba sasa Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Hotuba nzima ya Makadirio, Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2014/2015 iingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge na uniruhusu niwasilishe muhtasari tu unaobeba maudhui ya Hotuba nzima, vitabu vya Hotuba yangu na andiko maalum la Ukanda wa Kati, *The Central Corridor a wider concept note* vimesambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia zawadi ya uhai na kutuwezesha kukutana tena kujadili utendaji wa sekta ya Uchukuzi na hali ya hewa kwa mwaka 2013/2014 na mipango ya sekta hizo kwa mwaka 2014/2015 kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijawasilisha hoja ya Wizara yangu, naomba niungane na Wabunge wenzangu kuwalilia Wabunge wenzetu waliotutangulia mbele ya haki ninaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao pema peponi. Aidha, nawapongeza Wabunge wapya waliojiunga na sisi kwenye mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii vile vile kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Kyela kwa mafuriko makubwa yaliyoikumba Wilaya ya Kyela na kuwashukuru kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, naomba kumpongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msukumo alioutoa katika kuanzisha na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa program ya Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now)* ambayo imechochea mabadiliko makubwa katika kuufungua Ukanda wa Kati wa Uchukuzi kwa kutekeleza miradi ya Reli, Bandari na Barabara.

Mheshimiwa Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu nao nawapongeza kwa uchapakazi na uongozi wao thabiti na mahiri uliotutia nguvu na matumaini katika kufikia malengo ya *BRN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kukupongeza wewe mwenyewe na uongozi mzima wa Bunge kwa kazi nzuri mnayoifanya. Vilevile naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Mjini na Makamu wake Mheshimiwa Profesa Juma Athuman Kapuya, Mbunge wa Urambo Magharibi kwa kuendelea kunipa ushirikiano mimi na viongozi wenzangu wa Wizara katika kuiongoza Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi ya utangulizi, napenda kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu taarifa ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya sekta ya uchukuzi na hali ya hewa kwa mwaka 2013/2014 na mipango ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utendaji na mapitio ya utekelezaji wa mipango ya Wizara kwa mwaka 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara iliidhinisha bajeti ya shilingi bilioni mia tano ishirini na tisa nukta nne moja. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni mia nne ishirini nukta tano, mbili ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni mia moja na nane nukta nane, nane ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Fedha za maendeleo zinajumuisha shilingi bilioni mia mbili hamsini na mbili nukta sita nane fedha za ndani na shilingi bilioni mia moja sitini na saba nukta nane, nne fedha za nje. Hadi kufikia Aprili mwaka huu Wizara ilikuwa imepokea fedha za maendeleo shilingi bilioni mia mbili na moja nukta mbili moja kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni mia moja themanini nukta moja, tatu ni fedha za ndani sawa na 71.29% na shilingi bilioni ishirini na moja nukta sifuri nane, ni fedha za nje, sawa na 12.56%. Kwa kuzingatia mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha, ni dhahiri kuwa sehemu kubwa ya utekelezaji wa bajeti umefanywa kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa *BRN*; Itakumbukwa kuwa katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu iliteuliwa moja kati ya Wizara sita kuanza kutekeleza program ya *BRN*. Katika kipindi hicho Wizara imepata mafanikio na kufanya maandalizi yote muhimu katika kufikia malengo ya *BRN*. Wizara itaendelea kutekeleza miradi ya reli na bandari na kufikia malengo ya *BRN* katika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bandari, katika mwaka 2013/2014, Mamlaka imekamilisha majadiliano na Benki ya Dunia wakishirikiana na *Trade Mark East* Africa na Idara ya Serikali ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa *(DFID)* ili kupata fedha kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa mradi wa kupanua na kuchimba lango la kuingilia na kutokea meli katika bandari ya Dar es salaam. Mradi huu utatekelezwa sambamba na uboreshaji wa gati namba moja mpaka saba. Kazi za ujenzi zinataraijiwa kuanza mwezi Desemba, 2014 na kukamilika mwezi Agosti, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kazi za uchimbaji na upanuzi wa lango zinatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2015 na kukamilika mwezi Agosti, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa kwa lengo la kuboresha utendaji wa Bandari ya Dar es Salaam ni pamoja na:-

Ujenzi wa jengo lenye ghorofa 35 *(one stop center building)* la kuwaweka pamoja wadau muhimu wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam, ambalo hadi Mei, 2014 lilikuwa tayari na ghorofa 26 zilizojengwa na kazi inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2015; kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kuwaunganisha pamoja watoa huduma kwa njia ya mtandao *(Electronic Single Window System)* mwezi Aprili, 2014 na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2014; kuanza kuweka *(installation)* mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao *(Electronic Payment System)* ifikapo mwezi Juni, 2014 na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kupunguza msongamano bandarini, Mamlaka imepata maeneo kwa ajili ya kutumiwa katika shughuli za kibandari ikiwa ni pamoja na vituo vya kupokelea na kuhifadhia mizigo kwa muda kwa nchi jirani za DR Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Zambia. Maeneo hayo ni pamoja na eneo lenye ukubwa ekari 132 linalomilikiwa na Jitegemee *Trading Company Limited* lililopo katika bonde la Mto Msimbazi na eneo lenye ukubwa wa ekari 39 lililopo Kiwalani linalomilikiwa na *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji wa Mamlaka ya Bandari umeendelea kuwa bora kama inavyooneshwa katika viashiria mbalimbali vya utendaji. Muda wa meli kukaa bandarini umepungua kutoka wastani wa siku 6.3 mwaka 2012 hadi wastani wa siku 4.8 mwaka 2013; muda wa Makasha kukaa bandarini umepungua kutoka wastani wa siku 9.6 mwaka 2012 hadi wastani wa siku 9.3 mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uwezo wa bandari wa kupakua magari kwa kila shifti moja ya saa nane uliongezeka na kufikia magari 671 Desemba, 2013 ikilinganishwa na magari 400 Desemba, 2012. Mwezi Februari, 2014 ulisainiwa mkataba wa wadau wote wa Bandari kuanza utaratibu wa utoaji wa huduma katika bandari ya Dar es Salaam kwa saa 24 kwa siku zote na Mamlaka ya Bandari tayari inatekeleza utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki mbili, *NMB* na *CRDB*, tayari zimehamishia huduma za kibenki ndani ya bandari na ni matarajio ya Wizara kuona benki zingine zikifanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Mamlaka ya Bandari itaendelea na utekelezaji wa miradi iliyoainishwa katika Mpango wa *BRN*. Miradi hiyo ni pamoja na: uboreshaji wa Gati Na. 1-7, uongezaji wa kina na upanuzi wa lango la Bandari ya Dar es salaam na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli; kwa upande wa miundombinu ya reli ujenzi wa madaraja matatu umekamilika, ujenzi wa daraja lililopo kati ya stesheni za Bahi na Kintiku ulikamilika Novemba 2013 na ujenzi wa madaraja mawili

yaliyopo kilomita 303 na kilomita 293 kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe ulikamilika kwa kiwango cha kuweza kupitika kuanzia Machi, 2014. Kukamilika kwa madaraja haya kumeongeza uhakika na usalama wa huduma ya usafiri wa reli ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kushirikiana na Benki ya Dunia kugharamia mradi wa kuinua uwezo wa madaraja yaliyo chini ya tani 15 kwa *ekseli* ili kufikia tani 25 kwa ekseli kati ya Dar es Salaam na Isaka. Mshauri Mwelekezi atakayefanya kazi ya uthamini na usanifu wa madaraja yote yaliyo katika reli ya kati ili yawe na uwezo wa kubeba mzigo wenye uzito wa tani 25 kwa ekseli amepatikana. Aidha, katika mwaka 2014/2015 ujenzi madaraja 16 kati ya madaraja 25 yaliyo katika hali mbaya kati ya stesheni za Dar es Salaam na Tabora utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kutandika reli za ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni za Kitaraka na Malongwe urefu wa kilomita 89 umekamilika na matengenezo ya eneo la reli kati ya Kilosa na Gulwe lililoathiriwa vibaya na mafuriko, nayo yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa ujenzi wa njia ya reli kati ya stesheni za Malongwe na Kitaraka nilikoelezea hivi punde, kunafanya reli zilizotandikwa zenye uzito wa ratili 80 kwa yadi kati ya Dar es Salaam na Tabora kufikia jumla ya kilomita 527. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na utandikaji wa reli za uzito wa ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni za Igalula na Tabora ambayo ina urefu wa kilomita 37 na maeneo mbalimbali kati ya stesheni ya Dar es Salaam na Munisagara, urefu wa kilomita 283. Faida ya kuwa na reli nzito ni pamoja na kupunguza ajali za treni, kuongeza mwendokasi na uwezo wa treni kubeba mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la kujaa mchanga kwenye makaravati yaliyopo kati ya stesheni za Gulwe na Godegode kila mara mvua inaponyesha. Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kudhibiti hali hiyo:-

(1) Ujenzi wa daraja na miundombinu mingine ya kuepusha kujaa kwa mchanga karibu na karavati lililopo kilomita 349/450. Rasimu ya mkataba wa Mshauri Mwelekezi atakayefanya usanifu wa kina wa mradi huo ndani ya mwaka ujao wa fedha, umewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri;

(2) Kufanya usanifu na ujenzi wa mabwawa mawili makubwa ya kupunguza kasi ya maji maarufu kama "punguza". Bwawa la kwanza litajengwa sehemu ya Kimagai karibu na stesheni ya Godegode na bwawa la pili litajengwa karibu na stesheni ya Msagali kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015

(3) Shirika la Maendeleo la Ushirikiano wa Mataifa la Japani, *JICA* kwa kushirikiana na Serikali kupitia mradi wa *Tanzania Rail Intermodal Project (TIRP)* itatuma timu ya wataalam wake mwezi Julai mwaka huu kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la uharibifu wa mara kwa mara wa miundombinu ya reli kutokana na mvua kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014, Wizara ilipanga kuanza maandalizi ya kuunda Mfumo wa Kusimamia na Kufuatilia Mizigo na Vyombo vya Uchukuzi *(Cargo Tracking & Management System)*. Napenda kutoa taarifa kuwa, awamu ya kwanza ya usambazaji wa mfumo huu itaanza mwaka 2014/2015. Kukamilika kwa mfumo huu kutarahisisha ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu za kiutendaji kuhusu wingi wa shehena, usalama wake, mwendo wa vyombo vya uchukuzi wa shehena (pamoja na treni) na usalama wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa huduma za reli, Serikali imefanya maandalizi yafuatayo:-

(1) Ununuzi wa vichwa vipya vya treni 13. Mkataba wa manunuzi ulisainiwa Aprili, 2013 na malipo yote yamefanyika. Vichwa hivyo vinatarajiwa kuanza kuwasili nchini Desemba, 2014;

(2) Ununuzi wa mabehewa mapya 22 ya abiria. Mkataba ulisainiwa Machi, 2013 na malipo yote yamefanyika. Mabehewa hayo yanatarajiwa kuanza kuwasili nchini mwishoni mwa Septemba, 2014;

(3) Ununuzi wa mabehewa 274 ya mizigo. Mkataba ulisainiwa Machi, 2013 na malipo ya awali yalikamilika Februari, 2014. Malipo ya mwisho yanatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa Juni, 2014 na mabehewa hayo 274 yataanza kuwasili nchini Septemba, 2014;

(4) Ununuzi wa mabehewa 34 ya breki ulisainiwa Machi, 2013 na malipo yote yamekamilishwa. Mabehewa hayo yanatarajiwa kuanza kuwasili nchini Julai, 2014.

(5) Ununuzi wa mabehewa 25 ya kubebea kokoto. Malipo yote yamekamilika na mabehewa hayo yanatarajiwa kuanza kuwasili nchini Julai, 2014; na

(6) Kujenga upya vichwa vinane vya treni. Kazi ilianza Machi, 2013 kwenye karakana yetu ya Morogoro na hadi kufikia Aprili, 2014 vichwa vitatu vilikuwa vimekamilika. Vichwa vitano vilivyobaki vinatarajiwa kukamilika kufikia Septemba, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza miradi ya reli nchini, chini ya *BRN*, kwa mwaka 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya maendeleo ya shilingi bilioni 165.68. Hadi kufikia Aprili, 2014, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 145.08, sawa na asilimia 88 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi. Napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa kuweka kipaumbele katika utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya *BRN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka ujao wa fedha wa 2014/2015, Serikali imetenga shilingi bilioni 126.9 chini ya mpango wa *BRN*, kwa ajili ya kuunda upya vichwa vya treni vingine nane; kununua mabehewa mengine mapya ya mizigo 204; kununua vichwa vingine vya treni vipya 11 na kuendelea na matengenezo ya njia ya reli ya kati. Maelezo ya kina ya utekelezaji wa *BRN* yapo ukurasa wa saba mpaka ukurasa wa 16 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za uchukuzi kwa njia ya nchi kavu. Usafiri na Uchukuzi kwa njia ya Barabara. Katika mwaka 2013/2014, Sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarika na kutoa mchango wake katika kutekeleza shughuli za kiuchumi, kijamii na kimaendeleo. *(SUMATRA)* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kuchukua hatua kadhaa ili kukabiliana na matukio ya ajali za barabarani. Hatua hizo ni pamoja na kununua vifaa maalum kwa ajili ya kupima ulevi na mwendo kasi na kuvikabidhi vifaa hivyo kwa Jeshi la Polisi.

Hatua nyingine ni kusimamisha leseni za mabasi yanayohusika katika matukio ya ajali ambapo katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014, jumla ya leseni 34 za usafirishaji wa abiria zilisimamishwa na wamiliki wa mabasi walitakiwa kuwasilisha kwa maandishi mpango utakaotumika katika kudhibiti ajali za barabarani. Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango hiyo ili kupima matokeo na mafanikio yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za usafiri na uchukuzi Mikoani na Vijijini. Wizara kupitia *SUMATRA* imeendelea kuruhusu aina mbalimbali za usafiri kama vile pikipiki za magurudumu mawili na matatu, magari aina ya Noah na kadhalika. Hatua hizo zinakwenda sambamba na ukaguzi wa kushtukiza wa vyombo vyote vya usafiri, kutoa nauli elekezi na kutoa elimu, mafunzo na ushauri kwa watumiaji na watoaji wa huduma za usafiri wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za usafiri wa reli Jijiji Dar es Salaam; huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam kati ya stesheni za Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa na Mwakanga hadi Kurasini zimeendelea kukua na kupendwa na wananchi.Kampuni ya Reli *(TRL)* ilisafirisha abiria 1,343,763 katika mwaka 2013 ikilinganishwa na abiria 230,009 waliosafirishwa katika mwaka 2012. Aidha, kwa upande wa *TAZARA*, abiria 1,460,506 walisafirishwa

katika mwaka 2013 ikilinganishwa na abiria 148,524 waliosafirishwa katika mwaka 2012. Wizara inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma hii ukiwemo mpango wa kuvutia sekta binafsi kuwekeza kwenye usafiri wa treni Jijini.

Katika mwaka 2014/2015, Serikali itakamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia ya Reli Jijini Dar-es-salaam zikiwemo zile za kuenda maeneo ya Pugu, Mbagala Chamazi, Buguruni, Kibaha na Bunju Kerege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Reli. Licha ya sekta ya reli kukabiliwa na changamoto mbalimbali, miundombinu na huduma za reli zimeendelea kuboreshwa ili ziendelee kuchangia katika pato la Taifa na kuongeza mchango wa sekta ya uchukuzi kwa kupitia njia ya reli. Mwelekeo uliopo katika sekta ya uchukuzi ni kuhakikisha kuwa mizigo mizito na mingi inayosafirishwa umbali mrefu inatumia usafiri wa reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Mshauri Mwelekezi, Kampuni ya *COWI* kutoka Denmark alianza kazi ya usanifu wa uboreshaji wa njia ya reli ya Tanga – Arusha yenye urefu wa kilomita 438 Septemba 2013 na wanatarajiwa kukamilisha kazi hiyo Julai 2014.

Mshauri Mwelekezi mwingine, Kampuni ya *H.P. Gauff* kutoka Ujerumani alianza kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli mpya ya Arusha - Musoma Septemba, 2013 yenye urefu wa kilomita 660 mwezi Septemba 2013. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Septemba, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni 7.55 kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kufanya usanifu wa ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha; kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya kati ya Arusha – Musoma pamoja na matawi ya kwenda Engaruka na Minjingu; kukarabati njia ya reli ya Tanga hadi Arusha na kufanya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha reli itakayounganisha reli ya kati na ile ya kaskazini (yaani Tanga-Arusha)...kutokea stesheni ya Ruvu *Junction* hadi Mruazi kuwa katika kiwango cha Kimataifa na kuunganisha reli ya Mruazi na Bandari ya Mbegani, Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulipaji fidia kwa wakazi wa eneo la Mwambani-Tanga ili kupisha ujenzi wa sehemu ya kupanga mabehewa na kugeuzia treni. Jumla ya wakazi 607 kati ya 619 wamekwisha lipwa fidia ya jumla ya shilingi bilioni 4.7. Aidha, hadi Aprili, 2014 hundi 187 kati ya 188 za fidia ya makaburi zilikuwa zimelipwa. Hundi 13 zenye thamani ya shilingi milioni 231.4 bado hazijachukuliwa kutokana na zuio la Mahakama au wahusika kutojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, kazi ya ukarabati wa tuta la reli linalokatiza Mto Ugala pamoja na daraja lake iliyofanywa na Kampuni ya *R & A Works Limited* na kukamilika Oktoba, 2013. Aidha, kazi ya kuondoa reli nyepesi na zilizochakaa zenye uzito wa ratili 45 kwa yadi na kuweka reli zenye uzito wa ratili 56.12 kwa yadi kwa umbali uliobaki wa kilomita 4.59 kati ya tisa zilizobainishwa kuhitaji ukarabati wa haraka kati ya sehemu ya Lumbe - Mto Ugala - Katumba ilikamilika Februari, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuendelea na matengenezo ya njia ya reli kati ya Kaliua - Mpanda, kufanya usanifu wa kina wa uboreshaji wa njia ya reli kati ya Kaliua – Mpanda kuwa katika kiwango cha Kimataifa na kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Mpanda hadi Karema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kushirikiana na Serikali ya Rwanda na Burundi katika uendelezaji wa Mradi wa ujenzi wa reli ya Dar-es-Salaam-Isaka-Keza- Kigali, yenye urefu wa kilomita 1464 na Keza- Msongati Kilomita 197 kwa kiwango cha Kimataifa. Mshauri Mwelekezi kampuni ya *CANARAIL* kutoka Canada alikamilisha kazi ya kufanya upembuzi wa kina mwezi Februari, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na juhudi zake za kupata wawekezaji/fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli ya hiyo. Aidha, Machi, 2014 Serikali za Tanzania na Burundi zilitiliana saini ya Makubaliano ya Awali *(MoU)* ili kuendeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kutoka Uvinza hadi Msongati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha reli ya Isaka - Mwanza ilianza Septemba, 2013 na inatarajiwa kukamilika Julai, 2014. Aidha, Halmashauri ya Jiji la Mwanza imetenga eneo lenye ukubwa wa hekta 148 sehemu ya Buhongwa kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya kupanga mabehewa na kugeuzia treni *(marshalling yard)*. Mshauri Mwelekezi anayefanya tathmini ya ulipaji fidia anaendelea na kazi. Vilevile, katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni nne kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora – Kigoma na kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli za kutoka Uvinza hadi Msongati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – MbambaBay na michepuko ya kwenda Mchuchuma na Liganga Mtaalam Mwelekezi wa kufanya kazi hii ameshapatikana na Mkataba wa kutekeleza kazi hii utasainiwa wakati wowote kabla ya mwisho wa Juni, 2014 na kazi hiyo ya usanifu itakamilika baada ya miezi 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kituo cha kupakua na kupakia makasha *(ICD)* cha Mwanza. Kituo hiki kimepata mwendeshaji Kampuni ya *Transpark Limited*. Kukamilika kwa kituo hiki pamoja na kile cha Shinyanga kutasaidia kufikia malengo ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)* ya kuongeza mzigo unaosafirishwa katika njia ya reli ya kati na pia kupunguza muda wa mzunguko wa mabehewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, *TAZARA* ilianza kutengeneza itifaki ya 15 kwa kuagiza vichwa vya treni vipya vinne; vichwa vya sogeza vipya vinne; mabehewa ya abiria mapya 18; mashine za okoa mbili na mitambo na vifaa vya usalama. Vifaa hivyo vinatarajiwa kuanza kuwasili nchini Desemba, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, nilitoa taarifa kuhusu Serikali za Tanzania na Zambia kuendelea kurekebisha Sheria ya *TAZARA* Na. 23 ya mwaka 1975 kama ilivyohuishwa na Sheria Na. 4 ya mwaka 1995 Sura ya 143. Napenda kutoa taarifa kuwa marekebisho ya Sheria hiyo yalifanyika na Rasimu kuwasilishwa katika kila nchi mwanahisa ili kuboresha na kutoa maoni. Aidha, rasimu hii ya Sheria itawasilishwa kwenye Bodi ya *TAZARA* Juni, 2014 na kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri la *TAZARA* litakalokutana Julai, 2014 kwa ajili ya kupata idhini ya kuendelea na mchakato wa kutunga sheria. Maelezo ya kina kuhusu huduma za uchukuzi na usafiri yapo ukurasa wa 16 hadi 34 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini. Katika mwaka 2013/2014, udhibiti wa huduma za usafiri wa nchi kavu na majini umeendelea kusimamiwa na kutekelezwa na *SUMATRA* kwa kusogeza huduma zake karibu na wananchi. Hadi Machi, 2014, *SUMATRA* ilikuwa imefungua ofisi zake katika mikoa hiyo na hivyo kufanya Mamlaka kuwa na ofisi katika mikoa yote 25 ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, *SUMATRA* ilizifuatilia Halmashauri saba ambazo zilikuwa hazijasaini mkataba wa uwakala wa kusimamia utekelezaji wa kanuni za usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu katika maeneo ya Halmashauri zao. *SUMATRA* sasa imekwishaingia makubaliano na Halmashauri 135 baada ya kusaini makubaliano na Halmashauri hizo kwa sasa *SUMATRA* inaendelea kusaini makubaliano na Halmashauri nyingine mpya 29, utekelezaji wa makubaliano hayo utapunguza ajali na uhalifu unaohusisha matumizi ya pikipiki hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa usalama wa vyombo vya usafiri majini; *SUMATRA* na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar *(ZMA)* wameendelea kushirikiana katika kufanya ukaguzi na uhakiki wa ubora wa vyombo vya usafiri majini na kubadilishana taarifa kuhusu usalama wa vyombo vya usafiri majini na

uhifadhi wa mazingira. Aidha, Kituo cha Kuratibu Taarifa za Utafutaji na Uokoaji, Ulinzi na Usalama wa Majini *(MRCC)* kilichopo Dar es Salaam kiliendelea kupokea na kuratibu taarifa za utafutaji na uokoaji. Kwa upande wa Tanzania Bara kituo hicho kiliripoti ajali 13 ambapo watu 125 waliokolewa na wengine 24 kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu udhibiti wa usafiri wa nchi kavu na majini yapo ukurasa wa 34 hadi 42 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usafiri na Uchukuzi Majini, Huduma za Uchukuzi katika Maziwa; wakati nawasilisha bajeti ya mwaka 2013/2014 niliahidi kuanza ujenzi wa meli mpya tatu katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na ukarabati wa meli za *MV* Victoria, *MV* Umoja na *MV* Serengeti. Pamoja na kwamba mradi huu mkubwa tayari una Mshauri Mwelekezi Kampuni ya *OSK Shiptech* ya Denmark**,** umechelewa kuanza kutokana na gharama zake kupanda kwa asilimia 163 ya gharama zilizokadiriwa awali, Serikali inajadiliana na Serikali ya Denmark inayofadhili mradi huu kuhusu ongezeko hilo la gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na mahitaji makubwa ya uchukuzi katika Ziwa Tanganyika mradi huo sasa utajenga meli mpya Nne, moja katika Ziwa Victoria, mbili Ziwa Tanganyika na moja Ziwa Nyasa pamoja na kukarabati meli hizo tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Bandari; katika kipindi cha Julai 2013 hadi April 2014, Mamlaka ya Bandari ilihudumia shehena ya tani milioni 13.7 ambayo ni sawa na asilimia 96 ya lengo la mwaka. Matarajio ni kwamba kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2014 tutakuwa tumefikia lengo la tani milioni 13.84. Katika kipindi hicho kitengo cha makasha *(TICTS)* kilihudumia makasha 348,811 ambayo ni sawa na asilimia 76 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shehena zilizohudumiwa kwenda na kutoka nchi jirani za Zambia, Malawi, Jamhuri ya Congo, Burundi, Rwanda na Uganda katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 ilikuwa ni tani milioni 3.654 ikilinganishwa na tani milioni 3.182 sawa na ongezeko la asilimia 12.9 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/2013. Ongezeko hili linatokana na obereshaji wa huduma, uimarishaji wa usalama wa mizigo ya wateja na utoaji huduma za bandari kwa saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya mwaka jana tuliahidi utekelezaji wa miradi ya bandari kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa gati la bandari ya Mafia ambao ulikamilika Septemba 2013 na gati hilo kufunguliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete Rais wetu Mwezi Oktoba 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, katika mwaka 2014/2015, Mamlaka imetenga kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuweka kivuko cha kupanda na kushuka kwenye vyombo vidogovidogo kwa kutumia gati lililopo na kuimarisha usalama wa abiria kwa kuziba uwazi uliopo pembezeno mwa gati. Aidha, katika mwaka 2014/2015 *TPA* itakarabati na kuboresha gati la Nyamisati huko Mkuranga ili kuhudumia wasafiri wanaokwenda Mafia.

Pili, Ujenzi wa Gati la Bandari ya Kipiri katika ziwa Tanganyika umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na unatarajiwa kwisha Julai 2014. Kazi ya Ujenzi wa Magati ya Kalema, Lagosa na Sibwesa katika Ziwa Tanganyika zimetelekezwa na Mkandarasi *M/S Modspan*. Aidha, kazi ya ujenzi wa magati ya Kagunga katika Ziwa Tanganyika na Kiwira katika Ziwa Nyasa zilizokuwa zinatekelezwa na Mkandarasi *Cannopy International* hazijakamilika na Mkandarasi amekimbia eneo la kazi. Serikali imeiagiza Mamlaka ya Bandari kuchukua hatua zifuatazo mapema iwezekano:-

(1) Iwanyang'anye Makandarasi hao kazi hizo na kuzitangaza upya na washindi waanze ujenzi mwezi Agosti, 2014 na kukamilisha kazi mwezi Julai, 2015 chini ya usimamizi wa karibu wa mamlaka. Kazi hizo zimetangazwa upya tarehe 17 April, 2014.

(2) Iwashtaki Makandarasi hao kwa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma *PPRA*, Bodi ya Usajili wa Makandarasi *(ERB)* ili kuzifutia usajili kampuni hizo kazi hiyo imefanyika.

(3) Mamlaka iitishe dhamana walizoweka makandarasi hao (*Advance Guarantee* and *Performance Bond)* ili kufidia sehemu ya gharama. Wakati kazi hii inafanyika imebainika kuwa Mkandarasi *M/S Cannopy International* aliwasilisha Mamlaka ya Bandari nyaraka za kugushi za dhamana ya malipo ya awali na hivyo kupata kazi hiyo. Mamlaka imeagizwa imfungulie Mkandarasi huyo kesi ya Jinai haraka iwezekanavyo na ichunguze misingi ambayo Watendaji wake ndani ya Mamlaka walizipokea dhamana hizo za benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika mwaka 2014/2015, Mamlaka imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa gati katika bandari ya Ndumbi katika Ziwa Nyasa ili kurahisisha usafirishaji wa abiria na makaa ya mawe kutoka eneo la Ngaka.

(4) Ujenzi wa bandari ya Mbegani Bagamoyo, mnamo Disemba, 2013 Serikali ilisaini makubaliano ya kutekeleza mradi huo na Februari, 2014, Kampuni ya China *Mechants Holding International Limited* iliwasilisha andiko la mradi. Hivi sasa Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uchambuzi wa andiko hilo ili kuendelea na hatua zinazofuata ikiwa ni

pamoja na kukabidhi eneo la mradi kwa mwekezaji huo. Kazi ya tathmini ya mali zilizo kwenye eneo husika zitakamilika mwaka Juni 2014 na malipo ya fidia yatafanyika katika mwaka wa fedha 2014/15.

(5) Kuendelea na maandalizi ya kuanza kwa ujenzi wa bandari ya Mwambani Tanga na Mtwara ambapo zabuni zilitangazwa tarehe 27 Machi, 2014 na zitafunguliwa tarehe 26 Juni, 2014. Kazi inatarajiwa kuanza ifikapo Septemba 2014 na kukamilika mwisho wa mwaka 2016.

(6) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa magati ya Pangani, Tanga katika Bahari ya Hindi, Mtama na Lushamba katika Ziwa Victoria na Kabwe katika Ziwa Tanganyika. Gati la Pangani, Mkandarasi amepatikana ambaye ni *M/S Alpha Logistics* na ataanza kazi mwezi Juni, 2014 muda wa utekelezaji ni miezi 12, hivyo kazi itakamilika mwezi Julai 2015. Magati ya Mtama na Lushamba utekelezaji wake utaanza mwezi Juni, 2014. Kuhusu ujenzi wa gati la Kabwe utekelezaji wake utaanza mwezi Novemba, 2014.

(7) Kuimarisha usalama wa mzigo na bandari. Mamlaka imepanga kuanza utekelezaji wa mradi wa *Electronic Cargo Tracking System,*

(8) Ununuzi wa *scanners* kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo, *scanners* tatu zimeagizwa na zinatarajiwa kuwasili Septemba 2014; na

(9) Ulipaji fidia kwa wakazi wa Kibirizi ili kupisha ujenzi wa gati umeanza na unatarajiwa kukamilika kabla ya Juni 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za Serikali za kusogeza huduma za kibandari karibu na wateja tarehe Mosi Mei, 2014 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilifungua Ofisi Mjini Lubumbashi DR Congo na kupitia ofisi hii wateja walioko DRC hawatalazimika kusafiri kuja Dar es Salaam wakiwa wamebeba fedha kwa ajili ya kulipia mizigo yao, badala yake wataweza kulipia huduma za bandari wakiwa nchini kwao DRC na kupokea mizigo yao kule kule. Wizara sasa hivi inawasiliana na Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato, Tanzania kuona uwezekano wa kuwa na watumishi wa *TRA* katika ofisi hizo za Lubumbashi ili kuboresha ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uendelezaji wa kituo cha mizigo cha Kisarawe, Mtalaam Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kuendeleza eneo la Kisarawe amepatikana, mtalaam huyo *Royal Haskoning* wa Uholanzi anatarajiwa kuanza kazi mwezi Julai, 2014 na kukamilisha kazi mwezi Januari, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya mwaka jana niliahidi kuanza ujenzi wa gati Na.13 na Na.14, napenda kutoa taarifa kuwa mradi huu umechelewa kuanza kutokana na sababu kubwa tatu:-

(1) *Gharama za ujenzi wa gati hizo mbili wa dola za Marekani milioni 523, karibu shilingi bilioni 837 bado ni juu mno na inayoendelea kuzua maswali mengi yasiyojibika pale gharama za miradi mingine ya aina hiyo hiyo zinapoangaliwa ambazo ni chini ya nusu ya gharama hiyo ya dola za Marekani milioni 523.*

(2) *Gharama hiyo ya ujenzi wa dola za Marekani milioni 523 ilifikiwa ili kujenga gati mbili za kisasa na vifaa vyake zinazoweza kuhudumia meli kubwa hata za aina ya Panamax zenye urefu wa mita 294.13, upana wa mita 32.31 na kina cha mita 12.04, lakini Mkandarasi CCCC* na *CHEC hawakuwa wakweli kwani waliendelea na mchakato wa usanifu wa awali* hydrographical *na* topographical surveys *huku wakijua kuwa gati Na. 13 na Na.14 zisingeweza kuhudumia meli kubwa za aina hiyo ya* Panamax *kwani kipenyo cha kugeuza meli za ukubwa huo sehemu hiyo hakitoshi, mita 440 tu badala ya mita 600 ambazo kuzipata ni lazima tumege mita 160 za ardhi ya Jeshi upande wa pili wa Bandari.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, gharama za kuondoa mabomba ya mafuta chini ya bahari na kuyahamishia sehemu nyingine pamoja na kituo chake cha KOJ *ili kuhusu* dragging *ambayo ni lazima ifanyike kuweza kuhudumia meli kubwa zenye kina za mita 12.04 haikuzingatiwa kwenye gharama ya dola za Marekani milioni 523. Vile vile kwa kuzingatia taratibu za kiusalama katika Bandari na kwa watumiaji wa bandari huduma kama hiyo ya* KOJ *kuwa katikati ya magati ya bandari haiashirii mazingira salama. Hivyo, kwa kufumbia macho gharama hizo bayana kampuni hizi mbili hazina nia njema ya kufanya biashara ya kiungwana.*

(3) *Mchakato wa ujenzi wa gati Na. 13 na Na.14 ulisimama mwezi Septemba 2013 baada ya kampuni hizo mbili za Kichina CCCC na CHEC kuanza kuvutana kuhusu utekelezaji wa mradi huo. CCCC Kampuni Mama ya* CHEC *ambayo ilikuwa imefingiwa (ilikuwa black-listed* na *PPRA) na hivyo kutakiwa kuwaachia CHEC mradi huo haikutaka kuiachia CHEC mradi huo hivyo ikateua Afisa wake na kumpatia vitambulisho vya CHEC na CHEC ikamteua Afisa mwingine.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mvutano huo ukapelekea tuwe na watu wawili bandarini wote wakiwa na nguvu za kisheria wakivutana, wakidai kuiwakilisha CHEC. Kitendo hicho kikasababisha Deed of Novation iliyoandaliwa na TPA *na kuridhiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutosainiwa kati ya Mamlaka na Mkandarasi mpaka sasa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu hizo, Mamlaka ya Bandari inakusudia kuachana kabisa na Kampuni za *CCCC* na *CHEC* na hivyo kuanza taratibu za kushirikisha Kampuni zingine kutekeleza mradi huu kwa masharti yanayokubalika. Tayari Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameombwa ushauri kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Benki ya Dunia kupitia *International Bank for Reconstruction and Development (IBRD)* kwa kushirikiana na *DFID* na *TMEA* zimekubali kutoa mkopo wenye masharti nafuu kwa asilimia 65 na msaada *(grant)* wa asilimia 35 kwa ajili ya uendelezaji wa Gati namba 13 na 14, uboreshwaji wa Gati namba moja mpaka saba na uongezaji wa kina cha lango la Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na nia hiyo ya Benki na Washirika wake, *TPA* imeandaa Rasimu za Nyaraka za Zabuni *(Draft Tender Documents)* za utekelezaji wa miradi hii kwa njia ya Usanifu na Ujenzi *(Design and Build)*. Nyaraka zimewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukukarabati wa bandari za Mwanza na Kigoma kazi ya kukarabati chelezo, *(slip wap)* katika bandari ya Kigoma inaendelea na inatarajiwa kukamilika Agosti 2014. Aidha, Mkandarasi wa kufanya ukarabati wa *Crane* ya kupakua na kupokea mizigo amepatikana na ataanza kazi Juni 2014 na kukamilisha ukarabati mwezi Septemba 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Bandari ya Mwanza Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa kubainisha mahitaji ya kuendeleza bandari ya Mwanza, Bukoba na Kemondo ataanza kazi Julai 2014 na kukamilisha kazi mwezi Februari 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kazi nzuri na ya ufanisi ambayo Mamlaka ya Bandari imefanya ndani ya kipindi kifupi, Mamlaka imeamua kutumia faida iliyopata kuchochea nyenzo za uchukuzi pale zilipolala ili kuijengea Mamlaka mazingira ya kufanya kazi vizuri zaidi na hivyo kuchochea uchumi wa nchi kama ifuatavyo:-

(1) Ili kuondoa msongamano wa mizigo bandarini baada ya nchi kadhaa za jirani kuonesha nia ya kupitisha mizigo mingi zaidi katika Bandari ya Dar es Salaam, *TPA* imeamua kugharamia uundaji upya wa vichwa vitatu vya treni ambavyo vitatumika kuendeshea treni maalumu za mizigo (*block trains)* kwenda Kigoma kila wiki kuhudumia wafanyabiashara wa DRC, Burundi na wa Kigoma na kuendeshea treni maalum zingine za mizigo kwenda Mwanza kila wiki kuhudumia wafanyabiashara wa Rwanda na

Uganda kwa kushushia mizigo yao Isaka na Mwanza. *TPA* inatarajia wafanyabiashara wa Kigoma na Mwanza kuchangamkia fursa hii kwa hamasa.

(2) TPA vile vile inaendelea na mazungumzo na uongozi wa *TAZARA* ili kutoa huduma za namna hiyo hiyo kwa wafanyabiashara wa Zambia, Malawi na Mbeya ambapo vichwa viwili vya treni vinatarajiwa kuundwa upya. *TPA* inatarajia wafanyabiashara wa Mbeya watachangamkia fursa hii endapo mazungumzo kati yake na *TAZARA* yakifanikiwa.

(3) Ili kuchochea uchukuzi wa majini ambapo bandari zake kwenye Maziwa hazina shughuli za kutosha kutokana na uhaba wa meli, *TPA* inaanza mkakati wa kununua meli za abiria na mizigo kwa awamu katika Maziwa yote makubwa matatu kwa njia ya ubia. Kwa kuzingatia ratiba ya Serikali ya miradi ya utengenezaji wa meli mpya ambayo inaanzia Ziwa Victoria na Tanganyika mwaka ujao wa fedha. *TPA* itaanza mradi wake wa kwanza mwaka wa fedha wa 2014/2015 katika Ziwa Nyasa ambako usafiri wa majini ni wa mashaka. Mamlaka itanunua meli yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 100 za mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeendelea kusajili ndege nchini kulingana na masharti ya usajili ambapo hadi 2014 ndege 23 zilisajiliwa kwa mara ya kwanza hapa nchini. Vile vile viwanja vya Ndege vya Mwanza, Musoma, Bukoba, Kigoma, Tabora, Arusha, Tanga, Lindi Mtwara, Iringa, Songea, Nachingwea na Kilwa Masoko vilikaguliwa na kupewa leseni ya uendeshaji. Lengo la utoaji wa ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Kitaifa na Kimataifa za uendeshaji wa viwanja vya Ndege zinazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ya kuanzisha Mfuko Maalum kwa ajili ya kufadhili mafunzo ya Urubani na Uhandisi wa Ndege imeendelea kutekelezwa. Katika mwaka wa 2013/2014, Mfuko ulianza kutumika kufadhili wanafunzi watano katika mafunzo ya Urubani, katika mwaka 2014/2015 wanafunzi 10 watafadhiliwa kupitia Mfuko huu. Pamoja na kufadhili mafunzo haya, Mfuko umekabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kuweza kupeleka wanafunzi wengi zaidi mafunzoni. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri wa Anga inaendelea kutafuta vyanzo vingine vya mapato ili kutunisha fedha za Mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limejitokeza tatizo kubwa la uhaba wa ajira kwa marubani vijana wetu ambao wamesomeshwa na wazazi wao au wadhamini wengine huku ongezeko la marubani vijana kutoka nje ya nchi likionekana. Serikali inaiagiza *TCAA* kuhakikisha kuwa utoaji wa leseni kwa Marubani kutoka nje ya nchi unaambatana na vibali vya kazi *(work pemits)* na Chama cha

Marubani kishirikishwe katika mchakato wa kutoa vibali hivyo ili kuleta uwiano wa marubani wa ndani na nje wanaofanya kazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *TCAA* isimamie kikamilifu utekelezaji wa Kanuni za uendeshaji ndege (*Civil Aviation Operation of Aircraft Regulation)* za mwaka 2012 ili idadi ya marubani katika ndege wakati wowote isiwe chini ya mwongozo wa aina ya ndege husika *(aircraft flight manual)* na cheti kinachoruhusu ndege kuruka *(Certificate of Airworthiness)* kinachotambuliwa na *TCAA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi iliongezeka kutoka abiria 2,010,240 mwaka 2012/2013 hadi kufikia abiria 2,251,469 mwezi Aprili, 2014. Hii ni sawa na ongezeko la abiria kwa asilimia 12. Aidha, abiria wanaosafiri ndani ya nchi waliongezeka sana kutoka abiria 2,420,922 katika mwaka 2012/2013 hadi kufikia abiria 2,808,270 mwezi Aprili, 2014, sawa na ongezeko la asilimia 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya ongezeko la abiria wa safari za ndani ya nchi ni pamoja na kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa mashirika yanayotoa huduma ya usafiri wa anga, kufunguliwa kwa viwanja vipya kama Songwe, kukarabatiwa kwa viwanja vya Kigoma, Tabora na Arusha pamoja na kukua kwa utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, idadi ya abiria wanaotumia usafiri huu inatarajiwa kupanda kufikia milioni 5.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha usalama wa usafiri wa anga, Wizara imetenga shilingi bilioni 11.14 kwa ajili ya kununua *radar* mbili za kuongozea ndege za kiraia. Maelezo ya kina kuhusu udhibiti wa usafiri wa anga yapo ukurasa wa 62 mpaka ukurasa wa 73 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za Viwanja vya Ndege, ujenzi wa jengo la tatu la abiria, *Terminal Three* katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere umeanza rasmi Januari 2014 baada ya kukamilika kwa kazi ya kufanya usanifu wa kina. Aidha, tarehe 24 Aprili, Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete aliweka jiwe la msingi kuashiria kuanza kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ambao ni mkubwa katika historia ya usafiri wa anga nchini unatekelezwa kwa awamu mbili, awamu ya kwanza itahusu ujenzi wa jengo lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni 3.5 kwa mwaka kwa gharama ya shilingi bilioni 293. Awamu hii inatarajiwa kukamilika Oktoba, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa awamu ya pili utaongeza uwezo wa jengo hadi kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka na hivyo Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Nyerere kuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 7.2 kwa mwaka. Mradi huu utakuwa na maegesho ya ndege za aina zote, ikiwemo ndege kubwa kuliko zote duniani aina ya *Air Bus 380*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanja Ndege cha Songwe katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imempata mkandarasi wa kutoa huduma ya mafuta na sasa anaendelea na maandalizi ya kuanza kutoa huduma hiyo. Aidha, kazi ya ujenzi wa maegesho ya ndege na jengo la abiria zinaendelea na zitakamilika mwezi Desemba, mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ya uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora ambavyo viliwekewa Jiwe la Msingi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikamilika Juni, 2013. Zabuni kwa ajili ya kuwapata Makandarasi na Wahandisi Washauri kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya ukarabati wa viwanja hivi chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia zilifunguliwa Mei, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za awamu ya pili zitahusisha ujenzi wa jengo la abiria, maegesho ya magari, barabara za kuingia viwanjani na upanuzi wa maegesho ya ndege, kukamilika kwa awamu ya pili kutawezesha viwanja hivyo kuwa vya kisasa na kutumika kwa saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mafia uliogharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Changamoto la Milenia ulikamilika na kufunguliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Oktoba, 2013. Aidha, katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.05 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria. Maegesho ya magari, ukarabati wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani pamoja na kituo cha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014, Bunge lako Tukufu liliidhinisha fedha kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba. Napenda kutoa taarifa kuwa kazi za ukarabati na upanuzi wa kiwanja hiki kwa kiwango cha lami zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika Septemba, 2014. Aidha, tarehe 24 Julai, 2013 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi kuashiria kuanza kwa ujenzi wa kiwanja hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa viwanja 11 vya Iringa, Kilwa Masoko, *Lake* Manyara, Moshi, Musoma, Lindi, Njombe, Songea, Singida, Bariadi Mkoani Simiyu na Tanga umeshaanza. Mhandisi Mshauri ameanza kazi hiyo Aprili, 2014 na kazi hii itakamilika Februari, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2013/2014, Bunge lako Tukufu liliidhinisha fedha kwa ajili ya kuboresha Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Kukarabati viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga pamoja na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara. Napenda kutoa taarifa kuwa:-

(1) Kazi zinazoendelea katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza ni pamoja na kuchimba eneo la kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege. Ujenzi wa nguzo za jengo la mizigo na jengo la kuongozea ndege na ujenzi wa kalvati la kutolea maji ya mvua kutoka upande mmoja wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwenda upande mwingine.

(2) Zabuni za kuwapata makandarasi wa kazi za ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Shinyanga na Sumbawanga zinataajiwa kutangazwa Juni, 2014. Aidha, taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa majengo ya abiria katika viwanja hivyo zinaendelea na

(3) Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mtwara unaendelea na unatarajiwa kukamilika Julai, 2014. Aidha, kazi ya ukarabati wa muda katika barabara ya kuruka na kutua ndege ili kuwezesha kiwanja kitumike katika kipindi hiki ilikamilika Novemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukiboresha kiwanja cha ndege cha Arusha, mchakato wa kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya marejeo ya usanifu wa miundombinu ya kiwanja pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi umeshaanza. Aidha, zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kazi ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa urefu wa mita 200 itatangazwa mwezi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kudhibiti matukio ya usafirishaji wa madawa ya kulevya kupitia viwanja vyetu. Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imepata msaada wa vifaa vya kisasa vya utambuzi wa milipuko *(Explosive Test Detectors)* kutoka Serikali ya Uingereza na Mamlaka imenunua *TAA*, mashine za kisasa za ukaguzi wa mizigo zenye uwezo wa kutambua madawa ya kulevya. Vifaa hivyo vilisimikwa katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Nyerere. Serikali inaendelea na taratibu za kufunga vifaa kama hivyo katika viwanja vya ndege vya Kilimanjaro, Mwanza, Songwe na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro. Serikali na Uholanzi zilitiliana saini ya msaada wa shilingi bilioni 34.5, sawa na *Euro* milioni kumi na tano kwa ajili ya ukarabati wa kiwanja hiki. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, njia za viungio, jengo la abiria, njia ya kuruka na kutua ndege na ujenzi wa

mfumo mpya wa majitaka. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kiasi cha shilingi bilioni 47.15 kwa ajili ya kuendelea na awamu ya pili ya ukarabati wa *KIA*. Mradi huu utakapokamilika utaongeza uwezo wa *KIA* kuhudumia ndege nyingi kwa ufanisi mkubwa na usalama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(1) Kuendeleza ujenzi wa jengo la *Terminal Three*.

(2) Kukamilisha ujenzi wa maegesho ya ndege na jengo kubwa la abiria.

(3) Kuendelea na ujenzi wa uzio wa usalama na kusimika taa na mifumo ya kuongozea ndege katika kiwanja cha ndege cha Songwe.

(4) Kuendelea na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Mwanza. Serikali imetenga shilingi bilioni 12.05 kwa ajili ya kazi hiyo na kwa kiwanja cha *Mwalimu Nyerere Terminal Three* shilingi bilioni 44 zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi.

(5) Kukamilisha ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Bukoba na kulipa fidia kwa wakazi waliobaki, shilingi bilioni 3.33 zimetengwa. Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Kigoma katika kiwango cha lami ambapo Serikali imetenga shilingi bilioni 4.05 ili kukamilisha kazi hii.

(6) Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Tabora ambapo shilingi bilioni 12.87 zimetengwa kwa kazi hii.

(7) Kuanza ukabarati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Shinyanga, kwa kiwango cha lami ambapo shilingi bilioni 12.07 zimetengwa.

(8) Kuanza ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga kwa kiwango cha lami ambapo shilingi bilioni 11.75 zimetengwa.

(9) Kufanya kazi ya usanifu wa kina wa ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Msalato katika kiwango cha lami, ambapo Serikali imetenga shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kazi hiyo.

(10) Kufanya matengenezo ya kiwanja cha ndege cha Mtwara katika mwaka 2014/2015 Serikali imetenga shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa barabara kuruka na kutua ndege.

(11) Kuendelea na utaratibu za maandalizi ya ulipaji fidia, upimaji na upatikanaji wa haki miliki ya ardhi kwa maeneo ya viwanja vipya vya ndege vya Bagamoyo; Isaka, Shinyanga; Kisumba, Rukwa; Msalato, Dodoma; Ngungungu, Manyara; Omukajunguti, Kagera; Bariadi Simiyu; na Nyamsurura, Mara.

(12) Kukamilisha ufungaji wa magenereta mapya, kuweka madaraja mapya, kupandia na kushuka abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere; na

(13) Kuboresha mitambo na mifumo ya kufuatilia mienendo ya shughuli za usalama kiwanjani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu viwanja vyote vya ndege yapo ukurasa wa 73 mpaka ukurasa wa 83 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kusaidia Kampuni ya Ndege ya Tanzania *ATCL* ili iweze kuboresha huduma zake na kujiendesha kibiashara. *ATCL* imeendelea kutoa huduma ya kusafirisha abiria katika viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Mtwara, Tabora, Kigoma na Comoro kwa kutumia ndege yake ya aina ya *Dash Eight Q Three Hundred*. Aidha, kuwasili kwa ndege ya *CRJ Two Hundred* yenye uwezo wa kubeba abiria 50 mwezi Machi, 2014 kumeimarisha na kuboresha huduma za *ATCL* na hivyo kuanzisha safari za ndege kwenda Bujumbura, Mwanza, Arusha, Songwe na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATCL* inatarajia kununua ndege nyingine mbili zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 50 kila moja kwa ajili ya kuboresha huduma za usafiri wa anga ndani ya nchi. Ujio wa ndege hizi utaimarisha utendaji na kuiongezea mapato *ATCL*. Katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga shilingi bilioni mbili ili kusaidia utendaji wa *ATCL*. Maelezo mengi kuhusu usafiri wa ndege yapo ukurasa wa 83 mpaka 87.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma za Hali ya Hewa: Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhakiki na kuratibu utoaji wa huduma za hali hewa pamoja na kutoa tahadhari dhidi ya matukio mbaya ya hali ya hewa ili kuongeza mchango wa sekta hii katika kuendeleza sekta nyingine za kiuchumi na kijamii na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara ilipanga kukamilisha malipo ya kuunda na kufunga rada ya hali ya hewa Mkoani Mwanza. Napenda kutoa taarifa kuwa kazi ya ufungaji wa rada hii imeanza na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Rada hii ni muhimu kwani itasaidia

katika shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika Ziwa Victoria na kutoa tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa ilifunga mitambo 11 kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe katika sehemu mbalimbali nchini. Aidha, Ofisi ya utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa bahari ya Hindi katika Bandari ya Zanzibar ilianzishwa na maandalizi ya kuanzisha Ofisi ya kutoa huduma za hali ya hewa katika bandari za Mtwara, Kigoma na Itungi yanatarajiwa kukamilika Julai, 2014. Mamlaka pia iliboresha *Studio* ya kuandaa taarifa za hali ya hewa iliyoko Dar es Salaam kwa kufunga vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kazi zilizotekelezwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa katika mwaka 2013/2014 ni kama ifuatavyo:-

(1) Kukamilisha ukarabati wa vituo vya hali ya hewa vya Dodoma, Tabora, Mlingamo, pamoja na Ofisi ya Hali ya Hewa iliyoko Kiwanja cha Ndege cha Mwalimu Nyerere.

(2) Kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Kituo kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa ilikamilika Machi, 2014. Aidha, kazi ya kufanywa usanifu wa michoro ya jengo hilo kwa ajili ya kuanza ujenzi inatarajiwa kukamilisha Juni, 2014.

(3) Kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika kutoa mafunzo ya Shahada ya Hali ya Hewa mwezi Oktoba, 2013 jumla ya wanafunzi 15 walichaguliwa kujiunga na kozi hiyo. Kuanzishwa kwa kozi hii kutaboresha utoaji wa huduma ya hali ya hewa na kulipunguzia Taifa gharama za kusomesha wanafunzi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014/2015, Mamlaka imetengewa jumla ya shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza vifaa vya hali ya hewa, kujenga na kukarabati vituo vya hali ya hewa, kujenga uwezo wa watumishi, kuanza ujenzi wa jengo la Utabiri wa Hali ya Hewa na kutayarisha *program* ya Taifa ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu huduma hii yako ukurasa wa 87 mpaka 90 mwa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuvihudumia vyuo vyetu vya mafunzo kwa lengo la kuviwezesha kutoa taaluma na wanataaluma wa kada mbalimbali katika sehemu za Uchukuzi na Hali ya Hewa. Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Uchukuzi ni:-

NIT, DIM, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma. Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam, Chuo cha Bahari Dar es Salaam na Chuo cha Reli Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kutoa kipaumbele katika kuhudumia vyuo hivyo ili viendelee kutoa wataalam wa Sekta ya Uchukuzi na Hali ya Hewa na kuboresha utendaji wa sekta hiyo. Maelezo ya kina kuhusu Taasisi hizo yako ukurasa wa 97 hadi ukurasa wa 105.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mtambuka; kuzingatia masuala ya jinsia. Wizara yangu imeendelea kulipa kipaumbele suala la ushirikishwaji wa wanawake katika Sekta ya Uchukuzi kwa kuzingatia itifaki na kimikataba ambayo Tanzania imeridhia. Katika kuhakikisha ushirikishwaji wa wanawake katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Uchukuzi hivi sasa tuna wanawake madereva wa treni nane. Wawili wameajiriwa *TRA* na 6 wameajiriwa *TAZARA* nitawaleta hapa Jumatatu. Marubani wanawake nane, mmoja yuko *ATCL*. Wanne *Precision Air;* mmoja *TCAA;* mmoja yuko *TGFA*. Pia mwingine ni rubani wa *Helicopter*. Pia tuna waongoza ndege wanawake 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahandisi wa mitambo ya kuongozea ndege wanawake tunao 15, wako *TCAA* na Wahandisi 14 wa fani za umeme, mitambo, ujenzi na mawasiliano wako *TAA*. Nimalizie kwa kusema pamoja na ugumu wa kazi ya udereva wa magari ya masafa marefu, nafurahi kulitaarifu Bunge hili kuwa tuna madereva wanawake watatu wa mabasi na wawili wa malori kuelekea Lubumbashi Congo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa sasa kutoa shukrani tu zangu za dhati kwa waliotoa ushirikiano katika kufanikisha malengo ya Sekta. Kutokana na muda, shukrani zangu ziko katika kitabu changu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kusema kwa namna ya pekee kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Uchukuzi Dkt. Tizeba; Katibu Mkuu, Shaaban Mwinjaka; Naibu Katibu Mkuu, Monica Mwamunyange, Wakuu wa Idara wote na Vitengo mbalimbali kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2014/2015, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya sh. 527,933,790,000/=; kati ya fedha hizo sh. 93,306,391,000/= zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 434,627,399,000/= ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha sh. 33,027,991,000/= kwa ajili ya mishahara ya watumishi na sh. 60,279,100,000/= fedha za matumizi mengine *OC*. Fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha

shilingi bilioni 273,140,000,000/= fedha za ndani na shilingi bilioni 161,487,399,000/= fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize hotuba yangu kwa kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hoja ya Wizara yangu. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya *www.mot.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja hiyo imeungwa mkono. Nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri wewe na Watendaji wako, *you are doing a good job* na mkiongezewa pesa mnaweza mkafanya mambo mengi zaidi, lakini hata hizo chache mnazopata, mnaonyesha namna mnavyozitumia kwa uangalifu na kwa weledi mkubwa sana.

Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2014/2015 ya Wizara ya Uchukuzi Kama Ilivyowasilishwa Mezani

HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI, MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE (MB), MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA KWA MWAKA 2014/2015

KIREFU/TAFSIRI YA MANENO

ATCL	Kampuni ya Ndege Tanzania
BADEA	Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi kwa Afrika
BASA	Mikataba ya Usafiri wa Anga
BRN	Programu ya Matokeo Makubwa Sasa
CATC	Chuo cha Usafiri wa Anga Dar Es Salaam
CCM	Chama cha Mapinduzi
DFID	Idara ya Serikali ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa
DMI	Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam
DRC	Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
EAC	Jumuiya ya Afrika Mashariki
HSBC	Shirika la Benki ya Hongkong na Shanghai
IBRD	Benki ya Kimataifa ya Marekebisho na Maendeleo
ICAO	Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga
ICD	Kituo cha Kupakua na Kupakia Makasha
JNIA	Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere

Km	Kilometa
LNG	Meli ya kusafirisha Gesi
Mb	Mbunge
MCC	Shirika la Changamoto za Milenia la Marekani
Mhe	Mheshimiwa
MKUKUTA	Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania
MRCC	Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji Majini
MSCL	Kampuni ya Huduma za Meli
NACTE	Baraza la Vyuo vya ufundi
NIT	Chuo cha Taifa cha Usafirishaji
OFID	Mfuko wa OPEC wa Maendeleo ya Kimataifa
OPEC	Umoja wa Nchi Zinazosafirisha Petroli
RAHCO	Kampuni Miliki ya Rasilimali za Reli
Ro Ro	Meli ya Kubeba Magari
SADC	Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika
SINOTASHIP	Kampuni ya Meli ya Tanzania na China
SUMATRA	Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini
TAA	Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania
TACAIDS	Tume ya UKIMWI Nchini
TAMISEMI	Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
TAZARA	Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia
TCAA	Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania
TGFA	Wakala wa Ndege za Serikali
TICTS	Kitengo cha Makasha Bandari ya Dar es Salaam
TIRP	Programu ya Ukarabati wa Reli ya Kati
TIRTEC	Chuo cha Reli Tabora
TMA	Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
TMEA	TradeMark East Africa
TPA	Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania
TRL	Shirika la Reli Tanzania
TTFA	Wakala wa Uwezeshaji wa Biashara
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
VVU	Virusi vya UKIMWI
WEF	Jukwaa la Kiuchumi Duniani
ZMA	Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar

Wizara ya Uchukuzi

Dira

Kuwa Wizara inayoongoza katika ukanda wa Afrika Mashariki katika utoaji wa huduma za uchukuzi na hali ya hewa zinazokidhi viwango vya Kimataifa.

Dhima

Kuwezesha kuwa na huduma na miundombinu ya uchukuzi ambazo ni salama, zinazotegemewa, zilizo na uwiano na ambazo zinakidhi mahitaji ya usafiri na uchukuzi katika kiwango bora kwa bei nafuu na zinazoendana na mikakati ya Serikali ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii zikiwa endelevu kiuchumi na kimazingira.

HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI, MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015

1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuchambua bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na kuweka mezani taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu, naomba sasa Bunge lako likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka 2014/2015.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia zawadi ya uhai na kutuwezesha kukutana tena kujadili utendaji wa Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa kwa mwaka 2013/2014 na mipango ya Sekta hizo kwa mwaka 2014/2015 kwa maendeleo ya Taifa letu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijawasilisha hoja ya Wizara yangu, kwa masikitiko makubwa naungana na wabunge wenzangu katika kutoa pole kwa viongozi wetu wakuu, Bunge lako Tukufu, wananchi wa majimbo ya Kalenga na Chalinze, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na wapendwa wetu marehemu Mhe. Dkt. William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kalenga na marehemu Mhe. Said Ramadhan Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Chalinze. Michango ya marehemu Wabunge hawa ilikuwa ya muhimu sana katika kuboresha utendaji wa shughuli za Bunge, majimbo yao na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Aidha, nawapa pole wananchi katika maeneo mbalimbali nchini wakiwemo wapiga kura wangu wa Jimbo la Kyela kwa kupatwa na adha ya mafuriko na kupotelewa na ndugu, jamaa na marafiki. *Tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hawa mahala pema peponi - Amina.*

4. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kwa namna ya pekee kabisa, kumpongeza **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuridhia kuanza kwa mchakato wa kutunga Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitendo

hicho kinadhihirisha nia na dhamira ya dhati aliyonayo Mhe. Rais kuboresha maisha ya Watanzania, kuimarisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na kuleta maendeleo ya nchi. Aidha, nawapongeza Watanzania wenzangu kwa kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao umetimiza miaka 50.

5. Aidha, ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza **Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msukumo wa pekee alioutoa katika kuanzisha na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Programu ya Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now - BRN) ambayo umechochea mabadiliko makubwa katika kufungua Ukanda wa Kati wa Uchukuzi kwa kutekeleza miradi ya reli, bandari na barabara. **Waheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na **Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nao0nawapongeza kwa uchapakazi na uongozi wao thabiti wa mfano uliotutia faraja na matumaini katika kufikia malengo ya BRN.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda vilevile kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza **Mhe. Dkt. Asha Rose Migiro (Mb)**, kwa kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Katiba na Sheria. Pongezi zangu pia nazielekeza kwa **Mhe. Godfrey William Mgimwa (Mb),** Mbunge wa Kalenga na **Mhe. Ridhiwani Jakaya Kikwete (Mb),** Mbunge wa Chalinze kwa ushindi wao wa kishindo katika chaguzi ndogo za majimbo ya Kalenga na Chalinze. Ushindi huo unadhihirisha imani kubwa waliyonayo wapiga kura wao kwao na kwa Chama cha Mapinduzi (CCM). Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Uteuzi wao ni ishara ya imani kubwa aliyonayo Mhe. Rais kwao.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** niruhusu nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa. Aidha, kwa namna ya pekee naomba kuishukuru familia yangu na wapiga kura wa Jimbo la Uchaguzi la Kyela ambao wameendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Naomba kutumia fursa hii kuwaomba Wananchi wa Kyela kuwa tuendelee kushirikiana katika kipindi hiki kigumu ili kurudisha hali ya miundombinu yetu ya kiuchumi na kijamii iliyoharibiwa na mafuriko ya hivi karibuni.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nimalizie kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Peter Joseph Serukamba (Mb)**, Mbunge wa Kigoma Mjini na Makamu Mwenyekiti wa

Kamati **Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya (Mb)**, Mbunge wa Urambo Magharibi kwa kuendelea kunipa ushirikiano mimi na viongozi wenzangu wa Wizara katika kuiongoza Wizara ya Uchukuzi. Ushirikiano na ushauri wao umesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha utendaji wa sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa. Binafsi nina imani kubwa na Kamati na naichukulia kama *think tank* ya Wizara. Ninaihakikishia Kamati hii kuwa Wizara itaendelea kutoa ushirikiano wa karibu kwa lengo la kuendeleza Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya utangulizi, napenda kutoa ufafanuzi wa kina kuhusu taarifa ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa kwa mwaka 2013/2014 na mipango ya mwaka 2014/2015.

2.0 HALI YA UTENDAJI NA MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIPANGO YA WIZARA KWA MWAKA 2013/2014 NA MALENGO YA MWAKA 2014/2015

10. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2013/2014 Wizara iliendelea kutekeleza mipango iliyojiwekea kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo 2025, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, (2011/2012 – 2015/2016), Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2013/2014, MKUKUTA, Mpango wa Matokeo Makubwa sasa (Big Results Now - BRN) ambao umelenga kufungua Ukanda wa Uchukuzi wa Kati, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, na Ahadi na Maagizo ya Serikali.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara iliidhinishiwa bajeti ya Shilingi bilioni 529.41 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 420.52 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 108.88 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha za maendeleo zinajumuisha Shilingi bilioni 252.68 fedha za ndani na Shilingi bilioni 167.84 fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2014 Wizara ilikuwa imepokea fedha za maendeleo Shilingi bilioni 201.21. Kati ya fedha zilizopokelewa, Shilingi bilioni 180.13 ni fedha za ndani sawa na asilimia 71.29 na Shilingi bilioni 21.08 ni fedha za nje kutoka Benki ya Dunia na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi kwa Afrika (BADEA) /Mfuko wa OPEC wa Maendeleo ya Kimataifa (OFID) ambazo ni sawa na asilimia 12.56.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha ni dhahiri kuwa sehemu kubwa ya utekelezaji wa Bajeti umefanywa kwa fedha za ndani. Fedha za nje hazikuweza kutolewa kwa kiwango kilichotarajiwa kwa wakati kutokana na taratibu za manunuzi kuchukua muda mrefu. Aidha, fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Terminal III-JNIA zilichelewa kupatikana kutokana na kuchelewa

kukamilisha taratibu za kimkataba kati ya Serikali na Benki ya Uholanzi (HSBC).

2.1 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MATOKEO MAKUBWA SASA (BIG RESULTS NOW – BRN)

13. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu iliteuliwa kuwa moja kati ya Wizara sita kuanza kutekeleza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (Big Results Now – BRN) kwa kipindi cha mwaka 2013/2014 hadi 2015/2016. Katika utekelezaji wa Mpango huu, Wizara ililenga kutekeleza miradi ya reli na bandari.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa bandari katika mwaka 2013/2014 niliahidi kutekeleza mradi wa kupanua na kuchimba lango la kuingilia na kutokea meli katika bandari ya Dar es Salaam. Nilibainisha kuwa Mradi huu utatekelezwa sambamba na uboreshaji wa gati namba 1-7. Baada ya kukamilika upembuzi yakinifu wa magati hayo, Mamlaka imekamilisha majadiliano na Benki ya Dunia wakishirikiana na *TradeMark East Africa* (TMEA) na *Department for International Development* (DFID) ili kupata fedha kwa ajili ya kugharamia ujenzi. Nyaraka za zabuni kwa ajili ya kujenga kwa utaratibu wa usanifu na ujenzi (Design and Build) ziliwasilishwa Benki ya Dunia mwezi Aprili, 2014 kupata idhini (No Objection) ili kazi itangazwe mwezi Juni, 2014. Mkandarasi anatarajiwa kupatikana mwezi Novemba, 2014 na kazi kuanza mwezi Desemba, 2014 na kukamilika mwezi Agosti, 2016. Aidha, zabuni kwa ajili ya kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kufanya upimaji wa aina ya udongo na miamba (geotechnical investigation) katika lango la kuingilia meli bandarini ikiwa ni maandalizi ya kuanza utekelezaji wa mradi wa kuchimba na kupanua lango na utafiti wa athari za kimazingira na kijamii (Environmental and Social Impact Assessment) zitatangazwa mwezi Juni, 2014 na kazi za upimaji kuanza mwezi Septemba, 2014 na kukamilika Januari, 2015. Kazi za uchimbaji na upanuzi wa lango zinatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2015 na kukamilika mwezi Agosti, 2016.

15. ***Mheshimiwa Spika***, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa kwa lengo la kuboresha utendaji wa Bandari ya Dar es salaam ni pamoja na: ujenzi wa jengo lenye ghorofa 35 (one stop center building) la kuwaweka pamoja wadau muhimu wanaotoa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam, ambalo hadi Mei, 2014 lilikuwa tayari na ghorofa 26 zilizojengwa na kazi inatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 2015; kuanza kwa utekelezaji wa mradi wa kuwaunganisha pamoja watoa huduma kwa njia ya mtandao (Electronic Single Window System) mwezi Aprili, 2014 na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2014; kuanza

kuweka (installation) mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao (Electronic Payment System) ifikapo mwezi Juni, 2014 na mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2014.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kupunguza msongamano bandarini, Mamlaka imepata maeneo kwa ajili ya kutumiwa katika shughuli za kibandari ikiwa ni pamoja na vituo vya kupokelea na kuhifadhia mizigo kwa muda kwa nchi jirani za DR Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Zambia. Maeneo hayo ni pamoja na eneo lenye ukubwa ekari 132 linalomilikiwa na *Jitegemee Trading Co. Ltd* lililopo katika bonde la mto Msimbazi na eneo lenye ukubwa wa ekari 39 lililopo Kiwalani linalomilikiwa na TAZARA. Mamlaka vilevile kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, inaanzisha mradi wa maegesho ya magari makubwa ya mizigo eneo la Kurasini linalomilikiwa na Manispaa ya Temeke lenye ukubwa wa ekari 7.5. Makubaliano ya mwisho ya utekelezaji wa mradi huu yanatarajia kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha. Aidha, Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua za mwisho kupata eneo la Katosho na Kibirizi mkoani Kigoma. Vilevile, taratibu za kupata maeneo mengine zinaendelea.

17. ***Mheshimiwa Spika***, utendaji wa Mamlaka ya Bandari umeendelea kuwa bora kama inavyooneshwa katika viashiria mbalimbali vya utendaji. Muda wa meli kukaa bandarini (Ship Turnround Time) umepungua kutoka wastani wa siku 6.3 mwaka 2012 hadi wastani wa siku 4.8 mwaka 2013; muda wa Makasha kukaa bandarini (Dwell time) umepungua kutoka wastani wa siku 9.6 mwaka 2012 hadi wastani wa siku 9.3 mwaka 2013. Uwezo wa bandari wa kupakua magari (Roll On Roll Off capacity) kwa kila shifti moja ya saa 8 uliongezeka na kufikia magari 671 Desemba, 2013 ikilinganishwa na magari 400 Desemba, 2012. Mwezi Februari, 2014 ulisainiwa mkataba wa wadau wote wa Bandari kuanza utaratibu wa utoaji wa huduma katika bandari ya Dar es Salaam kwa saa 24 kwa siku zote na Mamlaka ya Bandari tayari inatekeleza utaratibu huo. Benki mbili, NMB na CRDB, tayari zimehamishia huduma za kibenki ndani ya bandari na ni matarajio ya Wizara kuona benki zingine zikifanya hivyo.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015 Mamlaka ya Bandari itaendelea na utekelezaji wa miradi iliyoainishwa katika Mpango wa BRN. Miradi hiyo ni: uboreshaji wa Gati Na. 1-7, uongezaji wa kina na upanuzi wa lango la Bandari ya Dar es salaam, ujenzi wa kituo cha kuhudumia mizigo Kisarawe, mradi wa kuwaunganisha wadau pamoja kwa njia ya elektroniki, kuweka mfumo wa ukaguzi wa mizigo inayoingia na kutoka (scanning), kuboresha barabara na reli za kuingia na kutoka bandarini, kuongeza nafasi ya kuhudumia mizigo kwa kuhamisha

maghala yaliyopo Bandarini na kukamilisha ujenzi wa jengo la bandari (one stop center).

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara iliahidi hapa Bungeni kukamilisha ujenzi wa madaraja makubwa matatu ya Reli ya Kati. Madaraja mawili yapo kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe na daraja moja kati ya stesheni za Bahi na Kintinku. Napenda kutoa taarifa kuwa ujenzi wa madaraja hayo matatu umekamilika. Ujenzi wa daraja lililopo kati ya stesheni za Bahi na Kitinku ulikamilika Novemba, 2013 na ujenzi wa madaraja mawili yaliyopo km 303 na km 293 kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe ulikamilika kwa kiwango cha kuweza kupitika kuanzia Machi, 2014. Kukamilika kwa madaraja haya kumeongeza uhakika na usalama wa huduma ya usafiri wa reli ya Kati ambao kwa nyakati tofauti ulikuwa ukikwamishwa kutokana na ubovu na uchakavu wa madaraja hayo.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kushirikiana na Benki ya Dunia kugharamia mradi wa kuinua uwezo wa madaraja yaliyo chini ya tani 15 kwa ekseli ili kufikia tani 25 kwa ekseli kati ya Dar es Salaam na Isaka. Mshauri mwelekezi atakayefanya kazi ya uthamini na usanifu wa madaraja yote yaliyo katika reli ya kati ili yawe na uwezo wa kubeba mzigo wenye uzito wa tani 25 kwa ekseli amepatikana. Aidha, katika mwaka 2014/2015 ujenzi madaraja 16 kati ya madaraja 25 yaliyo katika hali mbaya kati ya stesheni za Dar es Salaam na Tabora utaanza.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa kutandika reli za ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni za Kitaraka na Malongwe urefu wa km 89 umekamilika na matengenezo ya eneo la reli kati ya Kilosa na Gulwe lililoathiriwa vibaya na mafuriko, nayo yamekamilika.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa ujenzi wa njia ya reli kati ya stesheni za Malongwe na Kitaraka nilikoelezea hivi punde, kunafanya reli zilizotandikwa zenye uzito wa ratili 80 kwa yadi kati ya Dar es Salaam na Tabora kufikia jumla ya km 527. Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na utandikaji wa reli za uzito wa ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni za Igalula na Tabora (km 37) na maeneo mbalimbali kati ya stesheni ya Dar es Salaam na Munisagara (Km 283). Faida ya kuwa na reli nzito ni pamoja na kupunguza ajali za treni, kuongeza mwendokasi na uwezo wa treni kubeba mizigo.

23. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2013/2014, nilieleza juu ya tatizo la kujaa mchanga kwenye makaravati yaliyopo kati ya stesheni za Gulwe na Godegode kila mara mvua inaponyesha. Napenda kulitaarifu Bunge

lako Tukufu kuwa, Serikali imechukua hatua zifuatazo ili kudhibiti hali hiyo:

- Ujenzi wa daraja na miundombinu mengine ya kuepusha kujaa kwa mchanga karibu na karavati lililopo Km 349/450c. Rasimu ya mkataba wa Mshauri Mwelekezi atakayefanya usanifu wa kina wa mradi huo ndani ya mwaka ujao wa fedha, umewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri;

- Kufanya usanifu na ujenzi wa mabwawa mawili makubwa ya kupunguza kasi ya maji maarufu kama "punguza". Bwawa la kwanza litajengwa sehemu ya Kimagai karibu na stesheni ya Godegode na bwawa la pili litajengwa karibu na stesheni ya Msagali kuanzia mwaka wa fedha 2014/2015: na

- JICA kwa kushirikiana na Serikali kupitia mradi wa *Tanzania Rail Intermodal Project (TIRP)* itatuma timu ya wataalamu wake mwezi Julai mwaka huu kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la uharibifu wa mara kwa mara wa miundombinu ya reli kutokana na mvua kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2013/2014, Wizara ilipanga kuanza maandalizi ya kuunda Mfumo wa Kusimamia na Kufuatilia Mizigo na Vyombo vya Uchukuzi (Cargo Tracking & Management System). Napenda kutoa taarifa kuwa, awamu ya kwanza ya usambazaji wa mfumo huu itaanza mwaka 2014/2015. Kukamilika kwa mfumo huu kutarahisisha ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu za kiutendaji kuhusu wingi wa shehena, usalama wake, mwendo wa vyombo vya uchukuzi wa shehena (pamoja na treni) na usalama wake.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu uboreshaji wa huduma za reli, Serikali imefanya maandalizi yafuatayo:

- Ununuzi wa vichwa vipya vya treni 13. Mkataba wa manunuzi ulisainiwa Aprili, 2013 na malipo yote yamefanyika. Vichwa hivyo vinatarajiwa kuanza kuwasili nchini Desemba, 2014;

- Ununuzi wa mabehewa mapya 22 ya abiria. Mkataba ulisainiwa Machi, 2013 na malipo yote yamefanyika. Mabehewa hayo yanatarajiwa kuanza kuwasili nchini mwishoni mwa Septemba, 2014;

- Ununuzi wa mabehewa 274 ya mizigo. Mkataba ulisainiwa Machi, 2013 na malipo ya awali yalikamilika Februari, 2014. Malipo ya mwisho

yanatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa Juni, 2014 na mabehewa hayo 274 yataanza kuwasili nchini Septemba, 2014;

- Ununuzi wa mabehewa 34 ya breki ulisainiwa Machi, 2013 na malipo yote yamekamilishwa. Mabehewa hayo yanatarajiwa kuanza kuwasili nchini Julai, 2014;

- Ununuzi wa mabehewa 25 ya kubebea kokoto. Malipo yote yamekamilika na mabehewa hayo yanatarajiwa kuanza kuwasili nchini Julai, 2014;

- Kujenga upya vichwa vinane vya treni. Kazi ilianza Machi, 2013 kwenye karakana yetu ya Morogoro na hadi kufikia Aprili, 2014 vichwa vitatu vilikuwa vimekamilika. Vichwa vitano vilivyobaki vinatarajiwa kukamilika kufikia Septemba, 2014.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza miradi ya reli chini ya BRN, kwa mwaka 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa bajeti ya maendeleo ya Shilingi bilioni 165.68. Hadi kufikia Aprili 2014, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi bilioni 145.08 sawa na asilimia 88 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi. Napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Serikali kwa kuweka kipaumbele katika utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya BRN.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka ujao wa fedha wa 2014/2015, Serikali imetenga shilingi bilioni 126.9 kwa ajili ya kuunda upya vichwa vya treni vingine nane; kununua mabehewa mengine mapya ya mizigo 204; kununua vichwa vingine vya treni vipya 11 na kuendelea na matengenezo ya njia ya reli ya kati yenye mtandao wa urefu wa km 2,707.

2.2 HUDUMA ZA UCHUKUZI KWA NJIA YA NCHI KAVU

2.2.1 Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Barabara

28. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarika na kutoa mchango wake katika kutekeleza shughuli za kiuchumi, kijamii na kimaendeleo. Hii inatokana na ukweli kwamba sekta hii imeendelea kuhudumia zaidi ya asilimia 90 ya mizigo yote inayosafirishwa nchini ikiwa ni pamoja na ile inayopitia katika bandari zetu.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara kwa ujumla wake zimeendelea kukabiliwa na changamoto ya

kuongezeka kwa ajali za barabarani ambazo zimesababisha vifo, ulemavu wa kudumu, majeraha makubwa, upotevu wa mali na matatizo ya kisaikolojia kwa waathirika wa ajali na wategemezi wao. Taifa pia limekuwa likipata hasara kiuchumi na kijamii kwa kupoteza nguvukazi na fedha kwa ajili ya kuhudumia majeruhi. Katika mwaka 2013, jumla ya ajali za barabarani 23,842 ziliripotiwa ikilinganishwa na ajali 23,578 zilizotokea mwaka 2012. Hili ni ongezeko la ajali za barabarani kwa asilimia 1.12.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imeendelea kuchukua hatua kadhaa ili kukabiliana na matukio ya ajali za barabarani. Hatua hizo ni pamoja na kununua vifaa maalum kwa ajili ya kupima ulevi na mwendo kasi. Vifaa hivi tayari vimekabidhiwa kwa Jeshi la Polisi. Hatua nyingine ni kusimamisha leseni za mabasi yanayohusika katika matukio ya ajali ambapo katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014, jumla ya leseni 34 za mabasi ya abiria zilisimamishwa; mabasi yote ya Kampuni zilizohusika katika ajali yalikaguliwa na mkaguzi maalumu aliyeteuliwa na Kamanda wa Taifa, Kikosi cha Usalama Barabarani ili kuthibitisha iwapo yanakidhi viwango vya kiufundi na kiusalama; madereva wa mabasi walijaribiwa upya; wamiliki wa mabasi walitakiwa kuwasilisha kwa maandishi mpango utakaotumika katika kudhibiti ajali za barabarani na kuwasilisha mpango wa matengenezo ya mabasi yao. Wizara inaendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango hiyo ili kupima matokeo na mafanikio yake.

2.2.2 Huduma za Usafiri na Uchukuzi Mikoani na Vijijini

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) katika kuboresha miundombinu na huduma za uchukuzi wa barabara nchini katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji. Ushirikiano huu umesaidia katika kuboresha huduma za uchukuzi na kuleta ushindani mkubwa miongoni mwa watoa huduma. Wasafiri wanaoishi maeneo mbalimbali ya miji mikubwa nchini wameendelea kuwa huru kuchagua aina ya usafiri wa barabara wanaoutaka kwa kuzingatia kiwango cha nauli, muda wa usafiri na ubora wa huduma.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** utoaji wa huduma za usafiri vijijini umeendelea kuwa na changamoto nyingi kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu thabiti na hivyo kusababisha gharama za usafiri kuwa kubwa. Aidha, baadhi ya mabasi yanayotoa huduma vijijini yapo katika hali duni ya ubora na mtumiaji wa huduma hiyo hana uchaguzi. Hata hivyo, Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kuruhusu aina mbalimbali za usafiri kama

vile pikipiki za magurudumu mawili na matatu, magari aina ya Noah n.k. Hatua hizo zinaenda sambamba na ukaguzi wa kushtukiza wa vyombo vyote vya usafiri, kutoa nauli elekezi, na kutoa elimu, mafunzo na ushauri kwa watumiaji na watoaji wa huduma za usafiri wa barabara.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kutambua mchango wa sekta binafsi katika kutoa huduma za uchukuzi, imeendelea kushirikiana na wasafirishaji wa abiria na mizigo kupitia vyama vyao ili kuboresha huduma za uchukuzi wa barabara. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na sekta hiyo kwa lengo la kuboresha hali ya usafiri katika ngazi zote kuanzia mikoani hadi vijijini.

2.2.3 Huduma za Usafiri Mijini

34. ***Mheshimiwa Spika,*** kumekuwepo na ushindani mkubwa wa huduma ya usafiri katika majiji na miji hapa nchini. Kwa kiasi kikubwa huduma hii imeendelea kutolewa na sekta binafsi. Ni matarajio yangu kuwa wananchi wa mijini wataendelea kupata huduma hii kwa urahisi zaidi na gharama nafuu kutokana na kuwepo kwa ushindani. Hata hivyo, utoaji wa huduma hii unakabiliwa na tatizo la msongamano wa magari hasa katika Miji mikubwa ya nchi yetu na hivyo kuwafanya wananchi kushindwa kusafiri kwa raha na usalama. Aidha, msongamano huu huhatarisha usalama wa abiria, mali zao na hata kusababisha ajali. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali kwa kushirikisha Wizara za Uchukuzi, Ujenzi na Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI iliendelea kuboresha huduma hizo kwa kukarabati barabara mbalimbali zinazopunguza msongamano, kuboresha usafiri wa abiria Jijini Dar es Salaam kwa kuanzisha usafiri wa treni na kuendelea kuhamasisha utekelezaji wa Mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT). Jitihada nyingine zilizofanyika ili kukabiliana na tatizo la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam ni kuhimiza matumizi ya mabasi makubwa kutoa huduma katikati ya Jiji, kuainisha njia za magari makubwa kupita na hasa malori kuingia mjini pamoja na muda wa malori kuingia na kutoka jijini Dar es Salaam.

2.2.4 Huduma za Usafiri wa Reli Jijini Dar es Salaam

35. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014 tulitoa taarifa kuwa huduma za usafiri wa reli katika Jiji la Dar es Salaam kati ya stesheni za Dar es Salaam hadi Ubungo Maziwa na Mwakanga hadi Kurasini zilianza kutolewa. Napenda kueleza kuwa huduma hizi zimeendelea kukua na kupendwa na wananchi. Kampuni ya Reli (TRL) ilisafirisha abiria 1,343,763 katika mwaka 2013 ikilinganishwa na abiria 230,009 waliosafirishwa katika mwaka 2012. Aidha, kwa upande wa TAZARA, abiria 1,460,506 walisafirishwa katika mwaka 2013 ikilinganishwa

na abiria 148,524 waliosafirishwa katika mwaka 2012. Wizara inaendelea na mikakati mbalimbali ya kuboresha huduma hii ukiwemo mpango wa kuvutia sekta binafsi kuwekeza kwenye usafiri wa treni Jijini.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014 nilitoa taarifa ya Wizara kuunda Kamati maalum, chini ya uenyekiti wa Naibu Waziri wa Uchukuzi kwa ajili ya kuchambua, kuainisha na kushauri mipango na mikakati ya kuboresha usafiri wa abiria Jijini Dar es Salaam. Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014, Kamati hiyo ilikamilisha kazi ya kuchambua, kuainisha na kushauri mipango na mikakati ya kuboresha na kupanua huduma ya usafiri wa treni ya abiria Jijini Dar es Salaam. Mikakati iliyoainishwa inahusu kuongeza eneo la ujenzi wa miundombinu na uboreshaji wa usafiri jijini kutoka umbali wa kilometa 20 za sasa hadi kilometa 50 ili kujumuisha wilaya za Kibaha, Kisarawe, Mkuranga na Bagamoyo. Aidha, wazabuni tisa wamejitokeza kufanya upembuzi yakinifu wa kupanua huduma ya treni ya abiria kwenda maeneo ya Kibaha, Bunju, Mbagala na Pugu, sita kati yao wamewasilisha maandiko ya kina kuhusu mradi huo. Uchambuzi wa maandiko yao unaendelea ili kumpata Mtaalamu Mwelekezi mmoja ndani ya mwaka huu wa fedha. Kuhusu uwekezaji katika usafiri wa treni Jijini Dar es Salaam kwa utaratibu wa PPP, kampuni kadhaa za ndani na nje ya nchi zimeonyesha ari ya dhati. Serikali imewafungulia milango na kuwasubiri wapige hatua ya kwanza. Wizara kwa kushirikiana na TRL na RAHCO imeamua kuanzisha kampuni tanzu ya kutoa huduma za usafiri wa reli mijini ambayo itatoa fursa kwa sekta binafsi kushiriki.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuboresha huduma ya usafiri wa treni ya abiria Jijini Dar es Salaam. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha njia ya reli na vituo vya abiria, kuweka alama na vizuizi vya usalama kwenye makutano ya barabara na reli. Katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni 2.92 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia mpya za reli Jijini Dar es Salaam zikiwemo zile za kwenda maeneo ya Pugu, Mbagala/Chamazi, Luguruni/Kibaha na Bunju/Kerege na ujenzi wa mchepuo wa njia ya reli kutoka *Ilala block post* hadi Stesheni ili kuepusha mwingiliano wa treni ya abiria kutoka Stesheni kwenda Ubungo na ile ya mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam.

2.3 Usafiri na Uchukuzi kwa Njia ya Reli

38. ***Mheshimiwa Spika,*** licha ya sekta ya reli kukabiliwa na changamoto mbalimbali, miundombinu na huduma za reli zimeendelea kuboreshwa ili ziendelee kuchangia katika pato la Taifa na kuongeza mchango wa sekta ya uchukuzi kwa kupitia njia ya reli. Mwelekeo uliopo katika sekta

ya uchukuzi ni kuhakikisha kuwa mizigo mizito na mingi inayosafirishwa umbali mrefu inatumia usafiri wa reli. Aidha, Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) zimeendelea kutoa huduma za uchukuzi wa reli, wakati Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli nchini (RAHCO) imeendelea kusimamia mali za lililokuwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), kuboresha miundombinu ya reli ya kati pamoja na kufanya maandalizi ya miradi ya ujenzi wa njia mpya za reli kwenda kwenye maeneo mengine ya kimkakati kwa ajili ya kuboresha uchumi wa jamii husika, zikiwemo nchi za jirani.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** ni kipindi kirefu sasa kumekuwa na hitaji la kufufua reli ya Tanga hadi Arusha ili kuweza kutumia zaidi fursa zilizopo kaskazini mwa nchi yetu na hivyo kuwapunguzia wananchi wa Mikoa hiyo adha ya usafiri. Kukosekana kwa huduma ya usafiri wa treni katika njia hii kumesababishwa na uchakavu wa miundombinu ya reli na uhaba wa vitendea kazi kama vichwa vya treni na mabehewa.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa mchakato wa kuwapata washauri waelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kuinua kiwango cha reli ya Tanga - Arusha (km 438) na Arusha - Musoma (km 660) kuwa katika kiwango cha Kimataifa ulikamilika. Napenda kutoa taarifa kuwa mshauri mwelekezi, Kampuni ya *COWI* kutoka Denmark alianza kazi ya usanifu wa uboreshaji wa njia ya reli ya Tanga – Arusha Septemba, 2013 kwa gharama ya shilingi bilioni 5.02 na anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo Julai, 2014. Mshauri mwelekezi, Kampuni ya *H.P. Gauff* kutoka Ujerumani ilianza kazi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli mpya ya Arusha - Musoma Septemba, 2013 kwa gharama ya shilingi bilioni 5.7. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Septemba, 2014. Hii ni hatua muhimu katika kuelekea kwenye ukarabati na ujenzi wa reli hizo. Aidha, katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni 7.55 kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kufanya usanifu wa ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha; kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa reli mpya kati ya Arusha – Musoma pamoja na matawi ya kwenda Engaruka na Minjingu; kukarabati njia ya reli ya Tanga hadi Arusha na kufanya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha reli itakayounganisha reli ya kati na ile ya kaskazini (yaani Tanga-Arusha), kutokea stesheni ya Ruvu Junction hadi Mruazi kuwa katika kiwango cha kimataifa na kuunganisha reli ya Mruazi na Bandari ya Mbegani, Bagamoyo.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya mwaka 2013/2014, nilieleza juu ya hatua ambazo RAHCO na Mkoa wa Tanga wamefikia katika kukamilisha ulipaji fidia kwa wakazi wa eneo la Mwambani-Tanga ili kupisha ujenzi wa sehemu ya kupanga mabehewa na kugeuzia

(marshalling yard). Napenda kutoa taarifa kuwa, jumla ya wakazi 607 kati ya 619 wamekwisha lipwa fidia ya jumla ya shilingi bilioni 4.7. Aidha, hadi Aprili, 2014 hundi 187 kati ya 188 za fidia ya makaburi zilikuwa zimelipwa. Hundi 13 zenye thamani ya shilingi milioni 231.4 bado hazijachukuliwa kutokana na zuio la mahakama au wahusika kutojitokeza.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara ilipanga kufanya ukarabati wa tuta la reli linalokatiza mto Ugala pamoja na daraja lake. Nafurahi kulitaarifu Bunge hili kuwa kazi ya ukarabati wa tuta hilo iliyofanywa na Kampuni ya *R & A Works Ltd* ilikamilika Oktoba, 2013 kwa gharama ya shilingi milioni 430.6. Aidha, kazi ya kuondoa reli nyepesi na zilizochakaa zenye uzito wa ratili 45 kwa yadi na kuweka reli zenye uzito wa ratili 56.12 kwa yadi kwa umbali uliobaki wa km 4.59 kati ya 9 zilizobainishwa kuhitaji ukarabati wa haraka kati ya sehemu ya Lumbe - Mto Ugala - Katumba ilikamilika Februari, 2014.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Tanzania imeendelea kushirikiana na Serikali za Rwanda na Burundi katika uendelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya Dar es salaam – Isaka – Keza - Kigali (Km 1,464) na Keza – Musongati (km 197) kwa kiwango cha kimataifa. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mshauri mwelekezi, Kampuni ya *CANARAIL* kutoka Canada alikamilisha kazi ya kufanya upembuzi wa kina Februari, 2014. Kazi inayoendelea ni kumtafuta *Transaction Advisor* atakeyekuwa na jukumu la kuandaa, kusimamia na kuongoza zoezi la kuwapata wawekezaji wa kujenga reli hiyo kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi na sekta ya Umma. Sambamba na juhudi hizo za pamoja za kumpata *transaction advisor* katika kutafuta wawekezaji, Serikali inaendelea na juhudi zake za kupata wawekezaji/fedha kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa kwani sehemu yetu ya mradi huu ni zaidi ya asilimia 83 ya mradi mzima ambayo ni kubwa mno kumwachia *transaction advisor* peke yake. Aidha, Machi, 2014 Serikali za Tanzania na Burundi zilitiliana saini ya Makubaliano ya Awali (MoU) ili kuendeleza mradi wa ujenzi wa reli ya kutoka Uvinza hadi Musongati.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi ya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha reli ya Isaka - Mwanza ilianza Septemba, 2013 na inatarajiwa kukamilika Julai, 2014 kwa gharama ya shilingi bilioni 4.53. Kazi hii inafanywa na mshauri mwelekezi, Kampuni ya *COWI* kutoka Denmark. Hatua hii ni muhimu katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya kuboresha njia ya reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge). Aidha, Halmashauri ya Jiji la Mwanza imetenga eneo lenye ukubwa wa hekta 148 sehemu ya Buhongwa kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya kupanga mabehewa na kugeuzia treni (marshalling yard). Mshauri mwelekezi

anayefanya tathmini ya ulipaji fidia anaendelea na kazi ambapo kiasi cha shilingi bilioni 4.2 kimetengwa katika mwaka 2014/2015 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wamiliki wa maeneo ya mradi huu. Vilevile, katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni 4 kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora – Kigoma na kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli za kutoka Uvinza hadi Musongati.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, niliahidi kuanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Songea – MbambaBay na michepuko ya kwenda Mchuchuma na Liganga. Napenda kulitaarifu Bunge hili Tukufu kuwa Mtaalam mwelekezi wa kufanya kazi hii ameshapatikana *Kampuni ya Dong Myeong* kutoka Korea Kusini kwa gharama ya Shilingi billion 7.06. Mkataba wa kutekeleza kazi hii utasainiwa wakati wowote kabla ya mwisho wa Juni, 2014 na kazi hiyo ya usanifu itakamilika baada ya miezi 12.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, niliahidi Bunge lako Tukufu kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupakua na kupakia makasha (ICD) cha Mwanza. Napenda kutoa taarifa kuwa kazi ya ujenzi wa ICD hiyo uliogharimu shilingi bilioni 3.1 ulikamilika Desemba, 2013. Mradi huu kwa sasa upo katika kipindi cha uangalizi (defect liability period) na utakabidhiwa rasmi Juni, 2014. Kituo hicho kinaendeshwa na Kampuni ya *Transpark Ltd.* Kukamilika kwa kituo hiki pamoja na kile cha Shinyanga kutasaidia kufikia malengo ya Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN) ya kuongeza mzigo unaosafirishwa katika njia ya reli ya kati na pia kupunguza muda wa mzunguko wa mabehewa. Manufaa haya yataonekana vizuri baada ya utendaji kazi wa reli ya kati kuongezeka. Katika mwaka 2014/2015, Shilingi milioni 500 zimetengwa ili kukamilisha kazi za kuongeza urefu wa njia ya reli kwa ICD ya Mwanza na kuboresha jengo la utawala katika kituo cha Shinyanga.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya reli imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali zinazochangia kudorora kwa huduma ya usafirishaji kwa njia ya reli. Changamoto hizo ni pamoja na uchakavu wa miundombinu ya reli; uchakavu na uchache wa vifaa vya uendeshaji kama vile vichwa vya treni, mabehewa, mashine na mitambo ya kufanyia kazi. Uwepo wa changamoto hizo umepelekea kuendelea kwa sekta ndogo ya reli kuwa na mchango mdogo katika soko la usafirishaji wa mizigo na abiria ikilinganishwa na njia nyingine za uchukuzi, kama barabara. Aidha, changamoto hizo pia zimechangia katika kuliongezea Taifa gharama kubwa za ukarabati wa barabara, kwani zimeendelea kubeba mizigo mikubwa na mizito. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara kupitia

RAHCO imepanga kuendelea na ukarabati wa njia ya reli na vitendea kazi vyake.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga shilingi bilioni 5 kwa ajili ya kuendelea na matengenezo ya njia ya reli kati ya Kaliua - Mpanda, kufanya usanifu wa kina wa uboreshaji wa njia ya reli kati ya Kaliua – Mpanda kuwa kiwango cha kimataifa na kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa reli mpya ya kutoka Mpanda hadi Karema. Aidha, Shilingi bilioni 3.05 zimetengwa kwa ajili ya kufanya matengenezo ya uimarishaji wa maeneo yaliyoathiriwa na mvua kati ya stesheni za Kilosa na Gulwe. Kazi zitakazohusika ni pamoja na kufanya usanifu wa kina wa ujenzi wa daraja na matengenezo ya kuzuia tatizo la mafuriko na uharibifu wa miundombinu ya reli kati ya stesheni za Godegode na Gulwe.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za uchukuzi kwa njia ya reli katika ukanda wa kati zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Reli Tanzania (TRL). Aidha, katika mwaka 2013/2014 utendaji wa TRL haukufikia kiwango kilichotarajiwa kutokana na hali ya mtandao wa miundombinu na vifaa vya uendeshaji vilivyopo. Katika mwaka 2013, TRL ilisafirisha tani 154,341 za mizigo ikilinganishwa na tani 198,024 zilizosafirishwa katika mwaka 2012. Utendaji huu ni pungufu kwa asilimia 22.1. Katika mwaka 2013, abiria 492,377 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 506,934 waliosafirishwa mwaka 2012. Idadi ya abiria ilishuka kwa asilimia 2.9.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** kushuka kwa kiwango cha usafirishaji wa mizigo na abiria kunatokana na uhaba wa mabehewa na vichwa vya treni. Aidha, upungufu wa abiria katika mwaka 2013/2014 pia unatokana na kupunguzwa kwa mabehewa ya abiria wa daraja la tatu ili kutoa nafasi ya kufunga mabehewa ya daraja la pili na la kwanza kwa abiria waendao mikoa ya Kigoma na Mwanza. Mabehewa ya daraja la kwanza na la pili hupakia watu wachache ikilinganishwa na daraja la tatu.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014, TAZARA ilisafirisha jumla ya tani za shehena 222,300 ikilinganishwa na tani za shehena 156,521 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/2013. Hili ni ongezeko la asilimia 42.5 ya utendaji. Ongezeko hilo linatokana na kupatikana kwa vichwa vipya 6 vya treni. Kiwango hiki bado ni chini ya lengo la kusafirisha tani 60,000 za mizigo kwa mwezi. Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka ilisafirisha abiria 414,304 ikilinganishwa na abiria 521,707 waliosafirishwa kati ya Julai, 2012 hadi Machi, 2013. Hii ni pungufu kwa asilimia 20. Upungufu wa abiria waliosafirishwa unatokana na uhaba wa mabehewa ya abiria na

vichwa vya treni. Aidha, miundombinu ya njia ya reli, mabehewa na vichwa vya treni viliendelea kukarabatiwa ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama wa abiria na mizigo.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa mwaka 2012/2013, nililitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kupitia Itifaki ya 15 Serikali imepata mkopo wenye masharti nafuu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China wenye thamani ya Shilingi bilioni 67.2. Itifaki hii ilikuwa ianze kutekelezwa katika mwaka 2013/2014. Napenda kutoa taarifa kuwa, kupitia Itifaki hiyo, ununuzi wa vichwa vya treni vipya 4; vichwa vya sogeza vipya 4; mabehewa ya abiria mapya 18; mashine za okoa 2, mitambo na vifaa vya usalama ulikamilika. Vifaa hivyo vinatarajiwa kuanza kuwasili nchini Desemba, 2014.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014 nilitoa taarifa kuhusu Serikali za Tanzania na Zambia kuendelea kurekebisha Sheria ya TAZARA Na. 23 ya mwaka 1975 kama ilivyohuishwa na Sheria Na. 4 ya mwaka 1995 Sura ya 143. Napenda kutoa taarifa kuwa marekebisho ya Sheria hiyo yalifanyika na Rasimu kuwasilishwa katika kila nchi mwanahisa ili kuboresha na kutoa maoni. Aidha, rasimu hii ya Sheria itawasilishwa kwenye Bodi ya TAZARA Juni, 2014 na kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri la TAZARA litakalokutana Julai, 2014 kwa ajili ya kupata idhini ya kuendelea na mchakato wa kutunga sheria. Kwa upande wa Tanzania, rasimu hiyo inashughulikiwa na timu inayojumuisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha, Wizara ya Uchukuzi na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Serikali iliamua kutenga shilingi bilioni 12 katika bajeti yake kwa ajili ya kuipunguzia TAZARA mzigo wa madeni pamoja na shilingi bilioni 8.3 kwa ajili ya kuongeza mtaji. Fedha hizo zilikusudiwa kulipa madeni ya wastaafu wa TAZARA upande wa Tanzania. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeshatoa shilingi bilioni 5.87 kwa ajili ya malipo ya wastaafu na shilingi bilioni 4.69 kwa ajili ya kuongeza mtaji.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuimarika kwa utoaji huduma wa TAZARA, katika mwaka 2013/2014, Mamlaka ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja uwekezaji hafifu unaotokana na mtaji mdogo katika maeneo ya ukarabati wa mitambo, vifaa, mashine na miundombinu ya reli; madeni makubwa yanayotokana na malimbikizo ya stahili za wafanyakazi kwenye mifuko ya hifadhi za jamii na mmomonyoko wa ardhi kwenye reli ya upande wa Tanzania.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizo, Mamlaka ilijiwekea mikakati mbalimbali ili kuboresha huduma zake. Mikakati hiyo ni pamoja na kushirikiana na Kampuni nyingine katika kuboresha utendaji (Smart Partnership). Mkakati huu utaiwezesha Mamlaka kupata rasilimali kwa ajili ya miradi ya maendeleo badala ya kuendelea kutegemea wanahisa kuipatia fedha za uwekezaji na uendeshaji. Mkakati huu pia unatafsiri Mpango Biashara wa TAZARA wa mwaka 2013/2014 – 2017/2018. Chini ya Mpango huu, katika mwaka 2014/2015, miradi mingine itakayotekelezwa ni kufanya upembuzi wa kina wa ujenzi wa matawi ya reli za Kiwira – Uyole - Itungi (km 75), Tunduma – Sumbawanga – Kigoma (Km 700) na tawi la reli kwenda bandari ya Kasanga, reli kiungo ya Mlimba - Liganga – Mchuchuma – MbambaBay (km 260); kufanya matengenezo kwenye madaraja 265 na kuweka mawasiliano yanayotumia Mkongo wa Taifa.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Serikali kupitia TAZARA itakarabati karakana ya Dar es salaam na mitambo ya kiwanda cha kuzalisha kokoto na mataruma cha Kongolo. Miradi mingine itakayotekelezwa inahusu utekelezaji wa Itifaki ya 15 ambapo mabehewa mapya ya abiria 18 yatanunuliwa; vichwa vya treni vipya vitano, vichwa vipya vinne vya sogeza, mabehewa 150 ya mizigo na mabehewa 30 ya abiria yatanunuliwa; ukarabati wa vichwa vya treni, mabehewa ya mizigo, abiria, mitambo, mashine na vifaa vya usalama.

2.4 Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, udhibiti wa huduma za usafiri wa nchi kavu na majini umeendelea kusimamiwa na kutekelezwa na SUMATRA kwa kusogeza huduma zake karibu na wananchi. Aidha, katika hotuba ya mwaka 2013/2014 niliahidi kufungua ofisi katika mikoa ya Geita, Njombe, Katavi na Simiyu. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Machi, 2014, SUMATRA ilikuwa imefungua ofisi zake katika mikoa hiyo na hivyo kufanya Mamlaka kuwa na ofisi katika mikoa yote 25 ya Tanzania Bara.

2.5 Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Reli

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, SUMATRA ilielekeza juhudi zake katika kuimarisha usalama wa huduma za usafiri wa reli. Ili kubaini vyanzo vinavyohatarisha usalama na kuchukua hatua za kuzuia vihatarishi hivyo, SUMATRA ilishiriki katika uchunguzi wa ajali kubwa nne za treni za mizigo zilizotokea:-

i. Oktoba, 2013 kati ya Stesheni za Usoke na Urambo katika reli ya Kati;

ii. Novemba, 2013 kati ya stesheni za Kisaki na Msolwa katika njia ya reli ya TAZARA;

iii. Januari, 2014 kati ya stesheni ya Mbalizi katika Reli ya TAZARA; na

iv. Februari, 2014 kati ya Stesheni ya Ngerengere na Kinonko katika njia ya Reli ya Kati.

Uchunguzi ulibaini kuwa ajali hizo zilitokana na kutofanyika kwa matengenezo stahiki ya njia ya reli na makosa ya kibinadamu. RAHCO, TRL na TAZARA waliagizwa kuzingatia ratiba za matengenezo ya njia za reli na kuzingatia sheria na kanuni ili kupunguza makosa ya kibinadamu.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** SUMATRA imeendelea kufuatilia kwa karibu uundaji upya unaoendelea wa vichwa vya treni 8 unaofanywa na Kampuni ya Reli katika karakana yake ya Morogoro. Lengo la ufuatiliaji huu ni kuhakikisha kuwa uundaji huo unaofanyika unakidhi matakwa ya kiusalama.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, SUMATRA ilifanya ukaguzi wa Reli ya TAZARA kutoka Dar es Salaam hadi Tunduma na reli ya Kati kutoka Pugu – Tanga - Moshi - Arusha. Katika ukaguzi huo ulibainika upungufu ikiwemo uchakavu wa reli na mataruma pamoja na uharibifu na wizi wa reli, mataruma ya chuma na vifungio vyake katika stesheni za Mkumbara na Hedaru. Aidha, vyuma vya madaraja mengi katika reli ya TAZARA upande wa Tanzania vilibainika kuibiwa. Huu ni uharibifu mkubwa usiovumilika kwani unakwamisha juhudi za Serikali katika kuboresha na kufufua usafiri wa reli nchini. Wizara inawaasa wananchi wa maeneo hayo kuacha kutumia vyuma vya reli kwa ajili ya biashara ya chuma chakavu au matumizi mengineyo. Kufanya hivyo ni kudumaza maendeleo ya uchumi wa nchi.

2.6 Udhibiti wa Huduma za Usafiri kwa Njia ya Barabara

62. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Hotuba ya mwaka 2013/2014 nilitoa maagizo kwa SUMATRA kuhakikisha kuwa inaandaa utaratibu stahiki utakaowezesha kutoa leseni kwa magari aina ya Noah kwa kuzingatia usalama wa abiria na mali zao. Ninapenda kuliaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, SUMATRA iliandaa utaratibu huo na sasa magari aina ya Noah yamesajiliwa na kutoa huduma za abiria katika mikoa 18 ya Tanzania Bara. Ili kuhakikisha kuwa masharti ya leseni ya usafirishaji yanaeleweka na kutekelezwa, SUMATRA ilitoa elimu na taarifa kwa Umma kuhusu utaratibu ulioandaliwa na masharti yanayoambatana na leseni hiyo.

Aidha, SUMATRA ilifanya mikutano na wadau mbalimbali ili kufafanua utaratibu ulioandaliwa. Miongoni mwa mikutano hiyo ni ule uliofanyika Mkoani Kilimanjaro tarehe 15 Julai, 2013 na Mkoani Arusha tarehe 16 Julai, 2013. Mkutano wa viongozi wa vyama vya wamiliki wa magari aina ya Noah kuhusu utaratibu wa namna ya kuridhia nauli kutoka mikoa yenye vyama vya wamiliki wa magari aina ya Noah ulifanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 10 Septemba, 2013. Naendelea kuwaomba Viongozi wa Mikoa, Wilaya, Vyama vya wamiliki wa magari aina ya Noah na madereva wa magari hayo, waendelee kuzingatia masharti waliyopewa katika leseni zao za kutoa huduma. Ukiukwaji wa masharti hayo utapelekea kufutiwa leseni zao.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyosema awali kuwa huduma za usafirishaji kwa njia ya barabara ziliendelea kuimarika, katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014 jumla ya leseni za malori 47,571 zilitolewa ikilinganishwa na leseni 44,143 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/2013. Aidha, leseni za mabasi 32,387 zilitolewa katika kipindi hiki ikilinganishwa na leseni 25,196 zilizotolewa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/2013. Utoaji wa leseni uliambatana na ukaguzi wa utendaji wa watoa huduma ya usafiri wa barabara kwa magari ya abiria na mizigo. Lengo ni kuimarisha uzingatiaji wa masharti ya leseni za usafirishaji.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia SUMATRA imeendelea kuboresha mfumo wa utoaji leseni za magari ya abiria na mizigo ikiwa ni pamoja na upangaji wa ratiba za mabasi. Lengo ni kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara ili kuondoa kero kwa wamiliki wa magari, madereva na wateja wao. Pia, Wizara inaendelea kuwasihi wamiliki wa magari, dereva mmoja mmoja, vyama vya wamiliki wa magari na madereva wa magari ya abiria na mizigo kuendelea kuzingatia masharti ya leseni zao pamoja na kuzuia ujazaji wa abiria na mizigo kupita uwezo wa ekseli moja ulioruhusiwa ili kupunguza kero mbalimbali za barabarani.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya mwaka 2013/2014, nilitoa taarifa ya SUMATRA kuendelea kuzifuatilia Halmashauri saba ambazo zilikuwa hazijasaini mkataba wa Uwakala wa kusimamia utekelezaji wa kanuni za usafiri wa pikipiki za magurudumu mawili na matatu katika maeneo ya halmashauri zao. Napenda kuliarifu Bunge hili kuwa SUMATRA sasa imekwishaingia makubaliano na Halmashauri 135. Baada ya kusaini makubaliano na Halmashauri hizo, kwa sasa SUMATRA inaendelea kusaini makubaliano na Halmashauri nyingine mpya 29. Utekelezaji wa makubaliano hayo utapunguza changamoto zitokanazo na usafiri wa abiria kwa kutumia pikipiki za magurudumu mawili na matatu ikiwa ni

pamoja na kupunguza ajali na uhalifu unaohusisha matumizi ya pikipiki hizo.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Septemba, 2012, Wizara ilitoa agizo la kuzuia abiria wa mabasi ya masafa marefu kujisitiri katika maeneo yasiyo rasmi, maarufu kama *kuchimba dawa*. Katika utekelezaji wa agizo hili, Wizara kupitia SUMATRA iliendelea kutoa elimu kwa wasafirishaji ili watumie vituo vyenye staha kwa abiria badala ya kuwataka abiria kujisitiri katika vichaka au nyuma ya magari wanayosafiri nayo kwani kufanya hivyo kuna madhara makubwa kiafya, kimazingira na kiutamaduni. Nawashukuru wamiliki wa magari ya abiria yanayosafiri masafa marefu na madereva wao kwa mwitikio huo kwani sehemu kubwa ya mabasi ya abiria yameanza kusimama katika maeneo yenye staha kwa ajili ya abiria na wateja wao kujisitiri. Katika mwaka 2013/2014, SUMATRA iliandaa na kusambaza michoro ya mifano 12 mahsusi kwa ajili ya ujenzi wa maeneo ya kuwasitiri abiria wakiwa safarini na kuisambaza michoro hiyo katika Kampuni binafsi na Halmashauri. Serikali inaendelea kutoa wito kwa Halmashauri na wananchi kwa ujumla kujitokeza ili kuwekeza katika ujenzi wa vituo vya huduma kwa abiria. Wananchi pia wanaombwa kutokukubali kuendelea kujisitiri vichakani.

2.7 Udhibiti wa Usalama wa Vyombo vya Usafiri Majini

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia SUMATRA iliendelea kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri majini, abiria na mizigo yao. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wamiliki wa vyombo vya usafiri wa abiria na mizigo waliozingatia maelekezo ya Serikali kuhusu usalama wa safari za vyombo baharini na katika maziwa yetu yote. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwakumbusha wamiliki hao kufuata sheria na taratibu zote za usalama wa vyombo vya usafiri majini. Ni muhimu kuhakikisha kuwa vyombo hivyo vinakaguliwa na SUMATRA katika muda unaotakiwa na kuzingatia umuhimu wa kutoa mafunzo kwa abiria ya jinsi ya kutumia vifaa vilivyoko ndani ya vyombo vyao kila wanapobeba abiria.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Sheria ya Usafiri wa Vyombo vya Majini ya mwaka 2003, Kanuni zake pamoja na Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa iliyoridhiwa na nchi yetu. Katika mwaka 2013/2014, SUMATRA ilifanya ukaguzi wa vyombo vya majini na kuelekeza vyombo vyenye upungufu kufanyiwa marekebisho kabla ya kupewa vyeti vya ubora ili kuendelea na utoaji wa huduma. Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014, vyombo vidogo na vikubwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Kagera, Katavi, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Tanga na Pwani

vilikaguliwa. Katika ukaguzi huo, jumla ya vyombo vidogo (chini ya uzito wa tani 50) vya usafiri majini 3,755 vilikaguliwa na vyombo vikubwa (zaidi ya tani 50) vya usafiri majini 201 vilikaguliwa. Vyombo vilivyokidhi masharti vilipewa vyeti vya ubora na kuruhusiwa kuendelea kutoa huduma.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Kituo cha kuratibu taarifa za Utafutaji na Uokoaji, ulinzi na usalama Majini (MRCC) kilichopo Dar es Salaam kiliendelea kupokea na kuratibu taarifa za utafutaji na uokoaji. Kwa upande wa Tanzania Bara kituo hicho kiliripoti ajali 13 ambazo watu 125 waliokolewa na wengine 24 kupoteza maisha. Aidha, SUMATRA na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar (Zanzibar Maritime Authority-ZMA) wameendelea kushirikiana katika kufanya ukaguzi na uhakiki wa ubora wa vyombo vya usafiri majini na kubadilishana taarifa kuhusu usalama wa vyombo vya usafiri majini bandarini na uhifadhi wa mazingira.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, SUMATRA itatekeleza shughuli mbalimbali za kiudhibiti ili kutimiza malengo yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Pili wa Mamlaka. Mipango hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha ushindani na kuhakikisha huduma za usafiri wa nchi kavu na majini zinakuwa endelevu;

(ii) Kuimarisha usalama, ulinzi na ubora wa huduma za usafiri wa nchi kavu na majini;

(iii) Kufanya mapitio ya masharti ya leseni ili kurahisisha utoaji wa huduma za usafiri wa abiria kwenda na kutoka nchi jirani;

(iv) Kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji kwa kupitia Kituo cha Utafutaji na Uokoaji Majini (MRCC) kilichopo Dar es Salaam; na

(v) Kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya usafiri ili kuhakikisha usafiri wa nchi kavu na majini unazingatia utunzaji wa mazingira.

3.0 USAFIRI NA UCHUKUZI MAJINI

3.1 Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa

71. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika maziwa makuu ya Victoria, Nyasa na Tanganyika zimeendelea kutolewa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL). Katika kipindi cha

Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 jumla ya abiria 231,866 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 122,509 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/2013. Usafirishaji huu ni ongezeko la asilimia 89.3. Ongezeko hilo lilichangiwa na kuimarika kwa utoaji huduma wa Meli za MV Clarias, MV. Liemba na MV. Songea. Aidha, licha ya umri mkubwa wa meli ya MV. Liemba, meli hiyo imeendelea kuwa tegemeo la usafiri wa majini kwa wakazi wa mwambao wa Ziwa Tanganyika. Kuongezeka kwa mahitaji ya usafiri wa abiria katika Ziwa Nyasa kulisababisha Meli ya MV.Songea kufanya vyema ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014, Kampuni ilisafirisha tani 41,234 za mizigo ikilinganishwa na tani 51,553 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/2013. Hii ni pungufu kwa asilimia 20. Sababu zilizofanya MSCL kufanya vibaya katika usafirishaji wa mizigo ni pamoja na Meli ya MV. Umoja kuwa katika matengenezo makubwa kuanzia Agosti hadi Novemba, 2013, kukosekana kwa mizigo ya kutosha na utendaji usioridhisha wa reli ya kati uliokwamisha usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam kuelekea Mwanza na Kigoma. Aidha, Sekta binafsi imeendelea kujiimarisha katika kutoa huduma kwenye maziwa hayo.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** wakati nawasilisha bajeti ya mwaka 2013/2014, niliahidi kuanza ujenzi wa meli mpya tatu katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa na ukarabati wa meli za MV. Victoria, MV. Umoja na MV. Serengeti. Pamoja na kwamba mradi huu mkubwa tayari una Mshauri Mwelekezi (*Kampuni ya OSK Shiptech* ya Denmark), umechelewa kuanza kutokana na gharama zake kupanda kwa asilimia 163 ya gharama zilizokadiriwa awali. Serikali inajadiliana na Serikali ya Denmark kuhusu ongezeko hilo la gharama na hivyo kuanza kwa ujenzi na ukarabati wa meli hizo umesogezwa hadi Juni 2015 na kukamilika mwaka 2018. Mradi utagharimu shilingi bilioni 122.087 (sawa na USD milioni 74.9). Aidha, kutokana na mahitaji makubwa ya uchukuzi katika ziwa Tanganyika, mradi huo sasa utajenga meli mpya nne, moja katika Ziwa Victoria, mbili Ziwa Tanganyika na moja Ziwa Nyasa pamoja na kukarabati meli tatu.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba yangu ya mwaka 2013/2014, nilitoa taarifa kuhusu Serikali kuomba mkopo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Korea wa kujenga meli mpya tatu; moja katika kila ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Wizara inaendelea kufuatilia mkopo huo na hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kukamilisha upembuzi yakinifu na michoro ya meli zinazotarajiwa kujengwa.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2013/2014 nilitoa taarifa kuwa wangekuja wataalamu kutoka Ujerumani kwa ajili ya kufanya tathmini ya ukarabati wa MV Liemba kwa ahadi kuwa gharama za mradi huo zingebebwa na sekta binafsi ya Ujerumani. Wafadhili wa mradi huo wameghairi na hivyo Wizara imeamua kuipumzisha meli hiyo ambayo inatimiza umri wa miaka 100 mwakani na itaegeshwa sehemu maalumu kama urithi wa Taifa (National Heritage) kama ilivyotangazwa katika Gazeti la Serikali toleo Na. 288. MV Liemba inaaminika kuwa ni meli nzee kuliko zote duniani ambayo inaendelea kutoa huduma ya uchukuzi kwa nchi nne za Burundi, Tanzania, Kongo DR na Zambia na inatarajiwa kuwa kivutio kikubwa kwa watalii hasa kutoka Ujerumani ilikojengwa.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya kukarabati meli zilizo katika Ziwa Tanganyika, Victoria na Nyasa, kulipa madeni ya watoa huduma pamoja na bima za meli hizo. Kazi nyingine zitakazofanywa ni pamoja na kuimarisha kitengo cha masoko kwa lengo la kutafuta bidhaa na kutoa elimu kwa wananchi juu ya kuzingatia usalama na umuhimu wa kuwa waangalifu katika usafiri majini. Aidha, MSCL imelenga kusafirisha abiria 329,167 na tani 144,584 za mizigo. MSCL kwa kushirikiana na TPA, wanaangalia uwezekano wa kujenga meli moja katika Ziwa Nyasa kwa ajili ya kuimarisha uchukuzi wa mizigo.

3.2 Huduma za Uchukuzi Baharini

77. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za uchukuzi wa masafa marefu baharini zimeendelea kutolewa na Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (SINOTASHIP). Katika mwaka 2013/2014, meli ya Kampuni ilifanya safari 8 badala ya safari 9 zilizopangwa. Safari hizi zilisafirisha jumla ya tani 366,000 ikilinganishwa na tani 334,000 zilizosafirishwa katika mwaka 2012/2013. Pamoja na kuvuka malengo iliyojiwekea ya kusafirisha tani 350,000, Kampuni iliendelea na juhudi za makusudi za kubana matumizi kwa kuepuka gharama zisizo za lazima.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza mapato Kampuni ya SINOTASHIP imepanua wigo wa biashara kwa kuanzisha ushirikiano na meli za *Cosco Container Shipping Line* nchini *Tanzania*. Utaratibu huu utawezesha SINOTASHIP kutoa huduma za uchukuzi wa makasha katika Bandari ya Dar es Salaam. Nawashauri Watanzania kuanza kutumia meli za Kampuni hii katika kusafirisha mizigo yao. Katika mwaka 2014/2015 Kampuni itaendelea kutekeleza yafuatayo: kutoa huduma za usafirishaji wa mizigo ambapo jumla ya tani 350,000 zinatarajiwa kusafirishwa kwa kutumia meli moja; kutafuta aina ya shehena zinazosafirishwa kwa nauli

kubwa na masafa mafupi ili kuongeza mapato ya Kampuni na kupunguza gharama kwa kubana matumizi yasiyo ya lazima; kutafuta fedha za mkopo kutoka kwenye mabenki ili kujenga meli nyingine kwa kutumia fursa ya kushuka kwa gharama za ujenzi wa meli baada ya kusitisha ujenzi wa meli ya awali na kuangalia uwezekano wa kuwa na meli ya kusafirisha Gesi (LNG).

3.3 Huduma za Bandari

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) ina wajibu wa kusimamia, kuendesha na kuendeleza bandari za mwambao na zile za maziwa. Mamlaka pia inawajibika kuhifadhi mazingira katika bandari zake na fukwe za bahari. Bandari hizi ni muhimu kwa kuwa ndizo lango kuu la biashara ya nje kwa nchi yetu na nchi jirani za Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda. Kutokana na umuhimu huo, sekta ndogo ya bandari imeendelea kuchochea ukuaji wa biashara, uchumi, maendeleo ya sekta nyingine na ustawi wa Taifa kwa kiasi kikubwa. Takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya biashara zote nchini husafirishwa nje ya nchi na kuingizwa nchini kwa kupitia bandarini.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, niliahidi kuhudumia shehena ya tani milioni 13.84 ikijumuisha tani za makasha 430,600 yatakayohudumiwa katika kitengo cha TICTS. Napenda kutoa taarifa kuwa katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014, Mamlaka ilihudumia shehena ya tani milioni 11.26 ambazo ni sawa na asimilima 81 ya lengo la mwaka. Matarajio ni kwamba kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2014 tutakuwa tumefikia lengo la tani milioni 13.84. Katika kipindi hicho kitengo cha makasha (TICTS) kilihudumia makasha 348,811 ambapo ni sawa na asilimia 76 ya lengo la mwaka.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** shehena iliyohudumiwa kwenda na kutoka nchi jirani za Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda na Uganda katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Aprili, 2014 ilikuwa ni tani milioni 3.654, ikilinganishwa na tani milioni 3.182, (sawa na ongezeko la asilimia 12.9) zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2012/13. Ongezeko la shehena hii limetokana na jitihada zinazofanywa na Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuvutia wateja toka nchi jirani kuendelea kutumia bandari zetu. Aidha, uboreshaji wa huduma, uimarishaji wa usalama wa mizigo ya wateja na utoaji huduma za bandari kwa saa 24 kila siku umesaidia kurudisha imani kwa wateja kutoka nchi hizo.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto ya ufinyu wa lango la kuingilia na kutokea katika Bandari ya Dar es Salaam, tarehe 20 Oktoba, 2013, tulikabiliwa na changamoto ya kuruhusu au la meli kubwa ya Kampuni ya *Maersk Line* yenye urefu wa meta 249 na uwezo wa kubeba kontena 4,500 kutia nanga katika bandari ya Dar es Salaam. Ufinyu wa lango la kuingilia na kina chake ulitia mashaka ingawa mtaalamu wa Mamlaka ya Bandari, Kapteni Abdul Mwingamno, akathibitisha kuwa meli hiyo ataiingiza yeye na kuitoa. Akafanya hivyo kwa ustadi mkubwa, hivyo napenda kutumia fursa hii kumpongeza nahodha huyo na watumishi wenzake wote kwa juhudi walizoonesha katika kuihudumia meli hiyo. Aidha, ujio wa meli hiyo Tanzania umeandika historia mpya ya bandari ya Dar es Salaam. Hatua hii pia imesaidia kuboresha biashara hasa baada ya nchi za Zimbabwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) kupitishia mizigo yao katika bandari ya Dar es Salaam, hivyo utumiaji wa meli hizo kubwa utasaidia kupunguza gharama na kuongeza ushawishi kwa nchi jirani kutumia bandari zetu.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya mwaka 2013/2014 nilitoa ahadi ya kutekeleza miradi mbalimbali ili kukabiliana na changamoto zilizoko katika bandari zetu. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa miradi ya bandari kama ifuatavyo:

i. Ujenzi wa gati la bandari ya Mafia ulikamilika Septemba, 2013 na kufunguliwa rasmi na Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Oktoba, 2013. Vilevile, katika mwaka 2014/2015 Mamlaka imetenga kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya kuweka kivuko cha kupanda na kushuka kwenye vyombo vidogo vidogo kwa kutumia gati lililopo na kuimarisha usalama wa abiria kwa kuziba uwazi uliopo pembezoni mwa gati. Aidha, katika mwaka 2014/2015 Mamlaka imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kukarabati na kuboresha gati la Nyamisati (Mkuranga) ili kuhudumia wasafiri wanaokwenda Mafia;

ii. Ujenzi wa gati la bandari ya Kipiri katika Ziwa Tanganyika hadi mwezi Aprili, 2014, ulikuwa umekamilika kwa zaidi ya asilimia 90 na unatarajiwa kuisha Julai, 2014. Lakini kazi za ujenzi wa magati ya Karema, Lagosa na Sibwesa (Kalya) katika Ziwa Tanganyika zimetelekezwa na Mkandarasi M/S Modspan. Aidha, kazi za ujenzi wa magati ya Kagunga katika Ziwa Tanganyika na Kiwira katika Ziwa Nyasa zilizokuwa zinatekelezwa na Mkandarasi Cannopy hazijakamilika na Mkandarasi amekimbia eneo la kazi. Serikali imeiagiza Mamlaka ya Bandari kuchukua hatua zifuatazo mapema iwezekanavyo:

- Iwanyang'anye Makandarasi hao kazi hizo na kuzitangaza upya na washindi waanze ujenzi mwezi Agosti, 2014 na kukamilisha kazi mwezi Julai, 2015 chini ya usimamzi wa karibu wa Mamlaka. Kazi hizo zimetangazwa upya tarehe 17 Aprili, 2014;

- Iwashtaki Makandarasi hao kwa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA), Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) ili kuzifutia usajili Kampuni hizo. Kazi hiyo imefanyika;

- Mamlaka iitishe dhamana walizoweka Makandarasi hao (Advance guarantee and Performance Bonds) ili kufidia sehemu ya gharama. Wakati kazi hii inafanyika, imebainika kuwa Mkandarasi M/S Cannopy aliwasilisha Mamlaka ya Bandari nyaraka za kughushi za dhamana ya malipo ya awali na hivyo kupata kazi hiyo. Mamlaka imeagizwa imfungulie Mkandarasi huyo kesi ya jinai haraka iwezekanavyo na ichunguze misingi ambayo watendaji wake walizipokea dhamana hiyo ya Benki;

Vilevile, katika mwaka 2014/2015 Mamlaka imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa gati katika bandari ya Ndumbi katika Ziwa Nyasa ili kurahisisha usafirishaji wa abiria na makaa ya mawe kutoka eneo la Ngaka.

iii. Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inaendelea na mpango wa kujenga Bandari ya Mbegani (Bagamoyo) ili kuongeza uwezo wa kuhudumia shehena inayosafirishwa kutoka ndani na nje ya nchi. Kutokana na umuhimu wa uwepo wa Bandari hii, tarehe 25 Machi, 2013, Serikali ilisaini makubaliano (Framework Agreement) na Serikali ya watu wa China, ili kampuni ya *China Merchant Holdings International Limited* (CMHI) iendeleze eneo la *Special Economic Zone* (SEZ) Bagamoyo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa bandari ya Mbegani. Desemba, 2013 Serikali ilisaini makubaliano mengine (Implementation Agreement) na Februari, 2014 Kampuni ya *China Merchants Holdings International Limited* iliwasilisha andiko la mradi. Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uchambuzi wa andiko hilo ili kuendelea na hatua zinazofuata ikiwa ni pamoja na kukabidhi eneo la mradi kwa mwekezaji huyo. Kazi ya tathmini ya mali zilizo kwenye eneo husika itakamilika Juni, 2014 na malipo ya fidia yatafanyika katika mwaka wa fedha 2014/2015.

iv. Kuendelea na maandalizi ya kuanza kwa ujenzi wa Bandari za Mwambani (Tanga) na Mtwara, ambapo zabuni zilitangazwa tarehe 27 Machi, 2014 na zitafunguliwa tarehe 26 Juni, 2014. Kazi zinatarajiwa kuanza ifikapo Septemba 2014 na kukamilika Mwishoni mwa mwaka 2016. Aidha, nyaraka za zabuni (Request for Proposal) kwa ajili ya ujenzi wa

bandari za Lindi, Kilwa na Rushungi kwa njia ya sanifu jenga endesha na rejesha (DBOT) zilitolewa tarehe 17 Aprili, 2014 na zitafunguliwa tarehe 17 Julai, 2014. Kazi zinatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2014.

v. Maandalizi ya kuanza ujenzi wa magati ya Pangani (Tanga) katika bahari ya Hindi, Ntama na Lushamba katika Ziwa Victoria na Kabwe katika Ziwa Tanganyika yanaendelea, ambapo gati la Pangani Mkandarasi amepatikana ambaye ni *M/S Alpha Logistics* na ataanza kazi mwezi Juni, 2014 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.36 na muda wa utekelezaji ni miezi 12 na hivyo kazi zitakamilika mwezi Julai, 2015. Magati ya Ntama na Lushamba utekelezaji wake utaanza mwezi Juni, 2014 na kiasi cha shilingi bilioni mbili kimetengwa kwa ajili ya kuanza utekelezaji. Kuhusu ujenzi wa gati la Kabwe utekelezaji wake utaanza mwezi Novemba, 2014 ambapo kiasi cha shilingi bilioni moja kimetengwa na Mamlaka ya Bandari kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi katika mwaka 2014/2015. Serikali inaitahadharisha Mamlaka ya Bandari kuwa makini katika kutoa kazi kwa makandarasi ili matukio ya ujenzi wa magati ya Kalema, Lagosa na Sabwesa yasijirudie tena;

vi. Mradi wa mfumo wa Usalama Bandarini (Port Intergrated Security System) upo kwenye hatua za mwisho za manunuzi kwa kushirikiana na TMEA;

vii. Ili kuboresha upatikanaji wa takwimu, kuimarisha usalama wa mizigo na bandari, Mamlaka imepanga kuanza utekelezaji wa mradi wa *electronic cargo Tracking system* ambapo zabuni za mradi zimeshaandaliwa na zinatarajiwa kutangazwa mwezi Julai, 2014.

viii. *Scanners* tatu kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo zimeagizwa na zinatarajiwa kuwasili Septemba, 2014: na

ix. Ulipaji fidia kwa wakazi wa Kibirizi ili kupisha ujenzi wa gati umeanza na utakamilika kabla ya Juni, 2014.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali za kusogeza huduma za kibandari karibu na wateja, tarehe 1 Mei, 2014, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilifungua ofisi mjini Lubumbashi nchini DR Congo. Kupitia ofisi hii, wateja walioko DRC hawatalazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam wakiwa wamebeba fedha kwa ajili ya kulipia mizigo yao. Badala yake, wataweza kulipia huduma za bandari wakiwa nchini kwao DRC na kupokea mizigo yao kule kule. Aidha katika mwaka wa fedha 2014/15, Mamlaka imepanga kufungua ofisi nyingine katika nchi za Zambia, Burundi na Rwanda. Wizara inawasiliana na Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuona uwezekano wa kuwa na watumishi wa TRA katika ofisi hizo ili kuboresha ufanisi. Vile vile ili

kuboresha huduma za forodha (Single Customs Teritory – SCT) kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mamlaka imetenga eneo la ofisi katika jengo la Ex-NASACO katika bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya wafanyakazi kutoka katika nchi za Jumuiya. Taratibu za kubadilishana taarifa kwa njia ya kielektroniki zimeshakamilika ili kuwezesha utekelezaji wa kituo kimoja cha forodha (SCT).

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014, nilieleza kuhusu uendelezaji wa kituo cha mizigo cha Kisarawe (Kisarawe Freight Station) ili kuondoa msongamano wa mizigo katika eneo la bandari. Napenda kulitaarifu Bunge hili kuwa mtaalam mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kuendeleza eneo la Kisarawe amepatikana ambaye ni *Royal Haskoning* wa Uholanzi na anatarajiwa kuanza kazi mwezi Julai, 2014 na kukamilisha mwezi Januari, 2015 kwa gharama ya Shilingi 551,825,767 (Sawa na Euro 248,000) kwa ufadhili wa Benki ya Dunia.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014 niliahidi kuanza ujenzi wa gati Na. 13 na 14. Napenda kutoa taarifa kuwa mradi huu umechelewa kuanza kutokana na sababu kubwa tatu:

(i) Gharama za ujenzi wa gati hizo mbili ya Dola za Marekani milioni 523 (karibu shilingi bilioni 837), bado ni juu mno na inayoendelea kuzua maswali mengi yasiyojibika pale gharama za miradi mingine ya aina hiyo hiyo zinapoangaliwa ambazo ni chini ya nusu ya gharama hiyo ya Dola za Marekani milioni 523;

(ii) Gharama hiyo ya ujenzi ya Dola za Marekani milioni 523 ilifikiwa ili kujenga gati mbili za kisasa (na vifaa vyake) zinazoweza kuhudumia meli kubwa hata za aina ya *Panamax* zenye urefu wa mita 294.13, upana wa mita 32.31 na kina cha mita 12.04. Lakini mkandarasi CCCC/CHEC hakuwa mkweli kwani aliendelea na mchakato wa usanifu wa awali (hydrographical and topographical surveys) huku akijua kuwa gati namba 13 na 14 zisingeweza kuhudumia meli kubwa za aina hiyo ya *Panamax* kwani kipenyo cha kugeuza meli za ukubwa huo sehemu hiyo hakitoshi, mita 440 tu badala ya 600 ambazo kuzipata lazima tumege mita 160 za ardhi ya jeshi upande wa pili wa bandari. Aidha, gharama za kundoa mabomba ya mafuta chini ya bahari na kuyahamishia sehemu nyingine (pamoja na kituo chake cha KOJ) ili kuruhusu *dredging* ambayo ni lazima ifanyike kuweza kuhudumia meli kubwa zenye kina cha mita 12.04 haikuzingatiwa kwenye gharama za Dola za Marekani milioni 523. Vilevile kwa kuzingatia taratibu za kiusalama katika Bandari na kwa watumiaji bandarini, huduma kama hiyo ya KOJ kuwa katikati ya

Magati ya Bandari haiashirii mazingira salama. Hivyo kwa kufumbia macho gharama hizo bayana, kampuni hizi mbili hazina nia njema ya kufanya biashara ya kiungwana.

(iii) Mchakato wa ujenzi wa gati namba 13 na 14 ulisimama mwezi Septemba, 2013 baada ya kampuni hizo mbili za CCCC na CHEC, kuanza kuvutana kuhusu utekelezaji wa mradi huo. CCCC, kampuni mama ya CHEC ambayo ilikuwa imefungiwa (black-listed) na PPRA na hivyo kutakiwa kuwaachia CHEC mradi, haikutaka kuiachia CHEC mradi huo, hivyo ikateua afisa wake na kumpatia vitambulisho vya CHEC na CHEC ikamteua afisa mwingine. Mvutano huo ukapelekea tuwe na watu wawili bandarini wote wakiwa na nguvu za kisheria za kuiwakilisha CHEC. Kitendo hicho kikasababisha *Deed of Novation* iliyoandaliwa na TPA na kuridhiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutosainiwa kati ya Mamlaka na Mkandarasi mpaka sasa.

Kutokana na sababu hizo, Mamlaka ya Bandari inakusudia kuachana na Kampuni za CCCC na CHEC na hivyo kuanza taratibu za kushirikisha Kampuni zingine kutekeleza mradi huu kwa masharti yanayokubalika. Tayari Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameombwa ushauri kuhusu suala hili. Aidha, Benki ya Dunia kupitia *International Bank for Reconstruction and Development (IBRD)* kwa kushirikiana na DFID na TMEA zimekubali kutoa mkopo wenye masharti nafuu (soft loan) wa asilimia 65 na msaada (grant) wa asilimia 35 kwa ajili ya uendelezaji wa Gati namba 13 na 14, uboreshwaji wa Gati namba 1 – 7 na uongezaji wa kina cha lango la Bandari ya Dar es Salaam.

Kutokana na nia hiyo ya Benki na Washirika wake, TPA imeandaa Rasimu za Nyaraka za Zabuni (Draft Tender Documents) za utekelezaji wa miradi hii kwa njia ya Usanifu na Ujenzi (design and Build). Nyaraka zimewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2014/2015.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014, nilitoa taarifa ya kuendelea kutekeleza mradi wa kukarabati bandari za Mwanza na Kigoma. Napenda kulitaarifu Bunge hili kuwa kazi ya kukarabati chelezo (slipway) katika bandari ya Kigoma inaendelea na inatarajiwa kukamilika Agosti, 2014 kwa gharama ya shilingi milioni 200. Aidha, mkandarasi wa kufanya ukarabati wa kreni ya kupakua na kupakia mizigo amepatikana na ataanza kazi Juni, 2014 kwa gharama ya shilingi milioni 592 na kukamilisha ukarabati mwezi Septemba, 2014. Kwa upande wa bandari ya Mwanza mshauri mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa kubainisha mahitaji ya kuendeleza bandari za Mwanza, Bukoba na Kemondo ameshapatikana na ataanza kazi Julai,

2014 na kukamilika mwezi Februari, 2015 kwa gharama ya Shilingi bilioni 1.32 (sawa na Euro 572,000).

88. ***Mheshimiwa Spika*** kutokana na kazi nzuri na ya ufanisi ambayo Mamlaka ya Bandari imefanya ndani ya kipindi kifupi, Mamlaka imeamua kutumia faida iliyopata kuchochea nyenzo za uchukuzi pale zilipolala ili kuijengea Mamlaka mazingira ya kufanya kazi vizuri zaidi na hivyo kuchochea uchumi wa nchi:

(i) Ili kuondoa msongamano wa mizigo bandarini baada ya nchi kadhaa za jirani kuonesha nia ya kupitisha mizigo mingi zaidi katika Bandari ya Dar es Salaam, TPA imeamua kugharamia uundaji upya wa vichwa vitatu vya treni ambavyo vitatumika kuendeshea treni maalumu za mizigo (block trains) kwenda Kigoma kila wiki kuhudumia wafanyabiashara wa DRC, Burundi na wa Kigoma na kuendeshea treni maalumu zingine za mizigo kwenda Mwanza kila wiki kuhudumia wafanyabiashara wa Rwanda kwa kushushia mizigo yao Isaka, Uganda na Mwanza. TPA inatarajia wafanyabiashara wa Kigoma na Mwanza kuchangamkia fursa hii kwa hamasa.

(ii) TPA vilevile inaendelea na mazungumzo na uongozi wa TAZARA ili kutoa huduma za namna hiyohiyo kwa wafanyabiashara wa Zambia, Malawi na Mbeya ambapo vichwa viwili vya treni vinatarajiwa kuundwa upya. TPA inatarajia wafanyabiashara wa Mbeya watachangamkia fursa hii endapo mazungumzo kati yake na TAZARA yakifanikiwa.

(iii) Ili kuchochea uchukuzi wa majini ambapo bandari zake kwenye maziwa hazina shughuli za kutosha kutokana na uchache wa meli, TPA inaanza mkakati wa kununua meli za abiria na mizigo kwa awamu katika maziwa yote makubwa matatu kwa njia ya ubia. Kwa kuzingatia ratiba ya Serikali ya miradi ya utengenezaji wa meli mpya ambayo inaanzia Ziwa Viktoria na Tanganyika mwaka ujao wa fedha, TPA itaanza mradi wake wa kwanza mwaka wa fedha wa 2014/2015 katika Ziwa Nyasa ambako usafiri wa majini ni wa mashaka. Mamlaka itanunua meli yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 100 za mizigo.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakiki ujazo wa mafuta yanayoingia nchini, katika mwaka 2014/2015 Mamlaka imepanga kununua na kufunga mita za kupima ujazo wa mafuta (flowmeters) yanayoshushwa melini kwa gharama ya shilingi bilioni 7.4 (sawa na Dola za Kimarekani milioni 4.5), mita hizo zitafungwa katika boya jipya (SPM) la kushushia mafuta lililopo eneo la Kigamboni.

4.0 USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA

4.1 Udhibiti wa Usalama wa Usafiri wa Anga

90. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha na kuboresha huduma za usafiri wa anga, Serikali imeendelea kuzingatia vigezo na kanuni za usalama wa usafiri wa anga kama inavyoshauriwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO). Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeendelea kusajili ndege nchini kulingana na masharti ya usajili ambapo hadi Aprili, 2014, ndege 23 zilisajiliwa kwa mara ya kwanza hapa nchini. Uingizwaji wa ndege hizi umeendelea kuboresha huduma za usafiri wa anga nchini kwa kiwango kikubwa.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa usafiri wa anga katika viwanja vyetu vya ndege iliimarika kutokana na kuongezeka kwa kaguzi katika viwanja hivyo. Katika mwaka 2013/2014, viwanja vya ndege vya Mwanza, Musoma, Bukoba, Kigoma, Tabora, Arusha, Tanga, Lindi, Mtwara, Iringa, Songea, Nachingwea na Kilwa Masoko vilikaguliwa na kupewa leseni za uendeshaji. Lengo la utoaji wa leseni ya uendeshaji ni kuhakikisha kuwa utekelezaji wa sheria na kanuni za kitaifa na kimataifa za uendeshaji wa viwanja vya ndege zinazingatiwa.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara iliimarisha ushirikiano uliopo na wadau mbalimbali kwa lengo la kuboresha usalama katika viwanja vya ndege nchini. Wadau hao ni pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), kampuni za ndege, vyombo vya ulinzi na usalama na Kamati ya Usalama wa Usafiri wa Anga (National Civil Aviation Security Committee). Kuimarika kwa ushirikiano huo kuliwezesha kukamatwa kwa vifaa mbalimbali visivyoruhusiwa kubebwa katika ndege, vinavyohatarisha usalama wa ndege na vile vinavyochafua sifa za viwanja vyetu ikiwa ni pamoja na madawa ya kulevya.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014, nililiarifu Bunge lako Tukufu juu ya nia ya Serikali kugombea nafasi ya kuwa mjumbe wa Baraza Kuu katika Mkutano Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO Assembly) uliofanyika Septemba, 2013. Napenda kuchukua fursa hii kulitaarifu Bunge lako kuwa Tanzania ilishiriki katika mkutano huo na kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la ICAO baada ya kupata asilimia 83.5 ya kura zilizopigwa. Tunashukuru nchi wanachama wa SADC na marafiki zetu wengine waliotuunga mkono katika kinyang'anyiro hicho.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** nia ya Serikali ya kuanzisha Mfuko maalum kwa ajili ya kufadhili mafunzo ya urubani na uhandisi wa ndege imeendelea kutekelezwa. Serikali iliamua kuanzisha mfuko huu kutokana na ukweli kuwa, nchi yetu ina uhaba wa wataalam hao pamoja na gharama kubwa zinazohitajika katika mafunzo. Katika mwaka 2013/2014, Mfuko ulianza kutumika kwa kufadhili Wanafunzi 5 katika mafunzo ya urubani. Katika mwaka 2014/2015 wanafunzi 10 watafadhiliwa kupitia Mfuko huu. Pamoja na kufadhili mafunzo hayo, Mfuko unakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti kuweza kupeleka wanafunzi wengi mafunzoni. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri wa Anga inaendelea kutafuta vyanzo vingine vya mapato ili kutunisha fedha za Mfuko huu. Aidha, limejitokeza tatizo kubwa la uhaba wa ajira kwa marubani vijana ambao wamesomeshwa na wazazi wao au wadhamini wengine huku ongezeko la marubani vijana kutoka nje ya nchi likionekana. Serikali inaiagiza TCAA kuhakikisha kuwa utoaji wa leseni kwa marubani kutoka nje ya nchi unaambatana na vibali vya kazi (work pemits) na Chama cha Marubani kishirikishwe katika mchakato wa kutoa vibali hivyo ili kuleta uwiano wa marubani wa ndani na nje wanaofanya kazi nchini. Aidha, TCAA isimamie kikamilifu utekelezaji wa Kanuni za uendeshaji ndege (Civil Aviation Operation of Aircraft Regulation) za mwaka 2012 ili idadi ya marubani katika ndege wakati wowote isiwe chini ya mwongozo wa aina ya ndege husika (aircraft flight manual) na cheti kinachoruhusu ndege kuruka (Certificate of Airworthiness) kinachotambuliwa na TCAA.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi iliongezeka kutoka abiria 2,010,240 mwaka 2012/2013 hadi kufikia abiria 2,251,469 mwezi Aprili, 2014. Hii ni sawa na ongezeko la abiria kwa asilimia 12. Aidha, abiria wanaosafiri ndani ya nchi waliongezeka kutoka abiria 2,420,922 katika mwaka 2012/2013 hadi kufikia abiria 2,808,270 mwezi Aprili, 2014, sawa na ongezeko la asilimia 16.

    Sababu ya ongezeko la abiria wa safari za ndani ya nchi ni pamoja na kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa mashirika yanayotoa huduma ya usafiri wa anga, kufunguliwa kwa viwanja vipya kama Songwe - Mbeya, kukarabatiwa kwa viwanja vya Kigoma, Tabora na Arusha pamoja na kukua kwa utalii.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, idadi ya abiria wanaotumia usafiri huu inatarajiwa kufika 5,717,505. Vilevile, idadi ya abiria wa safari za nje inategemewa kuongezeka baada ya kupitia upya na kusaini mikataba ya usafiri wa anga kati ya Tanzania na nchi mbalimbali pamoja na mashirika ya *Fastjet, Mango na Proflight* kuanza safari za kimataifa.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, safari za ndege (aircraft movements) ziliongezeka kwa asilimia 7.8 kutoka safari 242,745 mwaka 2012/2013 hadi safari 261,763 Aprili, 2014. Kati ya hizo, safari za kimataifa ziliongezeka kutoka safari 40,426 mwaka 2012/2013 hadi kufikia safari 41,235 mwezi Aprili, 2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 2. Safari za ndani ya nchi pia ziliongezeka kutoka safari 202,319 mwaka 2012/2013 hadi kufikia 220,528 mwezi Aprili, 2014. Hili ni ongezeko la asilimia 9. Kuongezeka kwa safari za ndege kwa kiasi kikubwa kulichangiwa na mashirika kama *Fast* Jet na *Tropical Air* kuanza safari katika Kiwanja cha ndege cha Songwe na viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora kufunguliwa baada ya ukarabati.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** utoaji wa huduma za kusafirisha mizigo katika viwanja mbalimbali vya ndege nchini umeendelea kukua. Hadi Aprili, 2014, mizigo ya kwenda na kutoka nchini ilifikia tani 28,460.2 kutoka tani 27,631.23 zilizosafirishwa mwaka 2012/2013. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 3. Ongezeko hili lilichangiwa na mashirika mbalimbali ya kimataifa kama *Qatar Airways* na *Turkish Airlines* kuanza kutoa huduma za kusafirisha mizigo katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014, niliahidi kuboresha mikataba ya usafiri wa anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) kati ya Tanzania na nchi mbalimbali na kuanzisha mikataba mipya ili kukidhi mahitaji ya soko na kurahisisha usafiri katika sekta hii muhimu. Mikataba iliyopitiwa upya ni ile ya Tanzania na nchi za Qatar, Saudi Arabia, Seychelles, Swaziland, Yemen, Zimbabwe na nchi za Scandinavia (Norway, Sweden na Denmark). Aidha, tulianzisha mikataba mipya na nchi za Singapore, Brazil na Iceland. Mkataba kati ya Tanzania na Singapore ulisainiwa Septemba, 2013. Mikataba kati ya Tanzania na nchi za Brazil na Iceland inasubiri kusainiwa na majadiliano ya kuanzisha mikataba mipya baina ya Tanzania na nchi ya Canada na Australia yanaendelea. Katika mwaka 2014/2015, Tanzania inatarajia kuingia mikataba mipya ya usafiri wa anga au kupitia upya mikataba iliyopo na nchi za Australia, Italia, Sudan ya Kusini na Mauritius.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili, 2014, Tanzania ilikuwa imeingia makubaliano ya BASA na nchi 52 ikilinganishwa na nchi 48 zilizokuwa zimesaini mkataba huo Aprili, 2013. Kati ya mikataba hiyo, mikataba 21 ndiyo ambayo kampuni au mashirika yake ya ndege yanatoa huduma kati ya Tanzania na nchi husika. Aidha, hadi Aprili, 2014, mashirika ya ndege ya ndani na nje yanayotoa huduma nchini kwa utaratibu wa BASA yalifikia 25 ambapo safari za ndege kati ya nchi hizo na Tanzania zilikuwa 175.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, jumla ya kampuni mpya 17 za usafiri wa ndege ziliidhinishwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga ili kutoa huduma ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, kampuni nne kati ya hizo zinatoa huduma kwa kutumia vibali vya muda mfupi. Aidha, jumla ya kampuni mpya za ndege tano zinatoa huduma ya usafiri wa anga za ratiba (scheduled air services) na zisizo za ratiba (non-scheduled air services). Hii inafanya jumla ya kampuni za ndege zinazotoa huduma nchini kufikia 55 kutoka kampuni 44 zilizokuwa zinatoa huduma katika mwaka 2012/2013. Hili ni ongezeko la asilimia 25.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na majukumu ya kudhibiti na kusimamia shughuli na taratibu za usafiri wa anga nchini, Mamlaka ya Usafiri wa Anga pia hutoa huduma za uongozaji wa ndege katika anga lote la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na mwingiliano wa majukumu ya kudhibiti na kutoa huduma, katika mwaka 2014/2015, Wizara itaangalia uwezekano wa kutenganisha majukumu ya udhibiti na utoaji huduma ya uongozaji wa ndege ili majukumu haya mawili yasikae chini ya Mamlaka moja. Tutatekeleza hili kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003. Sera za kuboresha utendaji wa taasisi za Umma pamoja na Mikataba tuliyoingia na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga. Naliomba Bunge lako Tukufu mara litakapoona hoja hiyo inawasilishwa liiunge mkono, kwani kutenganisha majukumu ya Taasisi za Umma ndiyo matakwa ya utawala bora.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na jitihada za kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa anga zinaboreshwa na kuendelea kuzingatia kanuni na taratibu za usalama wa usafiri wa anga. Hali hii inajidhihirisha kutokana na kupungua kwa ajali za ndege ambapo katika mwaka 2013/2014 kulitokea ajali mbili (2) za ndege, ikiwa ni sawa na ajali 1.9 katika kila miruko 100,000 ya ndege, ikilinganishwa na ajali 3 zilizotokea katika mwaka 2012/2013. Aidha, kulikuwa na matukio kumi (10) ya ajali, ambayo ni sawa na matukio 9.8 katika kila miruko 100,000 ya ndege. Mamlaka ya Usafiri wa Anga inaendelea kuimarisha udhibiti wa usafiri wa anga, kampuni za ndege, waendeshaji wa viwanja vya ndege na marubani ili kuendelea kupunguza ajali. Mamlaka pia inaendelea kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa ajali ili kupitia taarifa za ajali na kuzifanyia tathmini kwa lengo la kujadili mbinu mpya ya kupunguza na kudhibiti ongezeko la ajali.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014, Wizara ilitoa ahadi ya kukamilisha mifumo na ramani ya taratibu za utuaji wa ndege kwa matumizi ya marubani (Instrument Approach Procedure) kwa ajili ya viwanja vya ndege vya Arusha na Songwe. Napenda kutoa taarifa kuwa kazi ya kuandaa mfumo na ramani hizo katika uwanja wa ndege

wa Songwe ilikamilika na kampuni ya *Fastjet* ilipewa ramani hizo kwa majaribio. Matumizi rasmi ya ramani hizo yaliidhinishwa Machi, 2014. Kwa upande wa kiwanja cha ndege cha Arusha, kazi hiyo ilisimama kutokana na ukarabati unaoendelea. Baada ya kazi ya ukarabati kukamilika, kiwanja hiki kitafanyiwa upimaji upya. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga inaendelea kukamilisha mifumo ya ramani za utuaji ndege kwa ajili ya matumizi ya marubani katika viwanja vya ndege vya Zanzibar na Mwanza.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usalama wa usafiri wa anga, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imetenga shilingi bilioni 11.14 kwa ajili ya kununua rada mbili (2) za kuongozea ndege za kiraia. Hivi sasa Wizara imeanza mazungumzo na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) ili kuweza kupata rada hizo kutoka kwa watengenezaji. Vilevile, Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeanza kutumia mitambo ya satelaiti iitwayo *Automatic Dependent Surveillance – Broadcast (ADS-B)* ili kuimarisha usalama wa usafiri wa anga wakati wa uongozaji wa ndege. Aidha, Mamlaka ilisaini mkataba na kampuni ya *COMSOFT GmbH* ya Ujerumani ili kuendelea na ufungaji wa satelaiti hizo katika nusu ya nchi yetu upande wa mashariki hadi juu ya bahari ya Hindi. Awamu ya kwanza ya ufungaji wa satelaiti hizo itakayogharimu shilingi bilioni 1.995 inatarajiwa kukamilika Novemba, 2014. Zabuni kwa ajili ya kufunga satelaiti hizo katika awamu ya pili itakayohusu nusu ya pili ya nchi iliyobakia ya maeneo ya magharibi wa nchi yetu hadi juu ya Ziwa Tanganyika ilifunguliwa Aprili, 2014. Kazi ya uchambuzi wa zabuni hizo inaendelea.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya mwaka 2013/2014 Wizara litoa ahadi ya kufunga redio za mawasiliano na mitambo ya kuongoza ndege zinazotua (Non Directional Beacon - NDB) katika eneo la Iwambi, Mbeya. Napenda kueleza kuwa ufungaji wa redio na mitambo hiyo ulikamilika Machi, 2014. Kazi ya kufunga mitambo ya kuboresha mawasiliano kati ya waongoza ndege na marubani wakiwa angani (VHF area cover relay station) huko Mnyusi, Tanga ilianza Septemba, 2013 na inatarajiwa kukamilika Julai, 2014. Mtambo huu utaimarisha mawasiliano kati ya muongoza ndege na rubani akiwa angani katika kanda ya Mashariki na juu ya eneo la Bahari ya Hindi. Aidha, ufungaji wa mitambo hii umeboresha mawasiliano kati ya waongoza ndege na marubani kutoka kiwango cha asilimia 95 katika mwaka 2012/2013 hadi asilimia 100 katika mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2014/2015, kituo kama hicho kitajengwa Mafinga, Iringa ili kuboresha mawasiliano baina ya mwongoza ndege na rubani katika Ukanda wa kusini.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, nilieleza juu ya Wizara kuendelea kuboresha mtandao wa utoaji na upashanaji habari wa safari za ndege. Mradi huu ulihusu kuhama kutoka katika mfumo wa sasa wa analojia katika kuunganisha viwanja vya ndege (aeronautical Fixed Telecommunication Network–AFTN) kwenda mfumo wa digitali wa mawasiliano (ATS Message Handling System - AMHS). Napenda kutoa taarifa kuwa mkataba wa kuunganisha viwanja vya ndege katika mfumo wa digitali wa mawasiliano ulioanza Mei, 2013 unatarajiwa kukamilika Septemba, 2014 kwa gharama ya shilingi bilioni 2.21 (sawa na Euro 959,490).

108. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa katika mwaka 2014/2015 ni pamoja na kuendelea kutoa huduma za kuongoza ndege katika anga lote la Tanzania kupitia viwanja vya ndege kumi na nne (14); kukamilisha mradi wa kubainisha alama za viwanja vya ndege vya Arusha, Kigoma, Mafia, Lindi, na Tabora kwa kutumia mfumo wa satelaiti; kukamilisha kazi ya ubadilishaji wa mfumo wa mawasiliano kutoka mfumo unaotumika sasa wa kutumia vituo katika viwanja vya ndege kwenda mfumo wa digitali wa mawasiliano na kukamilisha mfumo mpya na wa kisasa wa teknolojia ya ufuatiliaji safari za ndege.

4.2 Huduma za Viwanja vya Ndege

109. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea kuboresha miundombinu na huduma za viwanja vya ndege nchini ili kuwezesha ndege kubwa na ndogo kutua na kuruka kwa usalama. Uboreshaji huo unalenga kuviwezesha viwanja vya ndege nchini kutumika kwa majira yote ya mwaka na kuvutia mashirika mengi zaidi ya ndege nchini ili kuongeza ushindani na hivyo kupunguza gharama za usafiri wa Anga.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014, nilitoa taarifa ya kuanza ujenzi wa jengo la tatu la abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA). Napenda kutoa taarifa kuwa ujenzi huo ulianza rasmi Januari, 2014 baada ya kukamilika kwa kazi ya kufanya usanifu wa kina. Aidha, tarehe 24 Aprili, 2014 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete aliweka jiwe la msingi kuashiria kuanza kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria. Mradi huu ambao ni mkubwa katika historia ya usafiri wa anga nchini unatekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza itahusu ujenzi wa jengo lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni 3.5 kwa mwaka kwa gharama ya shilingi bilioni 293. Awamu hii inatarajiwa kukamilika Oktoba, 2015.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la tatu la abiria inatarajiwa kuanza mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa awamu ya kwanza. Ujenzi wa awamu ya pili utakaogharimu shilingi bilioni 225 kutaongeza uwezo wa jengo hadi kuhudumia abiria milioni 6 kwa mwaka na hivyo JNIA kuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 7.2 kwa mwaka. Mradi huu utakuwa na maegesho ya ndege za aina zote ikiwemo ndege kubwa kuliko zote aina ya Airbus 380 (A380).

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014 nilitoa taarifa ya Kiwanja cha ndege cha Songwe kuanza kutoa huduma ya usafiri wa anga. Kiwanja hiki kimekuwa kikikabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa huduma ya mafuta ya ndege.. Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imempata mkandarasi wa kutoa huduma za mafuta na sasa anaendelea na maandalizi ya kuanza kutoa huduma hiyo. Aidha, kazi za ujenzi wa maegesho ya ndege na jengo la abiria zinaendelea na zitakamalika Desemba, 2014.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014 nilieleza juu ya kuendelea na kazi za uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Tabora na Kigoma. Napenda kulitaarifu Bunge hili kuwa awamu ya kwanza inayohusu uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Kigoma na Tabora ulikamilika Juni, 2013. Aidha, tarehe 24 Julai, 2013, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete aliweka jiwe la msingi kuashiria kukamilika kwa kazi za awamu ya kwanza ya uboreshaji na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Tabora. Zabuni kwa ajili ya kuwapata makandarasi na wahandisi washauri kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili ya ukarabati wa viwanja hivi chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia zilifunguliwa Mei, 2014. Kazi za awamu ya pili zitahusisha ujenzi wa jengo la abiria, maegesho ya magari, barabara ya kuingia kiwanjani na upanuzi wa maegesho ya ndege. Kukamilika kwa awamu ya pili kutawezesha viwanja hivyo kuwa vya kisasa na kutumika kwa saa 24.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2013/2014 niliahidi kukamilisha ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Mafia kwa kiwango cha lami. Napenda kutoa taarifa kuwa ukarabati wa kiwanja hiki uliogharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Changamoto za Milenia (MCC) ulikamilika na kufunguliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete Oktoba, 2013. Aidha, katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni 1.05 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo jipya la abiria, maegesho ya magari, ukarabati wa barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani pamoja na kituo cha umeme.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2013/2014 Bunge lako Tukufu liliidhinisha fedha kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa Kiwanja cha ndege cha Bukoba. Napenda kutoa taarifa kuwa kazi za ukarabati na upanuzi wa kiwanja hiki kwa kiwango cha lami zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika Septemba, 2014. Aidha, tarehe 24 Julai, 2013, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliweka jiwe la msingi kuashiria kuanza kwa ujenzi wa Kiwanja hiki. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara za viungio na maegesho ya ndege kwa kiwango cha lami.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya mwaka 2013/2014 niliahidi kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa viwanja kumi na moja (11) vya Iringa, Kilwa Masoko, Lake Manyara, Moshi, Musoma, Lindi, Njombe, Songea, Singida, Bariadi (Mkoani Simiyu) na Tanga. Napenda kutoa taarifa kuwa, tayari Mhandisi Mshauri ameanza kazi hiyo Aprili, 2014 na inatarajiwa kukamilika Februari, 2015.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Bunge lako Tukufu liliidhinisha fedha kwa ajili ya kuboresha kiwanja cha ndege cha Mwanza; kukarabati viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga pamoja na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mtwara. Napenda kutoa taarifa kuwa:

i. Kazi zinazoendelea katika kiwanja cha ndege cha Mwanza ni pamoja na kuchimba eneo la kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa nguzo za jengo la mizigo na jengo la kuongozea ndege, na ujenzi wa kalavati la kutolea maji ya mvua kutoka upande mmoja wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwenda upande mwingine;

ii. Makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kuwapata makandarasi wa kazi za ukarabati na upanuzi wa viwanja vya ndege vya Shinyanga na Sumbawanga kwa kiwango cha lami yamekamilika. Zabuni za kuwapata Makandarasi hao zinatarajiwa kutangazwa Juni, 2014. Aidha, taratibu za kumpata mhandisi mshauri kwa ajili ya kufanya usanifu wa majengo ya abiria katika viwanja hivyo zinaendelea; na

iii. Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mtwara unaendelea na unatarajiwa kukamilika Julai, 2014. Aidha, kazi ya ukarabati wa muda katika barabara ya kuruka na kutua ndege ili kuwezesha kiwanja kitumike katika msimu mzima wa mwaka ilikamilika Novemba, 2013.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa kiwanja cha Ndege cha Arusha kinakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege za kubeba hadi abiria 70 ili kiendelee kuchangia katika uboreshaji na ukuaji wa sekta ya utalii nchini. Katika mkakati wa kukifanya kiwanja cha ndege cha Arusha kuwa katika viwango vya kimataifa, Machi 2014, Mamlaka ilifungua zabuni ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya marejeo ya usanifu wa miundombinu ya kiwanja pamoja na kuandaa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Aidha, zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kazi ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa urefu wa mita 200 itatangazwa Juni, 2014.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha na kuboresha ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege nchini hasa baada ya kushamiri kwa matukio ya usafirishaji wa madawa ya kulevya kupitia viwanja vyetu vya ndege. Ili kufanikisha azma hiyo, katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ilipata msaada wa vifaa vya kisasa vya utambuzi wa milipuko (Explosive Trace Detectors) kutoka Serikali ya Uingereza na Mamlaka imenunua mashine za kisasa za ukaguzi wa mizigo zenye uwezo wa kutambua madawa ya kulevya (Rapscan X-ray machines 600 series). Vifaa hivyo vilisimikwa katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Serikali inaendelea na taratibu za kufunga vifaa kama hivyo katika viwanja vya ndege vya Kilimanjaro, Mwanza, Songwe na Arusha.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea kununua vifaa mbalimbali ili kuimarisha usalama wa viwanja vya ndege kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Katika mwaka 2013/2014, mashine maalum za ukaguzi wa abiria na mizigo (x–ray machines) zilinunuliwa na kufungwa katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Tanga, Mpanda na Arusha. Aidha, programu ya usalama katika viwanja vya ndege vya Songwe, Mtwara, Lindi, Nachingwea, Arusha, Manyara, Kilwa Masoko, Mafia, Iringa, Dodoma, Songea na Tanga zilikamilika. Programu hiyo pamoja na masuala mengine pia ilihusisha mafunzo ya usalama kwa wafanyakazi wa viwanja vyote vya ndege vinavyoendeshwa na Mamlaka. Lengo la programu hii ni kuinua kiwango cha usalama wa viwanja vya ndege na watumishi walioko katika viwanja hivyo kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kisiasa Duniani.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio hayo, TAA imeendelea kukabiliwa na changamoto zifuatazo:

i. Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza uboreshaji wa huduma na miundombinu ya viwanja vya ndege;

ii. Viwanja vya ndege kutumika chini ya saa 24 kutokana ukosefu wa taa za kuongoza ndege usiku na hivyo kufanya mashirika ya ndege kutotumia ndege zao kwa ufanisi; na

iii. Gharama kubwa za kulipa fidia kwa wamiliki wa maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vipya vya ndege au upanuzi wa viwanja vya ndege vilivyopo.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) pamoja na miundombinu yake katika kiwanja cha JNIA. Shilingi bilioni 44 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi;

ii. Kukamilisha ujenzi wa maegesho ya ndege na jengo kubwa la abiria, kuendelea na ujenzi wa uzio wa usalama na kusimika taa na mifumo ya kuongozea ndege katika kiwanja cha Ndege cha Songwe (Mbeya) ambapo Shilingi bilioni 9.05 zimetengwa;

iii. Kuendelea na ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Mwanza. Serikali imetenga shilingi bilioni 12.05 kwa ajili ya kazi hiyo;

iv. Kukamilisha ukarabati wa Kiwanja cha ndege cha Bukoba na kulipa fidia kwa wakazi waliobaki. Shilingi bilioni 3.33 zimetengwa;

v. Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha ndege cha Kigoma katika kiwango cha lami ambapo Serikali imetenga shilingi bilioni 4.05 ili kukamilisha kazi hii;

vi. Kuendelea na ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha ndege cha Tabora ambapo Shilingi bilioni 12.87 zimetengwa kwa kazi hii;

vii. Kuanza ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Shinyanga kwa kiwango cha lami ambapo Shilingi bilioni 12.07 zimetengwa;

viii. Kuanza ukarabati na upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Sumbawanga kwa kiwango cha lami ambapo Shilingi bilioni 11.75 zimetengwa;

ix. Kufanya kazi ya usanifu wa kina wa ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Msalato katika kiwango cha lami ambapo Serikali imetenga shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kazi hiyo.

x. Kufanya matengenezo ya kiwanja cha ndege cha Mtwara. Katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege; na

xi. Kuendelea na taratibu za upimaji na upatikanaji wa hati miliki ya ardhi kwa maeneo ya viwanja vipya vya ndege vya Bagamoyo (Pwani), Isaka (Shinyanga), Kisumba (Rukwa), Msalato (Dodoma), Ngungungu (Manyara), Omukajunguti (Kagera), Bariadi (Simiyu) na Nyansurura (Mara).

123. ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2014/2015, miradi mingine itakayotekelezwa ni pamoja na kukamilisha ufungaji wa majenereta mapya, kuweka madaraja mapya ya kupandia na kushuka abiria (aerobridges) katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere na kuboresha mitambo na mifumo ya kufuatilia mienendo ya shughuli za usalama na uendeshaji wa kiwanja (CCTV) katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Mwanza na Arusha.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia uendeshaji wa shughuli za Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ili kuhakikisha kinakuwa bora na kuchangia katika ukuaji wa biashara za maua, mbogamboga, matunda na utalii. Katika ufanikishaji wa azma hii, tarehe 19 Februari, 2014 Serikali za Tanzania na Uholanzi zilitiliana saini ya msaada wa Shilingi bilioni 34.5 (sawa na Euro milioni 15) kwa ajili ya ukarabati wa Kiwanja hiki. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, njia za viungio, jengo la abiria, njia ya kuruka na kutua ndege na ujenzi wa mfumo mpya wa maji taka. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kiasi cha Shilingi bilioni 47.15 (sawa na Euro milioni 20.5) kwa ajili ya kuendelea na awamu ya pili ya ukarabati wa KIA. Mradi huu utakapokamilika utaongeza uwezo wa KIA kuhudumia ndege nyingi, kwa ufanisi mkubwa na usalama zaidi.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi zitakazotekelezwa katika mwaka 2014/2015 ni pamoja na kuanza ukarabati na upanuzi wa maegesho ya ndege, ukarabati wa njia za viungio, ukarabati wa jengo la abiria, ukarabati wa sehemu ya njia ya kurukia na kutua ndege na ujenzi wa mfumo mpya wa maji taka; kuhakiki eneo la mipaka ya Kiwanja ili kuwaondoa wavamizi na kuendelea kujenga uwezo wa kitaasisi.

4.3 Huduma za Usafiri wa Ndege

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusaidia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili iweze kuboresha huduma zake na kujiendesha kibiashara. ATCL imeendelea kutoa huduma ya kusafirisha abiria katika viwanja vya ndege vya Dar es Salaam, Mtwara, Kigoma na Hahaya-Comoro kwa kutumia ndege yake aina ya Dash 8 Q300. Aidha, kuwasili kwa ndege ya kukodi aina ya CRJ-200 yenye uwezo wa kubeba abiria 50 mwezi Machi, 2014 ni kwa lengo la kuendelea kutekeleza mkakati madhubuti wa kuimarisha na kuboresha huduma za ATCL ikiwa ni pamoja na kuanzisha safari mpya za ndege. Vilevile, katika mwaka 2013/2014, Serikali iliendelea na mpango wake wa kusafisha mezania ya ATCL ili Kampuni hiyo iweze kukopesheka na kumiliki mali (kama vile ndege mpya) bila mashaka ya mali hizo kukamatwa kutokana na madeni na kuiwezesha ATCL kuvutia wabia wakubwa katika sekta ya anga.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hotuba ya mwaka 2013/2014, niliahidi kuanza kutoa huduma ya usafari wa ndege katika maeneo ya Afrika Kusini, Bunjumbura, Mombasa na Songwe pamoja na kurejesha safari za Mwanza, Tabora, Arusha na Zanzibar. Ninapenda kutoa taarifa kuwa, huduma za safari za ndege katika vituo vya Bujumbura, Songwe, Tabora, Mwanza, Arusha na Zanzibar zinapatikana. ATCL inatarajia kununua ndege nyingine mbili zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 50 kila moja kwa ajili ya kuboresha huduma za usafiri wa anga ndani ya nchi. Ujio wa ndege hizi utaimarisha utendaji na kuongeza mapato ya ATCL.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kujitegemea, katika mwaka 2013/2014 ATCL imeendelea kuimarisha huduma zake katika viwanja vya ndege vya JNIA na Mwanza kwa kununua mitambo na vifaa mbalimbali vya kupakia na kupakua mizigo. Hatua hii iliwezesha ATCL kuokoa shilingi milioni 73.9. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi, 2014, ATCL ilisafirisha abiria 35,001 walioingiza mapato ya shilingi bilioni 7.7 kwa kutumia ndege yake moja aina ya Dash 8 ikilinganishwa na abiria 24,530 walioingiza shilingi bilioni 2.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2012/2013 kwa kutumia ndege aina ya Boeing-737. Utendaji huu ulisababisha mapato ya kampuni kuongezeka zaidi ya mara mbili katika mwaka 2013/2014 ikilinganishwa na mwaka 2012/2013.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, niliahadi kurejesha uanachama katika Chama cha Usafirishaji wa Anga Kimataifa (IATA) na kununua ndege moja. Ili kukamilisha utekelezaji wa ahadi hii, kazi ya uhakiki wa madeni haya imekamilika. Hatua inayofuata ni ulipaji

ambao ni sehemu ya kusafisha mizania ya ATCL na hivyo kuiwezesha Kampuni kuanza kutekeleza mpango-biashara ambao utaiwezesha ATCL siyo tu kurudishiwa uanachama wa IATA, bali pia kununua ndege na kuvutia wawekezaji.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni 2 ili kuboresha utendaji wa ATCL. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na ATCL kupanua wigo wake wa kutoa huduma za uwanjani (ground handling) kwa ndege za kampuni nyingine; kufufua ukumbi wake wa kupumzika abiria ulioko JNIA (Business Class Lounge) na kuanzisha huduma za kusafirisha abiria kutoka uwanja wa ndege (Airport Shuttle Bus Services).

131. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuisimamia Wakala wa Ndege za Serikali (TGFA) ili iweze kutoa huduma za usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Aidha, Serikali kupitia Wakala iliendelea kuhakikisha kuwa ndege zake nne, yaani Fokker 28, Gulfstream 550, Fokker 50 na Piper Navajo ziko salama ili kuhudumia viongozi wakuu wa Kitaifa. Ili kuweza kumudu majukumu ya kutoa usafiri wa anga uliosalama kwa viongozi wa kitaifa, katika mwaka 2013/2014, Wakala uliajiri wafanyakazi wanne. Aidha, marubani 10 na wahandisi 16 walipatiwa mafunzo ya kuhuisha leseni zao za kuhudumia ndege na Mhandisi mmoja anatarajiwa kumaliza mafunzo nchini Ethiopia Juni, 2015.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wakala ulikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na uchakavu wa ndege na mabadiliko ya teknolojia. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wakala umeendelea kuzifanyia matengenezo ndege zake kulingana na ratiba pamoja na kuendelea kuwapeleka mafunzoni watumishi wake. Aidha, katika mwaka 2014/2015, Serikali imetenga Shilingi bilioni 9.0 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya ndege nne za Serikali, kununua vipuri mbalimbali kwa ajili ya ndege hizo na kukarabati Hanga la Wakala wa Ndege za Serikali.

5.0 HUDUMA ZA HALI YA HEWA

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhakiki na kuratibu utoaji wa huduma za hali ya hewa pamoja na kutoa tahadhari dhidi ya matukio ya hali mbaya ya hewa ili kuongeza mchango wa sekta hii katika kuendeleza sekta nyingine za kiuchumi na kijamii na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara ilipanga kukamilisha malipo ya kuunda na kufunga Rada ya hali ya hewa mkoani Mwanza. Napenda kutoa taarifa kuwa kazi ya ufungaji wa Rada hii imeanza na inatarajiwa kukamilika Juni, 2014. Rada hii ni muhimu kwani itasaidia katika shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika Ziwa Victoria na kutoa tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014 nililiarifu Bunge lako Tukufu juu ya mpango wa kununua mitambo 11 ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe. Napenda kueleza kuwa Wizara kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa ilifunga mitambo 11 ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe katika sehemu mbalimbali nchini. Aidha, ofisi ya utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Bahari ya Hindi katika Bandari ya Zanzibar ilianzishwa na maandalizi ya kuanzisha ofisi za kutoa huduma za hali ya hewa katika Bandari za Mwanza, Kigoma na Itungi yanatarajiwa kukamilika Julai, 2014. Mamlaka pia iliboresha studio ya kuandaa taarifa za hali ya hewa iliyoko Dar es Salaam kwa kufunga vifaa vya kisasa.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa katika mwaka 2013/2014 ni kama ifuatavyo:

i. Kukamilisha ukarabati wa vituo vya hali ya hewa vya Dodoma, Tabora, Mlingano pamoja na ofisi ya Hali ya Hewa iliyoko Kiwanja cha JNIA;

ii. Kununua magari sita (6) na vitendea kazi vingine kwa ajili ya vituo vya hali ya hewa vya Zanzibar, JNIA, Songwe na Mwanza;

iii. Kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha Utabiri wa Hali ya Hewa (central forecasting office) ilikamilika Machi, 2014. Aidha, kazi ya kufanya usanifu wa Michoro ya jengo hilo kwa ajili ya kuanza ujenzi inatarajiwa kukamilika Juni, 2014;

iv. Kuendelea kutoa utabiri wa hali ya hewa kupitia magazeti matano, radio 23, luninga sita na Kampuni za simu za Tigo na Vodacom na mitandao mbalimbali ya kijamii; na

v. Wizara kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imeanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Hali ya Hewa (BSc. Met) tangu Oktoba, 2013. Katika kipindi hiki jumla ya wanafunzi 15 walichaguliwa kujiunga na kozi hiyo. Kuanzishwa kwa kozi hii kutaboresha utoaji wa huduma za hali ya hewa na kulipunguzia Taifa gharama za kusomesha wanafunzi nje ya nchi.

137. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Mamlaka ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchache wa mtandao wa vituo na vifaa vya kisasa vya kupima hali ya hewa. Ili kukabiliana na changamoto hizo, katika mwaka 2014/2015, Mamlaka itatekeleza mipango mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza vifaa vya hali ya hewa, kujenga na kukarabati vituo vya hali ya hewa, kujenga uwezo wa watumishi, kuanza ujenzi wa Jengo la Utabiri wa Hali ya Hewa na kutekeleza programu ya Taifa ya kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi (Climate Change Mitigation and Adaptation Program). Mikakati mingine ni kuanza kutumia rada ya pili ya hali ya hewa iliyoko Mwanza na mifumo ya kisasa ya utoaji wa utabiri.

6.0 USHIRIKI WA KIKANDA NA KATIKA JUMUIYA MBALIMBALI

138. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano na shughuli nyingine za Jumuiya za Kikanda kama za Africa Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC), kwa lengo la kujenga uhusiano bora katika kuendeleza Sekta za Uchukuzi na Hali ya Hewa.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** Machi, 2014, nilifanya ziara ya kikazi katika nchi za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Katika ziara hiyo niliongozana na Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Viongozi wa Chama cha Mawakala wa Forodha na Uondoshaji (TAFFA), Chama cha Mawakala wa Meli Tanzania (TASAA), Umoja wa Wamiliki wa Bandari Kavu Tanzania (CIDAT), SUMATRA, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), Shirika la Reli (TRL) na Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO). Lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kuwasilisha salamu maalum za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Mheshimiwa Rais wa DRC, kuimarisha ushirikiano katika Nyanja ya Uchukuzi na kufahamu mahitaji yao ili kuyazingatia katika mipango ya kuimarisha bandari na reli.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** ujumbe huu ulikutana na makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na viongozi mbalimbali wa DRC na Burundi pamoja na wafanyabiashara wa nchi hizo. Katika vikao hivyo maazimio mbalimbali yalifikiwa ambayo Serikali za Tanzania, DRC na Burundi zinatakiwa kuyatekeleza ili kuboresha mazingira ya biashara na kukuza uchumi wa nchi zote tatu. Kwa upande wetu tunatakiwa kuboresha Bandari za Dar es Salaam na Kigoma, kuimarisha miundombinu na huduma za reli ya kati, kuimarisha huduma za uchukuzi majini katika

ziwa Tanganyika na usafiri wa anga. Wizara imeziagiza taasisi zake zinazohusika kutekeleza maazimio ya vikao hivyo.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki katika Mkutano wa Jukwaa la Kiuchumi Duniani (World Economic Forum–WEF) uliofanyika Davos Uswiss Januari, 2014. Katika Mkutano huo, Ukanda wa Kati ulichaguliwa kuwa mradi wa mfano kutafutiwa wawekezaji kwa lengo la kuboresha miundombinu na huduma za Ukanda huo. Aidha, matokeo hayo yalipelekea Tanzania kuandaa taarifa ya kina (Wider Concept Note) ya kuonyesha fursa za uwekezaji zilizoko kwenye Ukanda huo. Rasimu ya taarifa hiyo iliwasilishwa kwenye mkutano wa ngazi ya juu ya wadau wa Ukanda huo uliofanyika tarehe 15 Aprili, 2014 Jijini Dar es Salaam. Matokeo ya mkutano huo wa wadau yaliwasilishwa kwenye mkutano wa Jukwaa la Kiuchumi Afrika (WEF, 2014 Africa) uliofanyika Abuja, Nigeria tarehe 7-9 Mei, 2014. Ni matarajio ya Wizara kuwa mchakato huu utasaidia kupata wawekezaji mahiri katika Ukanda wa Kati.

6.1 Ushiriki Katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC)

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki kwenye miradi ya pamoja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki katika sekta ya Uchukuzi na Hali ya Hewa. Mkutano wa Wakuu wa nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika tarehe 29 Novemba, 2012 ulianisha miradi ya kipaumbele kwa ajili ya kuendelezwa na kutafutiwa fedha za utekelezaji. Miradi hiyo ni pamoja na ile inayohusu sekta ndogo za Reli na Bandari. Miradi hiyo imepewa kipaumbele kutokana na ukweli kwamba haijaendelezwa ipasavyo. Wakuu wa nchi waliagiza kuwa miradi hii itafutiwe fedha kutoka Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), BADEA, EU na nchi washirika kama China, Marekani na Japan.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Tanzania, miradi iliyoidhinishwa na Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kutafutiwa fedha ni pamoja na:- ukarabati wa reli ya Dar es Salaam-Tabora-Mwanza/Kigoma; Kaliua-Mpanda na tawi la reli kuelekea Karema; ujenzi wa reli mpya ya Uvinza–Musongati; ujenzi wa reli ya Dar es Salaam–Isaka-Kigali/Keza-Gitega-Musongati kwa kiwango cha kimataifa, uendelezaji wa reli ya Mtwara-Mbamba Bay na tawi la kuelekea Liganga, Mlimba na Mchuchuma. Kwa upande wa sekta ndogo ya Bandari miradi iliyoainishwa ni pamoja na uboreshaji wa bandari ya Dar es Salaam ikijumuisha ujenzi wa gati namba 13 na 14; ukarabati wa gati namba 1 – 7 pamoja gati la Ro-Ro; Ujenzi wa kituo cha mizigo Kisarawe, uendelezaji wa bandari ya Maruhubi – Zanzibar;

ujenzi wa bandari za Mwambani; Tanga na Musoma; ujenzi na uendelezaji wa magati ya Kigoma, Mwanza, Itungi na Kasanga.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kurahisisha biashara katika nchi za Afrika Mashariki, Serikali imepanga kupunguza vituo vya ukaguzi barabarani kutoka 15 vilivyopo sasa hadi vitatu (3) ifikapo mwaka 2015. Vituo hivyo vitakuwa katika maeneo ya Vigwaza, Manyoni na Nyakanazi. Katika jitihada hizo hizo, Serikali imeanzisha matumizi ya kituo kimoja (one stop centre) katika bandari ya Dar es Salaam ambapo wadau wote hufanya kazi katika jengo moja na hivyo kuongeza ufanisi katika uondoshaji wa mizigo.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania imeendelea kushiriki katika vikao vya taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa Wakala wa Ulinzi na Usalama wa Usafiri wa Anga (Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency – CASSOA) ili kukabiliana na changamoto zilizoko katika sekta ya usafiri wa anga. Katika kutekeleza wajibu wake, Desemba, 2013, Mamlaka ilikamilisha kazi ya kuandaa na kuwianisha mfumo wa mitihani ya Marubani na Wahandisi wa ndege utakaotumika katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mfumo huu utawezesha wanataaluma hawa kutambulika katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

6.2 Ushiriki Katika Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Makubaliano ya Itifaki ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa ya Nchi Wanachama wa SADC ya mwaka 1998 (The SADC Protocol on Transport, Communications and Meteorology of 1998). Aidha, nchi imeendelea kutekeleza Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Miundombinu uliopitishwa na Wakuu wa Nchi na Serikali Agosti, 2012.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mpango huo, Sekretarieti ya SADC iliandaa Mpango Kazi wa Muda Mfupi ulioainisha miradi ya uchukuzi ya kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji. Miradi ya kipaumbele iliyoainishwa kwa upande wa Tanzania ni pamoja na:

i. Kufufua huduma za Kampuni ya Reli Tanzania;

ii. Ujenzi wa reli mpya ya Isaka – Keza – Kigali – Musongoti;

iii. Ujenzi wa reli mpya ya Mtwara – Liganga – Mchuchuma – Songea – MbambaBay;

iv. Ujenzi wa kituo cha kuhudumia makasha Kisarawe;

v. Kuendeleza bandari ya Mtwara na eneo la uwekezaji;

vi. Kuboresha uwanja wa ndege wa JNIA (Terminal II na III);

vii. Kuendeleza kiwanja cha ndege Mtwara;

viii. Kuendeleza kiwanja cha ndege Kigoma; na

ix. Ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani Tanga.

Miradi hii itaendelea kutangazwa katika mikutano mbalimbali ya wawekezaji ikiwa ni pamoja na mikutano inayotarajiwa kufanyika nchini China na Brazil mwaka 2014/2015.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushiriki katika majadiliano ya uoanishaji wa viwango na mifumo ya Sekta ya Uchukuzi kwa njia ya barabara, reli, anga, majini na hali ya hewa kwa kuzingatia makubaliano ya Itifaki ya Uchukuzi, Mawasiliano na Hali ya Hewa. Aidha, nchi wanachama zinaendelea na maandalizi ya kuwa na mikakati ya pamoja ya uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi hususan miradi ya barabara, reli, viwanja vya ndege na bandari itakayowezesha kupunguza gharama za usafirishaji na pia kuunganisha nchi yetu na nchi zingine wanachama wa SADC. Lengo kuu likiwa ni kuibua fursa za uwekezaji na uchumi, kupunguza umaskini na kuleta maendeleo kwa nchi wanachama.

7.0 MAENDELEO NA MAFUNZO YA WATUMISHI

149. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2013/2014 Wizara iliendelea kuimarisha hali ya utumishi kwa lengo la kuboresha utendaji wa kazi na kuleta ufanisi. Wizara iliwapandisha vyeo watumishi 43 wa kada mbalimbali na kuwathibitisha kwenye vyeo vya uteuzi Wakurugenzi wanne, Wakurugenzi Wasaidizi tisa na Mkuu wa Kitengo mmoja. Kuhusu mafunzo, Wizara iliandaa Mpango wa Mafunzo wa miaka mitatu ambao unaendelea kutekelezwa. Hadi Machi, 2014 jumla ya Watumishi 850 wa Wizara na Taasisi zake walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi. Kati ya hao, Watumishi 600 walipatiwa mafunzo ndani ya Nchi na Watumishi 250 mafunzo nje ya Nchi. Aidha, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Wizara ilinunua vitendea kazi mbalimbali kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwaongezea watumishi ujuzi, ufanisi na tija katika utendaji kazi, katika mwaka 2014/2015, Wizara pamoja na Taasisi zake zitaendelea kugharamia mafunzo ya watumishi kulingana na upatikanaji wa fedha. Aidha, kwa kuzingatia Mipango ya Mafunzo katika Wizara na taasisi zake, matarajio ni kuwapeleka kwenye mafunzo wafanyakazi 900 ndani na nje ya nchi. Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

8.0 TAASISI ZA MAFUNZO

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuvihudumia vyuo vyetu vya mafunzo kwa lengo la kuviwezesha kutoa taaluma na wanataaluma wa kada mbalimbali katika sekta za uchukuzi na hali ya hewa. Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Uchukuzi ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Chuo cha Hali ya Hewa - Kigoma, Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam, Chuo cha Bandari Dar es Salaam na Chuo cha Reli Tabora.

8.1 Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

152. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, DMI imeendelea kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali za uchukuzi baharini. Katika kipindi hiki, jumla ya wanafunzi 112 wa ngazi ya diploma na cheti, wakiwemo wanafunzi 33 kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na wanawake 12 walidahiliwa. Jumla ya Wanafunzi 3,413 wa kozi fupi na maafisa wa meli 72 walihitimu mafunzo. Katika kozi fupi, wahitimu 422 walitoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na wanawake walikuwa140. Aidha, Chuo kipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi wa Mkuranga ili kufanikisha uendelezaji wa eneo hilo.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa Chuo cha Bahari kinaimarisha mahusiano na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi ili kuweza kubadilishana uzoefu, kuongeza tija na fursa za kiushindani katika soko la ajira. Katika mwaka 2013/2014, Chuo kiliwatafutia ajira wahitimu 105 kwenye meli za nje na ndani ya nchi, kati yao mabaharia watatu ni wanawake. Aidha, Chuo Kikuu cha Dallian cha nchini China kimekamilisha kazi ya kujenga mtambo wa kufundishia (simulator) na unatarajiwa kuanza kutumika Julai, 2014.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Wizara kupitia DMI itaanzisha program za mafunzo katika sekta ya mafuta na gesi (mobile offshore training). Lengo ni kuwapatia Watanzania ujuzi na utaalam utakaowawezesha kuajiriwa katika sekta hii. Aidha, ujenzi wa Mtambo wa kufundishia (Simulator) umekamilika na unatarajiwa kuanza

kutumika mwezi Septemba, 2014. Chuo kimefanya mazungumzo na kampuni ya *Farstard Shipping* ya nchini Norway pamoja na Chuo kinachotoa mafunzo ya uchimbaji mafuta cha Ghana (*Ghana Oil Drilling Academy)* ili kuweza kushirikiana katika utoaji wa mafunzo. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya miradi ya uendelezaji wa miundombinu ya Chuo.

8.2 Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

155. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Chuo kimekuwa na jumla ya programu 27 ikilinganishwa na programu 21 zilizokuwepo katika mwaka 2012/2013. Hili ni ongezeko la program sita sawa na asilimia 29. Kati ya program hizo, moja ni ya Shahada ya Uzamili, tisa ni za Stashahada za Uzamili, saba ni za Shahada ya kwanza na 10 za Astashahada na Stashahada. Ongezeko la program limekwenda sambamba na ongezeko la udahili. Katika mwaka 2013/2014, Chuo kimedahili jumla ya wanafunzi 1,582 sawa na ongezeko la asilimia 32 ikilinganishwa na lengo la kudahili wanafunzi 1,200. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi. Katika mwaka 2013/2014 jumla ya kozi fupi 12 ziliendeshwa na kuweza kuvutia jumla ya washiriki 3,635. NIT ilitoa mafunzo kwa waendeshaji pikipiki katika mikupuo sita. Mikupuo hiyo ilishirikisha jumla ya washiriki 661 ukilinganisha na lengo la washiriki 600. Hili ni ongezeko la washiriki 61 sawa na asilimia 10.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kupata wataalam wenye sifa katika Sekta ya Uchukuzi, katika mwaka 2013/2014, Chuo kimehuisha mitaala katika ngazi ya Stashahada na Shahada, kimetengeneza mtaala mpya katika ngazi ya Stashahada ya Uzamili ya Menejimenti ya Usalama na Usafiri Barabarani, mitaala ya kufundishia madereva wa mabasi ya abiria, magari ya mizigo, magari ya viongozi, walimu wa madereva na mitaala ya ukaguzi wa magari imeboreshwa na sasa ipo katika kiwango kinachokubalika kimataifa.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya uchukuzi wa barabara inakabiliwa na changamoto ya uwepo wa magari chakavu barabarani. Ili kukabiliana na changamoto hii, katika mwaka 2013/2014, Chuo kilianza ujenzi wa Kituo cha kisasa cha ukaguzi wa magari baada ya kupata msaada wa seti nne za mitambo ya ukaguzi wa magari kutoka Benki ya Dunia. Mitambo hii ina uwezo wa kukagua magari 800 kwa siku. Aidha, baada ya Shirika la Viwango la Taifa kutoa kibali cha kukagua magari yaliyotumika na kuingia nchini bila kukaguliwa, Chuo kinaendelea na ujenzi wa kituo cha kukagua magari hayo. Ujenzi wa Jengo la kituo hiki umekamilika kwa asilimia 80 na seti moja ya mitambo ya ukaguzi tayari imesimikwa na itaanza kutumika mwezi Julai, 2014. Ukamilishaji wa

ujenzi wa kituo pamoja na usimikaji wa seti tatu za mitambo utakamilika katika mwaka wa fedha 2014/2015.

158. ***Mheshimiwa Spika***, kuhusu ujenzi wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo, kazi zilizotekelezwa ni kuweka mfumo wa baridi, umeme na dari. Ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 80. Aidha, Chuo kilifanya ukarabati wa mabweni mawili ya wanafunzi, Jengo la utafiti na ushauri elekezi na karakana ya magari.

159. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi kirefu Chuo kimekuwa kikikabiliwa na tatizo la msongamano wa wanafunzi madarasani, uhaba wa ofisi za walimu, ufinyu wa ukumbi wa maktaba, kukosekana kwa kumbi za mikutano na maabara za kompyuta. Napenda kulitaarifu Bunge hili kuwa kuanzia mwaka 2015/2016, matatizo haya yatapungua kwani jengo la Kituo cha Rasilimali Mafunzo litaanza kutumika.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya mwaka 2013/2014 niliahidi kuwa Chuo kitajipanua kwa kusogeza huduma zake katika mikoa ya Mbeya, Arusha, Dodoma, Mwanza na Kigoma. Napenda kutoa taarifa kuwa huduma za Chuo sasa zinapatikana katika mikoa hiyo. Katika mwaka 2014/2015, Chuo kitaendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kusomea.

161. ***Mheshimiwa Spika,*** wakati nawasilisha Hotuba ya bajeti ya mwaka 2013/2014, nilitoa taarifa ya Chuo kuanza kutumia viwanja vya ndege vya Dodoma na Tanga kwa ajili ya mafunzo ya marubani wa ndege. Maandalizi ya kuanza mafunzo ya urubani katika viwanja hivyo vya ndege yanaendelea ambapo mitaala na nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kuanza mafunzo hayo zimekamilika. Chuo kinaendelea kukamilisha taratibu za kupata ithibati ya mitaala ya kuendeshea mafunzo hayo kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA).

162. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, kazi nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na kudahili wanafunzi katika kozi ya muda mrefu ya Ufundi wa Ndege na Urubani; kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la maktaba na kukarabati majengo ya Chuo; kuanzisha programu tatu katika ngazi ya shahada ya kwanza na hivyo kuongeza udahili kwa asilimia 27 ili kufikia udahili wa wanafunzi 2,000. Aidha, Wizara itakamilisha taratibu za uanzishaji wa Bodi ya wanataaluma wa Logistiki na uchukuzi.

8.3 Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam

163. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam kimeendelea kutoa mafunzo kuhusu sekta ya anga katika maeneo ya taaluma za uongozaji ndege; mafundi wa mitambo ya kuongozea ndege; wataalam wa mawasiliano ya urukaji (Aeronautical Information Officers); usalama na upekuzi (aviation security); safari za ndege (Flight Operations Officers) na usimamizi wa viwanja vya ndege (Apron Management). Aidha, Chuo kinatoa mafunzo kwa wanafunzi wa ndani na nje ya nchi.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, jumla ya wanafunzi 373 walihitimu mafunzo hayo katika Chuo hiki. Kati yao wanafunzi 322 ni Watanzania na 51 ni kutoka nje ya nchi. Chuo kinaendelea na Mpango wake wa kuhakikisha kwamba viwango vya mafunzo vinaendelea kuboreshwa. Aidha, kazi ya kumtafuta Mtaalam Mshauri atakayetoa ushauri wa jinsi ya kukipanua chuo na kukidhi mahitaji halisi ya soko la mafunzo ya sekta ya anga barani Afrika itakamilika Julai, 2014. Lengo ni kukiwezesha Chuo kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi. Kazi inayoendelea sasa ni kuhakikisha kwamba viwango vya mafunzo vinaendelea kuboreshwa.

165. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2014/2015, Chuo kitaendelea na juhudi za kupata eneo la kutosha kwa ajili ya ujenzi wa Chuo kipya. Aidha, Chuo kitaendelea kuhakikisha kwamba viwango vya mafunzo vinaendelea kuboreshwa ili kukidhi matakwa ya Kitaifa na Kimataifa.

8.4 Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma

166. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kuboresha Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kiweze kutoa mafunzo yenye tija licha ya kukabiliwa na changamoto mbalimbali. Kazi zilizotekelezwa katika mwaka 2013/2014 ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa uzio wa kuzunguka eneo la Chuo na kuendelea na kazi ya usanifu wa michoro ya ujenzi wa hosteli za wanafunzi ambapo zabuni kwa ajili ya ujenzi huo itatangazwa Juni, 2014.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto zinazokikabili Chuo hiki ni pamoja na jinsi ya kukiboresha ili kiwe katika viwango vya kimataifa ikizingatiwa kuwa ni chuo pekee kinachotoa elimu ya awali na ya kati ya hali ya hewa nchini. Ili kukabiliana na changamoto hizi, katika mwaka 2014/2015, Serikali itakamilisha ujenzi wa hosteli ya Chuo.

8.5 Chuo cha Reli Tabora (TIRTEC)

168. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Chuo cha reli kimeendelea kutoa mafunzo katika fani mbalimbali za shughuli za reli. Chuo hiki kina uwezo wa kuhudumia wanafunzi 200 katika kampasi ya Tabora na wanafunzi 150 katika kampasi ya Morogoro. Aidha, katika mwaka 2013/2014 Chuo kimeendelea kutoa mafunzo kwa wanafunzi 160 katika kozi za Mastesheni masta wanafunzi 44; Magadi na wakaguzi wa tiketi wanafunzi 36; Wakaguzi wa njia ya reli Wanafunzi 26; Udereva wa treni Wanafunzi 24 na Wakaguzi wa mabehewa wanafunzi 30. Kwa sasa Chuo cha Reli kimesajiliwa na Baraza la Vyuo vya ufundi (NACTE) na kipo katika mchakato wa kupata udahili wa kudumu (full Accreditation). Aidha, Chuo kinakabiliwa na changamoto za uchakavu wa miundombinu ikiwa ni pamoja majengo, upungufu wa Wakufunzi na uhaba wa vifaa vya kufundishia. Katika mwaka 2014/2015 Chuo kinatarajia kuajiri wakufunzi wapya.

9.0 MASUALA MTAMBUKA

9.1 Kuzingatia masuala ya Jinsia

169. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kulipa kipaumbele suala la ushirikishwaji wa wanawake katika sekta ya uchukuzi kwa kuzingatia Itifaki na Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Katika kuhakikisha ushirikishwaji wa wanawake katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Uchukuzi, hivi sasa tuna wanawake madereva wa vichwa vya treni nane. Kati ya hao, wawili wameajiriwa TRL na sita wameajiriwa na TAZARA; Marubani wanawake saba; kati ya hao, mmoja yuko ATCL, wanne wako Precision Air, mmoja yuko TCAA na mmoja yuko TGFA. Aidha, tuna wahandisi wanawake wanne ambapo wawili wanafanya kazi TRL, mmoja yuko ATCL na mmoja TGFA. Pamoja na ugumu wa kazi ya udereva wa magari ya masafa marefu, nafurahi kuwaarifu kuwa tuna madereva wanawake watatu wa mabasi na wawili wa malori.

9.2 Utunzaji wa Mazingira

170. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2013/2014, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) ilifanya tathmini ya athari za mazingira na kukamilisha Mpango Mkakati wa kutunza mazingira (Strategic Environment Assessment - SEA) wa Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa mifumo ya Uchukuzi na Biashara (Comprehensive Transport and Trade Systems Development Master Plan). Mradi huu unajumuisha njia zote za usafiri yaani anga, nchi kavu na majini.

171. ***Mheshimiwa Spika***, hivi sasa Tanzania ina miradi mingi ya kutafuta na kuchimba gesi na mafuta baharini. Vilevile Tanzania iko karibu na njia kuu ya meli za kimataifa zinazobeba mafuta. Kutokana na hali hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais na Taasisi nyingine imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kulinda mazingira ya Bahari endapo mafuta yatamwagika baharini. Aidha, Bandari ya Dar es Salaam imekuwa inapakua kiwango kikubwa cha mafuta ghafi yanayokwenda nchi jirani ya Zambia. Mwaka 2013 pekee, mafuta ghafi yaliyopita katika Bandari ya Dar es Salaam kwenda Zambia yalikuwa tani 2,761,723. Ili kukabiliana na janga hili endapo mafuta yatamwagika baharini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa rasimu ya Mpango wa Taifa wa kukabiliana na mafuta yatakayomwagika baharini (National Marine Oil Spill Response Contigency Plan-NMOSCP).

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Denmark (DANIDA) kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imeanza mradi wa kujenga uwezo wa Bandari nchini ili kuwa na huduma ya kisasa ya kupokea uchafu (Waste Reception Facilities) kutoka melini. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu ni kufanya usanifu wa kina.

173. ***Mheshimiwa Spika,*** utunzaji wa mazingira ya miundombinu ya reli na barabara imeendelea kuwa changamoto kubwa kwa Wizara yangu. Shughuli za kijamii zinazofanyika katika milima karibu na njia ya reli sehemu za Kilosa hadi Gulwe zimeendelea kuathiri huduma za uchukuzi wa Reli ya Kati kwa kiasi kikubwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge, Madiwani na Viongozi wa Serikali za Mitaa waungane na Wizara katika kuelimisha Wananchi na kukemea vitendo vya kukata miti ovyo, kulima bila kufuata ushauri wa Wataalamu na kulima kwenye kingo za mito na reli. Vitendo hivyo vinaharibu miundombinu hiyo hasa wakati wa mvua hivyo kuigharimu Wizara yangu fedha nyingi za kufanya matengenezo.

9.3 Udhibiti wa UKIMWI

174. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia suala la kudhibiti maambukizi ya UKIMWI/VVU ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa watumishi kupima ili kujua afya zao. Aidha, Wizara kupitia TACAIDS ilifanya utafiti wa hali halisi (Situational Analysis) ili kutambua hali ilivyo kuhusu uelewa wa masuala ya UKIMWI kwa watumishi wake. Utafiti huo umebaini kuwa asilimia 98 ya watumishi wana uelewa mkubwa kuhusu UKIMWI na mbinu za kukabiliana nao. Huduma zimeendelea kutolewa kwa watumishi waliojitambulisha kuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI na kuhimiza matumizi sahihi ya dawa za kurefusha maisha ili kuwawezesha

kuishi kwa matumaini na kupata nafasi ya kuendelea kuchangia maendeleo ya nchi.

9.4 Mapambano Dhidi ya Rushwa

175. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuziba mianya ya rushwa kwenye maeneo yake. Katika mwaka 2013/2014 Wizara iliunda Kamati ya Maadili ambayo pamoja na mambo mengine ina jukumu la kuhakikisha kuwa watumishi hawajihusishi na rushwa. Aidha, Wizara ilitoa mada mbalimbali kwa wafanyakazi kuhusu vitendo vya rushwa, namna ya kuepukana navyo na uzingatiaji wa utekelezaji wa sheria ya manunuzi katika zabuni za ujenzi, ushauri na ununuzi wa vifaa. Katika mwaka 2014/2015, Wizara itaendelea kuliweka suala la rushwa kuwa moja ya agenda katika vikao vya mara kwa mara vya watendaji wakuu, watumishi na wadau wa sekta hii.

9.5 Habari, Elimu na Mawasiliano

176. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliendelea kuhakikisha kuwa elimu inatolewa kwa umma kupitia vipindi maalum vya luninga; mikutano, ziara na warsha mbalimbali zilizowashirikisha waandishi wa habari; tovuti ya Wizara na kushiriki katika maonyesho ya kitaifa kama maadhimisho ya siku ya Wakulima, miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar na miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Moja ya vipindi maalum vilivyoandaliwa ni pamoja na kipindi maalum cha Luninga kilichoeleza mafanikio ya Serikali. Kipindi hicho kilielezea miradi mbalimbali iliyotekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi chini ya Program ya Matokeo Makubwa sasa (BRN) na miradi mingine ya kimkakati. Aidha, mikutano na ziara mbalimbali zilitolewa taarifa ikiwa ni pamoja na hatua za maendeleo zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo.

177. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2013/2014 ulikuwa ni mwaka wa tatu mfululizo kwa Wizara kupata Ushindi wa tatu wa Wizara za Sekta ya Uchumi-Huduma na hivyo kupata cheti maalum na kikombe katika Maonesho ya Sikukuu ya Wakulima. Katika mwaka 2014/2015, Wizara na taasisi zake zitaendelea kutangaza shughuli mbalimbali zinazozifanya ikiwamo utekelezaji wa miradi ya BRN kwa kuandaa vipindi maalum na kuandika makala mbalimbali kwa kutumia njia za mawasiliano zikiwemo luninga na magazeti ili kuwaelimisha na kuwapa taarifa wananchi kuhusu utendaji wa sekta ya uchukuzi na hali ya hewa.

10.0 SHUKRANI

178. ***Mheshimiwa Spika,*** ningependa sasa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliotoa ushirikiano katika kufanikisha malengo ya sekta. Hawa ni pamoja na Washirika wa Maendeleo ambao tunasaidiana nao katika kufanikisha utekelezaji wa program na mipango mbalimbali ya maendeleo ya sekta za uchukuzi na hali ya hewa. Shukrani za dhati ziende kwa nchi na mashirika ya kimataifa yaliyochangia katika maendeleo ya sekta yetu. Nchi na mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Bahari Duniani (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), UNESCO, Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi kwa Afrika (BADEA), Kuwait Fund, Malaysia, Jamhuri ya Korea, OPEC Fund, Umoja wa Nchi za Ulaya, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uholanzi, Japan, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), TMEA, DFID, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Urusi, Sweden, Ufaransa, Finland, Singapore na wengine wengi. Napenda kuwaomba waendelee kushirikiana nasi katika kuimarisha sekta za uchukuzi na hali ya hewa.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuwashukuru viongozi wenzangu wa Wizara ya Uchukuzi, nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba (Mb.), Katibu Mkuu Dkt. Shaaban Ramadhan Mwinjaka, Naibu Katibu Mkuu, Bi. Monica Leander Mwamunyange, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti wa Bodi za SUMATRA, TCAA, TGFA, TTFA, KADCO, TAA, TPA, TRL, RAHCO, MSCL, TMA, SINOTASHIP, ATCL, DMI, NIT na TAZARA, viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi. Ninafarijika kwa ushirikiano wanaonipa katika jitihada za kuendeleza sekta za uchukuzi na hali ya hewa. Nikiri kuwa bila mchango wao mkubwa, kazi yangu ya kuongoza sekta hii, ingekuwa mgumu, na pengine kutoweza kabisa.

11.0 MAOMBI YA FEDHA

180. ***Mheshimiwa Spika,*** ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2014/2015, Ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi **527,933,790,000.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **93,306,391,000** zimetegwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **434,627,399,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha Shilingi **33,027,291,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **60,279,100,000** fedha za Matumizi Mengineyo (OC). Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha Shilingi **273,140,000,000** fedha za ndani na Shilingi **161,487,399,000** fedha za nje.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hotuba hii, nimeambatanisha jedwali la miradi yote itakayotekelezwa katika mwaka 2014/2015 pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza miradi hiyo. Naomba takwimu hizo zichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

182. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nimalize hotuba yangu kwa kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hoja ya Wizara yangu. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya: www.mot.go.tz.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge kwanza niwashukuru kwa ushirikiano wenu, wiki nzima hii tumekaa hapa, kazi kubwa sana ya Serikali tumefanya. Mafanikio haya yanatokana na ninyi wenyewe kutoa ushirikiano kwenye Meza. Nimshukuru Mheshimiwa Spika, nimshukuru Naibu, lakini vile vile niwashukuru Makatibu ambao tuko nao na hao wenzetu ambao wanatubebea hizi *note* zetu kwa kazi nzuri. Niwaombee *weekend* nzuri na Mungu akipenda basi mbele ya uhai tutakutana Jumatatu. Naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.47 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,
Tarehe 26 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)